

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA WA KUMI NA TANO**

**Kikao cha Ishirini na Mbili – Tarehe 7 Mei, 2019**

*(Bunge Lillianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaanza kama tunavyojua Waislamu tumeshaanza Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, kwa hiyo nitumie fursa hii kuwatakia mfungo mwema wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani Waislamu wote popote walipo. Pia nimwombe Mwenyezi Mungu alijalie Taifa letu la Tanzania lipate kheri na baraka zote za mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani. *(Makofi)*

Tunaendelea, Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**MHE. ROSE C. TWEVE – K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa Bajeti na majukumu ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI – K.n.y. MSEMaji MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI WA WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaweka Mezani taarifa hii, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba niwatakie Waislamu wote Wabunge wenzetu pamoja na Watanzania wote kheri na Baraka katika Mfungo huu wa Ramadhani. *(Makofi)*

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Wizara ya Afya, Maendeleo Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020

**MWENYEKITI:** Ahsante. Katibu tuendeleo.

**NDG. BAKARI KISHOMA - KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Shaabani Omari Shekilindi, Mbunge Lushoto, sasa aulize swali lake.

Na. 176

## Ukarabati wa Hospitali ya Lushoto

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI** aliuliza:-

Hospitali ya Wilaya ya Lushoto ni ya muda mrefu na hata ujenzi wa majengo yake ni wa kizamani ambao hauendani na utoaji huduma na Serikali ina utaratibu wa kukarabati na kuongeza majengo katika Hospitali za Wilaya:-

Je, ni lini Hospitali ya Wilaya ya Lushoto itakarabatiwa?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shaabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Wilaya ya Lushoto ni miongoni mwa Hospitali Kongwe za Wilaya nchini na imekuwepo tangu mwaka 1967. Tangu kuanzishwa kwake, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imefanya ukarabati na upanuzi wa majengo kama ifuatavyo:-

(i) Mwaka wa fedha 2006/2007, ujenzi wa jengo la mapokezi, jengo la wagonjwa wa nje, jengo la famasi, jengo la maabara na jengo la upasuaji kupitia mradi wa KfW;

(ii) Kwa mwaka wa fedha 2008/2009, ujenzi wa jengo la kuhifadha maiti kwa maana ya *mortuary* na uwekaji wa vigae (*tiles*) katika wodi zote;

(iii) Kwa mwaka wa fedha 2011/2012, ujenzi wa jengo kwa ajili ya ndugu wa wagonjwa kusubiria yaani *waiting bay*;

(iv) Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, ukarabati mkubwa wa jengo la upasuaji;

(v) Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, ukarabati wa jengo la mapokezi, jengo la wagonjwa wa nje, jengo la famasi, jengo la maabara, jengo la wodi ya watoto na ujenzi wa jengo la dawa za ziada la Halmashauri kwa maana ya *buffer store*;

(vi) Kwa mwaka wa fedha 2018/2019, ujenzi wa kichomea taka (*Incinerator*) na shimo la kutupia kondo la nyuma la uzazi kwa maana ya *placenta pit*;

(vii) Kwa mwaka wa fedha 2018/2019, ukarabati wa jengo la *CTC* linalovuja unaendelea kupitia ufadhili wa *AMREF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kukarabati miundombinu ya vituo vya kutolea huduma za afya nchini kwa kadri upatikanaji wa fedha utakavyokuwa unaruhusu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shaabani, nimekuona.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Waziri yenye kutia moyo lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa Serikali ina mpango wa kukarabati Vituo vya Afya na Hospitali za Wilaya na kutoa vifaatiba. Je, ni lini sasa itatoa *X-ray* mashine katika Hospitali ya Wilaya ya Lushoto ili kupunguza msongamano au usumbufu wa wananchi wangu kutoka Lushoto kwenda mpaka Tanga hadi Muhimbili? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Jimbo la Lushoto lina Kata 15 na Kituo cha Afya kimoja tu. Wananchi wa Kata za Gare na Ngwelo kwa nguvu zao wenyewe wameanza kujenga maboma hayo ya Vituo vya Afya. Je Serikali ina mpango gani wa kuongeza fedha au wa kuwapatia fedha

zile ambazo zinatolewa shilingi milioni 400 kwa ajili ya kujenga vituo hivyo? Nia na madhumuni ni kupunguza msongamano mkubwa uliopo katika Hospitali ya Wilaya ya Lushoto. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Shekilindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la kwanza juu ya uwepo wa *X-ray*, naomba nimtoa wasiwasi Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Lushoto kwamba mchakato uko kwenye hatua za mwisho kupitia *MSD*. Muda si mrefu *X-ray* ile itapatikana ili wananchi wa Lushoto na maeneo ya jirani waweze kupata huduma ya vipimo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika swali lake la pili, naomba nimpongeze yeye mwenyewe na Mheshimiwa Shangazi wamekuwa wakifuatilia sana kuhusiana na Hospitali ya Lushoto. Naomba pia niwapongeze wananchi ambao wameanza ujenzi wa Kituo cha Afya. Hakika pale ambapo wananchi wanaanza Serikali inawaunga mkono mara moja. Naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwa kadri bajeti itakavyoruhusu na fedha ikipatikana tunahakikisha tunapeleka maeneo ambayo tayari nguvu ya wananchi ilishakuwepo. Mchakato utakavyokamilika hakika hatutawasahau wananchi wa eneo alilolitaja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mary Chatanda.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Korogwe Mji tumekabidhiwa Hospitali ya Wilaya Magunga kutoka Korogwe Vijijini. Kwa bahati mbaya sana ina wodi moja tu ambayo wanalala

wajawazito pamoja na wale waliojifungua. Je, Serikali itakuwa tayari kusaidia tupate fedha angalau tuweze kujenga wodi ya wajawazito na watoto?

**MWENYEKITI:** Waziri majibu, Mheshimiwa Jafo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana ya ndugu yangu Mheshimiwa Shekilindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri wazi kwamba tumefika katika Hospitali ile anayoizungumzia Mheshimiwa Mama Chatanda mara kadhaa licha ya upungufu wa wodi lakini hospitali ile imekuwa ya wahenga sana, imekuwa kongwe. Kwa hiyo, ni mpango wetu kuhakikisha tunafanya maboresho ya hospitali za zamani. Nimhakikishie Mheshimiwa Chatanda kwamba licha ya wodi hizo lakini tutaangalia kwa jicho lingine jinsi gani tufanye hospitali ile ifafanane sasa na Halmashauri ya Mji wa Korogwe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Hospitali ya Wilaya ya Mji wa Tarime ambayo kiukweli inatoa huduma kama Hospitali ya Wilaya au ya Mkoa naweza nikasema na Kanda Maalum Tarime Rorya, Mheshimiwa Naibu Waziri alitembelea na akaona ni jinsi gani inaelemewa kwa utoaji wa huduma. Hivi ninavyoongea chumba cha kuhifadhia maiti kwa maana ya *mortuary* kwanza ni kifinyu lakini pia mashine yake kwa maana ya *compressor* haifanyi kazi na wale ndugu zetu ambao tunawahifadhi pale wakikaa muda mdogo wanaharibika. Nataka kujua *commitment* ya Serikali ya kuhakikisha kwamba inasaidia ukarabati au upanuzi wa *mortuary* ikiwemo kusaidia hiyo mashine ya *compressor* kwa sababu Halmashauri ya Mji wa Tarime haina kipato cha kutosha. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Esther Matiko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge nilipata fursa ya kutembelea hospitali ile ambayo ina *congestion* kubwa na bahati nzuri nilipata fursa nikiambata na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Maelekezo ambayo yalikuwa yametolewa, kwanza ni kuhakikisha kwamba dawa za kutosha zinatolewa ili kukidhi haja kwa sababu wananchi ni wengi wanaopata huduma pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hili ambalo amelisema kuhusiana na chumba hicho cha kuhifadhia maiti ambacho mashine imeharibika kiasi kwamba sasa mwili unaharibika ndani ya muda mfupi, naomba *seriously* tukitoka hapa tuwasiliane na Mheshimiwa Mbunge ili tuone hatua za haraka za kuchukua kuhakikisha kwamba mochwari ile inafanya kazi.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Zubeda Hassan Sakuru, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 177

**Kutokidhi Viwango vya Utoaji huduma kwa Hospitali na Vituo vya Afya nchini**

**MHE. JOSEPH L. HAULE (K.n.y. MHE. ZUBEDA H. SAKURU)** aliuliza:-

Hospitali na Vituo vya Afya vinatakiwa kukidhi viwango vya utoaji huduma kwa wagonjwa; lakini hospitali na Vituo vya Afya vingi havina viwango vya utoaji huduma.

Je, Serikali ina mkakati gani mahsusi wa kuhakikisha Vituo vya Afya na hospitali vinakidhi viwango vya utoaji huduma?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zubeda Hassan Sakuru, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuimarisha utoaji wa huduma za afya kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwenye maeneo mbalimbali ya vituo vya kutolea huduma za afya ili kukidhi viwango vya kutolea huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha viwango vya utoaji huduma za afya nchini, katika mwaka wa fedha 2017/2018 na 2018/2019, Serikali imetoa kiasi cha shilingi bilioni 285.17 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali za Halmashauri 67, ujenzi na ukarabati wa Hospitali za Wilaya tisa (9), Vituo vya Afya 304 na Zahanati 39. Vilevile, Serikali imejenga na kukarabati nyumba za watumishi wa afya nchini 301. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali imetenga shilingi bilioni 23.9 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali za Halmashauri mpya 27 na ujenzi na ukarabati wa Vituo vya Afya 52.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018 na 2018/2019, Serikali imeajiri jumla ya watumishi 8,444 wa kada mbalimbali za afya kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuboresha miundombinu ya afya, kuajiri wataalamu, kununua dawa, vitendanishi na vifaa tiba ili kuhakikisha vituo vya kutolea huduma vinakidhi viwango vinavyohitajika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Haule.



**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, pamoja na ujenzi wa hospitali na Vituo vya Afya lakini bado kuna upungufu mkubwa sana wa watumishi wa afya hapa nchini. Je, Serikali haioni sasa huu ni muda muafaka wakati wanajenga Vituo vya Afya, lakini pia watoe ajira mpya kwa watumishi wa afya na pia walipe stahiki za wale watumishi wa afya wengine ili kuongeza morali na tija? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Jimbo la Mikumi lina jiografia mbaya sana na tuna Vituo vinne vya Afya vya Kidodi, Mikumi, Ulaya na Malolo ambacho wananchi wanajenga kwa nguvu zao wenyewe. Je, Serikali haioni sasa huu ni muda muafaka ili kuokoa Watanzania wa Mikumi tuweze kupatiwa magari ya wagonjwa kusaidia akina mama na watoto ambao wanapata matatizo katika maeneo hayo? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Jafo, majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mheshimiwa Haule katika ziara kadhaa nilizofanya tulikuwa pamoja kule Jimboni kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mpango wa Serikali, kama tunavyofahamu kwamba Mheshimiwa Rais na Serikali kwa ujumla imefanya mchakato wa ujenzi wa Vituo vya Afya 352 hivi karibuni, Hospitali zetu za Wilaya 67 na mwaka huu tumeongeza 27 mpya, jambo hili linataka *human resources* kwa ajili ya kuweza kufanya kazi vizuri.

Kwa hiyo, ni mpango wa Serikali tutaangalia nini kifanyike. Licha kwamba mwanzo tuliajiri takribani watumishi wasiopungua 11,000; wale wa Serikali za Mitaa na Serikali Kuu lakini tutaangalia nini kifanyike kwa ajili ya kuongeza idadi ya watumishi katika vituo vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mikumi suala zima la kuongeza miundombinu, nikushukuru, lakini Mbunge hapa kwanza unge-*appreciate* kazi kubwa iliyofanyika pale Mikumi, nadhani na wewe unakumbuka, ilikuwa ni ya kusuasua sana. Serikali tumeenda tumefanya kazi kubwa na hivi sasa imekuwa ni miongoni mwa Kituo bora sana cha Afya katika eneo lile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo tutaendelea kuangalia nini kifanyike kwa maeneo mbalimbali yenye changamoto kubwa, siyo Mikumi peke yake. Ni mpango wa Serikali kuangalia nchi nzima tunahakikisha wananchi wanaopata shida ya huduma ya afya sasa inakuwa ni historia. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hongoli.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Lupembe katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ina vituo vinne lakini haijawahi kupata fedha kwa ajili ya uboreshaji wa vituo hivi na jiografia ya Jimbo lile ni mbaya sana. Tunashuruku kwamba mmetupatia Hospitali ya Wilaya lakini wananchi wanataka kujua ni lini Halmashauri ya Wilaya ya Njombe itapata fedha kwa ajili ya uboreshaji wa Vituo vya Afya vya Kichiwa, Sovi, Lupembe na Ikuna ambacho ujenzi wake karibia unakamilika? Naomba tupate majibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Jafo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi naomba nimpongeza Mheshimiwa Hongoli kwa vile nafahamu wazi na yeye anafahamu mpaka jana takribani saa tatu na nusu usiku tulikuwa tunaongea naye kuhusu suala zima la sekta ya afya. Hii inaonyesha jinsi gani anajali wananchi wake na kufuatilia masuala ya afya. Ndiyo maana katika awamu ya kwanza tulimpatia Hospitali ya Wilaya na

najua katika mpango wa bajeti ya mwaka huu tumemtengoa Kituo kimoja cha Afya lakini bado hali siyo nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nilikuhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba ni *commitment* yetu sisi Serikali na Mungu akijalia huenda kabla hata mwezi Julai haujafika, tutafanya kila liwezekanalo tukupatie Kituo kingine cha Afya bora zaidi ili wananchi wa Jimbo lile la Njombe DC waweze kupata huduma vizuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jafo. Mheshimiwa Peter Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili linafanana sana na Hospitali ya Frelimo Mjini Iringa. Hospitali yetu ya Frelimo inatoa huduma kubwa kwa maeneo mengi ukizingatia kwamba Iringa Mjini ndiyo kitovu na maeneo mbalimbali wanakuja kutibiwa pale. Katika mpango wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa mmekuwa mkitoa pesa za vifaa kwenye hospitali mbalimbali lakini cha kushangaza mwaka jana kwenye Hospitali yetu ya Frelimo hamkutoa mkiona kwamba ni Kituo cha Afya wakati ni hospitali. Nilitaka nipate majibu ni kwa nini hamkutoa vile vifaa kama hospitali zingine kwenye Hospitali yetu ya Frelimo ambayo kwa kweli inasaidia wagonjwa wengi sana katika Manispaa yetu ya Iringa Mjini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Msigwa na Mheshimiwa Msigwa anafahamu nimefika pale Flerimo mara kadhaa na nakumbuka tulikuwa na Mbunge pacha wako Mheshimiwa mama Kabati. Hospitali ile inachukua watu wengi sana na mimi nimefika pale nimeona. Naomba niwapongeze Madaktari wa pale wanafanya kazi vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *commitment* yetu sisi Serikali, naomba nikuhakikishie kwamba eneo lile tutaenda kuliboresha zaidi. Nilivyofika pale nimeona kuna kila sababu ya kufanya maboresha na rasilimali ni chache lakini lazima tutazigawanya. Kwa hiyo, ni mpango wa Serikali tutafanya kila liwezekanalo ili wananchi wa Iringa waweze kupata huduma vizuri katika Hospitali ya Flerimo. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mary Nagu.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Kituo cha Afya cha Endasak na Basotu nilishaongea na Mheshimiwa Waziri atusaidie kuboresha ili vionekane kama ni vituo kwa sababu havina hata wodi na havijafikia hadhi ile lakini vinajulikana na wananchi kama ni Kituo cha Afya. Naomba nijue Mheshimiwa Waziri anasema nini kuhusu vituo hivi viwili vya Hanang?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo la nyongeza

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumshukuru mama yangu Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu *senior MP* katika Bunge hili. Ni kweli niliongea na Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu na bahati nzuri nimefika kule Hanang, ni mpango wa Serikali naomba nikuhakikishie Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu kama tulivyozungumza ni *commitment* ya sisi Serikali tunatafuta fedha tutajitahidi kwa kadri iwezekanavyo vituo vile viweze kupata huduma kama tunayokusudia, kwa hiyo, hilo ondoa hofu Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu.

**MWENYEKITI:** Asante sana Mheshimiwa Jafo tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Esther Matiko kwa niaba.

Na. 178

### **Changamoto zinazoikabili Hospitali ya Mkoa Tabora**

**MHE. ESTHER N. MATIKO (K.n.y. MHE. HAWA S. MWAIFUNGA)** aliuliza:-

Hospitali ya Mkoa wa Tabora inakabiliwa na changamoto kubwa za majengo, Wauguzi, Madaktari na Wahudumu wengine wa Hospitali, pia kuna uhaba mkubwa wa vitanda hali inayosababisha wajawazito kuzalia chini:-

(a) Je, katika mwaka huu wa fedha Serikali imejipanga vipi kuwasaidia Wananchi wa Tabora kupata ahueni kwa kutatua kwa kero za Hospitali hiyo inayotegemewa na zaidi ya robo tatu ya wakazi wa mji wa Tabora

(b) Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kuwa Wilaya ya Tabora Mjini na Uyui nazo zinapata hospitali?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora katika ajira mpya za mwezi Julai, 2018 imeajiri watumishi wapya wapatao 49 katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora Kitete kati ya hao wakiwemo wauguzi, wateknolojia, wafamasia na madaktari na kufanya hospitali kuwa na jumla ya watumishi 357 kwa kada zote kati ya watumishi 468 wanaohitajika kulingana na ikama ya hospitali ambayo ni sawa na asilimia 76.3 ya mahitaji halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hospitali haina tatizo la vitanda na magodoro lakini kuna ufinyu wa majengo unaopelekea kuwa na vitanda vichache. Hivyo basi kwa kuwa hospitali za rufaa za mikoa zimekabidhiwa rasmi chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa Fedha 2019/2020 wizara imetenge bilioni 12 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa hospitali za rufaa za mikoa ikiwemo Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora ambapo itaweza kupunguza uhaba wa miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka fedha 2018/2019 Serikali imepanga kujenga hospitali za wilaya 67 nchi nzima katika jitihada za kuhakikisha kila mwananchi anapata huduma bora za afya kwa upande wa Wilaya ya Tabora Mjini na Uyui nazo zimepatiwa fedha kiasi cha bilioni 1.5 kwa kila moja kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali imeboresha vituo vya afya 13 katika Wilaya ya *Uyui DC, Tabora MC, Nzega TC, Kaliua DC, Igunga DC, Skonge DC, Urambo DC* na *Nzega DC*. Kukamilika na kuanza kutumika kwa hospitali na vituo vya afya hivi vitapunguza sana msongamano katika Hospitali ya Rufaa ya Kitete.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuwa Serikali imekiri kwamba imetenga bilioni 12 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa hospitali za rufaa za mikoa na nafikiri na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara kwangu itakuwepo. Na kwa kuwa Serikali imekiri kwamba kuna ufinyu wa majengo katika Hospitali ya Mkoa wa Tabora kupelekea hata vitanda kukosa sehemu ya kuweka na hivyo kupelekea msongamano wa wagonjwa na kudumaza utoaji wa huduma ya afya kwa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua sasa kati ya hizi bilioni 12 ni kiasi gani cha fedha kimetengwa *specifically* kwa ajili ya Hospitali hii ya Mkoa wa Tabora ili sasa kuondoa ufinyu wa majengo na kuweza kuondoa

msongamano na vitanda viweze kupata mahala pa kuweka na wananchi wa Tabora waweze kupata huduma stahiki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili ni dhahiri kabisa inatambulika kwamba tuna uhaba wa wauguzi kwa maana ya madaktari, manesi na madawa katika hospitali zetu nyingi nchini. Na tunatambua kwamba uhaba huu umepelekewa na sababu mbalimbali ikiwepo zoezi la vyeti feki ambalo Serikali ya Awamu ya Tano iliendesha, vifo na kustaafu. Hospitali yangu ya Mji wa Tarime ina ukosefu wa daktari ni wengi lakini *specifically* daktari wa meno ambaye amefariki kuanzia mwaka jana na nimekuwa nikiongea hapa. Ningetaka kujua sasa ni lini Serikali itaweza kutuletea daktari wa meno ili wananchi wa Tarime waendeleo kupata huduma hii ya meno?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya mawali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ameuliza *specifically* kiasi gani ambacho tumekitenga katika Hospitali ya Rufaa ya Mko wa Tabora hususan katika kuboresha miundombinu ile. Hiyo *data* sinazo hapa kwa hiyo nitamwomba tu Mheshimiwa Mbunge tukishamaliza kikao hichi tuongee na watendaji wetu ili waweze kutupatia hizo taarifa na niweze kumpatia taarifa ambayo kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali la pili ameuliza kuhusiana na daktari wa meno ni kweli Serikali imekuwa inaendelea na jitihada za kuziba mapengo wa vyeti feki na zile ajira nyingine. Na katika awamu ya kwanza tuliajiri takribani watumishi 3152 kuziba pengo la watumishi feki na Serikali baadaye ikaongeza watumishi takribani 8000 na sasa hivi tuko katika hatua za mwisho kuangalia hawa ambao walistaafu, wamefariki ili nao nafasi zao ziweze kuzibwa na tuko katika hatua za mwisho kabisa kuweza kuziba haya mapengo ya wale ambao wamefariki na wamestaafu ili sasa nafasi zao ziweze kujazwa. Na nikuhakikishie kwamba Tarime

huyo daktari ambaye wamemwitaji wa meno naye atapatikana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante kwa kunipa nafasi hii. Hospitali ya Mkoa wa Tanga Bombo ni miongoni mwa hospitali kongwe hapa nchini na inahudumia zaidi ya halmashauri 11 pia inahudumia kisiwa kizima cha Pemba. Miundombinu yake imechakaa sana kiasi kwamba sasa hivi hata sio rafiki kwa wagonjwa lakini pia kwa wenzetu wenye ulemavu kwa sababu hakuna lifti katika wodi za wagonjwa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha miundombinu ya hospitali hii kongwe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali tunakiri miundombinu ya hospitali ya Bombo ni hospitali moja kongwe sana ndani ya nchi na nimepata fursa ya kuitembelea hospitali hii na kuona hizo changamoto hususani klatika jengo la wazazi ambapo wagonjwa hakuna lifti pale na imekuwa inaleta adha kidogo kwa wagonjwa kuweza kufika kule juu gorophani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali tumeliona hilo na kama nilivyosema katika jibu langu la msingi Serikali tumekabidhiwa hospitali hizi za rufaa za mikoa, makusudio yetu ni kuziboresha hospitali zetu zote hizi za rufaa kwa kuanza tunataka tujielekeze katika huduma za dharura, huduma za ICU, huduma za theatre, na majengo ya akina mama na watoto. Kwa hiyo tathmini tumeshafanya na kadri fedha zitakapopatikana tutaendelea kufanya maboresho haya na kuhakikisha kwamba hospitali hizi za rufaa za mikoa ikiwa ni pamoja na Bombo zinafanyiwa marekebisho yanayostahiki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan Lyimo.



**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Tatizo kubwa la misongamano katika hospitali zetu ni tabia ya Serikali kupandisha hadhi vituo vya afya kwenda hospitali ya wilaya, hospitali ya wilaya kuwa hospitali ya mkoa, hospitali ya mkoa kuwa hospitali ya rufaa. Kwa mfano Hospitali ya Mwananyamala ilianza kama *clinic* lakini leo ni hospitali ya rufaa kwa hiyo wale watu waliokuwa wanatibia pale wanaenda wapi? Kwa hiyo, nilitaka kujua ni lini Serikali itaacha tabia hii mbaya ya kupandisha vituo kuwa hospitali badala yake kama wanataka kujenga hospitali wajenge hospitali na vituo vya afya vibaki kama vituo vya afya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kutoa ufafanuzi Serikali haina tabia mbaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kwamba idadi ya watu inazidi kuongezeka miji inazidi kukuwa na ndio maana na huduma zinazidi kuhitajika kwa wingi zaidi. Inawezekana tulianza kama zahanati ikaja kituo cha afya, hospitali za wilaya na zitakwenda mpaka ngazi ya rufaa. Lakini sisi kama Serikali tumeliona hilo na bahati nzuri Mheshimiwa Mbunge tulikuwa naye na ni mjumbe wa kamati yetu anajua kuna maboresho makubwa sana hata lile jengo ambalo tulikuwa limesuasua la jengo la uzazi hilo Serikali imeshapata fedha na tuko katika hatua sasa hivi za kutaka kulikamilisha lile jengo kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma katika hospitali ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambasamba na hilo Serikali imeendelea kuweka mikakati moja ya changamoto ambayo inaleta misongamano katika hospitali hizi nyingi za rufaa za mikoa *especially* pale katika Jiji la Dar es Salaam ni mfumo mzima wa rufaa. Kwa hiyo, uboreshaji wa hivi vituo vya afya ambavyo tunavyovijenga ujenzi wa hospitali hizi za wilaya naami nazo zitasaidia sana kupunguza ule mzigo mkubwa ambao unaonekana katika hospitali zetu nyingi za rufaa za

mikoa. Kwa hiyo, nimtoe tu wasiwasi Mheshimiwa Mbunge hili tumeliona na tumelifanyia kazi kwa kuimarisha sasa mifumo ya afya ya msingi ili sasa hospitali za rufaa za mikoa ziweze kutoa huduma zake za msingi kama hospitali za rufaa za mikoa.

**MWENYEKITI:** Ahsante tunaendelea na swali la Mheshimiwa Zainabu Nuhu Mwamwindi Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 179

### **Tatizo la Udumavu Na Utapiamlo Kwa Watoto Nchini**

**MHE. ZAINABU N. MWAMWINDI** aliuliza:-

Udumavu na Utapiamlo mkali ni tatizo kwa watoto wengi nchini:-

Je, Serikali ina mpango gani unaotekelezeka wa kukabiliana na hali hiyo ikiwemo kuzijengea uwezo Kamati za lishe za kata?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zainabu Nuhu Mwamwindi Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeazimia kutekeleza malengo la Baraza la Afya Duniani (*World Health Assembly*) la kutokomeza utapiamlo ifikapo mwak 2025, pamoja na kutekeleza maazimio mbalimbali ya kupunguza utapiamlo ya kitaifa kikanda na Afrika Mashariki. Kitaifa, Serikali kupitia sera ya Taifa ya afya mwaka 2007 ambayo kwa sasa inapitiwa

imeeleza wazi kuwa itaboresha huduma za lishe kwa wananchi wake. Kwa miaka ya karibuni Serikali imeongeza juhudu katika kupambana na tatizo la utapiamlo nchini kwa kushirikiana na wadau wetu wa maendeleo wa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi mbalimbali zilizofanyika ni pamoja kuandaa na kutekeleza mpango mkakati jumuishi wa kitaifa wa Utekelezaji wa Afya za Lishe (*National Multi-sectoral Nutrition Action Plan* ya mwaka 2016/2017 ambayo itaisha mwaka 2021/2022 ambayo una vipaumbele vinavyolenga kupunguza utapiamlo kufikiapo mwaka 2021 ambavyo ni pamoja na:-

(i) Kupunguza viwango vya hudumavu kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka 5 kutoka asilimia 34 mawaka 2015 hadi 28.

(ii) Kudhibiti viwango vya ukondefu kwa watoto wenye umri chini ya miaka 5 na kufanya viendelee kubakia chini ya asilimia 5 iliyopo sasa.

(iii) Kupunguza viwango vya watoto wanaozaliwa na uzito pungufu kutoka asilimia 7 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 5.

(iv) Kupunguza idadi ya wanawake walio katika umri wa uzazi miaka 15 - 49 wenye upungufu wa damu kutoka asilimia 44.7 kwa mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 33.

(v) Kupunguza tatizo la upungufu wa vitamin A kwa watoto wenye umri wa miezi 6 hadi miezi 59 kutoka asilimia 33 hadi kufikia asilimia 26.

(vi) Kudhibiti tatizo la uzito uliozidi kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano na kubakia chini ya asilimia 5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilianzisha muundo wa kada ya Maafisa Lishe chini ya Wizara ya afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto mwaka 2012 ambapo

jumla ya Maafisa Lishe 114 wameajiriwa katika mikoa na halmashauri za Serikali. Sanjari na hilo, Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais - TAMISEMI ipo katika mchakato wa kuangalia utaratibu wa kuajiri wahudumu wa afya, ngazi za jamii angalau wawili wawili kila kijiji ambapo pamoja na shughuli nyingine watatoa huduma za lishe katika ngazi ya kaya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwamwindi swali la nyongeza.

**MHE. ZAINABU N. MWAMWINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na jitihada kubwa za Serikali ambazo zinafanyika lakini bado tatizo la utapiamlo katika mikoa ambayo inazalisha chakula kwa wingi bado linaendelea kukua. Sasa je, Serikali ina mpango gani mkakati wa kuajiri watoa huduma za lishe katika vijiji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ukiangalia mikoa ambayo inazalisha chakula kwa wingi nchini ndio mikoa ambayo nayo inaoongoza sana kwa utapiamlo. Na siku zote nimeendelea kusema bado tuna changamoto watanania kula bora chakula kuliko kula chakula kilicho bora. Na hii tunaiona katika mtiririko mzima kwa maana ya udumavu vilevile tuna tatizo la Tanzania kuwa na lishe iliyopitiliza zaidi ya asilimia 10 ya watanania wana lishe ambayo imepitiliza kwa maana ya wanaviriba tumbo, kina mama wana vitambi na kina baba wote wana vitambi, vyote hivyo nayo inaonyesha kwamba ni lishe ambayo siyo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sisi kama Serikali tumeliona hilo na ndio maana tulifanya uzinduzi wa mpango mkakati wa masuala haya ya lishe na mpango mkakati huo ulizinduliwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu mwaka juzi hapa Dodoma na lengo ni kuweka msisitizo katika masuala haya ya lishe na katika sekta zote. Na mpango mkakati huu

unaratibiwa pale chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na sisi kama Wizara tuna nafasi yetu kubwa katika maeneo haya kuhakikisha kwamba tunapunguza udumavu kwa watoto wadogo lakini tunaanza kupambana na lishe iliyopitiliza kwa sababu nayo ina mahusiano ya karibu sana na magonjwa yasiyo ambukizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niendeleo tu kumsisitiza kwamba kuhusiana na suala ambalo Mheshimiwa Mbunge ameliuliza kwamba tunaendelea kutoa elimu kwa njia mbalimbali katika mikoa ile kuhakikisha kwamba watu katika mikoa ile wanapata elimu sahihi kuhusiana na masuala ya lishe. Sambamba na hilo tutaendelea kuajiri watumishi, maafisa lishe kadri uwezo wa Serikali utakapokuwa unaruhusu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selasini, Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, miaka minne ya makuzi ya mtoto ni ya muhimu sana kwa maisha yake yote tuko tulivyo kwa sababu ya malezi ya miaka minne ya mwanzo. Sasa zamani katika MSH pamoja na kuwapima uzito watoto pamoja na chanjo nakadhalika manesi na wataalam wa afya walikuwa wanafundisha akinamama namna ya kuwalea hawa watoto na MSH nyingine zilikuwa na vichezeo nakadhalika, sasa siku hizi hilo halipo.

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba malezi ya hawa watoto katika hii miaka minne yanazingatiwa ili tuweze kuwa na kizazi ambacho ni bora siku zijazo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba katika misingi ya afya siku muhimu katika uhai wa mtoto ni siku 1000 na siku hizi 1000 tunaanza kuzihesabu tangia

mimba inatungwa mpaka pale mtoto atakapokuwa anatizimiza miaka miwili. Katika kipindi hichi ndio tunapojenga msingi wa afya na ukuaji wa mtoto katika maisha yake yote, ukikosea pale unaanza na msingi mbovu kwa maana ya afya na ustawi wa yule mtoto. Ndio maana tunasisitiza kwamba utunzaji sahihi wa ujauzito, lakini unyonyeshaji wa mtoto kwa miezi sita na baada ya pale na mtoto anyonyeshwe mpaka miaka miwili akipewa na vyakula vingine ambavyo vinaweza vikamjenga mtoto sahihi katika afya sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili sisi kama Serikali tunaendelea kulisitiza na ndio maana katika moja ya maagizo ambayo tumeyafanya tumepiga marufuku matumizi ya vyombo vyetu vya habari kwa maana ya television kwenye vituo vyetu vya kutolea huduma za afya kuonyesha mpira, tamthilia na muziki badala yake tuwe tunatoa jumbe ambazo zinaweza zikawasaidia akina mama wanapokuja pale *clinic* kwa ajili ya chanjo ama huduma nyingine za afya basi waweze kupata elimu iliyokuwa sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumeanza kuwekeza katika watoa huduma katika jamii ili kuweza kutoa elimu sahihi kule kwenye jamii jinsi gani ya utunzaji wa ujauzito lakini kuhakikisha kwamba wazazi wanapewa elimu sahihi kuhusiana na maandalizi ya chakula sahihi ili watoto waweze kupata afya bora na katika ustawi bora ambao unatakiwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chacha.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka tu kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwenye Jimbo langu la Serengeti Kata ya Busawe, Kijiji cha Busawe, wananchi wamejenga kituo cha afya wameweka mpaka na vifaa vinavyostahili kwa ajili ya kituo cha afya, lakini ni muda mrefu sasa tangu waombe usajili wa kituo chao cha afya. Maombi yamekaa Wizarani muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizarani inawaambia nini wananchi wa Kata ya Busawe na Kijiji cha Busawe? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nawapongeza sana Mheshimiwa Ryoba, Mbunge wa Serengeti na wananchi kwa kujenga kituo chao cha afya. Sisi kama Serikali tuna wajibu wa kuhakikisha kwamba tunaungana na nguvu za wananchi pale ambapo wao wenyewe wametoa nguvu zao na wamejenga kituo chao cha afya. Ni wajibu wetu kama wataalam kwenda kukagua na kuhakikisha kwamba kinakidhi vile vigezo na kuweza kutoa huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu suala hili ndiyo nalisikia hapa kwa mara ya kwanza; na Mheshimiwa Ryoba ni rafiki yangu, siku zote tunakaa tunaongea, namwomba baada ya kipindi cha maswali na majibu awasiliane nami tujue tatizo ni nini na nimhakikishie ndani ya muda mfupi kituo chake kitapata usajili.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Mariam Nasoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 180

### **Kuwasaidia Watoto wanaoishi Gerezani na Mama Zao**

**MHE. MARIAM NASORO KISANGI** aliuliza:-

Wapo watoto wanaoishi Gerezani na huenda shule na kurudi Gerezani kulala na mama zao. Hali hiyo siyo nzuri kwa malezi ya mtoto hasa mambo wanayoyaona na kusikia wakiwa Gerezani:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia watoto hao waondokane na hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Mariam Nasoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Dar es Salaam kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto kuwepo magerezani inatokana na mama zao kuhukumiwa kutumikia adhabu ya kifungo wakiwa katika hali ya ujauzito au kuwa na mtoto aliye chini ya umri wa miaka miwili ambaye anapaswa kupata haki ya kunyonya maziwa ya mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kutoa maelezo ya ufafanuzi kama ifuatavyo: hakuna watoto wanaokwenda shule wakiwa magerezani isipokuwa kuna watoto walio chini ya miaka miwili wanaolazimika kubaki gerezani na mama zao ili kupata haki yao ya kunyonya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile yapo mazingira yakiwemo kukosekana kwa malezi mbadala kwa watoto zaidi ya miaka miwili na wasiozidi miaka mitano kubaki na mama zao gerezani, hivyo kulazimika kuhudhuria katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana (*Day Care Centres*) kwa madhumuni ya kupata huduma ya malezi changamshi ya awali ili kuchochea ukuaji na maendeleo ya kiakili, kimwili, kihisia, kijamii na kimaadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2015 kulikuwa na watoto 150, mwaka 2016 tulikuwa na watoto 85 na mwaka 2017 kulikuwa na watoto 108. Watoto hawa ni kwa mgawanyiko wa akina mama walioko mahabusu na wafungwa katika magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Sheria ya Mtoto Na. 21 ya Mwaka 2009 Kifungu cha 114, Kanuni za Ulinzi na Usalama wa Mtoto Mwaka 2015 na Sera na Uratibu wa Ulinzi na Mtoto katika Magereza ya Mwaka 2018, imeweka utaratibu wa kuhakikisha kuwa mtoto anapata malezi yanayohitajika ikiwemo mlo kamili, virutubisho, huduma za afya pamoja na chanjo kwa watoto wa chini ya miaka miwili.



Utaratibu wa watoto chini ya miaka mitano kuhudhuria kwenye vituo vya kulelea watoto wadogo mchana, unalenga kupunguza muda watoto kukaa gerezani na kutumia muda wa zaidi ya masaa sita katika vituo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chini ya Sheria ya Mtoto Na. 21 ya Mwaka 2009, Serikali imeanzisha program ya malezi mbadala kama vile walezi wa kuaminika, malezi ya kambo na kuasili. Lengo ni kuhakikisha watoto wote wanaolelewa katika taasisi wanapata malezi ya kifamilia. Pia watoto walio na mama zao gerezani ambao wamekosa malezi mbadala, wanapata fursa ya kupokelewa katika makao ya watoto kwa muda wakati jitihada nyingine zikiendea. Program hizo zinahakikisha watoto wa zaidi miaka mitano wanaondolewa gerezani na kuunganishwa na watoa huduma wa malezi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo nimeridhika nayo na napenda nitoe pongezi kwa Mkuu wa Gereza la Segerea kwa kutekeleza hayo yote ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyasema kupeleka watoto kwenye *Nursery* na kuwarudisha gerezani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa matatizo yanayowapata watoto magerezani yanatokana na makosa ya mama zao; na kwa kuwa zipo adhabu nyingi wanazoweza kupewa mahabusu au wafungwa wenye makosa yasiyo ya kijinai; kwa nini Serikali isitoe adhabu ya kifungo cha nje kwa akina mama wenye watoto wadogo ili waweze kuwalea watoto wao vizuri uraiani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa tatizo kubwa la akina mama waliopo katika gereza la Segerea na magereza mengine yote ni kutokana na kesi zao kutokupelekwa mahakamani kwa wakati, jambo ambalo linawafanya akina mama wale wakae muda mrefu

mahabusu bila ya kutambua hatima yao: Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa wanapeleka kesi mahakamani kwa wakati? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Masauni, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, naomba kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mariam Kisangi kwa kujali akina mama na watoto hawa. Nachukua fursa hii kumhakikishia Mheshimiwa Mariam Kisangi kwamba huu uchungu ambao aliokuwa nao yeye ni sawa sawa na uchungu ambao Serikali tunao. Ndiyo maana katika kushughulika na kesi hizi za hao akina mama wenye watoto, huwa Serikali inatoa kipaumbele maalum, hata mahakama hufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo basi, nimhakikishie kwamba hata inapokuja katika ule utaratibu ambao tunautumia kwa ajili ya kutoa kifungo cha nje na mipango mingine mbalimbali ya kupunguza mahabusu na kusamehe wafungwa, akina mama wenye watoto huwa wanapewa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili; vilevile katika suala la kuhakikisha kwamba tunaharakisha upelelezi na kesi hizi zinamalizika, tuna utaratibu wa kuharakisha kesi ziweze kwenda kwa haraka. Tunaweza kutumia njia mbalimbali kufanya hivyo, tunafanya ziara kwenye magereza kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria, lakini tunapobaini kwamba kuna kesi ambazo hazihitaji kukaa muda mrefu bila kuchunguzwa, hasa hizi zinazohusu akina mama na watoto tunakuwa tunazipa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimalizie kwa kumhakikishia Mheshimiwa Mariam Kisangi kwamba Serikali inaliangalia sana kwa karibu suala hili na haipendelei kuona watoto wadogo wakikaa magerezani kwa muda mrefu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Saleh.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kwa bahati ni siku ya watoto, yamekuja maswali mawili mfululizo na yakilenga juu ya suala la kudumaa, suala la makovu ya kuona mambo mabaya na ukuaji kiakili; lakini haya yote kama alivyosema Mheshimiwa Selasini yanaweza kwenda katika kitu kinaitwa *All Childhood Development*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina fursa ya kukopa kwa mkopo nafuu kutoka *World Bank* dola milioni 200 kwa miaka mitatu sasa; na Serikali haijafanya hivyo ili iweze kutekeleza hiyo program ya *All Childhood Development*. Je, Serikali ni lini itawasiliana, ita-finalize na *World Bank* ili mkopo huo uweze kupatikana na uweze kutumika kwa ajili ya *All Childhood Development* tupate watu wenye akili zaidi katika Taifa? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali tunafanya kazi kwa karibu sana na *World Bank* na katika programu mbalimbali za maendeleo ya awali ya watoto, moja ya maeneo ambayo tumejikita katika hizi huduma za afya, ama huduma za msingi katika hizi siku 1,000 za mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kuwa hili analoniambia Mheshimiwa Mbunge kwangu linaonekana kwamba ni jipya, basi namwomba anipe maelezo zaidi katika suala hili ili tuweze kufuatalia, lakini *World Bank* tunafanya kazi nao kwa karibu sana na tunashirikiana sana katika masuala ya ustawi na maendeleo ya watoto.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zaynabu Vulu.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na ukizingatia leo ni siku ya kwanza kwa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Nawatakia

kheri wale wote ambao wamejaaliwa kufunga na wasiojaaliwa Mungu awape *tahfifu* waweze kufunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua, Serikali ina mpango gani au ina mkakati gani kwa wale watoto ambao wamehukumiwa na kupelekwa magerezani ikiwa ni gereza la pale Upanga au kwa jina lingine Kisutu? Nini wanapewa katika masuala ya kujiendeleza kielimu ya kawaida au elimu ya ufundi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nipate majibu katika maswali haya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, swali hilo moja la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria, watoto chini ya miaka 18 hawapaswi kufungwa magereza ya watu wazima. Kwa hiyo, kuna utaratibu wa Serikali kuwa na mahabusu za watoto, lakini vilevile kuna maeneo ambayo tunaita Gereza la Watoto, ambapo wale watoto wanatuhumiwa kwa mujibu wa sheria wamehukumiwa kifungo gerezani, basi wanapelekwa kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo ni kuwarekebisha kitabia, siyo kuwaadhibu wale watoto, la hasha, Serikali ina lengo la kuhakikisha kwamba tunawarekebisha kitabia. Kwa hiyo, kule wanapata huduma zote za matunzo, lakini wanapata huduma za elimu na huduma za kuweza kuwasaidia kuwarekebisha kitabia ili hata baadaye wakitoka basi wawe ni sehemu ya raia wema katika jamii hii.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara, swali la Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, Mbunge wa Viti Maalum, litaulizwa na Mheshimiwa Anna Lupembe.

Na. 181

**Kulinda Biashara za Wazalishaji wa Ndani**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE (K.n.y. MHE. CATHERINE V. MAGIGE)** aliuiza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kulinda biashara za wazalishaji wa ndani ili kuwajengea uwezo kuelekea uchumi wa viwanda?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha biashara za wazalishaji wa ndani zinalindwa, Serikali imeendelea kutoa msamaha wa kodi kwa baadhi ya bidhaa zinazozalishwa ndani na kutoza kodi zaidi kwenye bidhaa zinazolingia nchini katika kiwango cha asilimia 10 kwa bidhaa ghafi na asilimia 25 kwa bidhaa zilizo tayari kutumiwa na mlaji. Aidha, viwango hivi vinaweza kutozwa zaidi ya asilimia 25 kulingana na umuhimu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali iliongeza kodi kati ya asilimia 25 hadi 35 kwenye mafuta ya kula yanayoingizwa nchini. Aidha, ili kulinda wazalishaji wanaotumia malighafi za ndani Serikali imeongeza kodi kwa bidhaa zinazotoka nje kwa mfano, mvinyo wa zabibu ulioingizwa toka nje ya nchi kutoka shilingi 2,349/= hadi shilingi 2,466/= kwa lita wakati unaozalishwa ndani ukitozwa shilingi 200/= tu kwa lita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali imeweka udhibiti na usimamizi maalum kwa kutoa vibali na leseni kwa baadhi ya bidhaa zinazolingizwa nchini kama vile sukari,

maziwa ya mtindi, mitumba na magunia au viroba vya kufungashia bidhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuimarisha vituo vya pamoja mipakani katika maeneo ya kuingiza bidhaa nchini. Aidha, udhibiti na ukaguzi umeimarishwa katika viwanja vya ndege na bandari ili kudhibiti bidhaa za magendo, hafifu, bandia kuingizwa nchini. Vilevile kupitia taasisi zake za mamlaka ya udhibiti, Serikali imeendelea kusimamia ubora wa bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya ndani pamoja na zinazotoka nje ya nchi kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara. Lengo ni kuhakikisha kwamba, bidhaa zinazolingia sokoni zinakidhi matakwa ya viwango husika ili kulinda afya, usalama, mazingira na kulinda biashara na viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mikakati ya kiseru, kisheria na kiutendaji niliyoeleza, Serikali imeendelea kuwawekea mazingira wezeshi wafanyabiashara wa ndani ili waweze kuzalisha bidhaa zenye ushindani katika soko, kuandaa na kutekeleza mpango wa kuboresha mfumo wa kudhibiti biashara nchini (*blue print*), kuanzisha vituo vya ushauri wa biashara ili kutatua changamoto zinazowakabili (*Business Clinics*) na Vituo vya Ushauri wa Kikodi, (*Tax Clinic*) ambavyo vinatoa elimu kuhusu namna bora ya kuanzisha kufanya biashara na aina ya kodi zinazohusiana na kila aina ya biashara nchini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anna Lupembe.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na jitihada za Serikali kama ilivyoeleza kwenye swali langu la msingi, lakini wafanyabiashara WENGI wanashindwa kufanikisha kutokana na utitiri wa kodi na vikwazo mbalimbali na kuwa siyo rafiki na *TRA* kutokana na ukusanyaji wa kodi. Je, ni lini sasa Serikali itaweka mikakati kuondoa vikwazo hivi? Maana wanapata vikwazo vingi sana, watu wa *TRA* wanawasumbua sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, kwa kuwa masoko hasa ya nje bado ni kikwazo kwa wajasiriamali na wazalishaji wa ndani, ni mkakati gani endelevu wa Serikali kutafuta na kuwaunganisha wazalishaji ambao ni wajasiriamali wetu na masoko ya nje? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza hapo awali ni kwamba Serikali baada ya kutambua changamoto zinazowakabili wafanyabiashara, ndiyo maana tulikuja na suala linaloitwa *blue print*. Katika mpango huu ambao sasa tuko katika hatua za mwisho za kuandaa mpango wa utekelezaji, ni kwamba taasisi zote za udhitibi ikiwemo *TRA*, tutaangalia vile vikwazo ambavyo tayari vimeshaainishwa, aidha viweze kuunganishwa na kutozwa na mamlaka moja badala ya kutozwa na mamlaka nyingi nyingi pamoja na kuondoa vikwazo vingine vinavyohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *TRA*, hivi juzi tu nimemsikia Mheshimiwa Waziri wa Fedha akitangaza kwamba iwe ni marufuku kwa mtu wa *TRA* kufungia biashara kwa kuweka makufuli, badala yake wazungumze na wafanyabiashara na kuona namna bora ya kulipa kodi zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, katika kutafuta masoko ya nje, napenda tu kuwaambia kwamba kimsingi kupitia taasisi yetu ya *TANTRADE*, tumekuwa tukifanya maonyesho na kuwashirikisha wafanyabiashara kuwaonesha masoko mbalimbali yaliyopo. Pia na sisi wenyewe tunasaidia kutafuta hayo masoko na kuhakikisha kwamba bidhaa zinazozalishwa zinakuwa na kiwango na zinafungashwa vizuri ili kuweza kutumika kwa ajili ya soko la nje.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Maftaha

Abdallah Nachuma, Mbunge wa Mtwara Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 182

**Kuvunja kwa Bodi za Wahandisi (*Engineers Registration Board*)**

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itavunja Bodi za Wahandisi kutokana na kauli ya Mheshimiwa Rais?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma, Mbunge wa Mtwara Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Usajili wa Wahandisi ilianzishwa chini ya Sheria ya Usajili wa Wahandisi Na. 15 ya mwaka 1997. Bodi hii inalo jukumu la kusajili wahandisi na makampuni ya kihandisi pamoja na kusimamia shughuli za uhandisi na mwenendo wa wahandisi na makampuni ya ushauri wa kihandisi hapa nchini. Kwa kuzingatia majukumu iliyopewa, Bodi ya Usajili wa Wahandisi tangu kuanzishwa kwake imekuwa ikitekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa na kwa mujibu wa sheria iliyoanzisha bodi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, moja ya Bodi zinazofanya kazi vizuri na kwa weledi wa kutosha ni Bodi ya Usajili wa Wahandisi na baadhi ya mafanikio yaliyopatikana kutokana na kuanzishwa kwa Bodi hiyo ni kusajili jumla ya wahandisi 25,263 katika madaraja tofauti hadi kufikia Machi, 2019. Sambamba na hilo, makampuni ya ushauri ya kihandisi yapatayo 338 yameweza kusajiliwa katika kipindi hicho zikiwemo maabara za upimaji vifaa vya ujenzi 32.



Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano haina kumbukumbu zozote zinazoonyesha kuwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliwahi kutoa kauli ya kuivunja Bodi ya Usajili wa Wahandisi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maftaha.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; ili haya makampuni ya kihandisi yapate usajili, inasemekana na wahandisi wenyewe kwamba kumewekwa tozo kubwa sana na hii Bodi. Je, Serikali iko tayari hivi sasa kupunguza tozo hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ili uweze kujenga nyumba, angalau ghorofa moja Tanzania ni lazima upate vibali vya makampuni ya kihandisi na vibali hivyo ni lazima uwe na kibali cha *architect, structure, quantity QS, Contractor* na pia ulipe malipo ya halmashauri na TRA. Sasa, je Serikali haioni kwa sababu ili upate vibali hivi, fedha ya tozo ya vibali vya wahandisi inaizidi fedha uliyokuwa nayo ya ujenzi. Je, haioni kwamba Serikali kwa kuruhusu suala hili wananchi wengi wanashindwa kujenga nyumba bora nzuri?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo mawili, kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nachuma almaarufu kama Mashine ya Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze tu Mheshimiwa Nachuma kwa kuwa mfuatiliaji mzuri, lakini kwa sababu huyu Mheshimiwa ni Mwalimu niombe tu hata baada ya majibu yangu, baadaye pia nikusheheni *documents* za kutosha ili kwanza aone kazi nzuri ambayo bodi inafanya,

lakini pia aweze kuona umuhimu wa kutumia taaluma hii. Taalum hii ni muhimu sana kwa sababu katika ujenzi lazima weledi uzingatiwe ili kuhakikisha kwamba hizi rasilimali zinazojengwa, majengo na huduma zingine kwa sababu bodi hii inasimamia wahandisi wa aina tofauti; wako wahandisi wa umeme, majengo, wako ma-*technician* na makundi mbalimbali. Kwa hiyo aone kazi hii kubwa inafanyika na kazi inafanyika vizuri. Pia Bodi hii inafanya kazi ya kusimamia zoezi zima la uadilifu katika sekta hii, lakini vile vile inasimamia kuhakikisha kwamba hata usalama unakuwa wa hali ya juu katika ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kujibu swali lake, anaona kwamba tozo ni kubwa. Ziko bodi m balimbali, kwa ulinganifu naona kwamba tozo ambayo inatozwa na bodi hii ukiwianisha na bodi zingine tofauti, sio ukubwa. Labda Mheshimiwa Mbunge tutaweza kuzungumza tuone ushauri wake unalenga nini ili tuone kama kutakuwa na jambo la kufanya kazi tutafanyia kazi, lakini kimsingi ukilinganisha tozo inayotozwa na huduma inayotolewa na gharama za rasilimali ambazo zinafanyika, kwangu naona kwamba bado ilikuwa ni *reasonable* na kwa muda mrefu hatujapata malalamiko mbalimbali kutoka kwa wateja ambao wanahudumiwa na bodi hii, lakini nalichukua pia kwa ajili ya kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vibali mbalimbali, kila tozo zinazotozwa kwenye vibali hivi, vingi amevitaja Mheshimiwa Mbunge inakuwa na sababu zake, lakini nijikite tu kwenye eneo hili kama nilivyosema, tutajaribu kuangalia lakini kwa sababu ziko taasisi mbalimbali zinatoza, tunaweza tukaangalia tuone kama kutakuwa na tozo ambayo itakuwa inaleta *meaning* moja basi hizo tutazifanyia kazi tukishirikiana na wenzetu ili tuhakikishe kwamba kusiwepo na tozo ambayo inafanana na madhumuni ya tozo nyingine ili tuwe na tozo ambazo kimsingi zitakuwa zinalenga kutoa huduma ambayo tumelenga tukusanye ili tuweze kufanya kazi nzuri kuhakikisha kwamba taaluma hii inawatendea haki Watanzania na kuimarisha uchumi na *asset* ambazo zinajengwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa, Mbunge wa Kalenga sasa aulize swali lake.

Na. 183

### **Vivutio vya Utalii – Jimbo la Kalenga**

**MHE. GODFREY W. MGIMWA** aliuliza:-

Jimbo la Kalenga lina vivutio vya utalii vinavyoweza kuingiza nchi yetu pesa za kigeni kama vile Isimila *Stone Age* na Makumbusho na Mtwā Mkwawa Mkwavinyika:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kushirikiana na Halmashauri ya Iringa Vijijini kuimarisha na kujenga mazingira na kuvitumia vivutio hivyo ili kuongeza Pato la Taifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu ya swali hilo.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa, Mbunge wa Jimbo la Kalenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Isimila *Stone Age* na Makumbusho ya Mtwā Mkwawa yanasimamiwa na Shirika la Hifadhi za Taifa (*TANAPA*) ambapo Shirika lina jukumu la kuhifadhi na kuendeleza vituo hivi. Aidha, kwa kuzingatia changamoto zilizopo katika vituo tajwa, Wizara kupitia Mradi wa Kusimamia Maliasili na Kuendeleza Utalii, Nyanda za Juu Kusini yaani (*Resilient Natural Resources for Tourism and Growth - REGROW*) na kwa kushirikiana na Halmashauri za Mkoa wa Iringa, itaimarisha miundombinu hiyo. Kwa kupitia mradi wa *REGROW* maeneo haya yataboreshwa ikiwa ni pamoja na kujenga ituo cha Kumbukumbu na Taarifa ili uhifadhi Kumbukumbu ya Mtwā Mkwawa na utamaduni wa Wahehe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sanjari na hatua hiyo, Wizara kwa kushirikiana na Mkoa wa Iringa pamoja na Chuo Kikuu cha Iringa imekarabati boma la Mjerumani na kulifanya kuwa Makumbusho ya Mkoa. Aidha, Wizara ilitoa wataalam wa ujenzi kuandaa na kupanga vioneshwa ndani ya makumbusho ya jengo hilo, duka la zawadi, mgahawa na studio ya kurekodi nyimbo za asili. Mapato yatokanayo na jengo hilo yanaingia katika Mkoa wa Iringa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mgimwa, swali la nyongeza.

**MHE. GODFREY W. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri, ingawa katika maeneo aliyozungumza kuhudu *REGROW* hajaeleza kiuwazi kwamba itakuwa ni lini makumbusho yatakuwa yameanza. Nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza ni kwamba, wananchi wa Jimbo la Kalenga hasa katika Kata husika ya Kalenga hawanufaiki na chochote kupitia Makumbusho haya ya Mkwawa Mkwavinyika, zaidi wanapata zile fedha ndogo ndogo kupitia watalii ambao wanakuja kununua bagia, maandazi na mbogamboga. Sasa sijui Serikali ina utaratibu gani kuhakikisha kwamba wananchi wa Kalenga hasa katika Kata husika ya Kalenga wananufaika na Makumbusho haya ya Mkwawa Mkwavinyika? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni kwamba, kutokana na utaratibu ambao umeanzishwa na Serikali kuhakikisha kwamba tunajenga au kuboresha barabara ya Iringa Mjini kuelekea Ruaha ambayo iko katika utaratibu wa *REGROW* ningependa kufahamu kupitia Mheshimiwa Waziri kwa sababu Ruaha *National Park* ni mbuga kubwa katika Bara la Afrika na Tanzania kwa ujumla. Ningependa sasa kufahamu, je, utaratibu wa ujenzi wa barabara hii ambayo inaenda Ruaha *National Park* ukoje ukizingatia kwamba Wizara ya Ujenzi imeshaeleza kwamba itaijenga barabara hii, lakini vile vile kwa sababu inakidhi mahitaji ya Wizara ya

Maliasili, je, kuna mawasiliano yoyote kati ya Wizara hizi mbili kujua barabara hii itaanza kujengwa lini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa ufupi ya maswali hayo ya nyongeza.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajibu maswali mawili ya Mheshimiwa Godfrey William Mchimwa kwanza niwape salamu Wanayanga wote, kamwene, mnogage. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya salamu hizo kwa Wanayanga, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Mchimwa kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza ni kwamba, Mtwaka Mkwavinyika Mnyigumba Mwamuyenga ni shujaa wa Taifa, ni alama ya Utanzania wetu na ni miongoni mwa watu mashuhuri ambao sisi watoto wa Tanzania tunajinasibu nao. Pia hawezi kuwa mtu ambaye anaweza kutupa historia inayoleta faida kwa watu wa Kalenga peke yake, kwa hivyo mafanikio yatakayopatikana kutokana na Mtwaka Mkwavinyika Mnyigumba kuwa ni Mtwaka wa Wahehe na ngome yake kuwa pale Kalenga ni kuvutia watalii kuja katika eneo lile na hiyo *multiplier effect* anayoizungumza kwamba watalii watalala, watatembelea maeneo mbalimbali, watajifunza historia ya Wahehe, wataacha pesa pale, lakini sio lazima moja kwa moja kwa kuwa Mtwaka Mkwavinyika alikuwa wa eneo lile, basi iwe tu ni kwa faida ya watu wa pale, huyu ameshakuwa alama ya Taifa. Kwa hivyo, kinachopatikana kutokana na utalii kinaingia kwenye taasisi za Serikali na wananchi wanafaidika na kodi inayotokana na Sekta ya Utalii kwa ujumla wake na pia wananchi wanafaidika kwa kufanya shughuli mbalimbali ambazo zinaendana na mnyororo mzima wa kazi au shughuli za utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuhusu barabara ya kutoka Iringa kwenda Msembe, ni barabara muhimu sana kiutalii na ni barabara ambayo tunaipa kipaumbele cha hali

ya juu katika kuifungua *circuit* ya Kusini hususan kuitumia Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kwa faida zaidi kiutalii. Pia ni barabara ambayo Serikali katika bajeti hii tutakapokuwa tukitoka hapa tuna uhakika itakuwa imepitishwa na katika mikakati yetu ni kwamba tutaanza sisi wenyewe kujenga barabara hii japokuwa tayari tuna fedha kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya barabara hii kuunganisha pia na Mradi wa Kuboresha Uwanja wa Ndege wa Nduli. Kwenye uwanja wa ndege wa Nduli uliopo pale Iringa tayari Mkandarasi atatanzwa muda si mrefu, tunabaki na hii barabara ya kuunganisha Iringa Mjini na Hifadhi ya Taifa Ruaha kwenye eneo la Msembe. Kwa hivyo, hii barabara najua vizuri japokuwa mimi sio Waziri wa uchukuzi wala wa Ujenzi kwa sababu ni barabara muhimu sana kiutalii kama anavyosema Mheshimiwa Godfrey Mgimwa. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Margaret Sitta.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza. Wananchi wa Urambo wanaoishi karibu na hifadhi za misitu wamekuwa na migogoro ya muda mrefu sana na hata kusababisha kuchomewa nyumba zao na mali zao hasa katika sehemu ya Kata ya Nsenga, Lunyeta, Ukondamoyo na Uyumbu. Je, Serikali inawaambia nini wananchi kuhusu lini watakwenda kutatua na hasa kwa vile ninavyokuwa na imani na Waziri husika. Lini anamaliza matatizo haya ili wananchi wafanye shughuli zao kwa raha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa ufupi ya swali hilo.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margareth Simwanza Sitta, Mbunge wa Jimbo la Urambo, mama yangu, kwa ufupi tu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia maelekezo ya Mheshimiwa Rais aliyoyatoa Januari 15, 2019 kwa Mawaziri wa Wizara nane ambazo ni wadau wa migogoro ya ardhi,

tumefanyia kazi jambo hilo kuhusiana na Lunyeta na maeneo mengine ya Mkoa wa Tabora na mikoa mingine hapa nchini na kwa sasa siwezi kusema nini itakuwa hatma yake, lakini kazi ya Mawaziri imekamilika na tumepeleka mbele ya meza ya Mheshimiwa Rais, tunasubiri mwongozo. Baada ya hapo Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa ujumla watapata kujua ni nini itakuwa hatma ya ufumbuzi wa migogoro ambayo imedumu kwa muda mrefu kwenye Sekta ya Ardhi na Maliasili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwamoto, swali fupi la nyongeza.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba nimuulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, katika historia ya Wahehe, moja ya sifa ni kumpiga Mjerumani na Mjerumani alipigwa katika Kijiji cha Lugalo Iringa na ikasababisha kiongozi wao Zelewisky kupigwa na kaburi lake liko pale. Je, Serikali sasa haioni kwamba kile kilikuwa ni kivutio kizuri tosha mpaka sasa hivi kimetelekezwa kwa miaka yote na Waziri yuko tayari kufika pale? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo, kwa ufupi.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Venance Mwamoto, *kamwene* bwana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, niko tayari kufika katika eneo hili na wakati wowote muda ukipatikana tunaweza tukachomoka na Mheshimiwa Mwamoto tukaenda kuona eneo hili, lakini kwa ujumla wake tu maeneo yote ya malikale na maeneo ya makumbusho kwa kweli tumeyafanyia mkakati mzuri sana wa kuyaboresha kwa sababu Idara ya Malikale ambayo iko chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii ilikuwa ina uwezo mdogo sana wa kuyasimamia maeneo haya kifedha, kwa hivyo ilikuwa inayaendeleza kidogo kidogo. Kwa kuzingatia umuhimu wa maeneo haya, kihistoria

lakini pia kama urithi kwa nchi yetu ambao unapaswa kudumu kwa vizazi na vizazi, tumeamua kuyakabidhi baadhi ya maeneo nyeti ikiwemo eneo la Kalenga na eneo la Isimila kwa taasisi za uhifadhi ambazo zina msuli mkubwa kidogo kifedha kwa mfano *TANAPA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano eneo la Kalenga na eneo la Isimila na vivutio vyote vilivyoko Mkoa wa Iringa vya Malikale tumewakabidhi Shirika la Hifadhi za Taifa (*TANAPA*) ili waweze kuviendeleza na kuvisimamia.

Kwa hivyo tumegawa maeneo haya kutokana na shirika lipi ambalo lina msuli mkubwa kifedha, liko jirani na maeneo haya. Kwa hivyo, maeneo mengi kwa kweli kwa sasa yataendelezwa yatakuwa na hadhi ya kisasa na yatatoa huduma nzuri zaidi kwa watalii wa ndani na wa nje.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kingwangalla, Waziri wa Maliasili na Utalii. Tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda sasa aulize swali lake.

Na. 184

### **Mradi wa *REA* katika Jimbo la Bunda**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE** aliuliza:-

Mapema mwaka 2016 Waziri wa Nishati alifanya uzinduzi wa Mradi wa Umeme wa *REA* na kuagiza Vijiji vya Sarakwa, Tingirima, Rakana, Nyang'aranga, Nyamakumbo, Saba-Osanza, Mmagunga, Nyabuzume, Bukama, Tiring'ati, Bigegu, Nyaburundu, Masaba, Nyansirori, Nyamuswa A, Saloka-Guta, Mahanga, Manchimweru, Nyangere, Makongoro A na B na Nyamuswa kupatiwa umeme:-

(a) Je, ni lini kifanyike ili miradi ya vijiji 21 ikamilike kwa wakati kama Serikali ilivyoahidi?



(b) Je, ni nani aliyepanga kijiji A kipate kilomita tatu, transfoma mbili au nguzo 20 na umeme upitie eneo bila kushirikisha vijiji na hata bila kujali wingi wa kaya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) inaendeelea kutekeleza mradi wa kupeleka umeme katika Vijiji vya Bunda vikiwemo vijiji 21 kupitia kampuni ya *Derm Electric Company Limited*. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2019, mkandarasi alishawasha umeme katika Vijiji vya Nyangere, Bukama, Mugaja *Centre*, Marambeka, Bunere, Shule ya Msingi Mugaja pamoja na kuunganisha umeme wateja wa awali 289.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa mkandarasi anaendelea na kazi ya kusimika nguzo, kuvuta nyaya na kufunga transfoma katika Vijiji vya Sarakwa, Tingirima, Rakana, Nyang'aranga, Nyabuzume, Tiring'ati, Bigegu, Nyaburundu, Guta B, Mahanga, Manchimweru na Makongoro A na B. Kazi za mradi wa kupeleka umeme katika vijiji hivyo inahusisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometa 74.8; njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilometa 120; ufungaji wa transfoma 53 za *KVA* 50 na 100; pamoja na kuunganisha umeme kwa wateja wa awali 1,141. Gharama ya mradi ni shilingi bilioni 7.08 na kazi ya kupeleka umeme katika vijiji hivi itakamilika ifikapo mwezi Juni, 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Vijiji vya Nyamakumbo, Saba – Osanza, Mmagunga, Masaba, Nyansirori na Nyamuswa vitapatiwa umeme kupitia mradi wa

REA III, mzunguko wa pili, unaotarajiwa kuanza Mwezi Julai, 2020 na kukamilika mwezi Juni, 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya upimaji hufanywa na Serikali kupitia TANESCO, REA na viongozi wa Serikali za Vijiji husika. Kipaumbele ni kupeleka umeme katika maeneo yasiyokuwa na miundombinu ya umeme na katika taasisi zinazotoa huduma za kijamii kama vile vituo vya afya, zahanati, shule na kadhalika. Hata hivyo, ukubwa wa wigo wa mradi wa usambazaji umeme katika mkoa, wilaya na kijiji husika hutegemea zaidi upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Meshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza, lakini niipongeze Wizara ya Nishati, Waziri wake Mheshimiwa Dkt. Kalemani na Mheshimiwa Subira, Naibu Waziri na Watendaji wake wote kwa kasi ambayo wanaionesha sasa kwenye Jimbo la Bunda. Natambua kuna Vijiji vya Nyabuzume, Tiring'ati, Bigegu, Nyaburundu, Mihingo, Rakana, Manchimweru, Nyang'aranga, Sarakwa na Tingirima, wameweka nguzo za umeme. Swali langu la kwanza hapa, ni lini sasa umeme utawaka kwenye maeneo haya kwa sababu ninapouliza swali hili sasa hivi hapa kuna akinamama zaidi ya 100 wanataka kusikiliza wamechoka na mambo ya vibatari kwenye maeneo yao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kuna maeneo ya Nyamatutu, Saba-Osanza, Mmagunga, Nyamakumbo, Sanzate, Nyansirori, Saloka-Guta, Nyamuswa A. Mheshimiwa Waziri rafiki yangu Dkt. Kalemani, kutoa transfoma nane kwenye maeneo ya taasisi kama vituo vya afya, shule za msingi, sekondari *survey* ilishafanywa na Serikali imetumia hela pale tangu 2016, ni lini sasa zile Taasisi zitapata umeme, kuweka transfoma nane shida iko wapi? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo ya nyongeza. Mheshimiwa Waziri Dkt. Kalemani.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri alivyojibu majibu mazuri kwenye swali la Mheshimiwa Mbunge Getere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge Getere anavyofuatilia masuala ya umeme katika Jimbo la Bunda Vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Getere, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza amependa kujua ni lini sasa vijiji vya Bunda ambavyo vinapelekewa umeme vitapata umeme. Kwanza nianze kusema hapa tunapongea wakandarasi wako *site* na hivi sasa vijiji takriban 11 wameshavifanyia kazi. Leo na jana wakandarasi wako *site, Derm Electric*, wanafanya kazi katika Vijiji vya Mwanchimweru, Nyanharanga, Mahanga, Lakani pamoja na Tingirima ambapo vyote watawasha umeme katika wiki inayokuja. Katika Jimbo la Mheshimiwa Getere vimebaki vijiji vitano tu vya Sarakwa, Nyabuzume, Tingirigi pamoja na vijiji anavyovitaja vitatu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala lake la pili ambalo ni la msingi kabisa, maeneo ya vijiji takribani 11 yana umeme na vitongoji vyake vina umeme shida ni shule za sekondari na zahanati ambazo hazijapata umeme. Nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge wakandarasi wameshaweka *design*, tuna mpango wa kuongeza umeme katika vitongoji unaoanza mwezi ujao. Kwa hiyo, maeneo yote ya Shule za Msingi za Nyamatutu, Saba Osama, Nyamakumbu, Maguga, Salokikwa pamoja na Musa na Makongolai A&B vitapelekewa umeme pamoja na taasisi zake. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Agness Marwa, swali fupi la nyongeza.

**MHE. AGNESS M. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa kwa Mheshimiwa Getere.

Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu hata wapiga kura wa Mheshimiwa Getere wako hapa ndani leo wamesikia na wanausubiri huo umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia swali hilihilo niulize kwa Mkoa mzima wa Mara, kuna Wilaya ya Rorya ambako mimi nimezaliwa, Wilaya ya Msoma Vijijini pia nilikozaliwa lakini pia kuna shangazi zangu wa Wilaya ya Serengeti na Tarime. Swali langu sasa, ni lini Serikali itapeleka huduma za umeme wa REA katika huduma za shule, zahanati, vituo vya afya kwa maeneo mengine yote yaliyobaki ya Mkoa wa Mara? (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nijibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Agness, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Mara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Mbunge Agness anavyofuatilia masuala haya ya umeme katika taasisi za umma. Napenda kusema tu kwamba mkandarasi katika Mkoa wa Mara atapeleka umeme kwenye vijiji vyote 172 vya Mkoa wa Mara pamoja na vitongoji 318 na yuko *site*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini cha msingi kabisa, katika Wilaya ya Rorya ameshapeleka umeme kwenye vijiji 17 na shule za sekondari 18. Katika Wilaya ya Msoma Vijijini, mkandarasi anaendelea na kazi. Niseme kwamba vijiji vyote vitapelekewa umeme kuanzia sasa na kuendelea na mwezi Juni, 2020 miradi yote itakamilika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joyce Sokombi, swali fupi la nyongeza.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lililoko Bunda ni la Mkoa mzima. Tumeona ufunguzi wa *REA Phase II* na *Phase III* umefanyika lakini kilichofanywa na wakandarasi ni kwenda kumwaga nguzo tu. Naomba kujua ni lini vijiji vya Kabulabula, Bugoji, Mhoji, Komoge na Kabage vitapata umeme?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, Dkt. Kalemani majibu ya swali hilo.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nijibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Sokombi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Kijiji cha Kabulabula kimeshapelekewa umeme isipokuwa vitongoji viwili kati ya vitongoji vinne. Niseme tu mahali ambapo wamemwaga nguzo siyo kwamba wamemwaga bali wameshakamilisha *survey*. Kijiji cha Kabulabula vitongoji vitatu vilivyobaki vitaanza kupelekewa umeme kuanzia mwezi Julai, 2019. (*Makoff*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya mwisho, Wizara ya Madini, Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 185

### **Uzalishaji wa Madini ya Niobium Wilaya ya Mbeya**

**MHE. ORAN M. NJEZA** aliuliza:-

Je, ni lini uzalishaji wa madini ya Niobium utaanza katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajibu swali, niungane na Watanzania wote kuwatakia kheri Waislam wote katika Mfungo wa Ramadhani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Waziri wa Madini, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Uchimbaji wa Madini ya Niobium unaomilikiwa na Kampuni ya *Panda Hill Mines Limited*, kampuni hii ina ubia na kampuni ya *Cradle Resources Limited* asilimia 50 na *Tremont Investment* asilimia 50. Kampuni hiyo inamiliki leseni tatu za Uchimbaji wa Kati wa Madini Na.237, 237 na 239 za mwaka 2006 zilizotolewa tarehe 16 Novemba, 2006 zikiwa na jumla ya kilomita za eneo la mraba 22.1. Mradi utausisha uchimbaji wa madini ya Niobium ambayo yataongezewa thamani kwa kuchanganywa na madini ya chuma na kuwa *Ferro-Niobium*, zao ambalo litauzwa kwa wanunuzi mbalimbali walioko Ulaya, Asia na Amerika ya Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwekezaji ameshafanya upembuzi yakinifu (*feasibility study*) uliokamilika mwaka 2016 na kujiridhisha uwepo wa mashapo ya kutosha utakaowezesha uhai wa mgodi huo ambao utadumu kwa takribani miaka 30. Hata hivyo, kufuatia mabadiliko ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2017, mwekezaji alilazimika kupitia upya na kurekebisha taarifa za upembuzi yakinifu ili kuzingatia viwango vipya vya mrabaha, kodi na hisa za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, mwekezaji amewasilisha andiko la mradi la kuomba ufafanuzi wa vipengele mbalimbali kwa sheria na kutoa mapendekezo yake juu ya utekelezaji wa mradi huo, pamoja na suala la fidia ya ardhi kwa Gereza la Mbeya ambalo linatakiwa kuhamishwa ili kupisha mradi huo. Baada ya kupokea andiko hilo, hatua mbalimbali zimechukuliwa ikiwemo majadiliano na mwekezaji ambapo Wizara inatarajia kutoa

mapendekezo yatakayowezesha kuanza kwa utekelezaji wa mradi huo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oran Njeza, swali la nyongeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Kutokana na majibu hayo, inaonyesha kuwa mgodi huu utakuwa ni neema sana kwa nchi yetu kwa sababu ya uzalishaji wa hayo madini ya *Ferro-Niobium* ambayo ni muhimu sana kwa ujenzi wa madaraja, Reli ya *Standard Gauge* pamoja na mabomba ya mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa umuhimu huo, napenda kuuliza maswali madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, je, ni kwa kiasi gani hayo madini ya *Ferro-Niobium* pamoja na *Niobium* yenyewe yataongezewa madini ya chuma? Ni kwa kiasi gani haya madini ya chuma tutatumia madini yanayochimbwa hapahapa nchini kwetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, vilevile imeonyeshwa kuwa kuna fidia kwa ajili ya Gereza la Songwe. Je, mwekezaji au wawekezaji wana mkakati gani badala ya kutoa fidia tu lakini waboreshe miundombinu ya gereza hilo ikiwa ni pamoja na kuboresha miundombinu ya barabara, vituo vya afya na huduma zingine za elimu hasa kwa wananchi wa Kata ya Bonde la Songwe ambapo kiwanda hicho na mgodi huo upo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo la nyongeza, kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Oran Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba *Ferro-Niobium* ni matokeo ya uchakataji wa madini hayo utakaofanyika. Pale Mbeya uchimbaji utakuwa ni wa *Niobium* peke yake lakini *Niobium* haiwezi kutumika peke yake ni mpaka pale utakapoichanganya na *iron*, ndiyo maana tunaita *Ferro-Niobium* kwa maana ya kutengeneza *high strength low-alloy*, kwa maana ya *material* ya kuunganisha vyuma. Ndiyo maana Mheshimiwa Mbunge anasema kwamba itatumika kwenye madaraja na kwenye *pipes*, ni kweli madini haya yakishakuwa *Ferro-Niobium* yanatumika katika kuunganisha vyuma vikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge analitambua hilo na sisi kama Serikali tunalitambua hili. Kwa umuhimu wa *material* haya ndiyo maana katika jibu la msingi nimesema kwamba hii kampuni ikishaweka pale kiwanda, kwa maana ikishachimba *Niobium* itachanganywa na hiyo *Ferro* kwa maana ya *iron* kisha itauzwa nchi za nje. Kwa mfano, Amerika Kaskazini wanahitaji sana bidhaa hii kwa ajili ya utengenezaji au uunganishaji wa vyuma vikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni *material* ambayo yanahitajika sana duniani na sisi kama Serikali tunatambua. Tunasema kabisa kwamba tukishaweka kiwanda hiki pale, wakishachimba *Niobium* yetu haitatosha mahitaji kwa sababu itakuwa ni kiwanda peke yake Afrika ambacho kitakuwa kimejengwa pale Songwe na *Niobium* itakayohitajika, itahitajika hata ile ambayo ni nje ya Tanzania, ina maana Congo na Zambia wataleta *Niobium* yao hapa. Kwa hiyo, tutatumia *Niobium* karibu ya Afrika nzima katika kiwanda hiki ambacho kitajengwa Songwe. Kwa hiyo, tunatambua umuhimu wa kiwanda hiki na sisi kama Serikali tumeshikamana kihakikisha kwamba sasa tunakwenda kuhakikisha machimbo haya yanaanza na utengenezaji wa kiwanda kwa maana ya kuongeza thamani kinaanzishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili, tunatambua kweli machimbo au mgodi huu, yako chini ya Gereza la Songwe. Tunapenda kusema kwamba ile ziara ya Mheshimiwa Rais aliyokuwa amekwanda Mbeya imekuwa



ni chachu kubwa sana kuhakikisha kwamba zile mamlaka husika kwa maana ya Wizara ya Mambo ya Ndani, Uwekezaji tunakweda kukaa pamoja kuangalia ni namna gani sasa mwekezaji huyu atalipa fidia na kuweza kuhamisha gereza lile kulipeleka pembeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua yuko tayari kulipa kiasi cha dola milioni saba kujenga gereza jipya ambalo litabeba wafungwa 500 na kujenga nyumba mpya kwa ajili ya wafanyakazi zaidi ya 120 na ataweka miundombinu ya umwagiliaji pamoja na barabara kuhakikisha kwamba anaboresha maisha na mazingira ya gereza lile ambalo litajengwa pale pembeni. Kwa hiyo, mamlaka husika zinafanya kazi kuhakikisha kwamba tunamsaidia mwekezaji huyu na masuala yote ya kodi tumeshayaweka sawa, tuna hakika kabisa tutakwenda kuanza mradi huu muhimu kwa Tanzania. Ahsante sana. *(Makoff)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, Stanslaus Nyongo.

Wahesimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali umemalizika na sasa nisome matangazo ambayo yako kwa muda huu.

Tutaanza na wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, wageni ambao wapo kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika, kuna wageni 63 wa Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ambao ni viongozi wa Wizara na wadau wa maendeleo. Kwanza ni Dkt. Zainabu Chaula - Katibu Mkuu Wizara ya Afya; Ndugu John Jingu - Katibu Mkuu Maendeleo ya Jamii; Prof. Muhammad Kambi - Mganga Mkuu wa Serikali; Dkt. Doroth Gwajima - Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI; Balozi Hodan Addou - Mwakilishi Mkazi *UNWOMEN*; Ndugu Bernard Konga - Mkurugenzi wa Bima ya Afya *NHIF*; Dkt. Richard Simbaiga - Mwenyekiti Bodi ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali; Ndugu Natalia Lobue -Mtendaji Mkuu *ABBOT* Fund; Ndugu Joseph Mbasha-*Program Manager Policy Helpage*; na Ndugu

Zakayo Shigongo - Mwenyekiti *Association of Schools of Social Welfare in Tanzania (ASWOT)*. (Makofi)

Wengine ni Ndugu Yassin Ally - Mkurugenzi Mtendaji KIVULINI; Ndugu Maria Maharindo - Mjumbe wa Bodi TARWOC; Ndugu Mary Ndaro - Mratibu wa Miradi *Care International Tanzania*; Dkt. Tigest Ketsela Mengustu-Mwakilishi – WHO; Ndugu Hiltruda Temba - *Deputy Coordinator for External Affairs PEPFAR*; Dkt. Eunice Mmari -*Association Director of Programs-CDC*; Ndugu Erick Msoffe - *Senor Advisor-GIZ*; Bwana Nelson Mushi - *Global Fund's Local Fund Agent*; na Ms. Brenda Msangi - Mkurugenzi Mtendaji CCBRT. Karibuni sana wageni wetu kutoka Wizara ya Afya. (Makofi)

Pia wapo Waganga Wafawidhi 28 wa Hospitali za Rufaa za Mikoa yote nchini. Wameambatana na Viongozi na Maafisa kutoka Wizarani. Karibuni sana maafisa wetu kutoka Wizara ya Afya. (Makofi)

Wageni wengine wa Mheshimiwa Ummy Mwalimu, ni viongozi saba kutoka Mkoa wa Njombe wakiongozwa na Mheshimiwa Luth Msafiri - Mkuu wa Wilaya ya Njombe; Mheshimiwa Valentino Hongoli - Mwenyekiti wa Halmashauri ya Njombe; Ndugu Ally Juma Ally - Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe. Karibuni sana. (Makofi)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni wageni watatu wa Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Naibu Waziri wa Kilimo, kutoka Wilaya ya Karagwe wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Wilaya hiyo, Ndugu Robinson Mtafungwa. Karibu sana ndugu yetu. (Makofi)

Wageni 10 wa Mheshimiwa Kassim Jamal ambao ni Wadau wa Afya ya Uzazi wa Mpango na Afya kwa ujumla kutoka Jijini Dar es Salaam, wakiongozwa na Ndugu Salvatory Hokororo. Karibuni sana wageni wetu. (Makofi)

Wageni 70 wa Mheshimiwa Agness Marwa ambao ni Wajumbe wa UWT (Madiwani, Wenyeviti na Makatibu) kutoka Wilaya ya Bunda, Mkoani Mara, wakiongozwa na

Mheshimiwa Diwani Ruth Mtani. Karibuni sana wageni wetu wa Mheshimiwa Agness Marwa. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Yosepher Komba ambao ni ndugu zake kutoka Mkoani Tanga, Ndugu Anitha Mganga na Ndugu Veronica Maganga. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Wageni 57 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni wanamaombi wa Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Mwalimu Mugisa Mtebe. Karibuni sana wanamaombi. *(Makofi)*

Wageni 69 wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba ambao ni kwaya ya Vijana wa Umoja wa Vijana wa Kanisa la KKKT Ipagala kutoka Jijini Dodoma wakiongozwa na Mzee wa Kanisa Ndugu Joseph Karani. Karibuni sana wanakwaya wetu. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Peter Serukamba ambao ni wadau wa afya kutoka SIKIKA, Ndugu Irene Kiria, Ndugu Richard Msittu na Ndugu Daniel Mugizi. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Wageni wa watatu wa Mheshimiwa Elias Kwandikwa ambao ni wanachuo wa Chuo Kikuu Huria wakiongozwa na Prof. Ruth Meena. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Fletei Massay ambaye ni mpigakura wake kutoka Mbulu, Mkoani Manyara, Ndugu Anold Tluway. Karibu sana mgeni wetu. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Aeshi Hillary ambao ni Viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga wakiongozwa na Mstahiki Meya wa Halmashauri ya Sumbawanga, Mheshimiwa Jastin Malisawa. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tuna matangazo mengine mawili, moja linatoka kwa Mheshimiwa Anna Lupembe

Mwenyekiti wa Ibada, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuhudhuria ibada katika *Chapel* ya Pius Msekwa leo, siku ya Jumanne, tarehe 7, Mei 2019, Saa 7.00 Mchana. Aidha, katika ibada hiyo Mwalimu Mgisa Mtebe atahudumu.

Tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa Mariam Kisangi, anasema anapenda kuwaarifu Wabunge wote wanaoishi kwenye nyumba za *TBA* kwamba leo saa 7.00 mchana kutakuwa na mkutano katika Ukumbi wa Msekwa. Kwa hiyo, anawatangazia Wabunge wote wanaoishi *TBA* wakutane baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa 7.00 katika Ukumbi wa Msekwa. Katibu tuendelee.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Hoja ya Haki za Bunge.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo.

**NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI**

#### HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 - Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto**

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Hoja ya Haki za Bunge.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba Mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7), sina haja ya kusoma kwa kuokoa muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati swali namba 180 linajibiwa kuhusiana na watoto walioko magerezani hasa watoto walioko kwenye Gereza la Mahabusu la Wanawake

la Segerea, Waziri ameelezea na akasema wanazingatia haki za watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kuomba Mwongozo kwa sababu wale watoto ambao unakuta wamepelekwa na mama zao na mahabusu wengi wanakuja na watoto, siyo kwamba wanakuja na mimba, watoto wale unakuta ni wenye umri kuanzia mwezi mmoja kwa wale ambao unakuta wamezaliwa pale mpaka miaka minne, mitatu au mitano. Waziri wakati anajibu amekiri kabisa kwamba siku 1,000 za mwanzo ni siku muhimu sana kwa makuzi ya watoto wetu. Sasa watoto wale wanavyokwenda kukaa kule ndani, wanachanganyika na wale akina mama ambao wengine ni wahalifu zaidi ya saa 16 na kwa mlundikano ulioko magereza wanaona kila tabia ambayo inafanyika kule, tunamjenga vipi huyu mtoto kisaikolojia baada ya kutoka pale? Tunaandaa taifa lipi? Unafikiri atajifunza nini kwa kile kipindi ambacho ubongo wake unakua na yeye yuko gerezani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nataka mwongozo wako uweze kuelekeza Serikali na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto walau wawe wanapita kule gerezani. Ukiangalia akina mama wale wengine wana kesi ambazo hawatakiwi kuwa gerezani kwa sababu zinadhaminika. Kuna akina mama wapo magerezani ni ombaomba, wanakaa miezi sita na watoto wadogo wakati kuna *alternative* Serikali ingeweza kufanya isipeleke wale watoto pale Gerezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba mwongozo wako Serikali iweze kusimamia haki za watoto na kuhakikisha kwamba watoto wale ambao wako magereza waweze kuondolewa. Ahsante. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wamama wamekuja kwa ajili ya omba omba wanakaa miezi sita na watoto wadogo wanakusanywa wakati kuna *alternative* Serikali ingeweza kufanya isipeleke wale watoto pale Gerezani. Kwa hiyo naomba Mwongozo wako Serikali iweze kusimamia haki

ya watoto na kuhakikisha kwamba wale watoto ambao wanakaa kule waweze kuondolewa Magerezani, ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Matiko umeeleweka, Mheshimiwa Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niruhusu nitoe hoja kwa mujibu wa Kanuni ya 51 juu ya suala linalohusu haki za Bunge. Mheshimiwa Spika alitoa Mwongozo juu ya utaratibu wa Jeshi la Polisi kuwakamata Wabunge wakati kipindi cha Bunge kikiwa kinaendelea kwamba ni kinyume na haki za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jana Mheshimiwa Spika, usiku Jeshi la Polisi katika eneo la Bunge tu wakitoka getini tu hapo limemkamata Mbunge wa Mbozi Mheshimiwa Haonga na limemlaza ndani mpaka leo na wakati tukiendelea na kipindi hiki cha maswali limekuja naye nje ya geti hapo kwa ajili ya kuwaomba Wabunge wengine kutoka kwenda naye nyumbani kwake kwenda kumsachi kwa kile kinachodaiwa kwamba kuandika ujumbe tu mwaka 2018 mwezi Mei kwenye kundi la Wabunge la mtandao wa *Whatsap*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi vitendo vya Polisi kuwa kamatakamata Wabunge wakati Bunge likiendelea vimekuwa vikikithiri. Kwa hiyo naomba ruhusa nitoe hoja jambo lijadiliwe na Bunge ili kukomesha hali hiyo Mheshimiwa Haonga achiwe mara moja aendelee na kazi zake za Bunge na utaratibu ufuatwe kama ambavyo Spika alitoa Mwongozo, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Miongozo hiyo inatosha, lakini hoja hiyo haiwezi kukubaliwa kwa sababu Mwongozo wa Mheshimiwa Spika ni kwamba mtu yoyote ambaye atatakiwa kukamatwa ndani ya Bunge ndiyo aweze kupata kibali cha Spika, lakini nje ya Bunge hana mamlaka hayo

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nje ya Bunge ni pamoja na *place entry* ya *Assembly* ya Bunge.

**MWENYEITI:** Na kuhusu suala la Mheshimiwa Esther Matiko litapatiwa majibu baadaye, tuendeleo! Tunaanza na Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Watoto ili awasilishe hotuba ya bajeti ya Wizara yake kwa mwaka wa fedha 2019/20 karibu Mheshimiwa Umy Mwalimu.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuwasilisha hotuba yangu niruhusu nitumie Bunge lako tukufu kuwatakia Waislam wote Ramadhan Mubarak, Mwenyezi Mungu akubali funga zetu na tuba zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ambayo imechambua bajeti ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, ninaomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Wizara ya Afya kwa mwaka 2018/19 na Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninaliomba Bunge lako likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Wizara kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu naomba nitumie fursa hii kwa heshima na unyenyekevu mkubwa kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake imara na pia kwa dhamira yake, maono yake na udhubutu wake ambao umekuwa dira sahihi katika utendaji wangu na katika kuimarisha utoaji wa huduma za Afya, Ustawi na Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenywekiti, ni dhahiri kuwa katika kipindi kifupi cha miaka mitatu ya uongozi wake Watanzania wameshuhudia mageuzi makubwa katika utoaji wa huduma za afya nchini ikiwemo ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya afya katika halmashauri na mikoa mbalimbali, kuimarisha upatikanaji wa dawa pamoja na kuimarisha huduma za matibabu ya kibingwa. Ninamuahidi Mheshimiwa Rais kuwa Wizara itaendelea kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ili kuhakikisha huduma za afya na ustawi wa Jamii zinawafikia watanzania walio wengi hususan wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais kwa kuwa mstari wa mbele katika jitihada za kuboresha huduma za afya hususan zinazohusu Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto, Lishe, mapambano dhidi ya Kifua Kikuu sambamba na kuhimiza usawa wa jinsia na uwezeshaji wa wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu pia nitumie Bunge lako Tukufu kumshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri unaosaidia kuleta tija na ufanisi katika utendaji na kuimarisha huduma zinazotolewa katika Sekta ya Afya, Ustawi na Maendeleo ya Jamii. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake aliyowasilisha tarehe 4 Aprili, ambayo imetoa dira ya jinsi Serikali itakavyotekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Spika wetu, Job Ndugai kwa kuliongoza Bunge letu vizuri, Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kusimamia vyema mijadala ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninapenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa Peter Serukamba, na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Juma Nkamia kwa ushauri na maelekezo yao ya mara kwa mara.



Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mzuri wanaonipatia ikiwemo kutoa ushauri na maoni yenye lengo la kuboresha huduma za afya. Ninawaahidi Waheshimiwa Wabunge wote kwamba, Wizara yangu itazingatia ushauri wenu na kuendelea kuwapa ushirikiano katika kutekeleza majukumu na kazi zetu za kuwatumikia wananchi ndani na nje ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Natoa pole kwako na watanania wote, waliopoteza ndugu, jamaa na marafiki zao kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na magonjwa, ajali, majanga pamoja na wahanga wa vitendo vya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia hususan watoto waliouawa kikatili katika Mkoa wa Njombe na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia natoa pole kwa wagonjwa na majeruhi wa ajali waliopo hospitalini na majumbani. Namuomba Mwenyezi Mungu awaponye haraka ili waweze kuendelea na ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo sasa niruhusu nieleze kwa ufupi kazi ambazo zimetetelezwa na Wizara katika mwaka wa 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara ilipanga kutekeleza afua mbalimbali zenye lengo la kuboresha utoaji wa Huduma za Afya, Ustawi na Maendeleo ya Jamii kama nilivyoanisha katika aya ya 12 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mapato na Matumizi ya Fedha Wizara kupitia Fungu 52 Idara Kuu ya (Afya) ilikadiriwa kukusanya kiasi cha Shilingi 308.7, kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato, hadi kufikia Machi, 2019 kiasi cha Shilingi bilioni 211.2 zilikusanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande, katika mwaka wa 2018/2019, Wizara kupitia fungu 52 (Afya) iliidhinishiwa na

Bunge kupokea na kutumia jumla ya Shilingi bilioni 866.2. Kati ya fedha hizo kiasi cha Shilingi bilioni 304 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, na Shilingi bilioni 87.5 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na Shilingi bilioni 216.9 ni kwa ajili ya Mishahara ya watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zilizopitishwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ni Shilingi bilioni 561.7. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 376.8 ni kutoka Serikali na Shilingi bilioni 184.9 ni kutoka kwa Wadau wa Maendeleo wanaochangia Sekta ya Afya kupitia Mfuko wa Afya wa Pamoja *Health Basket Fund*, Mfuko wa Dunia wa Kupambana na UKIMWI, TB na Malaria (*Global Fund*), Benki ya Dunia na wengineo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Machi, 2019 Wizara ilipokea jumla ya Shilingi bilioni 340.2 ya bajeti iliyoidhinishwa. Fedha zilizopokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ni Shilingi bilioni 249.1 na fedha zilizopokelewa kwa ajili ya mishahara ni Shilingi bilioni 179.6

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, hadi kufikia Machi 2019 kiasi cha Shilingi bilioni 91, kilipokelewa, Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 81, ni fedha za ndani na Shilingi bilioni 9.6 ni fedha za nje. Aidha, Wizara ilipokea jumla ya Shilingi bilioni 180, kutoka Mfuko wa Dunia wa Kupambana na Malaria, UKIMWI na Kifua Kikuu nje ya mfumo wa "*Exchequer*". Pia, Wizara ilipokea kiasi cha Shilingi bilioni 5.1 ambazo tulizipeleka moja kwa moja Ofisi ya Rais – TAMISEMI kupitia Mfuko wa pamoja wa afya kwa ajili ya ukarabati wa Vituo vya Afya ili viweze kutoa huduma bora za Afya ya uzazi na mtoto. Vilevile, katika kipindi cha Julai 2018 hadi Machi 2019, Wizara ilipokea Shilingi bilioni 50, kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya kutekeleza afua mbalimbali katika Sekta ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Fungu 53 (Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Wizara ilitarajia kukusanya kiasi cha Shilingi bilioni 3, kutokana na ada za wanafunzi kutoka Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii

pamoja na ada za mwaka na faini za Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Hadi kufikia Machi, 2019 Wizara pamoja na Taasisi zake imefanikiwa kukusanya kiasi cha Shilingi bilioni 1.4

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu liliidhinisha matumizi ya Shilingi bilioni 32.9. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 28, ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo Shilingi bilioni 12.9 ni fedha za Matumizi Mengineyo na Shilingi bilioni 15.1 ni kwa ajili ya Mishahara. Aidha, Wizara iliidhinishiwa Shilingi bilioni 4.9 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo Shilingi bilioni 1.5 ni fedha za ndani na Shilingi bilioni 3.4 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Machi, 2019 Wizara imepokea jumla ya Shilingi bilioni 17.8 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha zilizopokelewa, Shilingi bilioni 8, ni Matumizi Mengineyo, Shilingi bilioni 8.3 ni kwa ajili ya Mishahara na Shilingi bilioni 1.5 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu sasa kuzungumzia Utekelezaji Wa Majukumu chini ya Idara Kuu ya Afya, ambayo nimeainisha kuanzia ukurasa wa 16 hadi 95 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nitazungumza maneno makubwa matatu, kwa upande wa huduma za kinga, Wizara kupitia Mpango wa Taifa wa Chanjo iliweza kutoa huduma za chanjo za watoto chini ya umri wa mwaka mmoja kwa kiwango cha asilimia 98 ya lengo. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na wadau imefanikiwa kununua jumla ya majokofu yanayotumia nguvu ya jua 1,385 yenye thamani ya Shilingi bilioni 13.9 ambayo yaliyosambazwa katika Halmashauri zenye uhitaji katika Mikoa 14 nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Afya na Usafi wa Mazingira, Katika kipindi hichi wizara iliendelea kutekeleza kampeni yenye lengo la kuhimiza ujenzi na matumizi ya vyoo bora inayojulikana kama "Usichukulie Poa Nyumba Ni Choo".

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia kampeni hii idadi ya Kaya 617100 zilijenga au kuboresha vyoo vyao. Kukamilika kwa vyoo hivyo kumwezesha Kaya zenye vyoo bora nchini kufikia asilimia 55.4 kutoka asilimia 45.7 mwaka 2018. Aidha, kaya ambazo hazina vyoo bora kabisa nchini zimefungua na kufikia asilimia 2.7 kutoka asilimia 5.8 mwaka 2017/18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuwahimiza watazania kujenga na kutumia vyoo bora ili kujikinga na magonjwa. Aidha, ninapenda sana Bunge lako Tukufu kuipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ambayo imekuwa mshindi wa kwanza wa jumla kitaifa katika mashindano ya afya na usafi wa mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ndiyo maana nimeomba viongozi wa Halmashauri ya Njombe wawepo Bungeni ili kuonesha mfano kwa watazania kwamba tunaweza kujenga vyoo bora kwa sababu katika Halmashauri ya Njombe asilimia 99.8 ya Kaya za Njombe zina vyoo bora. Niruhusu niwanyanyue tena viongozi wa Njombe ili waweze kuwaonesha watazania kwamba inawezekana kuwa na Kaya zenye vyoo bora, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia imeendelea kudhibiti magonjwa yanayoambukiza na kusambaa Kimataifa ikiwemo ugonjwa wa Homa ya Manjano, ambapo tumeweza kukagua na kutoa huduma ya chanjo katika vituo vya afya mipakani kwa wasafiri takribani 6000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumeendelea kuimarisha utayari wa kukabiliana na tishio la mlipuko wa Ugonjwa wa Ebola ambao unaendelea nchini DRC, tumenunua vipimajoto 106 na kuvisambaza kwenye mipaka 31 iliyo katika Mikoa 14 yenye hatari ya kuingia kwa ugonjwa huu ambayo ni Mwanza, Songwe, Kigoma, Dar es Salaam, Rukwa, Ruvuma, Kagera, Katavi, Mbeya, Mara na Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia imeendelea kuimarisha huduma za afya ya uzazi na mama na mtoto ambapo, kwa upande wa huduma kabla ya Ujauzito, Wizara

kwa kushirikiana na wadau imenunua na kusambaza dawa mbalimbali kwa ajili ya uzazi wa mpango ili kuwezesha wanawake na wanaume kuamua lini, na ni watoto wangapi wanataka kuzaa na kwa kupishanisha muda gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha huduma za afya wakati wa ujauzito, jumla ya wajawazito 1,264,000 walihudhuria kliniki wakati wa ujauzito, kati ya hao wajawazito 892,000, walitimiza mahudhurio manne au zaidi ambapo ni sawa na asilimia 70.6 ikilinganishwa na asilimia 48 kwa kipindi kama hicho mwaka 2017. Nitumie fursa hii kuwahimiza wanawake wajawazito wote kuhudhuria kliniki kama inavyoshauriwa na wataalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa huduma wakati wa Kujifungua, Wizara ilinunua dawa za uzazi salama na kuzisambaza kupitia Bohari Kuu ya Dawa katika halmashauri mbalimbali nchini. Upatikanaji wa dawa hizo umewezesha kupunguza vifo vya akinamama vitokanavyo na uzazi pingamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kubuni mikakakti na kutafuta rasilimali fedha kwa ajili ya kuboresha vituo vya kutolea huduma za afya katika ngazi ya msingi ili viweze kutoa huduma bora ikiwa ni pamoja na huduma za uzazi wa dharura ikiwemo upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni (CEmONC). Ambapo kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI vituo vya afya 352 vimeendelea kuwezesha kutoa huduma za CEmONC pamoja na huduma zingine za upasuaji na hivyo kuongeza idadi ya akinamama wanaojifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kuwa idadi ya akinamama wanaojifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini imeongezeka na kufikia asilimia 79.2 mwezi Machi 2019 kutoka asilimia 68.5 Machi 2018. Napenda kutoa wito kwa wanawake wajawazito wote nchini, wajifungulie kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ili kupunguza vifo na changamoto za uzazi kwa mama na mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Wadau inatekeleza "Kampeni ya Jiongeze Tuwavushe Salama" yenye lengo la kuongeza kasi ya uwajibikaji katika ngazi zote ili kupunguza vifo vya akinamama na wajawazito na watoto. Kupitia kampeni hii chini ya ulezi wa Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, Wakuu wa Mikoa wote (26) walisaini Hati ya Makubaliano na Mheshimiwa Makamu wa Rais ili kuhakikisha wanaongeza kasi na uwajibikaji katika kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi na watoto wa umri wa chini ya miaka mitano katika ngazi zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha huduma kwa mtoto na mtoto mchanga, Wizara imefanya mapitio ya miongozo mbalimbali ya mafunzo, kutengeneza na kukamilisha toleo la kwanza la mwongozo wa kitaifa wa huduma za mtoto mchanga na uanzishwaji wa vyumba maalum vya kuhudumia watoto wachanga katika mikoa saba (7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, aya ya 37 hadi ya 40 ya hotuba yangu nimeainisha kazi mbalimbali zilizotekelezwa na Wizara katika kuimarisha huduma za lishe nchini. Katika kuimarisha afya na lishe ya watoto wizara katika mwezi Julai, 2018 ilitoa matone ya vitamini A kwa watoto milioni 8, ambao ni sawa na asilimia 97.2 ya lengo na mwezi Desemba imetoa matone ya vitamini A kwa watoto 8.3 ambao ni sawa na asilimia 97 ya watoto wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kutoa virutubishi muhimu vya madini na vitamini kwa ukuaji wa mwili na akili kupitia urutubishaji wa unga wa ngano, unga wa mahindi na mafuta ya alizeti. Katika kipindi cha mwaka 2018/2019 jumla ya mashine 62 za kusaga mahindi katika Mikoa ya Mbeya, Iringa, Shinyanga, Morogoro, Dodoma, Ruvuma, Tanga, Songwe, Njombe, Manyara na Dar es Salaam zimefungwa kifaa maalum cha kuongeza virutubishi na hivyo kufanya idadi ya mashine zinazofanya urutubishaji kufikia 213 tangu utaratibu huu ulipoanzishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa udhibiti wa ugonjwa wa UKIMWI, Wizara imeendelea na mapambano dhidi ya ugonjwa huu ambapo, Huduma za Ushauri Nasaha na Upimaji wa VVU zimeendelea kutolewa kwa wananchi wote bila malipo mijini na vijijini. Idadi ya watu waliopimwa VVU imeongezeka kutoka milioni 10.5 mwaka 2017/18 hadi kufikia watu milioni 14.3 Machi 2019 Wizara kwa kushirikiana na wadau inatekeleza Kampeni, ya Furaha Yangu, Pima, Jitambue, Ishi inayolenga kuongeza idadi ya watu wanaopima VVU na kutambua hali zao ili kuanza dawa za ARV mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa kwa kuwa balozi wa kampeni hii. Aidha ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote wakiongozwa na Mheshimiwa Spika waliojitokeza kupima VVU na kutambua hali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampeni hii imeongeza hasa kwa watanania hasa wanaume kujitokeza kupima VVU, ambapo idadi ya watu wanaokadiriwa kuwa na maambukizi ya VVU na wanaotambua hali zao imeongezeka kutoka milioni 138 hadi kufikia watu milioni 1.1 mwishoni mwa mwezi Machi 2019. Lakini idadi ya watu wanaotumia dawa za ARV ni asilimia 98 ya watu wapatao milioni 1.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile watu wanaotumia dawa za ARV na ambao wana kiwango cha chini cha virusi vya UKIMWI imefikia asilimia 88 ikilinganishwa na asilimia 84 mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto zimeendelea kutolewa, ambapo jumla ya akina mama wajawazito 2,196,000 sawa na asilimia 97.2 ya akina mama wajawazito walengwa walipatiwa huduma za ushauri nasaha na upimaji wa VVU. Kati yao asilimia 3.6 waligundulika kuwa wanaishi na VVU. Kiwango hicho cha maambukizi kinaashiria Tanzania kufikia lengo la dunia la kupunguza maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto ya chini ya 4%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia imeendelea kuongeza kasi ya ugunduzi wa wagonjwa wa Kifua Kikuu ambao katika mwaka 2018/2019 wagonjwa 58,000 waligunduliwa na kuwekwa kwenye matibabu. Kiwango cha ugunduzi wa wagonjwa wa Kifua Kikuu kilipanda kutoka asilimia 40 mwaka 2016 hadi kufikia asilimia 44. Pia tumeimarisha huduma za upimaji wa *TB* kwa kuongeza mashine za kisasa za *GeneXpert* zinazopima Kifua Kikuu kwa ufanisi na muda mfupi kutoka 65 hadi 218 kwa sasa. Mashine hizi hutoa majibu ndani ya masaa mawili ikilinganishwa na Hadubini ambazo hutoa majibu baada ya masaa 48.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea pia kuhakikisha tunatoa huduma za ukoma lakini pia kwa upande wa udhibiti wa Malaria, Serikali imeendelea kushirikiana na wadau kuhakikisha dawa za kutibu Malaria na vitenganishi zinapatikana katika vituo vya kutoa huduma za afya. Vile vile tumeendelea kuwakinga wananchi na maambukizi ya Malaria kwa kugawa jumla ya vyandarua milioni 7.5 vyenye dawa vila malipo kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumefanya kazi ya kuangamiza mbu wakiwa katika hatua ya viluwilwi kwenye mazalia kwa kununua viuadudu (*biolarvicides*) lita 60,000 na kuzisambaza katika mikoa mitano yenye kiwango kikubwa cha maambukizi ya Malaria ambayo ni Geita, Kagera, Kigoma, Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia imetekeleza pia zoezi la upulizaji wa dawa ukoko majumbani (*in door residual spray*) katika Halmashauri saba za mikoa minne yenye kiwango kikubwa cha maambukizi ya Malaria ambazo ni Ngara, Bukoba Vijijini, Misenyi, Chato, Nyang'hwale, Buchosa na Kakonko ambapo jumla ya nyumba 500,001 zilipulizwa dawa ukoko katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea pia na jitihada za kudhibiti ugonjwa wa Kipindupindu ambapo katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019, jumla ya wagonjwa 2,050 wa Kipindupindu na vifo 28 vilitolewa taarifa nchini ambapo



mikoa 23 kati ya 26 iliweza kudhibiti ugonjwa huu kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia imeendelea kudhibiti ugonjwa wa *Dengue* ambao umekuwa ni tishio. Hadi kufikia Machi, 2019, wagonjwa 523 wametolewa taarifa katika Mikoa ya Dar es Salaam na Tanga. Wizara imeshakamilisha mpango mkakati wa kudhibiti ugonjwa huu ambao unajumuisha kujenga uwezo wa watumishi wa afya katika kutambua, kupima, matibabu na udhibiti wa mbu wanaoeneza ugonjwa huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Bunge lako Tukufu, natoa rai kwa wananchi kuwa makini wapatapo homa na wahakikishe wanakwenda kupata huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya ili waweze kupimwa na kupatiwa tiba sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea pia na kazi ya udhibiti wa magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele ambapo nimeyaainisha katika ukurasa za 42 hadi 43 wa hotuba yangu. Tumetoa tiba kinga kwa ajili ya magonjwa ya minyoo ya tumbo, Kichocho kwa watoto, ugonjwa wa *Trachoma*, ugonjwa wa Usubi pamoja na ugonjwa wa matende na mabusha ambapo watu wapatao milioni 8.1 walipatiwa kingatiba ya matende na mabusha kwa mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea pia kutoa elimu kwa jamii kuhusu masuala mbalimbali ikiwemo lishe, kujikinga na magonjwa ya kuambukiza, magonjwa yasiyo ya kuambukiza na yale ambayo hayapewi kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa huduma za tiba, Wizara imeendelea kusimamia upatikanaji wa huduma za afya zinazitolewa kupitia vituo vya kutolea huduma vya Serikali, binafsi na Mashirika ya dini. Katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019, vituo vya kutolea huduma za afya nchini vimeongezeka kufikia 8,119 ikilinganishwa na vituo 7,678 mwezi Juni, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia imeendelea kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kwa kuiwezesha Bohari ya Dawa (*MSD*) kununua, kutunza na kusambaza dawa, vifaa na vifaa tiba kwenye vituo vya kutolea huduma za afya. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019 upatikanaji wa dawa muhimu aina 30 kwenye Vituo vya Serikali vya kutolea huduma za afya umefikia asilimia 94.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kwa dhamira yake ya dhati ya kuboresha upatikanaji wa dawa katika vituo vya kutoa huduma za afya. Aidha, katika kuboresha huduma za uchunguzi wa magonjwa, Wizara imenunua mashine za *X-Ray* 11 za digitali na kupelekwa katika hospitali za rufaa za Mikoa ya Ruvuma, Morogoro, Simiyu, Singida, Njombe, Kagera, Amana, Katavi na Hospitali za Wilaya za Magu, Chato na Nzega. Vilevile, Wizara imenunua na kusambaza vifaa na vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi bilioni 97.3 katika vituo vya afya 318 vilivyojengwa na kukarabatiwa katika Halmashauri mbalimbali nchini ili kuviwezesha kutoa huduma bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo Wizara ya Viwanda na Biashara tumeandaa mwongozo unaoainisha fursa mbalimbali za Uwekezaji katika viwanda vya dawa na vifaa tiba ambapo hadi kufikia Machi, 2019 viwanda nane vya dawa vinaendelea kujengwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Wizara imefuta tozo 14 na kupunguza tozo nyingine 17 zilizokuwa zinatozwa na Mamlaka ya Chakula na Dawa (*TFDA*) ikiwa ni mkakati wetu wa kuhakikisha tunaweka mazingira wezeshi ya kibiashara na kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi ili kuvutia uwekezaji wa ndani. Tumeweka katika kiambatisho Na. 10 na 11, tozo ambazo tumezipunguza na kodi ambazo tumezifuta ili kuvutia uwekezaji wa ndabi wa dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Mpango wa Taifa wa Damu Salama, Wizara imeweza kukusanya jumla ya chupa

za damu salama 235,381 ikilinganishwa na chupa 119 zilizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuboresha na kuimarisha huduma za matibabu ya kibingwa ili kuokoa maisha ya wananchi wengi sambamba na kupunguza idadi ya wagonjwa wanaopewa rufaa ya matibabu nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha 2018/2019, Hospitali za Rufaa za Kanda na Taifa ziliwasilisha Wizarani idadi ya wagonjwa 62 waliokuwa na mahitaji ya kupatiwa matibabu nje ya nchi ikilinganishwa na wagonjwa 114 katika kipindi 2017/2018. Maana yake, rufaa za wagonjwa nje ya nchi zimepungua kutoka 114 hadi 62 katika kipindi hiki na magonjwa yaliyoongoza kwa kupewa rufaa ni saratani, moyo, mifupa, mishipa ya fahamu, mishipa ya damu, figo na magonjwa mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yangu pia nimeeleza kazi mbalimbali zilizofanywa na hospital zetu. Kipekee nitataja kwa ufupi kazi ambazo zimefanywa na Hospital ya Taifa ya Muhimbili katika ukurasa wa 53 hadi wa 56 wa hotuba yangu nimeonyesha mafanikio makubwa yaliyopatikana katika Hospital ya Taifa ya Muhimbili. Kipekee nitaje mambo makubwa mawili:-

(i) Jumla ya wagonjwa 29 walipatiwa huduma ya upandikizwaji wa figo (*Renal transplant*) na kufikisha jumla ya wagonjwa 38 waliopata huduma hii. Gharama ya huduma hii katika Hospital ya Taifa ya Muhimbili ni shilingi milioni 20 mpaka 30 kwa mgonjwa mmoja wakati nje ya nchi ingetugarimu shilingi milioni 100 hadi shilingi milioni 120.

(ii) Hospitali ya Muhimbili pia imetoa huduma za kupandikiza vifaa vya usikivu kwa watoto (*cochlear implant*) kwa watoto 11 na kufikisha jumla ya watoto 21 waliopata huduma hii toka ilipoanza mwaka 2017. Gharama ya huduma hii nchini ni kati ya shilingi milioni 35 mpaka milioni 40 kwa

mgonjwa mmoja wakati tungewapeleka wagonjwa hawa nje ya nchi wangegharimu shilingi milioni 80 hadi milioni 100 kwa mtoto mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Mloganzila imeendelea pia kutekeleza majukumu yake kama nilivyoainisha kuanzia ukurasa wa 53 hadi 58 wa hotuba yangu. Katika kuimarisha usimamizi wa hospitali hii na kufuatia maelekezi ya Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli, tarehe 3 Oktoba, 2018, uendeshaji wa Hospitali ya Mloganzila ulikabidhiwa kwa Bodi na Menejimenti ya Hospitali ya Taifa Muhimbili kutoka Chuo Kikuu cha Afya Muhimbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya *MOI* imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kutoa huduma za matibabu ya mifupa, upasuaji mishipa ya fahamu ambapo mambo makubwa yaliyotekelezwa nimeainisha katika ukurasa wa 58 hadi 59 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete imeendelea pia kutekeleza majukumu mbalimbali ambayo nimeyaainisha katika hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 61 hadi ukurasa wa 62. Baadhi ya mafanikio makubwa yaliyopatikana katika Hospitali yetu ya Moyo ya Jakaya Kikwete ni kufanya upasuaji kwa wagonjwa 330 wenye matatizo ya mishipa ya damu. Wagonjwa 964 walipatiwa matibabu ya moyo kupitia mtambo maalum wa kisasa wa kufanya upasuaji wa moyo bila kufungua kifua (*Cathelab*).

Pia kukamilisha ukarabati wa jengo la wodi mpya ya watoto ambayo inalenga kutoa huduma bora kwa watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 62 hadi 65 wa hotuba yangu nimeonyesha mafanikio makubwa yaliyofikiwa na Hospitali na Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road*. Kipekee nitambue mambo makubwa mawili:-

(i) Serikali imewezesha kununua na kufunga mashine mbili za kisasa za kutibu Saratani (*Linac*) kwa shilingi bilioni 9.5 kwa kutumia fedha za ndani kwa asilimia 100. (*Makofi*)

Tanzania inakuwa nchi ya kwanza katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati kwa kuanza kutumia mashine zenye teknolojia hiyo. Hadi kufikia Machi 2019, jumla ya wagonjwa 244 walitibiwa kwa kutumia mashine hizi za kisasa ambapo wagonjwa 70 wangepelekwa nje ya nchi kwa matibabu haya na wangetumia shilingi milioni 50 kwa kila mgonjwa lakini Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road* imeweza kupunguza muda wa kusubiri kuanza tiba za mionzi kwa wagonjwa kuwa chini ya wiki tatu kutoka wiki sita Mwaka 2018. Hapo awali muda wa kusubiri tiba ya mionzi ilikuwa wiki 12.

(ii) Hospitali ya Saratani pia imeweza kupunguza idadi ya wagonjwa wakiopewa rufaa kutoka wagonjwa 164 mwaka 2016/2017 hadi wagonjwa 42 tu mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na jitihada za Serikali za kuimarisha huduma za matibabu ya Saratani nchini, niruhusu nitumie Bunge lako Tukufu kuhimiza Watanzania kupima Saratani angalau mara moja kila mwaka ili endapo wana dalili za Saratani waweze kupata matibabu haraka kwani Saratani inatibika ikigundulika mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali ya Benjamin Mkapa-Dodoma imeendelea kutoa huduma kama nilivyoonyesha kwenye ukurasa wa 66 hadi 67 wa hotuba yangu, lakini nitaje mambo makubwa mawili kwa upande wa Benjamin Mkapa:-

(i) Wameanza upandikizaji figo ambapo wagonjwa sba wamepata huduma hii tangu kuanzishwa.

(ii) Pia hospitali ya Benjamin Mkapa imeanzisha huduma ya uchunguzi na matibabu ya moyo kwa kutumia maabara maalum ya kisasa ya kufanya upasuaji wa moyo bila kufungua kifua (*Cathelab*) yenye thamani ya shilingi bilioni 2.4 ambapo jumla ya wagonjwa 12 wamenufaika na huduma hizi toka ilipozinduliwa Februari, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Afya ya Akili Mirembe pamoja na Taasisi ya Isanga imeendelea kutoa

huduma kwa wagonjwa wa akili ambapo hali ya upatikanaji wa dawa kwa wagonjwa wa akili ni asilimia 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Hospitali ya Rufaa ya Magonjwa ya Kifua Kikuu (Kibong'oto) imeendelea kutoa huduma za utambuzi na matibabu ya Kifua Kikuu, Kifua Kikuu Sugu na magonjwa ya kuambukiza. Taarifa ya kina imeainishwa kuanzia ukurasa wa 68 hadi 69 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya) imeendelea kutoa huduma za matibabu ya kibingwa hususan kwa wananchi wa mikoa sita ya Katavi, Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa ambapo kazi zilizotekelezwa nimeziainisha katika ukuarasa wa 69 hadi ukurasa wa 71 wa hotuba yangu. Hali ya upatikanaji wa dawa ni asilimia 95. Hospitali pia imenunua *CT-Scan* yenye thamani shilingi bilioni 1.1 ambayo ipo katika hatua ya ufungwaji na huduma zinategemewa kuanza kutolewa mwezi Mei, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa (Bugando) imeendelea kutoa huduma za kibingwa kwa wagonjwa kutoka Mikoa 6 ya Mwanza, Geita, Simiyu, Shinyanga, Kagera, Mara na Kigoma. Kazi zilizotekelezwa nimezionesha katika ukurasa wa 71 hadi 73 wa hotuba yangu. Mambo muhimu yaliyotekelezwa ni pamoja na kupanua huduma za kibingwa kwa kuanza kutoa matibabu yote ya Saratani baada ya kununua mashine ya tiba ya mionzi. Upatikanaji wa huduma hii umepunguza rufaa ya wagonjwa wa Saratani wa Kanda ya Ziwa kwenda Taasisi ya *Ocean Road-Dar es Salaam* kwa zaidi ya asilimia 95.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Rufaa ya Kanda Kaskazini (*KCMC*) imeendelea kuboresha na kutoa huduma kwa wananchi ambapo katika mwezi Julai, jumla ya wagonjwa 120,000 walipatiwa huduma. Asilimia 79 ya wagonjwa waliohudumiwa walitoka katika mikoa mitano ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Tanga na Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yangu pia nimeonyesha kazi mbalimbali ambazo zimetetelezwa na Hospitali za Rufaa za Mikoa. Katika kuimarisha utoaji wa huduma katika Hospitali za rufaa za Mikoa, Mheshimiwa Rais alielekeza hospitali hizi sasa zisimamiwe na Wizara ya Afya kutoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Kwa hiyo, kuanzia tarehe 01 Julai, 2018 hospitali hizi zimekuwa chini ya usimamizi wa Wizara ya Afya na zimeona jumla ya wagonjwa milioni 3.2 kama nilivyonyesha katika jedwali Na. 2 la hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeboresha huduma za uchunguzi katika Hospitali za Rufaa za Mikoa kwa kununua mashine za *X-Ray* nane za kidigitali. Pia ujenzi wa majengo ya kutoa huduma ya uzazi yanaendelea katika hospitali ya Sekotoure, Mwananyamala, Mawezi, Shinyanga na Njombe. Vile vile miundombinu ya huduma za dharura zinajengwa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa. Hotuba yangu imeonyesha kwa kirefu kazi zilizofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea na kazi ya kuhakiki ubora wa huduma za afya ambapo tumeweza kutafuta fedha kutoka Mfuko wa Dunia kwa ajili ya kuboresha huduma za afya katika vituo vya afya ngazi ya mamlaka ya Serikali za Mitaa pamoja na ngazi ya Hospitali za Rufaa za Mikoa. Katika fedha ambazo tumezipata shilingi bilioni 10.9, shilingi bilioni 10 tutazipeleka Hospitali za Rufaa za Mikoa, shilingi bilioni tatu tutazipeleka katika hospitali za Wilaya na shilingi bilioni tatu zimetengwa kwa ajili ya zahanati, shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea pia na kazi ya ugharamiaji wa huduma za afya ambapo tumeandaa Muswada wa kutunga Sheria ya Bima ya Afya kwa watu wote. Muswada huu unatarajiwa kuwasilishwa Bungeni mwezi Septemba, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu rasilimali watu katika Sekta ya Afya, jumla ya wanafunzi 18,500 walidahiliwa na vyo vya afya kwa ajili ya kusoma kozi mbalimbali za afya. Kwa upande wa watoa huduma, jumla ya vibali vya ajira

kwa watumishi 8,071 vilitolewa katika kipindi hiki. Vilevile nyumba za Watumishi wa Afya 318 zimejengwa kwa lengo la kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi wa Sekta ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia fursa hii kuzitaka Halmashauri zote nchini hasa za pembezoni kuweka mazingira mazuri na vivutio kwa watumishi wa afya kufanya kazi katika Halmashauri zao. Aidha, natoa rai kwa viongozi wenzangu, viongozi wa Mkoa, Wilaya na Halmashauri kuzingatia sheria, taratibu na kanuni katika kushughulikia nidhamu na uwajibikaji wa Wataalam wa Afya katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia kupitia Mabaraza ya Wanataaluma na Bodi za Ushauri zimeendelea kutekeleza kazi za kusimamia Wataalam wa Afya. Katika hotuba yangu, ukurasa wa 95 hadi 113 nimeonyesha kazi zilizotekelezwa na Taasisi mbalimbali ikiwemo Bohari ya Afya, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya pamoja na Mamlaka ya chakula na dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ningependa kueleza mafanikio tuliyoyapata ambapo mamlaka ya chakula na dawa (*TFDA*) imetunukiwa cheti cha ngazi ya tatu ya umahiri kitaalam (*Maturity level III*) Mwezi Novemba, 2018. Ngazi hii ni ya juu sana na hivyo kuifanya *TFDA* kuwa mamlaka ya kwanza Barani Afrika kufikia hatua hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Chakula na Lishe imeendelea kutekeleza kazi mbalimbali kwa ajili ya kuimarisha lishe za wanawake na watoto wachanga hasa katika siku 1,000 za mwanzo wa mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imeendelea kutekeleza kazi mbalimbali kama nilivyoonyesha katika ukurasa wa 107 hadi 108 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Utafiti ya Magonjwa ya Binadamu (*NIMR*) imeendelea kufanya miradi



mbalimbali pamoja na kufanya tafiti katika kutatua changamoto za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu chini ya Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii yaliyotekelezwa nimeeleza kuanzia ukurasa wa 113 hadi ukurasa wa 150 wa hotuba yangu. Kazi kubwa tulizofanya ni kuamsha ari ya wananchi kushiriki katika shughuli za kuleta maendeleo ambapo Wizara imeshiriki katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kwa kutumia nguvu kazi pamoja na rasilimali zinazowazunguka wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kutoa, kusimamia utaoji wa mafunzo kwa kada ya maendeleo ya jamii kupitia vyojo nane vya maendeleo ya jamii vya Buhare, Uyole, Rungemba, Mlale, Misungwi, Ruaha, Mabugai na Monduli ambapo katika mwaka 2018/2019, jumla ya wanafunzi 3,414 walidahiliwa kulinganisha na wanafunzi 2,676 waliodahiliwa mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuhakikisha uwepo wa haki za mtoto za kuishi, kuendelezwa, kushiriki, kulindwa na kutobaguliwa katika jamii ambapo kupitia Mabaraza ya Watoto 1,669 yaliyopo katika ngazi ya Taifa, Mikoa, Halmashauri, Kata na Vijiji yameendelea kuzitekeleza kazi hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuratibu upatikanaji wa huduma za msingi za chakula, malazi, kwa watoto walio katika mazingira hatarishi wanaoishi katika makao ya watoto yanayomilikiwa na Serikali na Taasisi Binafsi, ambapo jumla ya watoto 13,420 walipatiwa huduma za msingi ikilinganishwa na watoto 6,132. Inaonesha watoto wengi sasa hivi wanaishi katika makao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kupitia Bunge lako tukufu kutoa wito kwa jamii kuzingatia misingi na utamaduni wa Kitanzania kwa kutunza watoto, kwa kutunza ndugu na jamaa zao ili kuepusha watoto kulelewa katika vituo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeendelea kuwatambua na kuwawezesha huduma za msingi kwa watoto wanaoishi mitaani, ambapo watoto milioni 1.8 walitambuliwa na kupatiwa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia imeendelea kutoa huduma za msingi ikiwemo chakula, malazi, mavazi na matibabu kwa wazee wakiwemo wazee wasiojiweza katika makazi 17, lakini tumeendelea kutoa elimu na kuwahamasisha jamii kulinda na kuheshimu haki za wazee kupitia majukwaa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kufanyia kazi mashauri ya migogoro ya ndoa na matunzo ya watoto ambapo jumla ya mashauri ya migogoro ya ndoa 16,832 yalipokelewa na kufanyiwa usuluhishi katika mikoa mbalimbali ikilinganishwa na mashauri 13,382 yaliyofanyiwa kazi mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kuwezesha wanawake kiuchumi kupitia dirisha la wanawake la Benki ya Posta Tanzania ambapo mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni mbili imetolewa kwa wanawake wajasiliamali 3,035. Pia tumeendelea kuhimiza halmashauri kutoa mikopo ya uwezeshaji wanawake inayotokana na asilimia nne ya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali tumeendelea kuyasimamia ili yachangie kuleta tija katika maendeleo yetu. Jumla ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 617 yamesajiliwa na kupatiwa cheti cha usajili ikilinganishwa na mashirika 385 yaliyosajiliwa mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Taasisi zilizo chini ya Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii tumeeleza kazi mbalimbali zilizotekelezwa katika hotuba yangu, ukurasa wa 150 hadi ukurasa wa 151.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru imeendelea kutoa mafunzo ambapo katika mwaka huu wanafunzi 1,183 kwa fani ya Maendeleo ya Jamii wamedahiliwa ikilinganishwa na wanafunzi 743 mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Ustawi wa Jamii imeendelea pia kutoa mafunzo ya Ustawi wa Jamii ambapo katika mwaka huu wa fedha wanafunzi 1,064 wamedahiliwa ikilinganishwa na wanafunzi 1,185 waliodahiliwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende katika kuwasilisha vipaumbele vya Wizara na bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Vipaumbele vya Wizara yangu katika kipindi cha mwaka 2019/2020 vimeainishwa kuanzia ukurasa wa 155 hadi 167 wa hotuba yangu. Kwa upande wa Idara Kuu ya Afya katika mwaka wa 2019/2020 Wizara imejiwekea vipaumbele vifuatavyo:-

- (i) Kuendelea kuimarisha na kuboresha utoaji wa huduma za chanjo ili kuwakinga watoto chini ya mwaka mmoja dhidi ya magonjwa yanayozuilika kwa chanjo;
- (ii) Kuendelea kuimarisha hali ya lishe na usafi wa mazingira ili kuwezesha wananchi kujikinga na magonjwa;
- (iii) Kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa Tiba, vitendanishi katika vituo vya Umma vya kutolea huduma za afya;
- (iv) Kuendelea kuboresha huduma za Afya ya uzazi, mama na mtoto, ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na watoto wa chini ya umri wa miaka mitano;
- (v) Kuendelea na juhudi ya kupunguza pengo kati ya mahitaji halisi ya watumishi wa afya na idadi ya watumishi wa afya waliopo katika vituo vya Umma vya kutolea huduma za afya;

- (vi) Kuboresha Miundombinu na utoaji huduma katika Hospitali za Rufaa za Mikoa;
- (vii) Kuimarisha huduma za Kibingwa katika Hospitali za Taifa, Maalum na Kanda;
- (viii) Kuendelea kudhibiti magonjwa yasiyo ya kuambukiza ikiwemo, Saratani, Kisukari, Shinikizo la Damu na Magonjwa wa Moyo;
- (ix) Kuendelea na utekelezaji wa afua mbalimbali zenye lengo la kuimarisha na kupunguza maambukizi ya UKIMWI, TB na Malaria; pamoja na
- (x) Kukamilisha Mchakato wa maandalizi ya kutunga sheria ya Bima ya Afya itakayomtaka kila mwananchi kuwa na Bima ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipaumbele vilivyoainishwa katika mwaka 2019/2020, kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:-

Kununua na kusambaza chanjo kwa ajili ya kuwakinga watoto ambapo fedha za ndani shilingi bilioni 30 zimetengwa. Wizara pia itaendelea kutekeleza afua mbalimbali za huduma ya kinga ikiwa ni pamoja na kupunguza vifo vya akinamama wajawazito vitokanavyo na uzazi ambapo jumla ya shilingi bilioni tano fedha za ndani zimetengwa. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na ujenzi wa vituo 12 vya damu salama katika mikoa 12, pamoja na upanuzi wa wodi za wazazi na kutenga vyumba vya wagonjwa mahututi wanaotokana na uzazi katika hospitali za Rufaa za Mikoa mitano. Pia ukarabati wa ujenzi wa wodi maalum kwa ajili ya watoto wachanga utafanyika katika hospitali za Rufaa za mikoa saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kudhibiti magonjwa yasiyo ya kuambukiza hususani kisukari, magonjwa ya moyo na shinikizo la damu na saratani. Katika mwaka 2019/2020, Wizara itaanzisha mpango wa Taifa wa kudhibiti magonjwa yasiyo

ya kuambukiza ambapo afua mbalimbali zitatekelezwa kukabiliana na magonjwa haya. Tunataka kama tunavyoweka nguvu za kupambana na *TB*, kupambana na UKIMWI na *Malaria* kupitia mipango maalum ya Taifa ndivyo tunavyotaka kuweka nguvu za kupambana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza. Pia tutaendelea kuimarisha upatikanaji wa dawa ambapo fedha shilingi bilioni 200 fedha za ndani zimetengwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweka mezani pia *errata* ili kufanya marekebisho katika hotuba yangu ukurasa wa 158 ambapo kiasi kilichotengwa kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa damu salama, naomba kisomeke shilingi bilioni 2.2 badala ya shilingi bilioni 2. Pia katika *errata* ambayo nimeweka mezani ukurasa wa 159 *paragraph* ya 225 naomba isomeke:

Katika mwaka 2019/2020 Taasisi ya Saratani *Ocean Road* itaendelea kuimarisha huduma za kinga, uchunguzi, mafunzo na tiba ya saratani ambapo jumla ya shilingi bilioni 10 zimetengwa. Aidha, kwa upande wa hospitali ya Kanda ya Ziwa Bugando jumla ya shilingi bilioni 1.7 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa mashine ya *MRI* ili kuimarisha huduma za uchunguzi wa magonjwa na kuanza ujenzi wa wodi ya magonjwa ya saratani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika kuendelea kuimarisha huduma za kibingwa katika ngazi za hospitali za Rufaa za Mikoa jumla ya shilingi bilioni 12 zimetengwa fedha za ndani kwa ajili ya kuanzisha na kuboresha vitengo vya dharura na kuendelea kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma katika hospitali ya Mkoa wa Mara pamoja na hospitali za Rufaa za Mikoa mipya ya Katavi, Njombe, Geita, Simiyu na Songwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa huduma za matibabu ya kibingwa tumetenga bilioni nne kwa ajili ya hospitali ya Taifa Muhimbili ili waweze kuboresha huduma na pia tumetenga bilioni moja fedha za ndani kwa ajili ya hospitali ya Jakaya Kikwete na bilioni tano zimetengwa kwa

ajili ya *MO* ili kuwezesha utoaji wa matibabu ya kibigwa kwa maradhi ya mgongo, mishipa ya fahamu, mifupa, kuwaongea ujuzi wataalam wa upasuaji pamoja na vifaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, kazi ambazo zimetetelezwa nimezieleza pia katika hotuba yangu vipaumbele vikiwa ni kuamsha ari ya wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo, kukuza usawa wa jinsia na uwezeshaji wa wanawake kiuchumi, kuimarisha upatikanaji wa haki na maendeleo ya mtoto, kuimarisha huduma za ustawi wa jamii, kuimarisha usimamizi na uratibu wa mashirika ya Serikali, lakini kuboresha mafunzo ya ustawi wa jamii na maendeleo ya jamii ili kuendelea kuzalisha wataalam wenye ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nitumie fursa hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa ushirikiano mkubwa ambao nimeupata kutoka nchi rafiki, Mashirika ya Kimataifa na sekta nyingine zinazosaidia na kuchangia katika huduma za afya, ustawi na maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii ya kipekee kuzishukuru nchi saba zinachangia Mfuko wa Afya wa Pamoja (*Health Basket Fund*) ambazo ni Denmark, Uswisi, Ireland, Canada, Korea Kusini na Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa ya Benki ya Dunia na *UNICEF* kwa kuchangia Mfuko huu ambao umesaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha huduma za afya nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nayashukuru Mashirika yaliyo chini ya Umoja wa Mataifa yakiwemo *WHO*, *UNAIDS*, *UNFPA* na *UN Women* na pia napenda kuzishukuru nchi za China, Cuba, Japan, Marekani, Sweden, Uingereza, Ujerumani na Ufaransa na nchi nyingine ambazo zimeendelea kuisaidia Wizara yangu. Vilevile nayashukuru Mashirika mengine ya Kimataifa kwa ushirikiano wao walioutoa. Wadau wote hawa nimewaainisha kwenye hotuba yangu kuanzia aya ya 235 hadi 237.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nitambue mchango mkubwa wa Shirika la Kimataifa na Kupambana na *Malaria, TB* na Kifua Kikuu *Global Fund, GAVI Global Vaccine Alliance*, Mfuko wa Rais wa Marekani wa kupambana na *Malaria PMI, USAID, PEPFAR* pamoja na *Bill and Melinda Gate Foundation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha utendaji wa kazi nikiwa Waziri nimepata ushirikiano mkubwa kutoka kwa viongozi na wafanyakazi wa Wizara wa Afya. Kipekee nimshukuru sana sana Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndungulile, Naibu Waziri wa Afya kwa ushirikiano mkubwa anaonipatia katika utekelezaji wa majukumu yangu. Aidha, napenda kuwashukuru Dkt. Zainabu Chaula Katibu Mkuu Afya na Dkt. John Jingu Katibu Mkuu Maendeleo ya Jamii kwa mchango wao mkubwa katika kuwezesha utekelezaji wa majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile namshukuru Profesa Muhammad Bakari Kambi Mganga Mkuu wa Serikali, Makamishna, Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo vya Wizara. Nawashukuru pia Wakurugenzi Wakuu wa Hospitali za Taifa na Kanda ambao nimewaorodhesha katika aya ya 238 ya hotuba yangu. Nawashukuru Wakurugenzi na Wakuu wa Taasisi zote zilizo chini ya Wizara ambazo ni *MSD, NHIF, TFDA, NIMR*, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, *TFNC*, Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru pamoja na Mabaraza ya Kitaaluma na Bodi za usajili ikiwemo Baraza la Madaktari Tanzania pamoja na Baraza la Wauguzi na Wakunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya kwa kuwezesha utekelezaji wa majukumu yangu, Waganga Wafawidhi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa 28 ambao wako hapa, Waganga Wafawidhi wa Hospitali za Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati pamoja na Wakuu wa Vyuo vya Mafunzo vilivyo chini ya Wizara na wafanyakazi wote wa Wizara ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayashukuru Mashirika ya Dini, Mashirikia Yasiyo ya Kiserikali, Mashirika Binafsi ambao

kwa kiasi kikubwa wamechangia katika utekelezaji wa majukumu yangu. Nawashukuru wananchi wote kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaifanya katika kuhakikisha tunajenga Tanzania ya Viwanda iliyo na nguvu kazi yenye afya bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nitumie fursa hii kuishukuru sana familia yangu kwa uvumilivu wao, lakini pia kwa kunitia moyo katika kutekeleza majukumu yangu ya Kitaifa na kwa wananchi wa Mkoa wa Tanga hususan wananchi wa Jiji la Tanga, nawashukuru sana kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika kutekeleza majukumu yangu, naahidi kwamba nitaendelea kuwaenzi na kuwatumikia kwa nguvu zangu zote ili kuleta mabadiliko ya haraka ya maendeleo katika mkoa wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nipunguze kasi ili niweze kuomba fedha. Kwa upande wa Idara Kuu ya Afya - Fungu 52; katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara na Taasisi zilizo chini yake imekadiria kukusanya kiasi cha Sh.246,298,617,884, kati ya fedha hizi Sh. 26,031,607,827 zinatarajiwa kukusanywa kutoka vyanzo vya ndani vya Makao Makuu ya Wizara. Makusanyo haya ni sawa na ongezeko la asilimia 24 ikilinganishwa na shilingi bilioni 19.7 zilizoidhinishwa kukusanywa mwaka 2018/2019. Aidha, Mashirika yaliyo chini ya Wizara yanakadiria kukusanya Sh.220,267,010,057.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa matumizi kupitia Fungu 52, Wizara imepanga kutumia kiasi cha Sh.415,014,262,000 ili iweze kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo kiasi cha Sh.93,927,890,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo kiasi cha Sh.321,086,372,000 ni kwa ajili ya mishahara ya Wizara na Taasisi zilizo chini yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa shughuli za maendeleo, Wizara kupitia Fungu 52 - Afya inakadiria kutumia Sh. 544,137,902,597. Kati ya fedha hizo fedha za ndani ni Sh. 270,600,000,000 ambayo ni sawa na asilimia 49.6 na fedha za nje ni Sh. 275,537,900,297 sawa na asilimia 51.4.



Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya makadirio ya bajeti kwa mwaka 2019/2020, kwa Fungu 52 ni Sh.959,152,164,597. Kwa upande wa Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii - Fungu 53, katika mwaka 2019/2020 Wizara inakadiria kukusanya Sh. 4,763,596,000 kutokana na ada za wanafunzi kutoka Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Chuo cha Ustawi wa Jamii na ada ya usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya kawaida katika mwaka 2019/2020, Wizara inakadiria kutumia kiasi cha Sh. 28,777,370,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo Sh.12,951,892,000 ni mishahara ya watumishi na Sh.15,825,478,000 ni matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa shughuli za maendeleo, Wizara kupitia Fungu 53, inakadiria kutumia Sh.2,760,091,013 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo Sh.1,000,000,000 ni fedha za ndani na Sh.1,760,061,013 ni fedha za nje. Jumla kuu ya fedha inayoombwa kwa mwaka 2019/2020, kwa Fungu 53 ni Sh. 31,537,431,013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla kuu ya fedha ambazo naomba Bunge lako Tukufu lipitisha kwa ajili ya Wizara yangu kwa Mafungu yote mawili Fungu 52 na Fungu 53 ni Sh. 990,689,595,610. Kati ya fedha hizi Sh. 546, 897,963,610 ni kwa ajili ya maendeleo na Sh. 443,791,632,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba yangu kamili inapatikana katika tovuti za Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kama nilivyoonesha katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ummu Mwalimu, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto hoja imeungwa mkono.

Sasa namkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii. Mheshimiwa Peter Serukamba karibu.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kutoa *report* yangu naomba kufanya marekebisho katika taarifa ya Kamati yangu ukurasa wa 12 katika sehemu ya 2.5 matokeo na maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika aya ya kwanza sehemu inayosomelika mwaka wa fedha 2017/2018 na badala yake isomeke mwaka wa fedha 2018/2019. Naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni ya 99(9) katika Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu cha 6(5) na 7(1) vya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 Kamati hii ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni hizo Kamati hii ina wajibu pia kushughulikia bajeti ya kila mwaka ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Bunge imeweka sharti la Kamati ya Kisekta ikiwemo Kamati hii kufanya ukaguzi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyo chini ya usimamizi wa Kamati hii. Pia naomba

*report* yangu yote kama ilivyo kwenye kitabu iingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa taarifa ambayo inafuata mambo makubwa manne.

(i) Hali ya utekelezaji ya mapendekezo ya Kamati kwa mwaka 2018/2019.

(ii) Mapitio ya taarifa ya utekelezaji wa mpango ya bajeti ya mwaka 2018/2019 na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

(iii) Uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka 2019/2020 na maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Pili, utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Mapendekezo ya Kamati. Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Kamati ilitoa jumla ya maoni na ushauri na mapendekezo 19 kwa ajili ya kufanyiwa kazi na Wizara. Kati ya maoni hayo, yapo yaliyoweza kutekelezwa kikamilifu na baadhi yanaendelea kutekelezwa na mengine bado hayajatekelezwa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ushauri ambao umetekelezwa, Kamati inaipongeza Serikali na Wizara kwa jitihada hizo na yale ambayo yanaendelea kutekelezwa, Kamati inasisitiza Wizara kuendelea kusimamia utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara ilikadiria kukusanya shilingi bilioni 240.042 kupitia Fungu 52 – Idara Kuu ya Afya na kufikia Februari, 2019, Wizara imekusanya shilingi bilioni 168.7 sawa na asilimia 70.2. Aidha, Fungu Namba 53 – Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii ilikadiria kukusanya shilingi bilioni 3.09 na hadi Februari 2019 shilingi bilioni 1.48 sawa na asilimia 48 ya makadirio zilikuwa zimekusanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi mwezi Februari 2019 Fungu 52 – Wizara ilikuwa imepokea shilingi bilioni 489.807 sawa na asilimia 56.5 kati ya shilingi bilioni 866.23. Aidha, kwa ajili ya miradi ya maendeleo shilingi bilioni 561.759 zilitengwa na hadi kufikia Februari, 2019 shilingi bilioni 275.03 zilipokelewa sawa na asilimia 48.9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Fungu 53 hadi kufika mwezi Februari Wizara ilikuwa imepokea shilingi bilioni 15.807 sawa na asilimia 49.1 ya shilingi bilioni 32.14. Aidha, fedha za miradi ya maendeleo hadi kufika mwezi Februari shilingi bilioni 1.133 sawa na asilimia 23 tu zilipokelewa. Kamati inatoa rai kwa Serikali kuhakikisha fedha zilizobaki zinatolewa kabla ya mwaka wa fedha kuisha ili Wizara iweze kutekeleza miradi iliyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo kuhusu ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Kamati ilifanikiwa kufanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo miwili iliyo katika Mkoa wa Dar-es-Salaam na Pwani. Miradi hiyo ni pamoja na Mradi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mwananyamala, Dar-es-Salaam, Namba 5411 na Mradi wa uimarishaji wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Pwani, Tumbi, Namba 5411.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo na maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Baada ya Kamati kufanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka 2018/2019, kamati inatoa ushauri ufuatao:-

(i) Kama ilivyoelezwa kwenye taarifa ya ukaguzi wa wa miradi hakuna fedha yoyote iliyopokelewa kwa miradi ambayo Kamati ilitembelea kuikagua. Kamati inaona kuna umuhimu na ulazima wa Serikali kuhakikisha inapeleka fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu ili kufikia malengo ambayo tumejiwekea wenyewe.

(ii) Uhaba wa watumishi. Uhaba wa watumishi wa afya nchini ni takribani asilimia 50. Kamati inashuhudia uhaba huu katika taasisi za afya kama vile Hospitali ya

Mwananyamala ambayo ina upungufu wa watumishi 47. Kamati inaishauri Serikali kuiangalia hospitali hii na hospitali nyingine zote zenye upungufu kwa kuzipa umuhimu wa kipekee kuzipatia watalaam wa kutosha.

(iii) Motisha kwa watumishi wa afya. Kamati imebaini kuwa changamoto ya malipo mbalimbali zikiwemo motisha za posho ya nyumba, motisha ya saa za ziada kwa watumishi wa afya ni kubwa na inaweza kuathiri utendaji wa kazi. Kamati inaishauri Serikali kulibeba suala hili kipekee na kulitafutia ufumbuzi kwa haraka.

Aidha, kwa Hospitali ya Mwananyamala ambayo haina nyumba hata moja ya watumishi, Kamati inashauri Serikali kuharakisha ujenzi wa nyumba ya watumishi katika hospitali hiyo na hospitali nyingine yenye changamoto kama hizo ili kuboresha upatikanaji wa huduma ya afya kwa haraka.

(iv) Ukosefu na usahihi wa takwimu. Kumekuwa na changamoto ya upatikanaji wa takwimu sahihi katika taasisi mbalimbali za Serikali hasa za afya ambazo Kamati inaamini ndio msingi wa upangaji wa maendeleo katika taasisi hizo. Katika miradi ambayo Kamati imetembelea na kupokea taarifa yake imebainika dhahiri kuwa kuna ukosefu wa takwimu na zilizopo nyingi sio sahihi, Kamati inaona hili si jambo jema.

Hivyo, inashauri Serikali kuzisimamia taasisi zake kuhakikisha zinakuwa na takwimu za kutosha na zilizo sahihi kuweza kupanga mipango yetu kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa mpango wa makadirio ya mapato na matumizi ya Mwaka 2019/2020. Uchambuzi wa Ukusanyaji wa Maduhuli. Kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara kupitia Fungu 52 inakadiria kufanya makusanyo ya jumla ya shilingi bilioni 250.29 katika vyanzo mbalimbali vya Wizara. Aidha, kupitia Fungu 53 inakadiria kufanya makusanyo ya shilingi bilioni 4.763 katika vyanzo mbalimbali ikiwemo ada za wanafunzi wa Vyuho nane vya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa makadirio ya matumizi ya mwaka 2019/2020. Wizara kupitia Fungu 52 imekadiria kutumia shilingi bilioni 959.12. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 415.014 sawa na asilimia 43.3 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 544.13 sawa na asilimia 56.7 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Fungu 53 limekadiria kutumia shilingi bilioni 31.57. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 28.77 sawa na asilimia 91 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 2.760 sawa na asilimia 8.7 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo asilimia 33 inategemea fedha kutoka kwa wahisani na asilimia 67 ni fedha za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tatu, maoni na mapendekezo ya Kamati. Kamati ilimaliza kufanya uchambuzi wake wa bajeti ya mwaka 2019/2020 katika mafungu yote yaliyo chini ya Wizara hii. Kufuatia uchambuzi huo, Kamati inatoa maoni na ushauri na mapendekezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto unategemea bajeti iliyotengwa ambayo jambo moja, lakini jambo la pili upatikanaji wa fedha hizo na kwa wakati ili kuweza kutekeleza kikamilifu majukumu nyake. Bajeti ya Wizara kupitia Fungu 52 imeongezeka kwa asilimia 9.6 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2018/2019. Kamati inaipongeza Serikali kwa ongezeko hilo la bajeti, hata hivyo, inaendelea kusisitiza Serikali kutoa fedha hizo zote na kwa wakati, kama ilivyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kuhakikisha shughuli zilizopangwa zinatekelezwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa dawa (*essential medicines*) kwa wagonjwa. Kamati inatambua jukumu la kununua, kutunza na kusambaza dawa hapa nchini ni jukumu la Bohari Kuu ya Dawa ambayo inatekeleza majukumu yake kwa weledi mkubwa na kuhakikisha dawa,

vifaa na vifaatiba vinakuwapo katika maghala yote hapa nchini. Kamati inaipongeza Bohari Kuu ya Dawa kwa utekelezaji mzuri wa majukumu, licha ya changamoto za uhaba wa fedha kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua utoaji wa huduma za afya ni pamoja na upatikanaji wa dawa kwa mgonjwa. Kamati imebaini changamoto kubwa ipo katika vituo vya kutolea huduma ya afya inayotokana na utoaji wa orodha ya dawa, hasa dawa muhimu, pasipo kuzingatia mahitaji ya kituo cha kutolea huduma ya afya. Kwa mujibu wa takwimu za Wizara, matokeo ya mahitaji halisi ya dawa ya mwaka ni trilioni 1.4 lakini bajeti iliyotengwa wastani ni shilingi bilioni 250 na ambazo utolewaji wake umekuwa ni asilimia 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maoni ya Kamati kuwa ni muhimu vituo vya kutolea huduma ya afya kuanzia ngazi ya zahanati hadi hospitali za rufaa kuzingatia mahitaji ya dawa ya kituo ili kuondokana na ukosefu wa dawa muhimu katika vituo hivyo. Pili, Serikali ione umuhimi wa kuongeza bajeti ya dawa na kuhakikisha zote zinatolewa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwepo wa Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii (*Community Health Workers*). Wote tunafahamu kinga ni bora kuliko tiba. Kamati inatambua umuhimu wa Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii (*Community Health Workers*) ambao wana jukumu la kuhamasisha jamii katika masuala mbalimbali ya afya kama vile lishe bora, wanawake wajawazito kuhudhuria kliniki, kujifungua katika vituo vya kutolea huduma za afya, matumizi ya vyandarua, umuhimu wa kunywa maji safi na salama na umuhimu wa kuwa na vyoo. Si hivyo, tu, lakini wahudumu wa afya ngazi ya jamii wana jukumu la kutoa huduma za afya kama vile kutoa huduma ya kwanza kwenye jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mifano mizuri ya nchi ya Rwanda ambayo imefanikiwa kupunguza vifo vya watoto chini ya miaka mitano, vifo vya mama wajawazito na vifo vingine vitokanavyo na magonjwa kama malaria,

*pneumonia*, kuhara kutokana na kuwapo hawa wahudumu wa afya ngazi ya jamii. Kamati inafahamu kuwa hapa nchini kuna wahudumu wa afya ngazi ya jamii takribani 13,000 hawana ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati inafahamu pia kuwa makadirio ya bajeti ya mshahara ya mwaka 2019/2020 hayajagusia ajira wala motisha ya wahudumu wa afya ngazi ya jamii kitu ambacho Kamati inaona ni kinyume na Makadirio ya Mpango Mkakati wa Afya wa Nne inaolenga kurasimisha ajira 5,000 za wahudumu wa afya ngazi ya jamii ifikapo 2020. Kamati inaona hilo siyo jambo jema kwani, inatambua kuwa ajira za wahudumu wa afya ngazi ya jamii ni sehemu ya mkakati wa kupunguza vifo vya akinamama wajawazito na watoto chini ya miaka mitano. Kutokana na umuhimu huu, Kamati inaendelea kuishauri Serikali itoe ajira kwa hawa *Community Health Workers* ili kusaidia kuboresha huduma za mama, mtoto kwa ngazi ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati ya kuzuia magonjwa yasiyoambukizwa (*non communicable disease*). Tafiti zinaonesha kuwa katika miaka 10 iliyopita tishio kubwa limekuwa ni magonjwa yasiyoambukizwa ambayo ndio yaliyokuwa yanatishia maisha ya watu wengi. Kwa miaka ya hivi karibuni tafiti zinaonesha kuwa kuna ongezeko kubwa la magonjwa yasiyoambukiza yakiwemo saratani, shinikizo la damu, kisukari na mengine ambayo husababishwa na watu kutofanya mazoezi, ulaji usiozingatia kanuni za afya, msongo wa mawazo kutokana na hali za kiuchumi, kutopata matibabu mapema kwa magonjwa yanayoambukiza kwa sababu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magonjwa haya yanaongeza gharama kubwa za muda na rasilimali fedha kwa Serikali katika kuwatibu na mengi yanakuwa ni matibabu ya maisha yote kuanzia pale anapogundulika kuwa ni mgonjwa. Ni maoni ya Kamati:-

(i) Serikali iweke mipango madhubuti ya kuelimisha jamii juu ya manufaa na namna bora ya kuzuia



magonjwa badala ya kusubiri mpaka mgonjwa anakuja kutambulika.

(iii) Serikali ifanye kampeni kubwa ya uhamasishaji wa jamii kufanya mazoezi kila wiki au mwezi kwa ngazi zote, namna ya kupata lishe bora, kuwahi katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa magonjwa yanayoambukizwa ili yasisababishwe madhara ya kupata magonjwa yasiyoambukiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa huduma bora na uhakika za uzazi. Kamati inatambua mikakati mbalimbali ya Serikali katika kuhakikisha inatoa huduma bora na za uhakika za uzazi ili kupunguza changamoto mbalimbali zitokanazo na uzazi, vikiwemo vifo vya mama na mtoto. Vifo hivi vingi vinatokana na utokwaji wa damu nyingi, uzazi pingamizi, kuharibika kwa mimba, kifafa cha mimba na kukosa msaada wa mtaalamu katika vituo vya kutolea huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kuwa akina mama 24 wanapoteza maisha kila siku hapa nchini kutokana na matatizo haya ya uzazi. Aidha, takwimu zinaonesha kuwa sekta ya afya ina upungufu wa watumishi asilimia 48, changamoto zote hizi bado zinaendelea kugharimu maisha ya Watanzania walio wengi, hasa wale wanaoishi katika maeneo ambayo hayana huduma za uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto hizi Kamati inashauri ifuatavyo:-

(i) Serikali ifanye uboreshaji wa huduma za uzazi katika maeneo mbalimbali yenye changamoto hizo.

(ii) Serikali ihakikishe inaweka vifaa vya kisasa na watoa huduma pamoja na kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa wanawake wajawazito kwenda kujifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya ili kuweza kupunguza idadi ya vifo vya mama na mtoto.

(iii) Serikali, hususan Utumishi, ione umuhimu wa kutoa vibali vya ajira ili Wizara iweze kuajiri watumishi wa kutosha wakiwemo Madktari Bingwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishaji wa Bima ya Afya kwa Wote (*Universal Health Coverage*). Kwa kipindi kirefu sasa Kamati imekuwa ikisitiza Serikali kuharakisha mchakato wa Bima ya Afya kwa Wote ili kuondokana na changamoto ya wananchi kukosa huduma za afya kutokana na changamoto za kifedha. Aidha, taarifa zinaonesha kuwa asilimia 33 ya wananchi ndio wanaopata huduma ya afya kwa kutumia mfumo wa bima, kati yao hao asilimia 7 tu ndi7o wanapata huduma kupitia Mfuko wa Bima ya Afya, asilimia 25 kupitia Mfuko wa Afya ya Jamii, asilimia 1 kutoka bima binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo, zaidi ya asilimia 60 ya wananchi wa Tanzania hawana uhakika wa kupata huduma ya afya kwa kuwa upatikanaji wa huduma ya afya kwao unategemea upatikanaji wa fedha. Ni maoni ya Kamati kuwa hali hii inasababisha kukosa haki ya msingi ya afya na kuwafanya wengine hata kupoteza maisha yao kwa kukosa huduma ya afya pale wanapougua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kukamilisha mchakato wa uletwaji wa Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote Bungeni ili uweze kuwa sheria na kuanza utekelezaji wake kuhakikisha kila mwananchi afya yake inalindwa kwa kuwa na bima ya afya ya uhakika. Aidha, wakati mchakato unaendelea, Serikali ianze kupanga mikakati ya namna gani watahamasisha jamii kwa ajili ya kuelewa umuhimu wa bima ya afya ili wakati wa utekelezaji kusiwepo changamoto ya kutokubali licha ya kuwepo kwa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uimarishaji wa mikakati ya kuzuwia magonjwa yotakanayo na uhaba wa maji na uchafu wa mazingira. Ni dhahiri kuwa maji ni uhai na kila mtu anafahamu kuwa pasipo na maji ya uhakika kwa mwanadamu madhara yake ni makubwa sana, ikiwemo

mlipuko wa magonjwa mbalimbali kama vile kipindupindu, kuhara, kuhara damu, magonjwa ya njia za mkojo (*UTI*) na upele yakitajwa kwa uchache wake. Magonjwa haya yanaenda sambamba na mazingira machafu yanayosababishwa na kujisaidia sehemu za wazi na kupelekea kusambaa kwa kinyesi na kwenda kuchafua mazingira yakiwemo maji yanayotumiwa na binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa watalaamu wa afya magonjwa ya tumbo yakiwemo kipindupindu, yataepukika endapo kutakuwepo na maji safi na salama wakati wote. Si hivyo tu, lakini pia ni pamoja na pale watu watakapotunza mazingira yao, uwepo wa vyoo bora kwa kila kaya, kuvitumia kwa usahihi, usafi binafsi ikiwemo kunawa mikono wanapotoka chooni na hata kuoga kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya maji na usafi wa mazingira ni sekta mtambuka ambapo Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inawajibika katika kusimamia na kutekeleza miradi ya maji na usafi wa mazingira kwa ujumla wake. Wizara hii ina mlango mkuu wa matumizi makubwa ya bajeti ya afya kwa maana ya manunuzi ya dawa kwa ajili ya kutibu magonjwa yatoakanayo na uhaba wa maji, uchafu wa mazingira ikiwemo kuhara na kuhara damu, hasa kwa watoto chini ya miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua kwamba, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inatekeleza mikakati mbalimbali ya usafi kwa mazingira ikiwemo uendeshwaji wa kampeni za ujenzi wa vyoo bora katika kila kaya, ijulikanayo kama Kampeni ya Nyumba ni Choo. Kampeni hii inasaidia watu kujenga vyoo bora na hatimaye kuacha kujisaidia katika maeneo wazi na hivyo, kuepuka magonjwa ya mlipuko. Kampeni ya Nyumba ni Choo imekuwa na mafanikio makubwa kwani Wizara ilifanya uamuzi sahihi kushirikisha wadau mbalimbali ikiwemo sekta binafsi, vyombo vya habari kama vile *Clouds Media*, mitandao ya kijamii, wasanii wakubwa akiwemo Mrisho Mpoto katika kuwafikia wananchi wote wa hali na rika tofauti

kwa ajili ya kufikisha ujumbe na umuhimu wa matumizi sahihi ya choo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari za kujisaidia katika maeneo ya wazi ni uchafuzi mkubwa wa mazingira kwa tani za vinyesi kwa mwaka mzima (siku 365) kwa wastani wa nusu kilo kwa mtu mmoja kwa siku kuzagaa kama Kielelezo Namba 6 kinavyoonesha. Hesabu za haraka, kijiji chenye kaya 300 kwa mwaka kinazalisha kinyesi cha tani 201.6 sawa na malori 10 ya tani 20 yanasambaza kinyesi katika kijiji hicho. Maswali ya kujiuliza, Tanzania ina vijiji vingapi ambavyo havina vyoo bora na matumizi ya vyoo vilivyopo ni hafifu? Kamati inaona hii ni changamoto kubwa sana katika jamii yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kuwa vifo vingi vya watoto chini ya miaka mitano vinaongozwa na magonjwa mbalimbali, ikiwemo kuhara na kuhara damu, ikiwa ni ugonjwa namba tatu unaosababisha mwili kupoteza maji mengi na hatimaye kusababisha kifo. Kamati inatambua juhudi za Serikali katika kuhakikisha kunakuwa na maji safi na salama pamoja na usafi wa mazingira. Aidha, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inaunganisha nguvu kati ya Wizara ya Maji, Wizara ya Mazingira, Wizara ya Elimu kwa maana ya shule na Wizara ya Afya kwa ajili ya kuweka afua funganishi (*intergrated intervations*) kwa ajili ya kutatua matatizo ya maji na uchafu wa mazingira hatimaye kuondokana na tatizo la magonjwa yanayotokana na uhaba wa maji na mazingira machafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna msemu Slovakia unasema, naomba kunukuu: *"Pure water is the world first and foremost medicine"*. Kwa tafsiri isiyo rasmi ni kwamba, maji safi ni dawa ya kwanza duniani. Kwa mantiki hiyo ni wito wa Kamati kwa Serikali kwamba ni lazima kutafutia wananchi dawa ya kwanza ili wananchi wasiweze kupata magonjwa yanayotokana na uhaba wa maji na uchafu wa mazingira katika maeneo wanayoishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifahamike kuwa kinga ni bora kuliko tiba. Ni vyema kuhakikisha kunakuwa na maji safi

na salama katika mazingira safi ili kuweza kunusuru afya za Watanzania. Kwa kufanya hivyo, Wizara itaokoa fedha nyingi za dawa kwa ajili ya kutibu magonjwa ya tumbo, kuhara na kuhara damu, kipindupindu na hata kupunguza mzigo mkubwa wa wagonjwa wanaolazwa katika hospitali, hasa watoto chini ya miaka mitano na kubaki na yale magonjwa mengine yasiyotokana na maji na usafi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uimarishaji wa huduma na lishe. Lishe ya binadamu inapaswa kuangaliwa kuanzia kipindi cha mimba inapotungwa kwa wajawazito mpaka mtoto anapozaliwa, kipindi cha miaka mitano na hadi anapokuwa mtu mzima. Umuhimu wa lishe ni pamoja na ukuaji wa akili ya mtoto (*cognitive development*) ambayo ikikosewa wakati wa ujauzito na ukuaji wa mtoto kwa kipindi cha miaka mitano ya awali basi madhara yake yataonekana mtoto anapokuwa shule na hata baada ya shule kwa maana ya utekelezaji wa majukumu yake akiwa mtu mzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya umuhimu huo wa lishe kwa mtoto taarifa zinaonesha kuwa Tanzania tumekuwa tukitenga Sh.1,000 sawa na Dola 0.5 mbayo ni chini ya makubaliano ya kimataifa ya Dola 8.5 za Kimarekani kwa mtoto kwa ajili ya lishe. Kwa mantiki hiyo Serikali imefanikisha kutenga asilimia 5.8 tu ya makubaliano yaliyowekwa. Kiasi hiki hakiridhishi hata kidogo kwani kinaziweka afya za watoto katika hatari kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rai ya Kamati kwamba, ni wakati sasa Serikali kutoa kipaumbele kwa suala la lishe kwa watoto hasa wale chini ya miaka mitano ikiwemo kuhakikisha zinatolewa dawa za minyoo, virutubisho katika vyakula vyao na matone ya vitamin A. Lakini kama hii haitoshi, Wizara ihakikishe kwamba kunakuwa na kampeni kubwa ya kuhakikisha hakuna mtoto anafariki kwa kukosa lishe bora. Haya yote yanaweza kufanyika kwa kutenga fedha za kutosha angalau dola nne kwa kila mtoto ili angalau kupunguza tatizo la udumavu, utapiamlo ambalo madhara yake ni makubwa hapo baadaye kwa Taifa hili, kwani watoto wa leo ni taifa la kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapambano ya dhidi ya Virusi vya UKIMWI na Upungufu wa Kinga Mwilini. Mapambano dhidi ya UKIMWI yanafanyika na wadau mbalimbali wa UKIMWI wa ndani na nje ya nchi. Kwa mujibu wa taarifa ya *National HIV Impact Survey, 2016/2017* maambukizi mapya kwa mwaka ni watu 72,000 kwa maana nyingine ni kwamba, maambukizi kwa siku ni watu 197. Takwimu hizi zimegawanywa katika makundi ya rika mbalimbali makundi hayo ya umri, kundi ambalo linaongoza kwa maambukizi kwa kiasi kikubwa ya Virusi vya UKIMWI ni kundi la vijana wenye umri wa kati ya miaka 15 - 24 kwa asilimia 49 na katika kundi hilo wasichana wanaongoza kwa asilimia kubwa ikilinganishwa na wavulana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mkakati wa Serikali wa kupata tisini tatu 90 – 90 - 90 kwa maana ya asilimia 90 ya watu wote wanaokisiwa kuishi na Virusi Vya UKIMWI wanatambua hali zao za maambukizi, kuhakikisha asilimia 90 kati yao wanatumia dawa za kufubaza makali ya Virusi Vya UKIMWI (ARVs) na asilimia 90 ya wanaotumia dawa kwa usahihi kuhakikisha dawa hizo zinawawezesha kufubaza Virusi vya UKIMWI. Kwa mantiki hiyo, mpango mkuu ni asilimia 90 ya kwanza ndiyo itakayowawezesha Serikali kufikia malengo ya asilimia 90 ya pili na ya tatu kwa hizi mbili zinategemea 90 kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika utekelezaji wa afua ya UKIMWI ikiwemo upimaji wa virusi vya UKIMWI kwa hiari ili kuweza kuifikia asilimia 90 ya kwanza kumekuwa na vikwazo mbalimbali katika utekelezaji wake ikiwemo ukinzani wa Sheria ya UKIMWI iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu mwaka 2008 imeweka katazo la mtanzania mwenye umri chini ya miaka 18 kutopima VVU isipokuwa kwa ridhaa ya mzazi au mlezi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maoni ya Kamati kuwa Sheria hii inakinzana na takwimu ambao ndiyo uhalisia kama zilivyoelezwa hapo awali kuwa vijana wenye maambukizi makubwa ni vijana kati ya miaka 15 - 24 ambapo kuna vijana wa kuanzia miaka 17, 16, 15 wako katika kundi hatarishi la

kupata VVU. Kamati inashauri Serikali kuwa ni wakati sasa wa kufanya marekebisho ya Sheria hiyo ili kutanua wigo wa watu kuweza kupima na kutambua afya zao na hatimaye kuwaingiza katika utumiaji wa dawa za kufubaza makali ya VVU ambayo ni 90 ya pili na hatimaye kufubaza VVU na kufikia lengo la asilimia 90 ya tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanzi *data* ya majukumu ya Asasi Zisizo za Kiserikali (AZAKI). Asasi zisizo za kiserikali ni asasi zinazotoa mchango mkubwa katika jamii ili kutekeleza majukumu mbalimbali yakiwemo ya afya, maendeleo ya jamii, jinsia wazee na watoto kupitia Sera na mikakati mbalimbali ya Wizara hiyo. AZAKI hizo zinasajiliwa na kusimamiwa na Wizara hii. Ni maoni ya Kamati kuwa ni vyema Wizara ikatengeneza kanzidata ya AZAKI zote zinazotekeleza majukumu yake katika jamii pamoja na kupata taarifa ya utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufanyika tathmini ya vyuo vyote vya Maendeleo ya Jamii pamoja na mitaala yake. Ni maoni ya Kamati kuwa ni wakati sasa wa Serikali kufanya tathmini ya vyuo vilivyopo zaidi ya 50 pamoja na mitaala yake na kuweza kuona ni namna gani vyuo hivyo vinaweza kutoa elimu kuendana na wakati wa sasa kwa maana ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iboreshe Jela za watoto. Utungwaji wa Sheria ya Wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; napenda kuchukua nafasi hii, kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa muda wa kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako tukufu.

Pia napenda kumshukuru sana Waziri wa Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto Mheshimiwa Ummy Mwalimu (Mb) pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile (Mb) kwa ushirikiano wao mkubwa wanaoendelea kuutoa kwa Kamati wakati wote wa shughuli za Kamati. Aidha, napenda kuwashukuru Makatibu Wakuu wa Wizara Dkt. Zainab Chaula (Idara kuu Afya), Dkt. John

Jingu (Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii) pamoja na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake zote kwa ushirikiano wanaoutoa kwa Kamati yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru wadau wote wa Sekta ya Afya na Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto wakiwemo Taasisi ya Benjamini Mkapa, SIKIKA, AMREF, UMATI, JENGO kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya kwa wananchi wetu na kwa ushirikiano wao mkubwa kwa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kushirikiana zaidi na wadau hawa wa Afya kwani juhudi zao zote ni kwa ajili ya manufaa ya kiafya ya wananchi wa kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nafasi ya pekee kabisa naomba nimshukuru Makamu Mwenyekiti wangu Mhe. Juma Nkamia na Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai, Mkurugenzi Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athman Hussein na Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Dickson Bisile Makatibu wa Kamati yetu Ndugu Pamela Pallangyo na Ndugu Agnes Nkwera kwa kuisaidia na kuiwezesha kamati hii kutekeleza majukumu yake kwa weledi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto pamoja na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2019/2020, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja Fungu 52 shilingi 959,152,168,000 na Fungu 53 jumla ya shilingi 31,537,431,013.



**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA  
MAENDELEO YA JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU  
YA WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE  
NA WATOTO KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 - KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

---

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu kifungu cha 6(5) (a) na 7(1) vya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati hii ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni hizo, Kamati hii ina wajibu pia wa kushughulikia Bajeti ya kila Mwaka ya Wizara hii.

Vile vile, Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Bunge, imeweka sharti la Kamati za Kisekta, ikiwemo Kamati hii, kufanya Ukaguzi wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyopo chini ya usimamizi wa Kamati ambapo Kamati ilitembelea, ilikagua na kupokea Taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo miwili iliyotengewa Fedha kwa Mwaka 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya maelezo hayo, naomba kutoa taarifa hii ambayo inafafanua mambo manne (4) yafuatayo:-

- i. Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati kwa Mwaka wa fedha 2018/2019

- ii. Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo;
- iii. Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020; na
- iv. Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;

## SEHEMU YA PILI

---

### 2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

**Mheshimiwa Spika**, katika kikao cha Kamati pamoja na Wizara kilichofanyika tarehe 25 na 26 Machi, 2019, Kamati ilifanya Uchambuzi wa Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati, Mpango wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2018/2019 (ukusanyaji wa maduhuli, upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida pamoja na za kutekeleza miradi ya maendeleo pia iliangalia utekelezaji wa majukumu ya Wizara).

#### 2.1 Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2018/19, Kamati ilitoa jumla ya Maoni, ushauri na mapendekezo kumi na tisa (19) kwa ajili ya kufanyiwa kazi na Wizara. Kamati imefanya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo na kubaini kuwa, yapo yaliyoweza kutekelezwa kikamilifu, baadhi yanaendelea kutekelezwa na mengine bado hayajatekelezwa kabisa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ushauri ambao umetekelezwa, Kamati inaipongeza Serikali na Wizara kwa jitihada hizo na yale ambayo yanaendelea kutekelezwa Kamati inaisisitiza

Wizara kuendelea kusimamia utekelezaji wake. Aidha, kwa maeneo ambayo hayajatekelezwa kwa sababu mbalimbali ikiwemo ya kutopata Fedha kutoka Serikalini, Kamati inaiagiza Wizara kufuatilia Fedha hizo na kuyatekeleza mara moja kabla ya Mwaka wa Fedha 2018/2019 haujamalizika.


## 2.2 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha wa 2018/2019, Wizara Ilikadiria kukusanya kiasi cha shilingi **240,042,508,157.00** kupitia Fungu 52 (Idara Kuu Afya) na kufikia mwezi Februari, 2019 Wizara ilikuwa imefanikiwa kukusanya kiasi cha shilingi **168,716,161,480** sawa na **asilimia 70.2** ya makadirio. Kamati imebaini kuwa makadirio yaliyofanywa na baadhi ya Taasisi zilizo chini ya Fungu 52 kwa mwaka wa Fedha wa 2018/2019 yamefanyika vizuri na nyingine hazijafanya vizuri. Makusanyo ya juu kabisa ni kwa **asilimia 104** kutoka Baraza la Madaktari Tanzania na makusanyo ya chini ni kwa **asilimia 24** kutoka Baraza la Tiba Asili na Tiba mbadala. **Kamati inapongeza Taasisi hii na Taasisi zote zilizofanya vizuri katika makadirio yaliyovuka asilimia 75. Aidha, kwa Taasisi ambazo zipo chini ya Lengo, Kamati inashauri ziongeze juhudi za makusanyo kabla ya mwaka huu wa fedha kuisha.**

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Fungu 53 - Idara Kuu Maendeleo ya Jamii, kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/2019, Wizara ilikadiria kukusanya kiasi cha shilingi **3,090,796,000.00**. Kamati ilielezwa kuwa kufikia mwezi Februari, 2019 kiasi cha shilingi **1,483,465,065** sawa na **asilimia 48** ya makadirio kilikuwa kimekusanywa. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, makusanyo yasiyoridhisha ya Fungu 53 yanatokana na kuwa na vyanzo vichache lakini pia ni kutokana na kati ya vyanzo vyake vinne, vyanzo vitatu vinatokana na makusanyo ya ada za wanafunzi. **Kamati inaendelea kuishauri Wizara kupia Idara Kuu Maendeleo ya Jamii kubuni vyanzo vingine badala ya kutegemea mapato yatokanayo na ada za wanafunzi ambayo yanategemea na idadi ya wanafunzi watakaodahiliwa.**

**Mheshimiwa Spika**, Kielelezo Na.1 Kinaonyesha hali ya ukusanyaji wa maduhuli kwa Fungu 52 na Fungu 53 kwa Mwaka 2018/2019.

**Kielelezo Na. 1. Hali ya Ukusanyaji wa Maduhuli**



**Chanzo: Randama za Wizara (2019) na Usanifu wa Kamati**

**2.3 Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, Kuhusu hali ya upatikanaji wa fedha, Kamati ilielezwa kuwa, Fungu 52 - Idara Kuu Afya, kwa kipindi cha kuanzia Julai 2018 hadi Februari, 2019 Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha shilingi **489,807,109,084** sawa na asilimia **56.5** kati ya kiasi cha shilingi **866,233,475,000.00** kilichokuwa kimeidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa, shilingi **218,117,546,469** sawa na **asilimia 72** ya shilingi **304,473,000,000** zilizoidhinishwa na Bunge ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kati ya fedha hizo za Matumizi ya Kawaida fedha zilizopokelewa, kwa ajili ya mishahara zimepokelewa shilingi **155,661,000,000** sawa na **asilimia 72** ya lengo na fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo, kiasi cha shilingi **62,456,546,469** kimepokelewa sawa na **asilimia 71** ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya maendeleo, kiasi cha shilingi **561,759,999,000.00** kilitengwa. Kamati ilielezwa kuwa, kufikia mwezi Februari, 2019 kiasi cha shilingi **275,035,841,09** kilipokelewa sawa na **asilimia 48.9** ya fedha iliyotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya maendeleo. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kati ya fedha hizo za Miradi ya Maendeleo, kiasi cha shilingi **89,935,000,000** kilipokelewa kutoka Hazina, kiasi cha shilingi **5,100,000,000** kilipokelewa kupitia mfuko wa Afya wa pamoja (*Health Basket Fund*) na kiasi cha shilingi **180,000,000,000** kilipokelewa kutoka Mfuko wa Dunia wa Kupambana na Malaria, UKIMWI na Kifua Kikuu (*Global Fund*).

**Mheshimiwa Spika**, Katika Fungu 53 - Idara Kuu Maendeleo ya Jamii, Kamati ilielezwa kuwa, hadi kufikia mwezi Februari, 2019 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi **15,807,996,517.40** sawa na **asilimia 49.1** ya shilingi **32,140,649,000.00** zilizotengwa kwa ajili ya Fungu hili. Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi **7,420,762,793.80** sawa na **asilimia 49** kilikuwa kimepokelewa kwa ajili ya Mishahara na kiasi cha shilingi **7,253,727,292.60** sawa na **asilimia 59.9** kilikuwa kimepokelewa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

**Mheshimiwa Spika**, fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara kupitia Fungu 53, hadi kufikia mwezi Februari, 2019 kiasi cha shilingi **1,133,506,431.00** ambayo ni sawa na **asilimia 23.0** tu ya fedha yote iliyokuwa imetengwa kilikuwa kimepokelewa. **Kamati inatoa rai kwa Serikali kuhakikisha fedha hizi zinatoka kabla ya mwaka wa fedha kuisha ili Wizara iweze kutekeleza miradi iliyopanga.**

**Kielelezo Namba.2: Upatikanaji wa Fedha (Fungu 52 & 53)**

BAJETI		ILIYODHINISHWA		UPATIKANAJI WA FEDHA	
NA	FUNGU	MGAWANYO	KIUCHOIDHINISHWA	KILICHOPOKELEWA	ASILIMIA
1.	52	OC	87,514,048,000	62,456,546,469.00	71.37
		Mishahara	216,959,428,000	155,651,398,267.00	71.74
		Maendeleo	561,759,999,000	275,035,841,092.00	48.95
		<b>Jumla</b>	<b>866,233,475,000</b>	<b>493,153,387,561.00</b>	<b>57</b>
2.	53	OC	12,109,842,000	7,253,727,292.60	59.8
		Mishahara	15,116,962,000	7,420,762,793.80	49.0
		Maendeleo	4,913,845,000	1,133,506,431.00	23.0
		<b>Jumla</b>	<b>32,140,649,000</b>	<b>15,807,996,517.40</b>	<b>49.1</b>

**Chanzo: Randama ya Wizara (2019)**

**2.4 Maelezo kuhusu Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, Kamati ilifanya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 katika Wizara hii ambayo ina mafungu mawili kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, Idara Kuu Afya - Fungu 52 ilitengewa kiasi cha **shilingi 561,759,999,000.00**. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **shilingi 376,800,000,000.00** ambayo ni sawa na **asilimia 67** ni kutoka vyanzo vya ndani na kiasi cha shilingi **184,959,999,000.00** sawa na **asilimia 33** ni fedha kutoka vyanzo vya nje kwa maana ya Wahisani wa maendeleo wanaotoa mchango wao katika Sekta ya afya kupitia Mfuko wa Dunia wa kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria (Global Fund), Benki ta Dunia na wengine.

Aidha, kupitia **Fungu 53** Fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi mbalimbali ya Maendeleo Wizara ilitengewa kiasi cha shilingi **4,913,845,000.00** ambapo kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi **1,500,000,000** sawa na **asilimia 43.9** ya fedha iliyotengwa ni kutoka vyanzo vya ndani na **asilimia 56.1** ni fedha kutoka kwa Wahisani mbalimbali wa Maendeleo wakiwemo UNDP.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na uwepo wa miradi mingi iliyo sehemu mbalimbali nchini, kutokana na muda uliotengwa kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Toleo la Januari 2016, Kamati ilifanikiwa kufanya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo miwili (2) iliyo katika mkoa wa Dar es salaam na Pwani. Miradi hiyo ni kama ifuatavyo;

a) **Mradi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mwananyamala - Dar es salaam (Namba ya Mradi 5411 – Fungu 52);**

**Mheshimiwa Spika**, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mwananyamala ni moja kati ya Hospitali za Rufaa 28 ambazo zilitengewa kiasi cha shilingi **Bilioni 30** kwaajili ya ununuzi wa vifaa, vifaa tiba na ukarabati. Hadi Kamati inatembelea Hospitali hii, hakuna fedha yoyote iliyokuwa imepelekwa na Serikali. Kamati ilipohoji ilielezwa kuwa, malengo ya fedha hizo yalikuwa ni shilingi **Bilioni 10** ziende kwenye ujenzi wa Hospitali Mpya za Mikoa 6 ambayo ni Katavi, Njombe, Simiyu, Songwe, Geita na Mara na shilingi **Bilioni 20** zilizopangwa ziende kukarabati Hospitali za Rufaa 23.

**Mheshimiwa Spika**, hata hivyo, kutokana na ufinyu wa bajeti na changamoto zilizopo kwenye Hospitali za Rufaa za Mikoa yote, ilionekana ni vyema fedha zote **Bilioni 30** ziende kwanza kujenga Hospitali hizo mpya za Mikoa kwa ukamilifu wake na fedha zitakazoombwa kwa miaka ijayo ndiyo ziende kukarabati Hospitali za Rufaa zilizosalia. Mpaka Kamati inafanya ziara ilielezwa kwamba, kati ya fedha hizo **Bilioni 30** ni shilingi **Bilioni 6.5 tu sawa na asilimia 21.6** ndiyo zimepatikana na yalitolewa maelezo kuwa, Serikali imeahidi kiasi kilichobaki (**Bilioni 23.5**) kitatolewa kabla ya mwaka fedha wa 2018/2019 kuisha.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa na kujionea Mradi wa Jengo la ghorofa tano la kutolea Huduma za afya kwa wateja wa Bima ambao ulikuwa ukitekelezwa na Ofisi ya Kata ya Mwananyamala chini ya Ofisi ya Mhandisi wa Manispaa Kinondoni. Mradi huo ambao awali gharama zake zilikadiriwa kuwa kiasi cha shilingi **Bilioni 1.7** ambao ulianza kutekelezwa katika Mwaka wa fedha 2014/2015 kwa kutumia fedha za

*Local Government Capital Development Grant* na tayari **shilingi Milioni 485** zilikuwa zimepokelewa, kati ya hizo **Milioni 419** zimetumika kujenga Msingi wa Jengo pamoja na ghorofa ya kwanza na ya pili na shilingi **Milioni 65** zipo kwenye Akaunti ya Kata ya Mwananyamala.

**Mheshimiwa Spika**, Ujenzi huu umeshindwa kuendelea kutokana na kukosekana kwa fedha. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa kwa hesabu za sasa, gharama za Mradi huo ni shilingi **Bilioni 3** ikiwa ni ongezeko la shilingi **Bilioni 1.3** sawa na ongezeko la **asilimia 76** la makadirio ya awali. Mradi huu ni Mradi wa pili kati ya Miradi ambayo Kamati imeitembelea ambayo gharama zake zimeongezeka kutokana na kuchelewa kutolewa kwa fedha kwa wakati. **Kamati inasikitishwa na hali hii na inaona Serikali inapaswa kujifunza kutokana na makosa haya na kuanza kuyarekebisha.**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Hospitali ya Rufaa ya Mwananyamala, Kamati ilishuhudia msongamano mkubwa wa wagonjwa hususan katika Wodi za Watoto na Wanawake. Kwa mfano katika Wodi ya watoto chini ya miaka 5 na ile ya watoto wachanga zenye vitanda 20 kila wodi ikiwa na watoto zaidi ya 40 kwa wale wa chini ya miaka 5 na watoto zaidi ya 100 kwa wale wachanga hali iliyolazimu kitanda kimoja kuwa na wagonjwa zaidi ya mmoja na wengine kulala chini. **Kamati inaona kuna haja ya hatua za haraka kuchukuliwa ili kupunguza msongamano huu.**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na changamoto hii, Kamati ilielezwa changamoto nyingine kama vile uchakavu wa miundombinu inayohitaji ukarabati mkubwa, ukosefu wa nyumba za watumishi, ukosefu wa huduma za ufuaji na mlolongo mrefu wa manunuzi maalumu katika Bohari ya Dawa hasa kwenye vitendanishi vya Maabara.

**b) Mradi wa Uimarishaji wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Pwani - Tumbi (Namba ya Mradi 5411 – Fungu 52);**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea Hospitali hii ambayo hapo awali kabla ya kuhamishiwa Wizara ya Afya, ilikuwa ni



Hospitali Maalum ikisimamiwa na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kutokana na kazi kubwa iliyokuwa inaifanya ya kuhudumia majeruhi waliokuwa wakipata ajali katika maeneo mbalimbali hususan katika kipande cha barabara ya Dar es salaam na Chalinze na ilikuwa chini ya Shirika la Elimu Kibaha. Kamati ilielezwa kuwa, Serikali ilikuwa inatenga fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwa ajili ya uboreshaji wa huduma katika Hospitali hiyo. Mnamo Mwezi Julai, 2018, Hospitali ya Tumbi-Kibaha ilihamishiwa usimamizi wake katika Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kama zilivyokuwa Hospitali nyingine za Rufaa za Mikoa.

**Mheshimiwa Spika**, Hospitali ilianza kutekeleza Mradi wa Upanuzi wa Hospitali wenye thamani ya shilingi **Bilioni 20** katika Mwaka wa fedha wa 2008/2009 na shilingi **Bilioni 3.5** zilitolewa katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 kwaajili ya ujenzi wa hatua ya kwanza uliohusisha msingi, ghorofa ya kwanza na ghorofa ya pili na ulikamilika. Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 bajeti ya shilingi **Bilioni 5.7** iliidhinishwa na Bunge lako Tukufu lakini fedha iliyotolewa ni **Milioni 800** zilizowezesha Mkandarasi kutekeleza kazi hiyo kwa **asilimia 20** tu ambao ni ujenzi wa msingi na Mkataba huu ulivunjwa na Hospitali na kumlipa Mkandarasi faini ya shilingi **Milioni 200** kwa mujibu wa masharti ya Mkataba.

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha wa 2016/2017 Hospitali iliidhinishwa shilingi **milioni 610** kwaajili ya ujenzi wa njia ya kuwezesha wagonjwa kupita kwa urahisi (ramp) na maegesho ya magari ambapo kiasi cha shilingi **Milioni 305** kilipokelewa na Kamati ilishuhudia ujenzi ukiwa katika hatua za mwisho.

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha wa 2017/2018 Hospitali iliidhinishwa shilingi **Bilioni 3.9** ambayo iliingizwa katika akaunti ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Pwani (RAS). Kutokana na mvutano kati ya Ofisi ya RAS-Pwani na Shirika la Elimu Kibaha kuhusu matumizi ya fedha hizo kumekuwa na mgogoro hali iliyofanya kiasi hicho cha fedha kushindwa kutolewa na kutumika kama ambavyo ilikuwa imepangwa.

Mpaka Kamati inatembelea Mradi fedha hizo zilikuwa hazijatoka kutokana na mgogoro huo uliosababisha pia ukiukwaji wa taratibu za fedha na hivyo fedha hizo kurejeshwa Hazina.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imesikitishwa na hali ya kutoelewana kulikosababisha kiasi cha shilingi **Bilioni 3.9** zilizodihinishwa na Bunge katika mwaka wa fedha wa 2017/2018 kushindwa kutumika na hivyo kufanya Mradi huu kuchelewa kukamilika na kuwanyima wananchi wa Mkoa wa Pwani na wa maeneo mengine kupata huduma bora zaidi za afya. Kamati ilibaini pia taarifa iliyowasilishwa kuwa na mkanganyiko mkubwa wa uandishi na takwimu hali iliyolazimu kuelekeza Taarifa iandaliwe vizuri na iwasilishwe kwenye Kamati ili kujua ukweli wa Mradi huu.

Aidha, kuhusu hali ya upatikanaji wa fedha katika mwaka wa fedha wa 2018/2019, kama ilivyokuwa kwa Mradi wa Uimarishaji wa Hospitali ya Rufaa ya Mwananyamala, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Pwani –Tumbi nayo haijapelekewa fedha kutokana na sababu zile zile.

## **2.5 Matokeo na Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya Kamati kufanya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018 kama ambavyo taarifa yake imeeleza, Kamati inatoa Ushauri ufuatao;

### **a) Upatikanaji wa Fedha**

Kama ilivyoelezwa kwenye Taarifa ya Miradi, hakuna fedha yoyote iliyopokelewa kwa miradi ambayo Kamati iliitembelea na kuikagua. **Kamati inaona kuna umuhimu na ulazima kwa Serikali kuhakikisha inapeleka kwa fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu ili kufikia malengo ambayo tumejiwekea.**

**b) Uhaba wa Watumishi**

Uhaba wa Watumishi wa Afya nchini ni takribani asilimia 50. Kamati imeshuhudia uhaba huu katika Taasisi za Afya kama vile Hospitali ya Mwanayamala ambayo ina upungufu wa watumishi kwa **asilimia 47. Kamati inashauri Serikali kuiangalia Hospitali hii na Hospitali nyingine zenye upungufu na kuzipa umuhimu wa kipekee wa kuzipatia wataalam wa kutosha.**

**c) Motisha kwa Watumishi wa Afya**

Kamati imebaini kuwa changamoto ya malipo mbalimbali zikiwemo motisha ya posho ya nyumba, motisha ya masaa ya ziada kwa watumishi wa afya ni kubwa na inaweza athiri utendaji kazi wao. **Kamati inashauri Serikali kulibeba suala hili kipekee na kulitafutia ufumbuzi wa haraka. Aidha, kwa Hospitali ya Mwananyamala ambayo haina nyumba hata moja ya watumishi, Kamati inashauri Serikali kuharakisha ujenzi wa nyumba za watumishi katika Hospitali hiyo na hospitali nyingine yenye changamoto kama hizi ili kuboresha upatikanaji wa huduma za afya kwa haraka.**

**d) Ukosefu na usahihi wa Takwimu**

Kumekuwa na changamoto ya ukosekanaji wa takwimu sahihi katika taasisi mbalimbali za Serikali hasa za afya ambazo Kamati inaamini ndiyo msingi wa upangaji wa maendeleo katika taasisi hizo. Katika Miradi ambayo Kamati imeitembelea na kupokea Taarifa yake imebainika dhahiri kuwa kuna ukosefu wa takwimu na zile zilizopo nyingi siyo sahihi, **Kamati inaona hili si jambo jema. Na hivyo inashauri Serikali kuzisimamia Taasisi zake na kuhakikisha zinakuwa na takwimu za kutosha na zilizo sahihi ili kuweza kupanga mipango yake kwa ukamilifu.**

**3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020.**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha wa 2019/2020 Wizara inatarajia kutekeleza malengo mbalimbali kupitia **Fungu 52 & 53** kama ambavyo imeainishwa katika Mpango

wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2019/2020 iliyotafsiriwa katika mikakati mbalimbali ya Wizara


### 3.1 Uchambuzi wa Ukusanyaji wa Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020, Wizara kupitia Fungu 52 inakadiria kufanya makusanyo ya jumla ya **shilingi 250,290,247,988.00** kutoka katika vyanzo mbalimbali vya Wizara pamoja na Taasisi zake. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, Makusanyo ya mwaka huu wa fedha ni ongezeko la kiasi cha shilingi **10,247,739,831.00** sawa na **asilimia 4.2** ikilinganishwa na makadrio ya makusanyo kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019. **Kamati inapongeza Wizara kwa kuendelea kuongeza Makadirio ya Makusanyo.**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa katika makusanyo hayo, kiwango kidogo cha makusanyo kinategemewa kutoka katika Baraza la Mazingira ambapo kiasi cha **shilingi 59,949,955** kinakadiriwa kukusanywa. Aidha, fedha nyingi zinatarajiwa kukusanywa kutoka katika **Hospitali ya Taifa Muhimbili** ambapo kiasi cha **shilingi 53,342,538,765** kinatarajiwa kukusanywa kutokana na uchangiaji wa huduma za afya katika Hospitali hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Fungu 53 (Idara Kuu Maendeleo ya Jamii) inakadiria kufanya makusanyo ya kiasi cha **shilingi 4,763,596,000,000** kutoka katika vyanzo vya ada za wanafunzi wa Vyuo nane vya Maendeleo ya Jamii, Chuo cha ustawi wa jamii Kisangara pamoja na ada na tozo za usajili wa mashirika yasiyo ya Kiserikali. Kiasi cha makadirio haya ni ongezeko la kiasi cha **shilingi 1,672,800,000** sawa na **asilimia 35** ya makadirio ya mwaka wa fedha wa 2018/2019 ya **shilingi 3,090,796,000.00**. **Kamati inapongeza jitihada hizi za kuongeza Makadirio ya makusanyo ya maduhuli na ina amini kufikia mwisho wa mwaka wa fedha 2019/2020 lengo litakuwa limefikwa.** Kielelezo Na. 3 kinaonesha ulinganisho wa Makusanyo ya Maduhuli kati ya Mwaka 2018/2019 na 2019/2020 kwa mafungu yote mawili (Fungu 52- Idara Kuu Afya na Fungu 53- Idara Kuu Maendeleo ya Jamii).

**Kielelezo Na. 3: Ulinganisho wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli**



**Chanzo: Randama za Wizara (2019) na Usanifu wa Kamati**

**3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha wa 2019/2020 Wizara inatarajia kutekeleza malengo mbalimbali kupitia **Fungu 52 & 53** kama ambavyo imeainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2019/2020 iliyotafsiriwa katika mikakati mbalimbali ya Wizara.


**Mheshimiwa Spika**, kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake yaliyo chini ya Fungu 52 (Idara Kuu Afya), Wizara imekadiria kutumia kiasi cha shilingi **959,152,164,597.00** kati ya fedha hizo shilingi **415,014,262,000.00** sawa na **asilimia 43.3** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikiwemo Mishahara (PE) na Matumizi Mengineyo (OC) na shilingi **544,137,902,597.00** sawa na **asilimia 56.7** ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa, Makadirio haya ya fedha ni ongezeko la **asilimia 9.7** ikilinganishwa na bajeti ya Fungu 52 kwa mwaka wa fedha uliopita wa 2018/2019. **Kamati inapongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza Bajeti ya Fungu hili.** Pamoja na ongezeko hilo la

bajeti, hata hivyo, Kamati imebaini kuwa kuna baadhi ya Taasisi zimefunguziwa fedha ikilinganishwa na mwaka wa fedha wa 2018/2019. Baadhi ya Taasisi hizo ni pamoja na Bohari Kuu ya Dawa ambayo bajeti yake imefungua kutoka shilingi **Bilioni 240 mwaka 2018/2019** hadi shilingi **Bilioni 200** mwaka 2019/2020 sawa na upungufu wa **asilimia 16**.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia, Fungu 53 (Idara Kuu Maendeleo ya Jamii) kwa Mwaka wa Fedha wa 2019/2020 imekadiria kutumia kiasi cha **shilingi 31,537,431,013.00** kati ya fedha hizo kiasi cha **shilingi 28,777,370,000.00** sawa na **asilimia 91.2** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambayo ni Mishahara (PE) na Matumizi Mengineyo (OC) na **shilingi 2,760,061,013.00** sawa na **asilimia 8.7** ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya Fedha za kutekeleza Miradi ya Maendeleo **asilimia 33** inategemea fedha kutoka kwa wahisani na **asilimia 67** ni fedha za ndani. Idara pamoja na kuwa na Miradi inayohitaji fedha lakini fedha zinazotengwa kwa ajili ya Maendeleo ni kidogo kama inavyooneshwa kwenye kielelezo Na.4

#### Kielelezo Na.4 Mchanganuo wa Bajeti ya Fungu 53 kwa Mwaka 2019/2020




Chanzo: Randama ya Wizara (2019) na Usanifu wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati unaonesha kuwa, Makadirio haya ya fedha kwa mwaka huu yamepungua kwa takribani **asilimia 1.8** ikilinganishwa na makadirio ya Fungu 53 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ya kiasi cha **shilingi 32,140,649,000**. Pamoja na kupungua kwa bajeti yote ya Fungu 53 kwa mwaka wa fedha 2019/2020, bajeti ya Matumizi Kawaida imeongezeka kwa shilingi **Bilioni 1.5** sawa na **asilimia 5.6** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2018/2019. Kwa upande wa fedha za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, Kamati imebaini kuwa fedha zimepungua kutoka shilingi **Bilioni 4.91** mwaka 2018/2019 hadi kufikia shilingi **Bilioni 2.76** mwaka 2019/2020 sawa na upungufu wa **asilimia 43.78**. **Kamati inaona hili siyo jambo jema hasa ikizingatiwa Wizara hii ina miradi ambayo ni muhimu hata hivyo imekuwa haitengewi fedha za kutosha na wakati mwingine zimekuwa hazitolewi kama vile Taasisi ya Ustawi wa Jamii Kijitonyama na Vyuvo vya Maendeleo ya Jamii.**

**Mheshimiwa Spika** Kielelezo Na. 5 Kinaonesha Ulinganisho wa Bajeti kwa Mwaka 2018/2019 na 2019/2020

**Kielelezo Na. 5: Ulinganisho wa Bajeti (Fungu 52 na 53) kwa Mw**



**Chanzo: Randama ya Wizara (2019) na Usanifu wa Kamati**

## SEHEMU YA TATU

---

### 4.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilimaliza kufanya Uchambuzi wake kwa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2019/2020 katika mafungu yote yaliyo chini ya Wizara hii. Kufuatia uchambuzi huo, Kamati inatoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo kama ifuatavyo;

### 4.1 Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2019/2020

**Mheshimiwa Spika**, Utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, unategemea Bajeti iliyotengwa ambalo ni jambo moja lakini jambo la pili ni upatikanaji wa fedha hizo zote na kwa wakati ili kuweza kutekeleza kikamilifu majukumu yake. Bajeti ya Wizara kupitia Fungu 52 imeongezeka kwa **asilimia 9.6** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2018/2019. **Kamati inaipongeza Serikali kwa ongezeko hilo la bajeti. Hata hivyo inaendelea kuisisitiza Serikali kuitoa fedha hiyo yote na kwa wakati kama ilivyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kuhakikisha shughuli zilizopangwa zinatekelezeka kwa wakati.**

### 4.2 Upatikanaji wa Dawa Muhimu (*Essential Medicines*) kwa wagonjwa

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua jukumu la kununua, kutunza na kusambaza wa dawa hapa nchini ni jukumu la Bohari Kuu ya Dawa ambayo inatekeleza majukumu yake kwa weledi mkubwa na kuhakikisha dawa, vifaa na vifaa tiba vinakuwepo katika maghala yao yote hapa nchini. Kamati inaipongeza Bohari Kuu ya Dawa kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yao licha ya changamoto ya uhaba wa fedha kutoka Serikalini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua utoaji wa huduma za afya ni pamoja na upatikanaji wa dawa kwa mgonjwa. Kamati imebaini changamoto kubwa ipo katika vituo vya kutolea huduma za afya inayotokana na utoaji wa orodha ya dawa hasa dawa muhimu pasipokuzingatia mahitaji ya



kituo cha kutolea huduma ya afya. Kwa mujibu wa Takwimu za Wizara, maoteo ya mahitaji halisi ya Dawa kwa Mwaka ni **Trilioni 1.4** lakini bajeti inayotengwa kwa wastani ni shilingi **Bilioni 250** na ambazo utolewaji wake umekuwa hauzidi asilimia 50.

**Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati kuwa;**

- a) **Ni muhimu vituo vya kutolea huduma ya afya kuanzia ngazi ya Zahanati hadi Hospitali za Rufaa kuzingatia mahitaji ya dawa ya kituo ili kuondokana na ukosefu wa dawa muhimu katia vituo hivyo; na**
- b) **Serikali ione umuhimu wa kuongeza Bajeti ya Dawa na kuhakikisha zote zinatolewa kwa wakati.**

#### **4.3 Uwepo wa Wahudumu wa Afya ngazi ya Jamii (Community Health Workers)**

**Mheshimiwa Spika**, wote tunafahamu kinga ni bora kuliko tiba. Kamati inatambua umuhimu wa Wahudumu wa Afya ngazi ya Jamii (*Community Health Workers*) ambao wanajukumu la kuhamasisha jamii katika masuala mbalimbali ya afya kama vile lishe bora, wanawake wajawazito kuhudhuria kliniki na kujifungulia katika vituo vya kutolea huduma ya afya, matumizi ya vyandarua, umuhimu wa kunywa maji safi na salama, umuhimu wa kuwa na vyoo. Si hivyo tu lakini Wahudumu wa Afya ngazi ya Jamii wana jukumu la kutoa huduma za afya kama vile kutoa huduma ya kwanza kwenye jamii.

**Mheshimiwa Spika** tuna mifano mizuri ya Nchi ya Rwanda ambayo imefanikiwa kupunguza vifo vya watoto chini ya miaka mitano, vifo vya wajawazito na vifo vingine vitokanavyo na na magonjwa kama malaria, numonia na kuhara katika jamii kutokana na uwepo wa hawa Wahudumu wa Afya ngazi ya Jamii.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inafahamu kuwa, hapa nchini kuna Wahudumu wa Afya ngazi ya Jamii takribani 13,000 hawana ajira. Aidha, Kamati inafahamu pia kuwa Makadirio

ya Bajeti ya Mishahara kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 hayajagusia ajira wala motisha kwa Wahudumu wa Afya ngazi ya Jamii kitu ambacho Kamati inaona ni kinyume na Makadirio ya Mpango Mkakati wa Afya wa Nne yaliyolenga kurasimisha ajira 5000 za Wahudumu wa Afya ngazi ya Jamii ifikapo 2020. Kamati inaona hili siyo jambo jema kwani inatambau kuwa ajira za Wahudumu wa Afya ngazi ya Jamii ni sehemu ya mkakati wa kupunguza vifo vya akina mama wajawazito na watoto chini ya miaka mitano.

**Mheshimiwa Spika, Kutokana na umuhimu huu Kamati inaendelea inashauri Serikali itoe ajira za CHWs ili kusaidia kuboresha huduma za mama na mtoto katika ngazi ya jamii**

#### **4.4 Mikakati ya kuzuia magonjwa yasiyoambukiza (*Non communicable Diseases*)**

**Mheshimiwa Spika**, tafiti zinaonesha kuwa, katika miaka kumi iliyopita tishio kubwa lilikuwa ni magonjwa ya kuambukiza ambayo ndiyo yaliyokuwa yanatishia maisha ya watu wengi. Kwa miaka ya hivi karibuni, tafiti zinaonesha kuwa kuna ongezeko kubwa la magonjwa yasiyoambukiza yakiwemo Saratani, shinikizo la damu, kisukari na mengine ambayo husababishwa na watu kutofanya mazoezi, ulaji usiozingatia kanuni za afya, msongo wa mawazo kutokana na hali za kiuchumi, kutopata matibabu mapema kwa magonjwa yayayoambukiza na sababu nyingine.

**Mheshimiwa Spika**, Magonjwa haya yanaongeza gharama kubwa za muda na rasilimali fedha kwa Serikali katika kuwatibu na mengi yanakuwa ni matibabu ya maisha yote kuanzia pale mtu anapogundulika na kuwa na magonjwa hayo. **Ni maoni ya Kamati kuwa;**

a) **Serikali iweke mipango madhubuti ya kuelimisha jamii juu ya manufaa na namna bora ya kuzuia magonjwa badala ya kusubiri mpaka ugonjwa unakuja kutambulika; na**

b) **Serikali ifanye kampeni kubwa ya uhamasishaji wa jamii wa kufanya mazoezi kila wiki au mwezi kwa ngazi zote,**

**namna bora ya kupata lishe bora na kuwahi kufika katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa magonjwa yanayoambukizwa ili yasisababishie madhara ya kupata magonjwa yasiyoambukiza.**

#### **4.5 Upatikanaji wa Huduma Bora na Uhakika za Uzazi**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua mikakati mbalimbali ya Serikali katika kuhakikisha inatoa huduma bora na za uhakika za uzazi ili kuweza kupunguza changamoto mbalimbali zitokanazo na uzazi zikiwemo vifo vya mama na mtoto. Vifo hivi vingi vimekuwa vinatokana na utokwaji wa damu nyingi, uzazi pingamizi, kuharibika kwa mimba, kifafa cha mimba na kukosa msaada wa mtaalamu katika vituo vya kutolea huduma za afya. Takwimu zinaonesha kuwa akina mama 24 wanapoteza maisha kila siku hapa nchini kutokana na matatizo haya ya uzazi. Aidha, takwimu zinaonesha kuwa Sekta ya Afya ina upungufu wa watumishi kwa **asilimia 48**. Changamoto zote hizi bado zinaendelea kugharimu maisha ya watanzania walio wengi hasa wale wanaoishi katika maeneo ambayo hayana huduma za uhakika.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na changamoto hizi Kamati inashauri;

- a) Serikali ifanye uboreshaji wa huduma za uzazi katika maeneo mbalimbali yenye changamoto hizo;
- b) Serikali ihakikishe inaweka vifaa vya kisasa na watoa huduma pamoja na kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa wanawake wajawazito kwenda kujifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya ili kuweza kupunguza idadi ya vifo vya mama na mtoto; na
- c) Serikali na hususan UTUMISHI ione umuhimu wa kutoa vibali vya Ajira ili Wizara iweze kuajiri watumishi wa kutosha wakiwemo Madaktari bingwa.

#### 4.6 Uanzishwaji wa Bima ya Afya kwa Wote (*Universal Health Coverage*)

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kipindi kirefu sasa Kamati imekuwa ikiisistiza Serikali kuharakisha mchakato wa Bima ya Afya kwa wote ili kuondokana na changamoto ya wananchi kukosa huduma ya afya kutokana na changamoto ya kifedha. Aidha, taarifa zinaonesha kuwa ni **asilimia 33** tu ya wananchi ndiyo wanaopata huduma ya afya kwa kutumia mfumo wa Bima ya afya ambapo kati ya hao ni **asilimia 7** tu ndiyo wanaopata huduma kupitia Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa, **asilimia 25** kupitia mfuko wa afya ya jamii na **asilimia 1** ni kutoka Bima binafsi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mantiki hiyo ni zaidi ya **asilimia 60** ya wananchi wa Tanzania hawana uhakika wa kupata huduma ya afya kwa kuwa upatikanaji wa huduma ya afya kwao unategemea na upatikanaji wa fedha. Ni maoni ya Kamati kuwa hali hii inawasababishia kukosa haki ya msingi ya afya na kuwafanya wengine hata kupoteza maisha yao kwa kukosa huduma ya afya pale wanapougua.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kukamilisha mchakato wa uletwaji wa Muswada wa Sheria ya Bima ya afya kwa wote Bungeni, ili iweze kuwa Sheria na kuanza utekelezaji kwa kuhakikisha kila mwananchi afya yake inalindwa kwa kuwa na Bima ya Afya ya uhakika. Aidha, wakati mchakato huo unaendelea Serikali ianze kupanga mikakati ya namna gani watahamasisha jamii kwa ajili ya kuelewa umuhimu wa bima hiyo ili wakati wa utekelezaji kusiwepo na changamoto ya kutokubali licha ya uwepo wa sheria.

#### 4.7 Uimarishaji wa Mikakati ya Kuzuia Magonjwa yatokanayo na uhaba wa maji na uchafu wa mazingira

**Mheshimiwa Spika**, Ni dhahiri kuwa maji ni uhai na kila mtu anafahamu kuwa pasipo na maji ya uhakika kwa mwanadamu madhara yake ni makubwa sana ikwemo

mlipuko wa magonjwa mbalimbali kama vile kipindupindu, kuhara na kuhara damu, magonjwa ya njia za mkojo (UTI) na upele yakitajwa kwa uchache wake. Magonjwa haya yanaenda sambamba na mazingira machafu yanayosababishwa na kujisaidia sehemu za wazina kuoelekea kusambaa kwa vinyesi na kwenda kuchafua mazingira yakiwemo maji yanayotumiwa na binadamu.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa wataalamu wa afya, magonjwa ya tumbo kikiwemo kipindupindu yataepukika endapo kutakuwepo na maji safi na salama wakati wote. Si hivyo tu, lakini pia pale watu watakapotunza mazingira yao (uwepo wa vyoo bora kwa kila kaya na kuvitumia kwa usahihi), Usafi binafsi ikiwemo kunawa mikono wanapotoka chooni na hata kuoga kila siku.

**Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Maji na Usafi wa Mazingira ni sekta mtambuka ambapo Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inawajibika katika kusimamia na kutekeleza miradi ya maji na usafi wa mazingira kwa ujumla wake. Wizara hii ni mlango mkuu wa matumizi makubwa ya bajeti ya Afya kwa maana ya ununuzi wa dawa kwa ajili ya kutibu magonjwa yatokanayo na uhaba wa maji na uchafu wa mazingira ikiwemo kuhara na kuhara damu hasa kwa watoto chini ya miaka mitano.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kwamba, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inatekeleza mikakati mbalimbali ya usafi wa mazingira ikiwemo uendeshaji wa kampeni ya ujenzi wa vyoo bora katika kila kaya ijulikanayo kama "**Kampeni ya Nyumba ni Choo**". Kampeni hii imesaidia watu kujenga vyoo bora na hatimaye kutojisaidia katika maeneo ya wazi na hivyo kuepuka magonjwa ya mlipuko. Kampeni ya "**Nyumba ni Choo**" imekuwa na mafanikio makubwa kwani Wizara ilifanya uamuzi sahihi wa kushirikisha wadau mbalimbali ikiwemo sekta binafsi, vyombo vya habari kama vile **Clouds Media**, mitandao ya kijamii na wasanii wakubwa akiwemo **Mrisho Mpoto** katika kuwafikia wananchi wote wa hali na rika tofauti

kwa ajili ya kufikisha ujumbe wa umuhimu wa matumizi sahihi ya choo.

**Mheshimiwa Spika**, athari za kujisaidia katika maeneo ya wazi ni uchafuzi mkubwa wa mazingira kwa tani za vinyesi kwa mwaka mzima (siku 365) kwa wastani wa nusu kilo kwa mtu mmoja kwa siku kuzagaa kama Kielelezo Namba 6 kinavyoonesha.

**Kielelezo Na. 6 Uzalishaji wa kinyesi (Kilo) kwa kwa siku, wiki, mwezi na Mwaka**

Na.	Maelezo	Uzalishaji kwa siku	Jumla (kgs)
1.	Mtu 1 kwa siku anazalisha kinyesi wastani wa nusu kilo	Kilo0.5xMtu1	Kilo 0.5
2.	Kaya ya wastani watu 4 kwa siku	Kilo0.5x watu4	Kilo 2
3.	Kijiji chenye wastani wa kaya 300 kwa siku 1	Kilo2x kaya.300	Kilo 600
4.	Kijiji chenye wastani wa kaya 300 kwa wiki (Siku 7)	Kilo600x siku 7	Kilo 4200
5.	Kijiji chenye wastani wa kaya 300 kwa mwezi (Wiki 4)	Kilo 4200 X wiki 4	Kilo 16,800
6.	Kijiji X kwa mwaka (miezi 12)	Kilo16,800 X miezi 12	Kilo 201,600

**Chanzo: Usanifu wa Kamati, 2019**

**Mheshimiwa Spika**, kwa hesabu za haraka kijiji chenye kaya 300 kwa mwaka kinazalisha kinyesi cha tani 201.6 sawa na malori 10 ya tani 20 yanasambaza kinyesi katika kijiji hicho. Maswali ya kujiuliza Tanzania ina vijiji vingapi ambavyo havina vyoo bora au matumizi ya vyoo vilivyopo ni hafifu? Kamati inaona hili ni changamoto kubwa sana katika jamii yetu.

**Mheshimiwa Spika**, Takwimu zinaonesha kuwa vifo vingi vya watoto chini ya miaka mitano vinaongozwa na magonjwa mbalimbali ikiwemo kuhara na kuhara damu ikiwa ni ugonjwa namba tatu unaopelekea mwili kupoteza maji mengi na hatimaye kusababisha kifo. **Kamati inatambua juhudi za Serikali katika kuhakikisha kunakuwa na maji safi na salama pamoja na usafi wa mazingira. Aidha, kamati inaishauri**

Serikali kuhakikisha inaunganisha nguvu kati ya Wizara ya maji, Wizara ya mazingira, Wizara ya Elimu kwa maana (Shule) na Wizara ya Afya kwa ajili ya kuweka afua fungamanishi (Integrated interventions) kwa ajili ya kutatua matatizo ya maji na uchafu wa mazingira hatimaye kuondokana na tatizo la magonjwa yatokanayo na uhaba wa maji na mazingira machafu.

**Mheshimiwa Spika**, Kuna msembo wa Slovakia unasema naomba kunukuu *“Pure Water is the World’s First and Foremost Medicine.”* Kwa tafsiri isiyo rasmi ni kwamba, maji safi ni dawa ya kwanza duniani. Kwa mantiki hiyo ni wito wa Kamati kwa Serikali kwamba ni lazima kutafutia wananchi dawa hiyo ya kwanza ili wananchi waweze kupona magonjwa yatokanayo na uhaba wa maji na uchafu wa mazingira katika maeneo yao wanayoishi.

**Mheshimiwa Spika**, ifahamike kuwa kinga ni bora kuliko tiba, ni vyema kuhakikisha kunakuwa na maji safi na salama katika mazingira safi ili kuweza kunusuru afya za watanzania. Kwa kufanya hivyo, Wizara itaokoa fedha nyingi za dawa kwa ajili ya kutibu magonjwa ya tumbo, kuhara na kuhara damu, kipindupindu na hata kupunguza mzigo mkubwa wa wagonjwa wanaolazwa katika hospitali hasa watoto chini ya miaka mitano na kubaki na yale magonjwa mengine yasiyotokana na maji na usafi wa mazingira

#### 4.8 Uimarishaji wa Huduma za Lishe

**Mheshimiwa Spika**, Lishe kwa binadamu inapaswa kuangaliwa kuanzia kipindi cha mimba inapotungwa (kwa wajawazito) mpaka mtoto anapozaliwa, kipindi cha miaka mitano na hadi anapokuwa mtu mzima. Umuhimu wa lishe ni pamoja na ukuaji wa akili ya mtoto (*Cognitive Development*) ambayo ikikosewa wakati wa ujauzito na ukuaji wa mtoto kwa kipindi cha miaka mitano ya awali, basi madhara yake yataonekana mtoto anapokuwa shule na hata baada ya shule kwa maana ya utekelezaji wa majukumu yake akiwa mtu mzima.

**Mheshimiwa Spika**, licha ya umuhimu huo wa lishe kwa mtoto, taarifa zinaonesha kuwa Tanzania tumekuwa tukitenga kiasi cha shilingi elfu moja tu (**Tsh.1000**) sawa na **dola za Marekani 0.5** ambayo ni chini ya makubaliano ya kimataifa ya **dola 8.5** za Marekani kwa kila mtoto kwa ajili ya lishe. Kwa mantiki hiyo, Serikali imefanikisha kutenga kwa **asilimia 5.8** tu ya makubaliano yaliyowekwa. Kiasi hiki hakiridhishi hata kidogo, kwani tunaziweka afya za watoto katika hatari kubwa.

**Mheshimiwa Spika**, Ni rai ya Kamati kwamba, ni wakati sasa Serikali kutoa kipaumbe kwa suala la lishe kwa watoto hasa wale chini ya miaka mitano ikiwemo kuhakikisha zinatolewa dawa za minyoo, virutubisho katika vyakula vyao na matone ya vitamin A. Lakini kama hii haitoshi, Wizara ihakikishe kwamba kunakuwa na kampeni kubwa ya kuhakikisha hakuna mtoto anafariki kwa kukosa lishe bora. Haya yote yanaweza kufanyika kwa kutenga fedha za kutosha angalau dola nne kwa kila mtoto ili angalau kupunguza tatizo la udumavu, utapiamlo ambalo madhara yake ni makubwa hapo baadae kwa Taifa hili, kwani watoto wa leo ni taifa la kesho.

#### 4.9 Mapambano ya dhidi ya Virusi vya UKIMWI na Upungufu wa Kinga Mwilini (VVU/UKIMWI)

**Mheshimiwa Spika**, Mapambano dhidi ya UKIMWI yanafanyika na wadau mbalimbali wa UKIMWI wa ndani na nje ya nchi. Kwa mujibu wa taarifa ya **National HIV Impact Survey, 2016/2017** maambukizi mapya kwa mwaka ni **watu 72,000** kwa maana nyingine ni kwamba, maambukizi kwa siku ni watu **197**. Takwimu hizi zimegawanywa katika makundi ya rika na katika makundi hayo ya umri, kundi ambalo linaongoza kwa maambukizi kwa kiasi kikubwa ya Virusi vya UKIMWI ni kundi la vijana wenye umri wa kati ya miaka 15 - 24 kwa **asilimia 49** na katika kundi hilo wasichana wanaongoza kwa asilimia kubwa ikilinganishwa na wavulana.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Mkakati wa Serikali wa kupata **Tisini tatu 90 -90-90** kwa maana ya **asilimia 90** ya watu wote wanaokisiwa kuishi na Virusi Vya UKIMWI wanatambua hali



zao za maambukizi, kuhakikisha **asilimia 90** kati yao wanatumia dawa za kufubaza makali ya Virusi Vya UKIMWI (ARVs) na **asilimia 90** ya wanaotumia dawa kwa usahihi kuhakikisha dawa hizo zinawawezesha kufubaza Virusi vya UKIMWI. Kwa mantiki hiyo, mlango mkuu ni asilimia 90 ya kwanza ndiyo itakayowawezesha Serikali kufikia malengo ya asilimia 90 ya pili na ya tatu kwa kuwa hizi mbili zinategemea 90 kwanza.

**Mheshimiwa Spika**, Katika utekelezaji wa afua za UKIMWI ikiwemo upimaji wa virusi vya UKIMWI kwa hiari ili kuweza kuifikia asilimia 90 ya kwanza kumekuwa na vikwazo mbalimbali katika utekelezaji wake ikiwemo ukinzani wa sheria ya UKIMWI iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu mwaka 2008 imeweka katazo la mtanzania mwenye umri chini ya miaka 18 kutopima VVU isipokuwa kwa ridhaa ya mzazi au mlezi wake. **Ni maoni ya Kamati kuwa Sheria hii inakinzana na takwimu ambao ndiyo uhalisia kama zilivyoelezwa hapo awali kuwa vijana wenye maambukizi makubwa ni vijana kati ya miaka 15-24 ambapo kuna vijana wa kuanzia miaka 17, 16, 15 wako katika kundi hatarishi la kupata VVU. Kamati inashauri Serikali kuwa ni wakati sasa wa kufanya marekebisho ya Sheria hiyo ili kutanua wigo wa watu kuweza kupima na kutambua afya zao na hatimaye kuwaingiza katika utumiaji wa dawa za kufubaza makali ya VVU ambayo ni 90 ya pili na hatimaye kufubaza VVU na kufikia lengo la asilimia 90 ya tatu.**

#### **4.10 Kanzi data ya Majukumu ya Asasi zisizo za kiserikali (AZAKI)**

**Mheshimiwa Spika**, Asasi zisizo za kiserikali ni asasi zinazotoa mchango mkubwa katika jamii ili kutekeleza majukumu mbalimbali yakiwemo ya afya, maendeleo ya jamii, jinsia wazee na watoto kupitia Sera na mikakati mbalimbali ya Wizara hiyo. AZAKI hizo zinasajiliwa na kusimamiwa na Wizara hii. **Ni maoni ya Kamati kuwa ni vyema Wizara ikatengeneza kanzidata ya AZAKI zote zinazotekeleza majukumu yake katika jamii pamoja na kupata taarifa ya utekelezaji wa majukumu yake na taarifa hizo kuwasilishwa mbele ya Kamati**

ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya jamii. Kwa kufanya hivyo kutaondoa sintofahamu ya utekelezaji wa majukumu yasiyoendana na Sheria na taratibu za nchi yetu ikiwemo uhamasishaji wa mapenzi ya jinsia moja.

#### 4.11 Tathmini ya vyuo vyote vya Maendeleo ya Jamii pamoja na mitaala yake

**Mheshimiwa Spika**, Vyuo vya maendeleo ya jamii na vyuo vya ustawi wa jamii ni vyuo vinavyotoa elimu kwa ajili ya kupata wataalamu wa masuala ya maendeleo ya jamii pamoja na ustawi wa jamii. Vyuo hivi vimeanzishwa miaka mingi sana kutokana na hali iliyokuwa hapo awali kama vile kwa ajili ya uhamasishaji wa masuala ya ujamaa na kujitegemea, watu kujiletea maendeleo yao binafsi.

**Mheshimiwa Spika**, Ni maoni ya Kamati kuwa ni wakati sasa wa Serikali kufanya tathmini ya vyuo vilivyopo zaidi ya 50 pamoja na mitaala yake na kuweza kuona ni namna gani vyuo hivyo vinaweza kutoa elimu kuendana na wakati wa sasa kwa maana ya sayansi na teknolojia. Kwa kufanya hivyo kutasaidia wataalamu wanaozalishwa katika vyuo hivyo kuendelea kutoa usaidizi wa utatuzi wa changamoto katika jamii ikiwemo watoto wadogo kuharibikiwa kimaadili kwa njia za simu, Kompyuta mpakato, ulawiti wa watoto kwa watoto, kuvunjika kwa ndoa nyingi na hata unyanyasaji mwingine wa kijinsia.

#### 4.12 Serikali iboreshe Jela za watoto

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu, uvunjifu wa sheria hauzingatii umri wa mtu kama ni mkubwa au mtoto. Iwapo mtoto anapatikana na hatia kuna jela za watoto ambako tunaamini mtoto kwa kufungwa katika jela zao za watoto ni kwa ajili ya kumkuza katika kutambua kosa lake lakini huku akiendelea kupata haki zake za msingi kama mtoto.

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wa Kamati, imebainika kuwa, jela za watoto zina changamoto nyingi ikiwemo miundombinu mibovu, uangalizi hafifu kwa maana kulingana

na umri wao na hata kufikia katika jela hizo zinazoitwa za watoto kufungwa na watu wazima.

**Mheshimiwa Spika**, ni maoni ya Kamati kuwa, Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuhakikisha jela za watoto zinaboreshwa katika hali zote ikiwemo miundombinu, huduma za uangalizi pamoja na haki nyingine kwakuwa ni watoto na bado wanakua, kwa kuwa mtoto akiharibika akiwa mtoto kumrejesha katika hali yake hapo baadae inakuwa kazi na kuleta madhara makubwa kwa Taifa.

#### 4.13 Utungwaji wa Sheria ya Wazee

**Mheshimiwa Spika**, Licha ya kuwepo kwa Sera ya Wazee, hakuna sheria ya Wazee mpaka sasa iliyotungwa kwa ajili ya kusimamia haki zao za msingi ikiwemo matunzo ya chakula, huduma za afya na malazi. Licha ya changamoto nyingi zinazowakumba wazee hawa, Serikali bado haijaona umuhimu wa kutunga Sheria kwa ajili ya kuwatunza wazee wa taifa hili.

**Mheshimiwa Spika**, wazee wetu wakidhalilika taifa letu ndilo linalodhalilika kwa kuwa sisi ambao bado hatujafika uzeeni hatuwajibiki ipasavyo katika kuwatunza wazee wa nchi hii. **Ikumbukwe kwamba, vijana wa leo ni wazee wa kesho na wazee wa nchi hii ni hazina ya vijana. Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inafanya mchakato wa utungaji wa Sheria ya Wazee kwa ajili ya kuwanusuru wazee wa nchi hii kwa mateso na upokwaji wa haki zao ikiwemo kuuwawa bila hatia, kunyimwa huduma za matibabu kwa kukosa fedha za matibabu na hata muda mwingine kukosa mahali pa kulala mfano marehemu mzee wetu aliyetengeneza ngao ya taifa aliyekuwa analala vichochoroni kwenye maboksi na kuja kusaidiwa baadae na Serikali siku chache kabla umauti haujafika. Huo ni mfano tu wa wazee wengi wa nchi hii wanaoteseka kwa kukosa matunzo yao ambayo kimsingi ni haki yao kama binadamu na watu waliotumikia taifa hili kwa namna moja au nyingine.**

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kuchukua nafasi hii, kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa muda wa kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia napenda kumshukuru sana Waziri wa Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto Mheshimiwa Umyy A. Mwalimu (Mb) pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Faustine E. Ndugulile (Mb) kwa ushirikiano wao mkubwa wanaoendelea kuutoa kwa Kamati wakati wote wa shughuli za Kamati. Aidha, napenda kuwashukuru Makatibu Wakuu wa Wizara akiwemo Dkt. Zainab Chaula (Idara kuu Afya), Dkt. John Jingu (Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii) pamoja na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake zote kwa ushirikiano wanaooutoa kwa Kamati hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru Wadau wote wa Sekta ya Afya na Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto wakiwemo SIKIKA, AMREF na UMATI kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya kwa wananchi wetu na kwa ushirikiano wao mkubwa ambao wamekuwa wakiipa Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kushirikiana zaidi na wadau hawa wa Afya kwani juhudi zao zote ni kwa ajili ya manufaa ya kiafya ya wananchi wa kitanzania na wakati mwingine hulazimika kufika pale ambapo Serikali kwa namna moja au nyingine imeshindwa kufika kutoa huduma kwa wananchi wake.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa nafasi ya pekee kabisa naomba nimshukuru Makamu Mwenyekiti wangu Mhe. Juma Nkamia na niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Pamoja na changamoto ya muda, lakini wajumbe wamekuwa tayari kutekeleza majukumu yao. Kwa heshima kubwa, naomba kuwatambua kwa majina Waheshimiwa wafuatao:

1. Mhe. Peter J. Serukamba, Mb	Mwenyekiti
2. Mhe. Juma S.Nkamia, Mb	Mjumbe
3. Mhe. Deogratius F. Ngalawa, Mb	Mjumbe
4. Mhe. Amina N. Makilagi, Mb	Mjumbe
5. Mhe. Khalifa M. Issa, Mb	Mjumbe
6. Mhe. Grace V. Tendega, Mb	Mjumbe
7. Mhe. Rose C. Tweve, Mb	Mjumbe
8. Mhe. Oscar R. Mukasa, Mb	Mjumbe
9. Mhe. Selemani S. Bungara, Mb	Mjumbe
10. Mhe. Susan A. Lyimo, Mb	Mjumbe
11. Mhe. Joseph O. Mbilinyi, Mb	Mjumbe
12. Mhe. Joseph L. Haule, Mb	Mjumbe
13. Mhe. Bernadeta K. Mushashu, Mb	Mjumbe
14. Mhe. Salma R. Kikwete, Mb	Mjumbe
15. Mhe. Khamis Y. Machano, Mb	Mjumbe
16. Mhe. Mch. Dkt. Getrude P. Rwakatare, Mb	Mjumbe
17. Mhe, Maulid S. Mtulia, Mb	Mjumbe
18. Mhe. Hawa A. Ghasia, Mb	Mjumbe
19. Mhe. Hussein M. Bashe, Mb	Mjumbe
20. Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mb	Mjumbe
21. Mhe. Kabwe Z. R. Zitto, Mb	Mjumbe
22. Mhe. Vicky P. Kamata, Mb	Mjumbe
23. Mhe. John P. Kadutu, Mb	Mjumbe
24. Mhe. Mgeni J. Kadika, Mb	Mjumbe
25. Mhe. Peter A. Lijualikali, Mb	Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge, wakiongozwa na Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai, Mkurugenzi Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athman Hussein na Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Dickson Bisile kwa kuisaidia na kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kwa weledi mkubwa. Kipekee nawashukuru sana Makatibu wa Kamati yetu Ndg. Pamela Pallangyo na Ndg. Agnes Nkwera kwa kufanya kazi kwa weledi mkubwa wa kuishauri Kamati ili kutekeleza vyema majukumu yetu na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato

na Matumizi ya Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto pamoja na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja **Fungu 52** jumla ya shilingi **959,152,164,597.00** na **Fungu 53** jumla ya shilingi **31,537,431,013.00**

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja.  
(*Makofi*)

Peter Joseph Serukamba (Mb),  
**MWENYEKITI**  
**KAMATI YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII**  
**07 Mei, 2019**

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Peter Serukamba kwa taarifa ya kamati. Sasa namkaribisha Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ili awasilishe taarifa ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Esther Matiko. (*Makofi*)

**MHE. ESTHER N. MATIKO – K.n.y. MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwenye hotuba ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka wa fedha 2018/2019 na Makadirio na mapato ya matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/2020 inayotolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utangulizi; kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia uhai, afya njema na kunipa nguvu na uwezo wa kusimama mbele ya Bunge lako tukufu ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Makadirio

ya mapato na matumizi ya fedha kwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa napenda kuwashukuru wanachama pamoja na Watanzania wote ambao waliacha majukumu yao na kusafiri kutoka majumbani kwao ndani na nje ya Jiji la Dar es Salaam kuja hadi Gereza la Segerea kutujulia hali mimi na Mheshimiwa Mwenyekiti wa chama, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani na Mbunge, Mheshimiwa Freeman Mbowe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, niwashukuru sana wananchi na wanachama wote wa Tarime Mjini kwa kunivumilia na kuwa na mimi kwa sara na maombi kwa kipindi chote cha siku 104 nilizokuwa gerezani. Kwa umuhimu wa kipekee ni kwa familia yangu ambayo iliendelea kusimama na mimi katika kipindi hicho kigumu kwao ambacho sikuwa pamoja nao. Aidha, napenda kuwatia moyo viongozi wengine wakuu wa CHADEMA ambao wanakaribiwa na kesi za uchochezi au kufanya mikutano ya kisheria katika mahakama mbalimbali hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu ni kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa ushirikiano mkubwa wanaouonyesha katika kipindi hiki kigumu cha Bunge la Kumi na Moja kwani mazingira ya ufanyaji kazi ndani na nje ya Bunge hayaakisi haki yetu ya Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Afya nchini na utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019 inapatikana kwenye aya ya 5 mpaka ya 14.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya afya inakabiliwa na changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na msongamano mkubwa wa wagonjwa katika Hospitali za Wilaya, hospitali za mkoa, Hospitali za Rufaa za Mkoa, Hospitali za Rufaa za Kanda na Hospitali ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunatambua umuhimu wa sekta ya afya katika maendeleo ya Taifa. Hakuna na wala hakutakuwepo kamwe Tanzania ya viwanda pasipo kuwa na taifa la watu wenye afya bora. Nguvu kazi ya Taifa lolote duniani ni uwepo wa watu wenye afya bora ya mwili na akili. Ni jambo la kushangaza sana kuona zaidi ya asilimia 71 ya bajeti ya afya iliyotolewa kwa mwaka wa fedha 2017/18 ilitegemea wahisani huku fedha za ndani ikiwa ni asilimia 29 tu. Hii maana yake ni kuwa asilimia 71 ya maisha ya Watanzania imewekwa rehani kwa wahisani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi majigambo ya Serikali kwamba imeboresha sekta ya afya nchini ni kujitafutia umaarufu wa kisiasa tu. Hii ni kwa sababu bajeti ya afya kwa mwaka mpya wa fedha 2018/19 ilipungua kutoka shilingi trilini 1.07 kwa mwaka 2017/18 hadi kufikia shilingi bilioni 866.233 kwa mwaka 2018/19 ikiwa ni punguzo la shilingi bilioni 211. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni anguko la asilimia 19.6 la bajeti ya Wizara ya Afya kwa kulinganisha na mwaka wa fedha 2017/18 uliopita. Na kama ilivyo kawaida ya Serikali hii kutotekeleza bajeti inayopitishwa na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya utekelezaji iliyotolewa na Waziri Mwezi Machi, 2019 inaonesha kuwa fedha ambazo zimepokelewa hadi mwezi Februari, 2019 ni shilingi 304.7 kati ya shilingi 866.2 zilizokuwa zimeombwa na kuidhinishwa na Bunge lako tukufu. Kati ya fedha hizo fedha za maendeleo zilizokuwa zimepokelewa ni shilingi bilioni 89.9 sawa na asilimia 16 ya shilingi bilioni 561.8 zilizokuwa zimeidhinishwa na Bunge kama fedha za miradi ya maendeleo. Aidha, shilingi bilioni 180 ambazo ni takribani mara mbili ya fedha za ndani zilipokelewa kutoka Mfuko wa Dunia *(Global Funds)* wa kupambana na Malaria, UKIMWI na Kifua Kikuu nje ya mfumo wa *exchequer*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lakini ukiangalia Randama ya Mpango na Matumizi kwa fungu 52 iliyotolewa mwezi Machi, 2019 ukurasa wa tatu inasema fedha zilizopokelewa



kutoka Global Fund ni shilingi 75.4. Hii inatoa mkanganyiko wa takwimu kwa taarifa hizo mbili ile ya utekelezaji wa mwaka 2018/2019 na hii ya 2019/2020 fungu hilo hilo. Kambi Rasmi ya Upinzani inaomba kupatiwa taarifa sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ina maana kuwa afya ya watanzania imewekwa rehani na Serikali ya Awamu ya Tano. Siku tusipokuwa na Mfuko wa Dunia ni dhahiri Tanzania itapoteza sifa yake ya kuwa ni Taifa lenye watu wenye nguvu na afya bora na sio taifa lenye watu dhaifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha huu ni ushahidi wa wazi kwamba sasa afya si kiupaumbele tena cha Serikali hii ya Awamu Tano, jambo ambalo ni hatari kwa afya za watanzania na ukuaji wa uchumi wa Taifa ambao hutegemea nguvu kazi yenye afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio la Abuja lililofanyika miaka 15 iliyopita linazitaka nchi kutenga asilimia 15 ya fedha zote za bajeti ya nchi katika sekta ya afya, ambapo nchini mwetu lengo halijafikiwa kwa kuwa bajeti ya sekta ya afya ni chini ya asilimia 10.

Mheshimiwa Spika, upungufu wa rasilimali watu kwenye Sekta ya Afya. Upungufu wa rasilimali watu katika Sekta ya Afya inapatikana aya ya 15 – 27. Sekta ya Afya hapa nchini inakabiliwa na tatizo kubwa la upungufu wa rasilimali watu. Wizara hii ilikuwa na upungufu wa watumishi kwa asilimia 49 katika mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, pamoja na kuwa serikali hajatoa tathimini ya uhitaji wa jumla wa watumishi katika sekta hii, katika taarifa ya utekelezajiwa bajeti ya Wizara (fungu 52) inaonyesha kuwa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilitoa nafasi za ajira 3,152. Katika nafasi hizo, ajira za madaktari bingwa zilikuwa 24, madaktari wasaidizi 45, wauguzi daraja wa pili 137 na nafasi 2 za madaktari washauri 2 *(Medical Consultant)* na wengine walipelekwa kwenye kada mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alipokuwa akifungua mkutano wa 48 wa Chama cha Madaktari uliofanyika Novemba 2016, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Ummu Mwalimu alisema sekta ya afya inakabiliwa na upungufu mkubwa wa takribani asilimia 52 ya wataalamu wa afya katika kila ngazi ya vituo vya kutolea huduma za afya huku akiutaja upungufu huo kuwa umezidi kuwa juu zaidi kwenye maeneo ya vijijini ambapo ulifikia asilimia 74.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado rasilimali watu katika sekta ya afya nchini ni tatizo hususani katika maeneo ya vijijini. Bado wataalam wetu wa afya wanafanya kazi kubwa kutokana na ongezeko kubwa la wagonjwa japokuwa wataalam wengi waliondolewa kwa kilichoitwa vyeti feki bila ya kuziba nafasi kwa idadi ya walioondolewa kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hivi karibuni Serikali ilikiri uhaba mkubwa wa madaktari. Kwa mujibu wa kumbukumbu, Serikali hii ya Awamu ya Tano iliwahi kutaka kuwapeleka madaktari 500 nchini Kenya ilhali nchi ikikabiliwa na tatizo kubwa na sugu la uhaba wa madaktari. Uchambuzi uliofanywa na *The Citizen* Tanzania mwaka 2016 ulionyesha uwiano kuwa daktari 1:25,000, kinyume na muongozo wa Shirika la Afya Duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ongezeko hilo kubwa la idadi ya watu, Serikali imeshindwa kuzalisha ajira za wataalamu na wanataaluma watakaoweza kukabiliana na changamoto zinazoibuka kila siku ikiwemo mlipuko wa magonjwa yale ya kuambukiza na hata yasiyo ya kuambua. Wengi huishia kuajiriwa na mashirika yasiyo ya Kiserikali, kuajiriwa kwenye sekta za ujuzi tofauti na hata kujiajiri wenyewe. Hii imejionyesha wazi kwenye randama ya Wizara ukurasa wa 50 ambapo idadi ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na vyuo vya afya nchini walikadiriwa kuwa 47,269 huku ajira zilionekana kutolewa chache sana Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashangaza sana kuona Serikali ilitoa nafasi mbili tu kwa madaktari washauri (*medical*

*consultant*) ambapo hata hivyo Serikali imekiri kushindwa kujaza nafasi hizo mbili. Nchi nyingi duniani hasa zile za uchumi wa kati na zile zilizoendelea zimeweza kupiga hatua kubwa katika kuwekeza kwenye afya za wananchi wao. Viwanda haviwezi kuzalisha pasipo watu kuwa na uhakika wa tiba bora na uwezo wa kuonana na tabibu pale wanapomuhitaji. Pamoja na hilo tafiti za magonjwa, chanjo na tiba zinaweza tu kufanyika vyema hapa nchini kama Serikali ikijikita kwenye kuwekeza kwenye afya. Kwa mantiki hiyo, uwekezaji katika afya ndiyo unatoa mweleko wa wawekezaji katika sekta nyingine na hivyo kichocheo kikuu cha maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini katika ubora wa huduma, hivyo itaanzisha mchakato wa kutathmini kwa wahudumu wa afya kwa ajili ya maisha yao hapa Tanzania, viwango vyao vya maslahi, na ubora kwa ajili ya utoaji wa huduma tutakapokabidhiwa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwajibishaji wa watumishi wa Sekta ya Afya, aya ya 24 mpaka 32. Kwa mujibu wa taratibu na sheria zilizowekwa juu ya uwajibishaji wa watumishi wa sekta ya afya hasa madaktari, zipo hatua na taratibu za kinidhamu kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma kwa madaktari wote waajiriwa. Na kwa mujibu wa Sheria na Kanuni hizo hatua hizo ni pamoja na Baraza la Madaktari Tanganyika (*MCT*) ama Baraza la Wauguzi kwa upande wa wauguzi wenye kupewa mamlaka ya kutoa onyo na kuwasimamisha ama kuwafutia sifa za udaktari, madaktari ama wauguzi watakaokutwa na hatia baada ya malalamiko ya kutowajibika ama makosa yao kufikishwa kwenye baraza husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani kumekuwapo na wimbi kubwa la wanasiasa na hasa wasiokuwa na mamlaka ya kinidhamu kuwawajibisha madaktari pasipo kufuata taratibu na kanuni zilizowekwa na hivyo kuzua sintofahamu katika jamii na kushusha hadhi za mamlaka za kinidhamu zinazostahili kuwawajibisha madaktari walioajiriwa wa umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na muendelezo wa matukio si tu yanayodhalilisha taaluma za watumishi wa sekta ya afya bali pia yanayoishusha thamani Awamu ya Tano na kuzipoka mamlaka husika wajibu wake na matukio haya ni kama nilivyoainisha hapa kwa uchache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mosi; mwezi Machi mwaka 2017, Mkuu wa Wilaya ya Kilwa Christopher Ngubiagai alitangazwa na Jumuiya ya Madaktari Tanzania kuwa adui namba moja wa afya baada ya Mkuu huyo wa Wilaya kumuweka mbaroni Mganga Mkuu wa Wilaya ya Kilwa, Dkt. Vitalis Katalyeba. Dkt. Katalyeba alisimimashwa kazi kwa kutuhumiwa kuchelewesha gari la kubebea wagonjwa na kusababisha kifo cha mgonjwa huyo. Mara baada ya kusimamishwa, Dkt. Katalyeba alihudhuria mkutano ambapo kitendo hicho kilimuudhi DC huyo na kuagiza Dkt. Katalyeba kutiwa mbaroni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukio lingine ni la Mkuu wa Mkoa wa Singida Bi. Rehema Nchimbi alipomuweka Rumande Mganga Mkuu wa Wilaya ya Singida Mjini Dr. Bakuza, pamoja na kuwa kulikuwa na upungufu wa kiutendaji bado taratibu za uwajibishwaji wa kinidhamu zilitakiwa kufuatwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika tukio lingine Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Ndugu Mrisho Gambo, alimtaka Mganga Mkuu wa Wilaya ya Monduli kutoa maelezo ya malimbikizo mbalimbali ya stahiki za watumishi wa afya huku akijua wazi kuwa siyo jukumu la Mganga wa Wilaya. Ikumbukwe kuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha anaendelea kuwa katika historia mbaya na madaktari kuanzia alipokuwa Mkuu wa Wilaya Awamu ya Nne ya CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukio lingine ni Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi. Mwezi Septemba, 2018 alimsimamisha kazi – kwa madai ya wananchi kudhalilishwa Mganga Mkuu wa Kituo cha Afya cha Ukami, Dkt. Andrew Kitwanga. Hii ilipelekea kuwepo kwa mjadala mzito na hata Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo, aliomba radhi kwa

niaba ya Mkuu huyo wa Mkoa na kuahidi kutoa mwongozo kwa viongozi hawa juu ya hatua za kinidhamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Aprili, 2019 mambo haya hayakukoma, tuliendelea kuona zaidi tena Daktari wa Kituo cha Afya cha Ngarenano, Dkt. Japhet Kivuyo, Mkoani Arusha baada ya kukutwa hayuko kazini, uamuzi wa kufukuzwa kwake ulitolewa na Katibu Mwenezi wa Chama cha Mapinduzi, Kata ya Levelosi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kuwa matukio haya ya kudhalilisha hata kama yana uhalali na iwapo hayafuati taratibu na kanuni zilizowekwa, hupunguza morali kwa watumishi hawa muhimu. Kuongezeka kwa vitendo vya viongozi wa Umma na sasa imehamia kwa viongozi wa Chama Tawala kufanya ili kutafuta umaarufu wa kiasiasa, havina nia ya dhati ya kukabiliana na changamoto ya Sekta ya Afya nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kukosekana kwa vitendea kazi, ikiwemo magari ya wagonjwa, vifaatiba na kutokana na ufinyu wa bajeti za afya na pia ukosefu wa watumishi wa kutosha kwa kada hii muhimu kunasababisha haya yote kutokea. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutekeleza wajibu wake ikiwemo kuhakikisha watumishi na vitendea kazi katika Sekta ya Afya vinapatikana vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali itimize wajibu wake wa kuwalipa stahiki watumishi wa afya pamoja na kuwapandisha madaraja watumishi wanaostahili na kuacha kuwasingizia Waganga Wakuu majukumu yasiyo ya kwao pale inaposhindwa kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Afya kwa Wote *(Universal Health Coverage)*, hii inapatikana aya ya 33 mpaka 38. Malengo ya afya kwa wote, Serikali kupitia Waziri wa Afya kwenye hotuba yake mwaka 2018/2019 aya ya 118, alisema Serikali inalenga kufikia mwaka 2020 Watanzania zaidi ya asilimia 70 wawe na Bima ya Afya, lakini taarifa inaendelea kusema kuwa kwa sasa watu walio kwenye mfumo wa Bima

ya Afya ni asilimia 32. Maana yake ni kuwa kati ya Watanzania 100 ni Watanzania 32 tu ndio wana uhakika na matibabu ya afya zao na waliobakia 68 maisha yao yako mashakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli ya Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake ni kauli ambayo haioneshi umakini wa Serikali katika afya za Watanzania. Hivyo, Kambi ya Upinzani Bungeni haikuona kama kuna mkakati wowote ambao Serikali iliweka ili kuhakikisha watu hawa 68 kati ya watu 100 nao wanajunga na bima ya afya. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa taarifa Bungeni ni wananchi wangapi mpaka sasa wamejiunga na Bima ya Afya na hasa wale wa kipato cha chini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri Serikali kufanya yafuatayo:-

Kwanza, kutangaza kuwa inataka kusiwepo na Mtanzania anayekosa huduma ya afya kwa kutokuwa na fedha;

Pili, kuleta mpango mahususi wa mfumo utakaotumika kuhakikisha watu wa hali ya chini wanakuwa na Bima ya Afya;

Tatu, kupitisha na kutekeleza Mkakati wa Kugharimia Huduma za Afya (*National Health Financing Strategy*);

Nne, kuweka malengo ya kuongeza matumizi kwenye Sekta ya Afya kufikia 4% mpaka 5% ya Pato la Taifa kama inavyopendekezwa na Shirika la Afya Duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufafanuzi zaidi wanaweza wakarejea Sera ya CHADEMA, ukurasa wa 44 mpaka 47. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufikia kiwango hicho cha 4% mpaka 5% cha *GDP* kilichopendekezwa na Shirika la Afya Duniani kinawezekana kama Serikali itakuwa na nidhamu ya kujikita na kubakia kwenye Mpango wa Maendeleo wa

Miaka Mitano kama ulivyopitishwa na Bunge lako Tukufu. Tumeona hivi sasa miradi mikubwa inatumia fedha za ndani na mikopo ya kibiashara wakati mpango upo wazi miradi mikubwa ya kimkakati inatakiwa kutekelezwa kwa ubia na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya mama na mtoto inapatikana katika aya ya 39 mpaka 43. Katika hotuba yake ya mwaka 2017/2018, Mheshimiwa Waziri alilieleza Bunge lako Tukufu kuwa kuanzia mwezi Oktoba ulianzishwa utaratibu wa kutaka kila Halmashauri na mkoa nchini kutoa taarifa ya vifo vinavyotokana na uzazi kila mwezi. Ikiwa imepita takribani miaka miwili kutoka utaratibu huo kuanzishwa, Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza, hadi sasa ni halmshauri ngapi nchini zimetokeleza utaratibu huo na kwa Halmashauri na mikoa iliyoshindwa kufanya hivyo kwa maana ya kutekeleza utaratibu huo, zimechukuliwa hatua gani. Pia kwa mujibu wa takwimu na taarifa hizo: Je, Wizara imefanikiwa kwa kiwango gani kwa kutumia taarifa hizo katika kukabiliana na vifo vya mama na mtoto?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kuwa takwimu za vifo vinavyotokana na uzazi nchini zimeendelea kupotosha hali halisi kwani akina mama wengi na watoto hasa wa vijijini wanafariki na idadi inaongezeka kutokana na kutokuwa na huduma bora ya afya, kuongezeka kwa gharama ya maisha, ukosefu wa umeme, vilevile miundombinu duni pamoja na upungufu mkubwa wa watumishi wa afya, hasa Madaktari wa Akina Mama na kukosekana kwa vitendea kazi na vifaatiba vinavyotokana na ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifike mahali sisi kama Taifa tuweke mbali siasa katika masuala muhimu nchini, hasa masuala ya uzazi ili kufanikisha azma ya kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi. Aidha, huduma ya afya bila malipo kwa wanawake wajawazito na watoto chini ya miaka mitano ni mojawapo ya sehemu ya Sera ya Afya ya Tanzania, lakini mpango huu bado una upungufu mkubwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa takwimu, bado wanawake 11,000 hupoteza maisha nchini, sawa na akina mama 30 kila siku. Bado katika hospitali mbalimbali na vituo vya afya, akina mama wajawazito wanatakiwa kujinunuliwa vifaa vya kujifungulia kama pamba, nyembe, *gloves* na hata wakati mwingine huambiwa wanunue mipira ya kulalia wakati wa kujifungua pamoja na kuwa Serikali imesisitiza kuwa vifaa hivi hupatikana hospitali bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kumekuwa na malalamiko kuwa baadhi ya vifaatiba vinavyotolewa na Bohari ya Dawa (*MSD*) havina ubora unaotakiwa na kuwa vinaharibika mapema na hivyo kuongeza changamoto katika huduma za kujifungulia. Ni lazima Wizara iwajibike katika kuhakikisha changamoto hizi zinatatuliwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakunga wa jadi; hili linapatikana aya ya 44 mpaka 47. Ni dhahiri kuwa ukosefu wa huduma ya afya nchini bado umeendelea kuwa changamoto hasa katika masuala ya uzazi hususan maeneo ya vijijini. Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Shirika la Afya Duniani (*WHO*) zinaonesha kuwa zaidi ya asilimia 60 ya wanawake wanaojifungulia vijijini nchini hukosa usaidizi wa wataalam na hivyo kusababisha akina mama hao kutafuta huduma za wakunga wa jadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya habari zilizowahi kuripotiwa na vituo vikubwa vya habari ulimwenguni ni pamoja na habari iliyoripotiwa na Shirika la Habari la Uingereza (*BBC*) tarehe 17 Aprili, 2019 iliyokuwa na kichwa cha habari, "Wakunga wa Jadi wazalisha wanawake kwa kutumia mifuko ya rambo Tanzania."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa chapisho hilo la habari ilionekana kuwa baadhi ya vijiji Mkoani Tabora, hasa Wilaya ya Sikonge Wakunga wa Jadi hulazimika kuzalisha akina mama majumbani na mara nyingi hulazimika kutumia mifuko ya rambo; na hii huongeza hatari ya magonjwa siyo tu kwa akina mama, hata kwa wakunga wanaosaidiana pamoja na watoto wanaozaliwa.



Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na marufuku iliyotolewa na Wizara ya Afya ya kuwapiga marufuku Wakunga wa Jadi kuzalisha akina mama majumbani, Wizara ilieleze Bunge lako ni njia gani akina mama wa vijijini watumie hasa ukizingatia kuwa kuna matatizo ya usafiri na uhaba wa vituo vya afya vijijini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwazuia Wakunga wa Jadi siyo tu kunaongeza idadi ya vifo vya mama na mtoto, bali kunaathiri akina mama wengi hasa ukizingatia kuwa Wakunga wa Jadi ni wakombozi wa akina mama ambao wengi wanaishi katika umasikini uliokithiri. Kambi ya Upinzani Bungeni inaitaka Wizara ya Afya kuweka mkakati wa kutoa elimu na mafunzo ya awali kwa wakunga hawa na kuwawezesha ili kuwa mbadala wa watoaji huduma za afya, hasa pale kunapokua na changamoto isiyotarajiwa katika maeneo husika na kupunguza idadi ya vifo vinavyotokana na uzazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kuwa ikiwa Wakunga wa Jadi watapewa mafunzo stahiki, basi Taifa litaondokana na changamoto hii kama ambavyo kwa upande wa Zanzibar wamefanikiwa kuwashirikisha Wakunga wa Jadi na Wataalam wa Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ugonjwa wa Homa ya Ini unapatikana aya ya 48 mpaka 50. Ugonjwa wa Homa ya Ini (*Hepatitis*) unatokana na kirusi kinachoambukizwa kupitia damu na majimaji mengine ya mwili, ambacho huvamia ini na kusababisha vifo vya watu wapatao 650,000 kila mwaka, wengi wao wakiwa katika nchi za kipato cha chini na kipato cha wastani. Shirika la Afya Duniani, *WHO* ambalo ni kinara katika magonjwa, mathalan Homa ya Ini (*Hepatitis*), hivi karibuni limetoa mwongozo wake wenye mapendekezo sita kuhusu matibabu ya ugonjwa huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Tanzania imesema kuwa maambukizi ya Ugonjwa wa Homa ya Ini (*Hepatitis*), yameongezeka mara mbili yakilinganishwa na Virusi vya Ukimwi nchini. Aidha, Ugonjwa wa Homa ya Ini (*Hepatitis*)

unaongoza kwa kuua Watanzania kutokana na maambukizi yake kufikia asilimia 16, huku Virusi vya Ugonjwa wa UKIMWI, ikiwa ni asilimia 5.3. Ugonjwa huo hua taratibu ukilinganishwa na magonjwa mengine kwa kuwa dalili zake huchukua muda mrefu kuweza kujulikana na kujitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuweka wazi kwa Watanzania ni jinsi gani Ugonjwa wa Homa ya Ini umeenea, na kinga au chanjo yake inapatikana vipi ili kuinga maambukizi, matibabu yapi yatumike awali na yapi yafuatie ikiwa ya awali hayakufanya kazi na pia jinsi ya kufuatilia mambo hayo manne tajwa sambamba na kuangalia kama kuna Saratani ya Ini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maambukizi ya VVU na UKIMWI nchini, yanapatikana aya ya 53 mpaka 65. Mapema mwezi Machi, 2019, Tume ya Kudhibiti UKIMWI nchini (*TACAIDS*) ilitoa ripoti yake kuhusu maambukizi mapya ya VVU nchini. Katika ripoti yake ilibaini kuwa takribani Watanzania 225 huambukizwa Virusi vya UKIMWI kwa siku, huku Watanzania takribani 6,750 huambukizwa kwa mwezi na kwa mwaka Watanzania takribani 82,125 huambukizwa Virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ripoti hiyo, maambukizi makubwa yalionekana kati ya vijana wenye umri wa miaka 15 mpaka 20 na wengi wao wakiwa ni vijana wa kike. Kwa mujibu wa Tume ya Taifa ya Takwimu, mpaka 2017 takribani watu milioni 1.4 walikuwa na maambukizi ya UKIMWI. Hii inaonesha ongezeko la maambukizi tofauti na tafiti zilizofanyika mwaka 2010-2015 ambapo maambukizi yalipungua kwa asilimia 20 kwa mujibu wa ripoti ya *UNAIDS* 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana nzima ya 90, 90, 90, iliyoanzishwa na Umoja wa Mataifa kuhusu *HIV/AIDS* mwaka 2013 kwamba ili kufikia mwaka 2020 kusiwepo na maambukizi ya UKIMWI duniani, kwa maana ya 90% ya watu walioambukizwa Virusi vya UKIMWI wawe wametambulika na 90% ya waliotambulika wawe wanatumia ARVs na 90%

ya wanaotumia ARVs waweze kufubaza virusi hivyo na hivyo hakutakuwa na maambukizi mapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati huo ulikuwa unajaribu kuzuia na kudhibiti maambukizi ya HIV kwa kutumia kanuni kuu ya kupima na kutibu (*test and treat*) wale wote wenye virusi ili kufikia lengo la 90, 90, 90. Kwa upande wa Afrika, nchi ya Botswana ndiyo inayokaribia kufikia lengo la 90, 90, 90 kwa kupima, kutibu na kufubaza virusi. Hii imewezekana kwa nchi hiyo kwani ilikuwa nchi ya kwanza katika Afrika kutoa matibabu ya ARVs bure kwa watu wake wote wenye HIV tangu mwaka 2002.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kongamano la siku latu lililofanyika Jijini Dodoma kuanzia Juni 20 mpaka 23, 2018 kuhusu jukumu na wajibu wa viongozi katika kufika lengo la HIV la 90, 90, 90 kwa mwaka 2020 Tanzania, ambalo liliandaliwa na Kamati ya Bunge ya UKIMWI kwa pamoja na Baraza la Watu Waishio na HIV/AIDS (NACOPHA) ambao waliratibu wadau na asasi zisizo za kiraia chini ya Waziri Mkuu, Spika wa Bunge na Mjumbe kutoka USAID wakiwa waongoza jopo. Waziri Mkuu alisema kuwa Serikali kupitia TACAIDS inatekeleza mkakati wa kufikia lengo la 90, 90, 90.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kufahamu hadi sasa katika kufikia lengo la 90, 90, 90, Tanzania tumefikia wapi? Kwani tumebakiza mwaka mmoja na nusu kufikia muda uliowekwa na Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magonjwa yasiyo ya kuambukiza (*Non Communicable Diseases – NCD*) ni magonjwa ambayo yanaua kwa kasi na yanatumia rasilimali kubwa sana. Ipo kwenye aya ya 66 mpaka aya ya 70.

Mheshimiwa Mwenyekiti, visababishi vikubwa vya Magonjwa yasiyoakuambukiza ni kutofanya mazoezi, kukaa muda mrefu darasani, ofisini, kuangalia runinga, kutumia lifti, kupanda magari na kutoshiriki michezo mbalimbali; ulaji usiofaa, kula chakula kuzidi mahitaji ya mwili na hivyo kunenepa, kula mafuta na chumvi zaidi na kutokula mboga

mboga na matunda kiasi cha kutosha; kula nafaka zilizokobolewa, matumizi ya pombe, tumbaku na madawa ya kulevywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ni jukumu la Wizara hii kuweza kuelimisha Umma ili kuweza kuepukana na magojwa yasiyoambukiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Chakula na Lishe, kwa sababu ya muda ipo aya ya 76 mpaka 79.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa umuhimu kabisa, hali ya afya ya ugonjwa wa akili inapatikana aya ya 88 mpaka 89.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye maendeleo ya jamii nitapenda kuzungumzia maendeleo ya makuzi ya awali kwa mtoto (*Early Childhood Development*). Eneo muhimu katika maendeleo ya binadamu ni malezi na makuzi ya mtoto katika siku 1,000 za mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakadiriwa kuwa takribani asilimia 80 ya makuzi ya ubongo wa mtoto hufanyika kipindi hiki. Maendeleo na makuzi ya mtoto katika siku hizi 1,000 yana umuhimu katika maisha ya utu uzima kimwili, kihisia, kisaikolojia. Hivyo kuwekeza katika umri huu ni kutengeneza ustawi mzuri wa watu wazima wa baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Benki ya Dunia, kuwekeza dola moja katika kipindi hiki kunakadiriwa kurudisha dola kati ya 6 mpaka 17 kwa baadaye. Madhara ya kutowekeza katika makuzi ya watoto yana athari katika kipindi chote cha maisha. Madhara hayo huwa katika maeneo ya uwezo wa kufikiri, afya, uwezo wa kuzalisha (*human capital*), kipato na usawia (*equity*). Kikubwa zaidi ni udumavu wa akili ambao unajitokeza katika kipindi ambacho mtu mzima anafanya maamuzi yake kulingana na mazingira yaliyomzunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Mheshimiwa Waziri mwaka wa fedha 2018/2019 kuanzia aya ya 179 hadi 181 aliliambia Bunge lako Tukufu idadi ya vituo vya kulelea watoto (*Day Care Centers*) kwamba ni 1,046 na kuwa Chuo cha Kisangara ndicho pekee kinachodahili na kutoa wahitimu na kuwa Serikali ilifundisha walezi 600 kutoka Manispaa nne za Dar Es Salaaam (Ubungo, Temeke, Ilala na Kigamboni). Serikali haikubainisha mikakati ya kuwafikia watoto wengine katika mikoa na wilaya nyingine za Tanzania na huko ndiko jamii kubwa ya wananchi ilipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kulipa eneo hili kipaumbelee kwa kupanga mikakati ya kuwa na vyuo vya kufundisha wataalam wa malezi na watoto wadogo, kupanua wigo wa *Early Childhood Development* zaidi ya *Early Childhood Education*, kutenga bajeti maalum kwa ajili ya eneo hili, kuweka mikakati ya kufikia wilaya zote kwenye eneo la *Early Childhood Development* ili kuwa na kizazi chenye ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inahitaji majibu kwa maswali haya:-

- Je, Serikali ina mpango gani wa kupanua wigo wa *ECD* kutoka *ECE* na kushirikisha maeneo ya afya, lische na maji?

- Wizara imepanga kiasi gani cha fedha kwa mwaka huu kwa ajili ya *ECD*? Kwa vile Benki ya Dunia iko tayari kuikopesha Tanzania Dola za Marekani Milioni 200 tangu Novemba, 2017, ni lini Serikali itachukua hatua ya kuomba hela hiyo?

- Je, Serikali inaongeza lini vyuo vya kufundisha wataalamu wa *ECD* ili kukidhi mahitaji ya nchi kulingana na sensa ya watoto chini ya miaka mitano?

- Je, Serikali ina mpango gani kufundisha walezi kwenye Halmashauri nyingine mbali na wale waliofundishwa kwenye Manispaa za Dar es Salaam?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, kuna ukiukwaji wa haki za watoto unaofanywa na Jeshi la Polisi, Sheria za Ndoa za Utotoni. kuna pensheni ya wazee imeongelewa kwa kina kabisa tutai-coverkwenye michango yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kwamba afya ya Taifa ni jambo muhimu kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii na kwamba utoaji wa huduma za afya za kibingwa kwa wakati zinaokoa muda wa uzalishaji na hivyo kuongeza ufanisi. Aidha, utoaji wa dawa za kuzuia magonjwa (chanjo) zina muhimu sawa na dawa za kuponya magonjwa kwa kuwa zinasaidia kwa kiwango kikubwa kujenga ustawi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufikia azma ya Taifa lenye afya, Kambi Rasmi ya Upinzani kupitia Sera ya Afya ya CHADEMA itashirikisha Sekta Binafsi kupitia ubia na Sekta ya Umma (*PPP*), kujenga, kuendeleza na kutumia miundombinu ya afya, pia kuongeza udahili wa mafunzo ya watendaji katika sekta ya afya ili kukidhi mahitaji ya jamii kwa mfumo wa ubia lakini Serikali ikibakia kuwa ni mbia mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani tunaamini kuwa teknolojia ya afya ni matokeo ya tafiti bora za kitabibu, ambapo matumizi ya ujuzi na elimu katika Sekta ya Afya hususan dawa, vifaa tiba, chanjo na mbinu vinatumika kutatua matatizo ya kiafya na kuboresha afya kwa wananchi. Hivyo tutahakikisha tunakuza sayansi ya tiba na kuboresha vifaa tiba na mbinu mbalimbali za utoaji huduma ya afya. Sambamba na hilo, tutahakikisha usajili wa taasisi za utafiti, tiba asili na tiba mbadala kwa ajili ya kuboresha Sekta ya Afya. Rejea Sera za CHADEMA, uk 44 -48. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hotuba yangu yote iingie kwenye *Hansard* na ninaomba Waheshimiwa Wabunge muisome kwa makini. (*Makofi*)

**HOTUBA YA MSEMaji MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI  
BUNGENI KATIKA WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA  
JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO,  
MHESHIMIWA CECILIA DANIEL PARESSO (MB),  
KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO MWAKA  
WA FEDHA 2018/19 NA MPANGO WA MAKADIRIO YA  
MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA, KWA MWAKA WA FEDHA  
2019/2020 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*Inatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za  
Bunge, Toleo la Januari, 2016*

---

**A. UTANGULIZI**

**1. Mheshimiwa Spika**, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kunijalia uhai, afya njema na kunipa nguvu na uwezo wa kusimama mbele ya Bunge lako tukufu ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**2. Mheshimiwa Spika**, kwa heshima kubwa napenda kuwashukuru wanachama pamoja na watanzania wote ambao waliacha majukumu yao na kusafiri kutoka majumbani kwao ndani ya jiji na nje ya Jiji la Dar es salaam kuja hadi gereza la Segerea kututakia hali mimi na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Chama, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzania na Mbunge wa Hai Mheshimiwa Freemani Mbowe.

**3. Mheshimiwa Spika**, aidha niwashukuru sana wananchi na wanachama wote wa Tarime Mjini kwa kunivumilia na kuwa na mimi kwa sala na maombi kwa kipindi

chote cha siku 104 nilizokuwa gerezani, kwa umuhimu wa kipekee ni kwa familia yangu ambayo iliendelea kusimama na mimi katika kipindi hicho kigumu kwao ambacho sikuwa pamoja nao. Aidha napenda pia kuwatia moyo, Viongozi wengine wakuu wa CHADEMA ambao wanakabiliwa na kesi za uchochezi au kufanya mikutano ya kisheria katika mahakama mbalimbali hapa nchini.

4. **Mheshimiwa Spika**, Mwisho lakini sio kwa umuhimu ni kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa ushirikiano mkubwa mnaouonesha katika kipindi hiki kigumu cha Bunge la 11, kwani mazingira ya ufanyaji kazi ndani na nje ya Bunge hayaakisi haki yetu ya kisheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge.

**B. SEKTA YA AFYA NCHINI na UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

5. **Mheshimiwa Spika**, Sekta ya afya inakabiliwa na changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na msongamano mkubwa wa wagonjwa katika hospitali za wilaya, hospitali za mkoa, hospitali za rufaa za mkoa, hospitali za rufaa za kanda na hospitali ya taifa.

6. **Mheshimiwa Spika**, sote tunatambua umuhimu wa sekta ya afya katika maendeleo ya Taifa. Hakuna na wala hakutakuwepo kamwe Tanzania ya viwanda pasipo kuwa na taifa la watu wenye afya bora. Nguvu kazi ya taifa lolote duniani ni uwepo wa watu wenye afya bora ya mwili na akili. Ni jambo la kushangaza sana kuona zaidi ya **asilimia 71** ya bajeti ya afya iliyotolewa kwa mwaka wa fedha 2017/18; ilitegemea wahisani huku fedha za ndani ikiwa ni asilimia 29 tu. Hii maana yake ni kuwa asilimia 71 ya maisha ya Watanzania imewekwa rehani kwa wahisani.

7. **Mheshimiwa Spika**, kimsingi majigambo ya Serikali kwamba imeboresha sekta ya afya nchini ni katika kujitafutia umaarufu wa kisiasa tu. Hii ni kwa sababu bajeti ya afya kwa mwaka mpya wa fedha 2018/19 imepungua kutoka shilingi trilini 1. 07 kwa mwaka 2017/18 hadi kufikia shilingi bilioni



866.233<sup>1</sup> kwa mwaka 2018/19 ikiwa ni punguzo la shilingi bilioni 211.468.

**8. Mheshimiwa Spika**, hili ni anguko la asilimia 19.622 la bajeti ya Wizara ya Afya kwa kulinganisha na mwaka wa fedha 2017/18. Na kama ilivyo kawaida ya Serikali hii kutotekeleza bajeti inayoidhinishwa na Bunge.

**9. Mheshimiwa Spika**, taarifa ya utekelezaji iliyotolewa na Wizara Mwezi March, 2019 inaonesha kuwa fedha ambazo zimepokelewa hadi mwezi February, 2019 ni **shilingi 304,707,109,084.00** kati ya **shilingi 866,233,475,000.00** zilizokuwa zimeombwa na kuidhinishwa na Bunge, Kati ya fedha hizo fedha za maendeleo zilizokuwa zimepokelewa **ni shilingi 89,955,841,092.00** sawa na **asilimia 16** ya **shilingi 561,759,999,000.00** zilizokuwa zimeidhinishwa na Bunge kama fedha za miradi ya maendeleo. Aidha, **shilingi 180,000,000,000.00** ambazo ni takribani mara mbili ya fedha za ndani zilipokelewa kutoka Mfuko wa Dunia (Global Fund) wa kupambana na Malaria, UKIMWI na Kifua Kikuu nje ya mfumo wa Exchequer.

**10. Mheshimiwa Spika**, Lakini ukiangalia Randama ya Mpango na Matumizi kwa fungu 52 iliyotolewa mwezi March, 2019 uk. wa 3 inasema fedha zilizopokelewa kutoka Global Fund **ni shilingi 75,427,463,684.27**. **Hii ni mkanganyiko wa takwimu kwa taarifa hizo mbili ile ya utekelezaji wa mwaka 2018/19 na hii ya 2019/20 fungu hilo hilo. Kambi Rasmi ya Upinzani inaomba kupatiwa taarifa sahihi.**

**11. Mheshimiwa Spika**, hii maana yake ni kuwa afya ya watanzania imewekwa rehani na Serikali, siku tusipopokea fedha za mfuko wa dunia ni dhahiri Tanzania itapoteza sifa yake ya kuwa ni Taifa lenye watu wenye nguvu na afya bora na sio taifa lenye watu dhaifu.

---

<sup>1</sup>Tazama Randama ya Wizara mwaka 2018/19 (fungu 52) uk. 193 ambapo Matumizi ya Kawaida ni shilingi 304,473,476,000/= na Matumizi ya Maendeleo ni shilingi 561,759,999,000/=

**12. Mheshimiwa Spika**, aidha huu ni ushahidi wa wazi kwamba sasa afya si kiupaumbele tena cha Serikali hii ya awamu tano jambo ambalo ni hatari kwa afya za wataanzania na ukuaji wa uchumi wa taifa ambao hutegemea nguvu kazi yenye afya.

**13. Mheshimiwa Spika**, upungufu huu wa bajeti ya afya hauendani kabisa na ongezeko la watu ambao pia hupelekea ongezeko la watu wenye matatizo mbalimbali ya kiafya. Aidha, bajeti hii haiakisi haja ya kufanya tafiti mbalimbali juu ya magonjwa mapya yanayoibuka mara kwa mara. Sekta ya Afya ina changamoto nyingi ambazo huongezeka siku hadi siku. Kitendo cha kupunguza bajeti ya afya hakuendani na kuongezeka kwa changamoto hizo.

**14. Mheshimiwa Spika**, Azimio la Abuja lililofanyika miaka 15 iliyopita linazitaka nchi kutenga asilimia 15 ya fedha zote za bajeti ya nchi katika sekta ya afya, ambapo nchini mwetu lengo halijafikiwa kwa kuwa bajeti ya sekta ya afya ni chini ya asilimia 10.

**i. Upungufu wa Rasilimali Watu kwenye Sekta ya Afya**

**15. Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Afya hapa nchini inakabiliwa na tatizo kubwa la upungufu wa rasilimali watu. Kwa mujibu wa Ripoti ya Madaktari wenza wa Afrika (Africa Cuamm); Wizara hii ilikuwa na upungufu wa watumishi kwa asilimia 49 katika mwaka wa fedha 2016/17. Hata hivyo, pamoja na kuwa serikali haijatoa tathimini ya uhitaji wa jumla wa watumishi katika sekta hii; katika taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara (fungu 52) inaonyesha kuwa; Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilitoa nafasi za ajira 3,152. Katika nafasi hizo, ajira za Madaktari Bingwa zilikuwa 24, Madaktari Wasaidizi 45, Wauguzi Daraja wa Pili 137 (nurses) na nafasi 2 za Madaktari Washauri 2 (Medical Consultant) na wengine walipelekwa kwenye kada mbalimbali.

**16. Mheshimiwa Spika**, Alipokuwa akifungua mkutano wa 48 wa chama cha madaktari uliofanyika Novemba 2016, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na

Watoto, Ummu Mwalimu alisema sekta ya afya inakabiliwa na upungufu mkubwa wa takribani asilimia 52 wa wataalamu wa afya katika kila ngazi ya vituo vya kutolea huduma za afya huku akiutaja upungufu huo kuwa umezidi kuwa juu vijijini ukikadiriwa kufikia asilimia 74.

**17. Mheshimiwa Spika,** bado rasilimali watu katika sekta ya afya nchini ni tatizo hususani katika maeneo ya vijijini. Bado wataalamu wetu wa afya wanafanya kazi kubwa kutokana na ongezeko kubwa la wagonjwa japokuwa wataalam wengi waliondolewa kwa kilichoitwa “vyeti feki” bila ya kuziba nafasi kwa idadi ya walioondolewa kazini. Pamoja na kuwa serikali imesema imetoa ajira tukumbuke kuwa ni serikali hiyo hiyo ndio inayotaka kufanya tafiti za upungufu wa watumishi na ndio hiyo hiyo inayoamua iseme nini kwa umma kuhusiana na ajira au mapungufu ya watumishi jambo ambalo linaathiri uhalisia wa matatizo katika sekta mbalimbali. Jambo ambalo linatia mashaka katika utatuzi wa changamoto mbalimbali zinazoikabili serikali.

**18. Mheshimiwa Spika,** tukumbuke kuwa pale ambapo taasisi au watu mbalimbali wanakuwa huru kufanya tafiti ndipo serikali inaweza kujikosoa na kufanya maboresho. Upungufu wa watumishi katika sekta ya afya ni tatizo linalohitaji umakini na weledi mkubwa la kulishugulikia kwani kuna hatari ya kuwepo kwa ongezeko kubwa la vifo vinavyotokana na ukosefu wa tiba kwa wakati.

**19. Mheshimiwa Spika,** ni hivi karibuni serikali ilikiri uhaba mkubwa wa madaktari. Kwa mujibu wa kumbukumbu, Serikali hii ya awamu ya tano iliwahi kutaka kuwapeleka madaktari 500 nchini Kenya ilhali nchi ikikabiliwa na tatizo kubwa na sugu la uhaba wa madaktari. Kwa mujibu wa Sensa ya Taifa ya Mwaka 2012 idadi ya madaktari na wauguzi kwa Tanzania ilikadiriwa kufikia 2,250 ambapo ni sawa na uwiano wa madaktari 0.5 kwa watu 10,000. Kwa mujibu wa gazeti la Guardian on Sunday mwaka 2013 nchi ilikuwa na upungufu wa madaktari 2,700<sup>2</sup>. Uchambuzi uliofanywa na the Citizen

---

<sup>2</sup> <https://www.ipppmedia.com/en/news/govt>

Tanzania mwaka 2016 unaonyesha uwiano kuwa daktari 1:25,000 kinyume na muongozo wa Shirika la Afya Duniani (WHO)

**20. Mheshimiwa Spika**, Serikali hiyo hiyo leo inatoa ajira 24 kwa madaktari na madaktari wa daraja la pili 45 tu kwa nchi nzima bila kujali ongezeko kubwa la watu kuanzia mwaka 2012 baada ya sensa ya taifa; ambapo idadi ya watu ilikuwa milioni 44 tofauti na sasa idadi ya watu kwa nchi yetu inakadiriwa kufikia takribani milioni 52.55 mpaka mwaka 2017 kwa mujibu wa Tume ya taifa ya takwimu. Kwa mujibu wa ripoti ya Benki ya Dunia inaonyesha uwepo wa idadi ya watu takribani milioni 56 mpaka mwaka 2017 huku nchi yetu ikitajwa kati ya nchi 5 Afrika zenye watu wengi zaidi kwa mujibu wa hotuba Waziri wa Fedha na Mpango ya mwaka 2017 kuhusu hali ya uchumi 2016 na Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Mwaka 2017/2018<sup>3</sup>.

**21. Mheshimiwa Spika**, Pamoja na ongezeko hilo kubwa la idadi ya watu serikali imeshindwa kuzalisha ajira za wataalamu na wanataaluma watakaoweza kukabiliana na changamoto zinazoibuka kila siku ikiwemo mlipuko wa magonjwa yale ya kuambukiza na hata yasiyo ya kuambuzi. Hata hivyo kwa mujibu wa The Citizen Tanzania, kuna wanafunzi wengi wanaohitimu mafunzo ya tiba na afya lakini ni wachache sana wanaopata ajira ya serikali kwani wengi huishia kuajiriwa na mashirika yasiyo ya kiserikali, kuajiriwa kwenye sekta za ujuzi tofauti na hata kujajiri wenyewe. Hii imejionyesha wazi kwenye randama ya Wizara Ukurasa wa 50 ambapo idadi ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na vyuo vya afya nchini walikadiriwa kuwa 47,269 huku ajira zilionekana kutolewa chache sana.

**22. Mheshimiwa Spika**, inashangaza kuona serikali ilitoa nafasi 2 tu kwa Madaktari washauri (Medical Consultant) ambapo hata hivyo serikali imekiri kushindwa kujaza nafasi hizo mbili<sup>4</sup>. Nchi nyingi duniani hasa zile za uchumi wa kati na

---

<sup>3</sup><https://habarileo.co.tz/index>.

<sup>4</sup> Tazama Randama ya mwaka 2018/19 Wizara ya Afya Fungu 52 uk 51.

zile zilizoendelea zimeweza kupiga hatua kubwa katika kuwekeza kwenye afya za wananchi wao. Viwanda haviwezi kuzalisha pasipo watu kuwa na uhakika wa tiba bora na uwezo wa kuonana na tabibu pale wanapomuhitaji. Pamoja na hilo tafiti za magonjwa, chanjo na tiba zinaweza tu kufanyika vyema hapa nchini kama serikali ikijikita kwenye uwekezaji wa afya. Mfano; kwa kupitia Bodi ya Madaktari wa California (Medical Board of California) mwaka 2015, katika ajenda zake kuu ni kuhakikisha kunakuwepo na madaktari na wataalamu wabobezi wa afya ambao watahakikisha maendeleo ya nchi yanaakisi uimara wa afya za raia. Kwa mantiki hiyo, uwekezaji katika afya ndio unaotoa mwelekeo wa uwekezaji katika sekta nyingine. Naweza kusema kuwa sekta ya afya ndio uhai wetuna ndio kichocheo kikuu cha maendeleo. (Health sector is paramount of all other sectors).

**23. Mheshimiwa Spika,** ukiangalia Randama ya Utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2018/19 uk 21& 22 unaonesha idadi ya wagonjwa waliopata huduma kwenye Hospitali za Rufaa za Kanda, Hospitali Maalum na Hospitali ya Taifa kwa kipindi hicho kuwa ni 920,245, ni jambo jema ila hatuambiwi wagonjwa hao wamehudumiwa na madaktari, manesi na wataalam wengine waliopo kwenye sekta ya afya wangapi? Ni vyema tueleze kwa uwazi rasilimali watu iliyopo na inayohitajika katika sekta ya afya ni kiasi gani kwa kila hospitali kwenye kanda zetu na mikoa pia?

**24. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kuwa afya ya Taifa ni jambo muhimu kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii; na kwamba utoaji wa huduma za afya za kibingwa kwa wakati zinaokoa muda wa uzalishaji na hivyo kuongeza ufanisi. Aidha, dawa za kuzuia magonjwa ni muhimu sawa na zile za kuponya magonjwa kwa kuwa zinasaidia kwa kiwango kikubwa kujenga ustawi na Taifa kuwa na afya.

**25. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi inaamini kwamba *utoaji wa huduma za afya sio tu huduma za kijamii bali pia ni biashara ambapo sekta binafsi* inashirikishwa kama mdau

mkubwa katika kutoa mafunzo ya kitabibu na kutoa huduma za afya. Hivyo basi, ni lazima ushirikishwaji wa sekta binafsi kupitia ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP) kujenga, kuendelea na kutumia miundombinu ya afya, kuongeza udahili wa mafunzo ya watendaji katika sekta ya afya ili kukidhi mahitaji ya jamii kupitia ubia kati ya sekta binafsi na sekta ya umma lakini Serikali ikibaki kuwa mbia mkuu.

**26. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini katika ubora wa huduma, hivyo itaanzisha mchakato wa kujitathmini kwa wahudumu wa afya kwa ajili ya maisha yao hapa Tanzania, viwango vyao vya maslahi, na ubora kwa ajili ya utoaji wa huduma<sup>5</sup>.

**27. Mheshimiwa Spika**, Randama inaonesha kuwa mwaka 2018/19 jumla ya wanafunzi 18,539 sawa na 123.59% ya malengo ya wanafunzi 15,000 ifikapo mwaka 2020 walichaguliwa kujiunga na masomo katika vyuo mbalimbali vya afya. Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza hivi ukidahili wanafunzi wa kuingia vyuo vya afya, ni kuwa tayari umekuwa na wataalam wa afya, je wakiondolewa kwa kushindwa masomo? Hii ni sawa na kuwa na mayai alafu unasema nina kuku tayari!!!!

## ii. Uwajibishaji wa watumishi wa sekta ya afya

**28. Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa taratibu na sheria zilizowekwa juu ya uwajibishaji wa watumishi wa sekta ya afya hasa madaktari; zipo hatua na taratibu za kinidhamu kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma kwa madaktari wote waajiriwa. Na kwa mujibu wa Sheria na Kanuni hizo hatua hizo ni pamoja na Baraza la Madaktari Tanganyika (MCT) ama Baraza la Wauguzi kwa upande wa wauguzi wenye kupewa mamlaka ya kutoa onyo na kuwasimamisha ama kuwafutia sifa za udaktari, madaktari ama wauguzi watakaokutwa na hatia baada ya malalamiko ya kutowajibika ama makosa yao kufikishwa kwenye Baraza husika.

---

<sup>5</sup> Sera ya Chadema uk. 44 hadi 48.

**29. Mheshimiwa Spika**, tangu Serikali ya awamu ya 5 iingie madarakani kumekuwapo na wimbi kubwa la wanasiasa na hasa wasiokuwa na mamlaka ya kinidhamu kuwawajibisha madaktari pasipo kufuata taratibu na kanuni zilizowekwa na hivyo kuzua sintofahamu katika jamii na kushusha hadhi za mamlaka za kinidhamu zinazostahili kuwawajibisha madaktari waajiriwa wa umma.

**30. Mheshimiwa Spika**, kumekuwana muendelezo wa matukio si tu yanayodhalilisha taaluma za watumishi wa sekta ya afya bali pia yanayoishusha thamani awamu ya tano na kuzipoka mamlaka husika wajibu wake na matukio haya ni kama ifuatavyo kwa uchache wake:

*i. Mwezi Machi mwaka 2017, Mkuu wa Wilaya ya Kilwa Christopher Ngubiagai alitangazwa na Jumuiya ya Madaktari Tanzania kuwa adui namba moja wa afya baada ya Mkuu huyo wa Wilaya kumuweka mbaroni Mganga Mkuu wa Wilaya ya Kilwa, Dkt Vitalis Katalyeba. Dkt Katalyeba alisimimashwa kazi kwa kutuhumiwa kuchelewesha gari la kubebea wagonjwa na kusababisha kifo cha mgonjwa huyo. Mara baada ya kusimamishwa, Dkt Katalyeba alihudhuria mkutano ambapo kitendo hicho kilimuudhi DC huyo na kuagiza Dkt. Katalyeba kutiwa mbaroni.*

*ii. Tukio jingine ni la Mkuu wa Mkoa wa Singida Bi. Rehema Nchimbi alipomuweka Rumande Mganga Mkuu wa Wilaya ya Singida Mjini Dr. Erivk Bakuza, pamoja na kuwa kulikuwa na mapungufu ya kiutendaji bado taratibu za uwajibishwaji wa kinidhadmu zilitakiwa kufuatwa.*

*iii. Katika tukio jingine, Mkuu wa Mkoa wa Arusha Ndg. Mrisho Gambo alimtaka Mganga Mkuu wa Wilaya ya Monduli kutoa maelezo ya malimbikizo mbalimbali ya stahiki za watumishi wa afya huku akijua wazi kuwa sio jukumu la Mganga wa Wilaya, Ikumbukwe kuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha ameendelea kuwa na historia mbaya na Madaktari kuanzia alipokua DC katika awamu ya nne ya CCM.*

iv. **Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi mwezi Septemba 2018 alimsimamisha kazi kwa madai ya wananchi ya kudhalilishwa na Mganga Mkuu wa Kituo cha Afya cha Ukami, Dk. Andrew Kitwanga. Hii ilipelekea kuwapo kwa mjadala mzito na hata Waziri wa TAMISEMI, Mhe. Suleiman Jaffo aliomba radhi kwa niaba ya Mkuu huyo wa Mkoa na kuahidi kutoa mwongozo kwa viongozi hawa juu ya hatua za kinidhamu.**

v. **April 2019, Daktari wa Kituo cha Afya Ngarenaro, Dkt. Japhet Kivuyo, mkoani Arusha baada ya kukutwa hayuko kazini uamuzi wa kufukuzwa kwake ulitolewa na Katibu Mwenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Levelosi.**

31. **Mheshimiwa Spika**, ikumbukwe kuwa matukio haya ya kudhalilisha hata kama yana uhalali na iwapo hayafuati taratibu na kanuni zilizowekwa, hupunguza morali kwa watumishi hawa MUHIMU. Kuongezeka kwa vitendo vya viongozi wa umma na sasa imehamia kwa viongozi wa Chama Tawala, kunafanywa ili kutafuta umaarufu wa kisiasa na havina nia ya dhati ya kukabiliana na changamoto za kipaumbele za sekta ya afya nchini.

32. **Aidha Mheshimiwa Spika**, ikumbukwe kuwa kukosekana kwa vitendea kazi ikiwemo magari ya wagonjwa na vifaa tiba ni kutokana na ufinyu wa bajeti za afya na pia ukosefu wa watumishi wa kutosha wa kada hii muhimu. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutekeleza wajibu wake ikiwemo kuhakikisha watumishi na vitendea kazi katika sekta ya afya vinapatikana. Vilevile, Serikali itimize wajibu wake wa kuwalipa stahiki watumishi wa afya pamoja na kuwapandisha madaraja watumishi wanaostahili na kuacha kuwasingizia waganga wakuu majukumu yasiyo yao pale Serikali inaposhindwa kutekeleza majukumu hayo.

iii. **Afya kwa wote (Universal Health Coverage)**

33. **Mheshimiwa Spika, Malengo ya afya kwa wote:** serikali kupitia Waziri wa Afya kwenye hotuba yake ya mwaka 2018/19 aya ya 118 alisema serikali **inalenga kufikia** mwaka 2020



Watanzania asilimia 70 wawe na bima ya afya. Lakini taarifa inaendelea kusema kuwa kwa sasa watu walio kwenye mfumo wa bima ya afya ni asilimia 32 na asilimia 68 ambao hawako katika mfumo huo. Maana yake ni kuwa kati ya watanzania 100 ni watanzania 32 tu ndio wana uhakika na matibabu ya afya zao na waliobakia 68 maisha yao yako mashakani.

**34. Mheshimiwa Spika,** kauli ya Waziri kwenye hotuba yake ni kauli ambayo haioneshi umakini wa serikali katika afya ya watanzania, hivyo Kambi ya Upinzani Bungeni haikuona kama ina mkakati wowote ambao serikali iliweka ili kuhakikisha watu 68 kati ya mia wanajiunga na bima ya afya. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa taarifa Bungeni ni wananchi wangapi mpaka sasa wamejiunga na bima ya afya hasa wale wa kipato cha chini.

**35. Mheshimiwa Spika,** nchi nyingi zimeweka utaratibu na mfumo wa kuhakikisha wananchi wake wanajiunga na bima ya afya. Mambo ya msingi ili kufikia lengo hilo ni pamoja na kuwa na mkakati wa kifedha wa kugharimia huduma za afya (Health Financing Strategy), mfumo wa kutoa ruzuku ya bima kwa watu wa hali ya chini (subsidized insurance), Sera na sheria jumuishi (Social participation). Mpaka sasa Serikali haijapitisha mkakati wa kugharimia huduma za afya toka mwaka 2015, na wala haijaweka mfumo wa kutoa ruzuku ya bima kwa watu wa kipato cha chini.

**36. Mheshimiwa Spika,** matokeo ya kutokuwa na bima ya afya kwa wote ni kuwa mtu akiugua na hana hela na huacha kwenda kutibiwa, na matokeo yake ni kuwa ugonjwa huwa mkubwa zaidi, husababisha usugu wa dawa na hatimaye kutozalisha na hata kusababisha kifo. Matokeo yake serikali na familia hutumia hela nyingi kumtibu mgonjwa aliyezidiwa kwa gharama kubwa. Familia zinaweza kusukumwa kwenye umasikini kwa sababu hizo.

**37. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri serikali kufanya yafuatayo: (a) Kutangaza kuwa inataka kusiwepo na Mtanzania anayekosa huduma za afya

kwa kutokuwa na hela, (b) Kuleta mpango mahususi wa mfumo utakaotumika kuhakikisha watu wa hali ya chini wanakuwa na bima ya afya, (c) Kupitisha na kutekeleza mkakati wa kugharimia huduma za afya (National Health Financing Strategy) na (d) Kuweka malengo ya kuongeza matumizi kwenye sekta ya afya kufikia asilimia 4-5 ya pato la taifa kama inavyopendekezwa na Shirika la Afya Duniani. ***Kwa ufafanuzi zaidi rejea sera ya Chadema uk 44 -47***

**38. Mheshimiwa Spika**, kufikia kiwango hicho cha asilimia 4-5 cha GDP kilichopendekezwa na shirika la afya la dunia kinawezekana kama Serikali itakuwa na nidhamu ya kujikita/ kubakia kwenye mpango wa maendeleo wa miaka mitano kama ulivyopitishwa na Bunge. Tumeona hivi sasa miradi mikubwa inatumia fedha za ndani au mikopo ya kibiashara wakati mpango upo wazi miradi mikubwa ya kimkakati inatakiwa kutekelezwa kwa ubia na sekta binafsi.

**iv. Huduma ya mama na mtoto**

**39. Mheshimiwa Spika**, Katika hotuba yake ya mwaka 2017/18 Wizara ilieleza Bunge lako tukufu kuwa kuanzia mwezi Oktoba ilianzisha utaratibu wa kutaka kila halmashauri na mikoa nchini kutoa taarifa ya vifo vinavyotokana na uzazi kila mwezi. Ikiwa imepita takribani miaka miwili toka utaratibu huo kuanzishwa Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza hadi sasa ni halmashauri ngapi nchini ambazo zimetokeleza utaratibu huo na kwa halmashauri na mikoa iliyoshindwa kufanyia kazi utaratibu huu zimechukuliwa hatua gani? na kwa mujibu wa takwimu na taarifa hizo je Wizara imeafanikiwa kwa kiwango gani kwa kutumia taarifa hizo katika kukabiliana na vifo vya mama na mtoto?

**40. Mheshimiwa Spika**, mojawapo ya malengo ya mkakati wa afya ya uzazi na mtoto wa mwaka 2016-2020 ni pamoja na kupunguza vifo vya watoto wa chini ya mwezi mmoja kutoka 21 hadi 16 ifikapo mwaka 2020 katika kila vizazi hai 1000 pamoja na vifo vya watoto wa chini ya umri wa mwaka mmoja kutoka 45 hadi 25 katika kila vizazi hai 1000 na vilevile vifo vya watoto wa chini ya miaka mitano kutoka 54 hadi 40 kwa kila vizazi hai 1000.

**41. Mheshimiwa Spika**, ni ukweli usiopingika kuwa takwimu za vifo vinavyotokana na uzazi nchini zimeendelea kupotosha hali halisi kwani kina mama wengi na watoto hasa vijijini wanafariki na idadi inaongezeka kutokana na kutokuwa na huduma bora za afya, kuongezeka kwa gharama za maisha, ukosefu wa umeme lakini vilevile miundombinu duni pamoja na upungufu mkubwa wa watumishi wa afya hasa madaktari wa akina mama na kukosekana kwa vitendea kazi na vifaa tiba vinavyotokana na ufinyu wa bajeti.

**42. Mheshimiwa Spika**, ifike mahali sisi kama Taifa, tuweke mbali siasa katika masuala muhimu nchini hasa masuala ya uzazi ili kuhakikisha adhema ya kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi.

Aidha, huduma ya afya bila malipo kwa wanawake wajawazito na watoto chini ya miaka mitano ni mojawapo ya sehemu ya Sera ya Afya ya Tanzania lakini mpango huu bado una mapungufu makubwa nchini. Kwa mujibu wa Takwimu bado wanawake 11000 hupoteza maisha nchini sawa na kina mama 30 kila siku. Bado katika hospitali mbalimbali na vituo vya afya kina mama wajawazito wanatakiwa kujinunulia vifaa vya kujifungulia kama pamba, nyembe, gloves na hata wakati mwingine huambiwa wanunue mipira ya kulalia wakati wa kujifungusa pamoja na kuwa serikali imesititiza kuwa vifaa hivyi hupatikana bure hospitali.

**43. Mheshimiwa Spika**, bado kumekuwa na malalmiko kuwa baadhi ya vifaa tiba vinavyotolewa na Bohari ya Dawa (MSD) havina ubora unaotakiwa na kuwa vinaharibika mapema na hivyo kuongeza changamoto katika huduma za kujifungulia.ni lazima wizara, iwajibike katika kuhakikisha changamoto hizi zinatatuliwa kwa wakati.

**v. Wakunga wa jadi**

**44. Mheshimiwa Spika**, ni dhahiri kuwa ukosefu wa huduma za afya nchini bado umeendelea kuwa changamoto hasa katika masuala ya uzazi hususani maeneo

ya vijijini. Kwa mujibu wa Takwimu zilizotolewa na Shirika la Afya Duniani (WHO), zinaonesha kuwa zaidi ya asilimia 60 ya wanawake wanaojifungua vijijini nchini hukosa usaidizi wa wataalamu na hivyo kupelekea kina mama hao kutafuta huduma za wakunga wa jadi.

**45. Mheshimiwa Spika**, mojawapo ya habari zilizowahi kuripotwa na vituo vikubwa ulimwenguni vya habari ni pamoja na habari iliyoripotwa na SHIRIKA LA HABARI LA UINGEREZA (BBC) tarehe 17 Aprili 2019 iliyokuwa na kichwa cha habari "Wakunga wa jadi wawazalisha wanawake kwa kutumia mifuko ya Rambo Tanzania. kwa mujibu wa chapisho hilo la habari ilionekana kuwa baadhi ya vijiji mkoani Tabora hasa wilaya ya Sikonge, wakunga wa jadi hulazimika kuwazalisha kina mama majumbani na mara nyingi hulazimika kutumia mifuko ya Rambo na hii uongeza hatari ya magonjwa sio tu kwa kina mama hata kwa wakunga wanaowasaidia hata kwa watoto wanaozaliwa.

**46. Mheshimiwa Spika**, pamoja na marufuku iliyotolewa na Wizara ya Afya ya kuwapiga marufuku wakunga wa jadi kuwazalisha kina mama majumbani, Wizara ilieleze Bunge lako ni njia gani kina mama wa vijijini watumie hasa ukizingatia kuwa kuna matatizo ya usafiri na uhaba wa vituo vya afya vijijini. Kuwazuia wakunga wa jadi sio tu kunaongeza idadi ya vifo vya mama na mtoto bali kunaathiri kina mama wengi hasa ukizingatia kuwa wakunga wa jadi ni wakombozi wa kina mama ambao wengi wanaishi katika umasikini uliokithiri. Kambi ya Upinzani Bungeni inaitaka Wizara ya Afya kuweka mkakati wa kutoa elimu na mafunzo ya awali kwa wakunga wa jadi na kuwawezesha ili kuwa mbadala wa watoaji huduma za afya hasa pale kunapokua na changamoto isiyotarajiwa katika maeneo husika na kupunguza idadi ya vifo vinavyotokana na uzazi.

**47. Mheshimiwa Spika**, ni wazi kuwa ikiwa wakunga wa jadi watapewa mafunzo stahiki basi Taifa litaondokana na changamoto hii kama ambavyo kwa upande wa Zanzibar wamefanikiwa kuwashirikisha wakunga wa jadi na wataalam wa afya.

vi. **Hali ya ugonjwa wa homa ya ini- (Hepatitis)**

**48. Mheshimiwa Spika**, ugonjwa wa Homa ya Ini au Hepatitis hutokana na kirusi kinachoambukizwa kupitia kwenye damu na majimaji mengine ya mwili, na ambacho huvamia ini na kusababisha vifo vya watu wapatao 650,000 kila mwaka, wengi wao wakiwa katika nchi za kipato cha chini na kipato cha wastani.

**49. Mheshimiwa Spika**, Shirika la Afya Duniani, WHO ambalo ni kinara katika magonjwa mathalani homa ya ini aina ya Hepatitis hivi karibuni limetoa mwongozo wake wenye mapendekezo sita kuhusu matibabu ya ugonjwa huo.

**50. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Tanzania imesema kuwa, maambukizi ya ugonjwa wa Homa ya Ini au Hepatitis, yameongezeka mara mbili yakilinganishwa na Virusi vya Ukimwi (HIV) nchini. Aidha, ugonjwa wa Homa ya Ini (Hepatitis) unaongoza kwa kuu Watanzania kutokana na maambukizi yake kufikia asilimia 16, huku virusi vya ugonjwa wa Ukimwi, ikiwa ni asilimia 5.3. Ugonjwa huo huua taratibu ukilinganishwa na magonjwa mengine kwa kuwa dalili zake huchukua muda mrefu kuweza kujulikana na kujitokeza wazi kwa magonjwa.

**51. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuweka wazi kwa watanzania ni jinsi gani ugonjwa wa homa ya Ini umeenea, na kinga au chanjo yake inapatikana vipi ili kukinga maambukizi, Matibabu yapi yatumike awali na yapi yafuatie ikiwa ya awali hayakufanya kazi, na pia jinsi ya kufuatilia mambo hayo manne tajwa sambamba na kuangalia kama kuna saratani ya ini, na kiasi gani ugonjwa wa ini unavyoendelea.

**52. Mheshimiwa Spika**, takwimu za shirika la afya la Dunia zinaonesha kuwa inakadiriwa watu milioni 240 kote duniani wana kirusi cha Hepatitis, idadi kubwa ya maambukizi ikipatikana Bara Afrika na Asia<sup>6</sup> hasa kwa watu ambao ni masikini.

---

<sup>6</sup> <https://news.un.org/sw/story/2015/12/437292-madhara-na-tiba-dhidi-ya-ugonjwa-wa-homa-ya-ini-aina-ya-hepatitis-b>

vii. **Hali ya maambukizi vvu na ukimwi nchini**

**53. Mheshimiwa Spika**, mapema mwezi Machi mwaka huu wa 2019, tume ya kudhibiti Ukimwi nchini (TACAIDS) ilitoa ripoti yake kuhusu maambuzi mapya ya VVU nchini. Katika ripoti yake ilibaini kuwa takribani Watanzania 225 huambukizwa virusi vya UKIMWI kwa siku. Huku Watanzania takribani 6,750 huambukizwa kwa mwezi na kwa mwaka takribani watu 82,125 huambukizwa virusi vya Ukimwi. Katika ripoti hiyo maambukizi makubwa yalionekana kati ya vijana wenye umri wa miaka 15-24 na wengi wao wakiwa ni vijana wa kike. Kwa mujibu wa tume ya taifa ya takwimu (NBS) mpaka 2017 takribani watu milioni 1.4 walikutwa na maambukizi ya Ukimwi<sup>7</sup>. Hii inaonyesha ongezeko la maambukizi tofauti na tafiti zilizofanyika mwaka 2010-2015 ambapo maambukizi yalipungua kwa asilimia 20 (UNAIDS 2017).<sup>8</sup>

**54. Mheshimiwa Spika**, dhana nzima ya 90- 90- 90 iliyoanzishwa na Umoja wa Mataifa kuhusu HIV/AIDS mwaka 2013 kwamba ili kufikia mwaka 2020 kusiwepo na maambukizi ya UKIMWI Duniani. Kwa maana ya kuwa 90% ya watu walioambukizwa virusi watakuwa wametambulika, 90% ya walioamtambulika watakuwa tayari wapo kwenye matibabu ya ARV na 90% ya walio kwenye matumizi ya ARV, virusi vitakuwa vimefubaa na hivyo hakutakuwa na maambukizi mapya. **Hiyo ndiyo dhana nzima ya 90 90 90**

**55. Mheshimiwa Spika**, Mkakati huo ulikuwa unajaribu kuzuia na kudhibiti maambukizi ya HIV kwa kutumia kanuni kuu ya kupima na kutibu (test and treat) wale wote wenye virusi ili kufikia lengo la 90 90 90. Kwa upande wa Africa nchi ya Botswana ndiyo inayokaribia kufikia lengo la 90-90-90 kwa kupima, kutibu na kufubaza virusi, na hili liliwezekana kwa nchi hiyo kwani ilikuwa nchi ya kwanza katika Africa kutoa matibabu ya ARV bure kwa watu wote wenye HIV tangu mwaka 2002.

---

<sup>7</sup><http://www.mwananchi.co.tz/habari/Wilaya-vinara-kupima-VVU-kwa-hiari/1597578-3471102-5txvow/index.html>

<sup>8</sup>[www.avert.org/professionals/hiv/around-world/sub/saharan-africa/tanzania](http://www.avert.org/professionals/hiv/around-world/sub/saharan-africa/tanzania).

**56. Mheshimiwa Spika**, katika kongamano la siku latu lililofanyika **Dodoma-** kuanzia (June 20, 21, and 23, 2018) kuhusu jukumu na wajibu wa viongozi katika kufika lengo la HIV la 90-90-90 kwa mwaka 2020 Tanzania, ambalo liliandaliwa na Kamati ya Bunge ya UKIMWI kwa pamoja na Baraza la Watu Waishio na HIV/AIDS Tanzania (NACOPHA) ambao waliratibu wadau na asasi zisizo za kiraia chini ya Waziri Mkuu, Spika wa Bunge na Mjumbe kutoka USAID wakiwa waongoza jopo. Waziri Mkuu alisema kuwa Serikali kupitia TACAIDS inatekeleza mkakati wa kufikia lengo la 90-90-90.

**57. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kufahamu hadi sasa katika kufikia lengo la 90-90-90 Tanzania tumefikia wapi kwani tumebakiza mwaka mmoja na nusu kufikia muda uliowekwa na Umoja wa Mataifa?

**58. Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Takwimu za UNAIDS za mwaka 2018 zinaonesha kuwa Tanzania ina watu milioni 1.5 wanaoishi na virusi vya Ukimwi (HIV) na 4.5% ni watu wenye umri wa kati ya miaka 15-49 wenye maambukizi na kuweza kueneza HIV, watu 65,000 wana maambukizi mapya(*New HIV Infections*) na vifo 32,000 vilisababishwa na UKIMWI, 68% ya watu wazima wapo kwenye matibabu ya ARV na 46% ni watoto walio kwenye matibabu ya ARV.

**59. Mheshimiwa Spika**, hali hii inatisha sana hasa tukizingatia kuwa maambukizi kwa vijana hawa wadogo ni asilimia 46. Wengi wa vijana hawa ni wale wenye umri wa kumaliza shule ya msingi mpaka chuo kikuu. Maana yake ni kuwa nguvu kazi ya taifa inapungua kwa kasi sana na pengine tatizo hili lisipochukuliwa kwa uzito mkubwa pengine miaka kadhaa mbele tutakakosa kabisa vijana wenye afya bora wa kulijenga taifa letu.

**60. Mheshimiwa Spika**, kuna haja sasa kuwekeza nguvu zaidi katika njia za kuzuia maambukizi mapya badala ya kutenga fedha nyingi katika kutibu magonjwa nyemelezi. Kwani kinga ni bora kuliko tiba. Ni muhimu kufanya tafiti zenye tija ili kuweza kubaini sababu zinazopelekea maambuzi

makubwa kwa vijana wenye umri huu mdogo tofauti na miaka ya nyuma ambapo vijana wenye umri wa kati kuanzia miaka 35-49 ndio waliobainika kuathirika zaidi.

**61. Mheshimiwa Spika**, kubadilika kwa mfumo wa maisha, hali ngumu sana ya uchumi ambapo kwa sasa vijana hutumia lugha isiyo rasmi kuwa 'vyuma vimekaza', kupungua kwa jitihada za kupaza sauti na elimu juu ya masuala ya Ukimwi, ongezeko la ngono zembe na pengine changamoto za upatikaji wa dawa za kufubaza virusi zinaweza kuwa miongoni mwa sababu za maambukizi makubwa na ya kutisha kwa vijana hawa wadogo.

**62. Mheshimiwa Spika**, pamoja na hayo pameibuka wimbi kubwa la ulawiti wa watoto hasa wa kiume. Jambo hili sio la kufumbia macho hata kidogo. Serikali na wadau mbalimbali lazima tuungane kukemea vitendo hivi viovu wanavyofanyiwa watoto. Japokuwa mambo haya huchukuliwa pia kwa usiri mkubwa kutokana na mila na desturi zetu lakini hatuna budi kama taifa kuanza kukemea hadharani mambo haya. Vitendo vya ushoga navyo vimeshamiri jambo ambalo linachochea kwa kasi maambuzi mapya ya virusi vya Ukimwi<sup>9</sup>

**63. Mheshimiwa Spika**, vile vile pamekuwa na malalamiko kwenye jamii juu ya uwepo wa takwimu zinazotolewa zisizo za kweli kuhusu maambukizi kwa sababu za kujipatia fedha kutoka kwa wafadhili. Takwimu za maambukizi zinatumiwa kama sehemu ya 'miradi ya upigaji'. Novemba 28, Mwaka 2017 Waziri Mkuu aliitoa kauli ya kukemea matumizi mabaya ya fedha za miradi ikiwemo miradi ya UKIMWI jambo ambalo linaonyesha dhahiri fedha nyingi za serikali zinazotengwa katika kupambana na janga la UKIMWI zinatumiwa kinyume na mpango wa matumizi na hivyo kuathiri juhudi za kupambana na janga hili.

---

<sup>9</sup> Mpondo B, Gunda D, Kilonzo S. (2017): HIV Epidemic in Tanzania; The possible Role of the key population – TZ.



**64. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka huu wa fedha takribani bilioni 84.9 zimetengwa kwa ajili ya kudhibiti maambukizi na kuboresha huduma kwa watu wanaoishi na virusi. Fedha hizi ni nyingi sana na hivyo ni lazima jitihada za makusudi zichukuliwe sasa ili kupunguza tatizo hili la sivyo, bajeti kubwa ya serikali itaendelea kutumika katika kupambana na ugonjwa huu bila mafanikio. Katika hotuba ya Waziri Mkuu aliyotoa akifungua kongamano la kitaifa la maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani Jijini Dar es Salaam alitoa kauli ya maazimio ya kumaliza tatizo la Ukimwi nchini ifikapo mwaka 2030.

**65. Mheshimiwa Spika**, Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali iliambie Bunge lako; ina mikakati gani ya kumaliza tatizo hili ifikapo mwaka 2030 iwapo kasi ya maambukizi kwa vijana wadogo inaongezeka, upatikanaji wa dawa za kufubaza virusi ni wa kusuasua na maeneo mengi nchini hayapati dawa kwa wakati. Serikali ituambie ni nini mkakati wake katika kukabiliana na ongezeko kubwa la vitendo vya ulawiti na ushoga nchini ambapo tafiti mbalimbali zinaonyesha maambukizi ni makubwa zaidi hasa kwa wanaume wanaoshiriki ngono za jinsia moja (MSM).

**viii. Magonjwa yasiyo ya kuambukiza (Non communicable diseases- NCD)**

**66. Mheshimiwa Spika**, magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama vile kisukari, magonjwa ya moyo, maradhi yanayohusiana na upumuaji na saratani yanazidi kuongezeka kwa kasi na yanaendelea kuwa chanzo kikuu cha vifo duniani kote. Inakadiriwa Kisukari pekee kimeathiri maisha ya watu takriban 371 milioni duniani kote, huku 80% ya idadi hiyo ikiishi katika nchi zenye uchumi wa kati na nchi masikini. Kwa upande wa Tanzania, takriban watu wazima 9 kati ya 100 wana ugonjwa wa kisukari, na mtu mzima 1 kati ya 3 ana tatizo la shinikizo la juu la damu.

**67. Mheshimiwa Spika**, gharama ya kukabiliana na Magonjwa yasiyo ya kuambukiza duniani kote ni mabilioni ya dola na hivyo kusababisha upotevu mkubwa wa rasilimali

finyu zilizopo. Kwa mwaka 2010 Shirika la Afya Duniani lilikadiri kuwa jumla ya gharama za huduma za afya zinazohusiana na kisukari zilifikia dola 378 bilioni duniani kote, na kiasi hiki cha fedha kinaweza kufikia dola 490 bilioni ifikapo mwaka 2030.

**68. Mheshimiwa Spika**, nchi zinazoendelea kama vile Tanzania (na hata nchi zilizoendelea pia) hazina rasilimali za kutosha kutibu watu wote wanaobainika kuwa na kisukari. Hivyo, jitihada za kukabiliana na tatizo hili ni budi zikajikita zaidi katika mitazamo jumishi inayolenga kukinga ili kupunguza kiwango cha Magonjwa yasiyo ya kuambukiza kwenye jamii yetu. Kinga ni bora kuliko tiba!!!!

**69. Mheshimiwa Spika**, tatizo la Magonjwa yasiyo ya kuambukiza linakua kwa kasi katika nchi zinazoendelea, kama Tanzania. Inakisiwa kuwa mwaka 2020 magonjwa haya yasiyo ya Kuambukiza yatasababisha asilimia 73% ya vifo vyote duniani na asilimia 60% ya ukubwa wa tatizo la magonjwa duniani.

**70. Mheshimiwa Spika**, visababishi vikubwa vya magonjwa yasiyoyakuambukiza ni: **(a)**. Kutofanya mazoezi - kukaa darasani, ofisini, kuangalia runinga, kutumia lifti, kupanda magari na kutoshiriki michezo mbalimbali; **(b)**. Ulaji usiofaa - kula chakula kuzidi mahitaji ya mwili na hivyo kunenepa, kula mafuta na chumvi zaidi ya mahitaji ya mwili, kutokula mbogamboga na matunda kiasi cha kutosha; kula nafaka zilizokobolewa; **(c)** Matumizi ya pombe- tumbaku na madawa ya kulevya;**(d)** Msongo wa mawazo

#### **ix. MATIBABU NJE YA NCHI**

**71. Mheshimiwa Spika**, taarifa ya CAG ya mwaka 2016/17 ilionesha kuwapo kwa mapungufu katika usimamizi wa madeni kwenye matibabu nje ya nchi kwamba kulikuwa na kiasi kikubwa cha madeni kilichofikia Shilingi trilioni 2.68 kiasi ambacho ni ongezeko la Shilingi trilioni 0.793 sawa na asilimia 36 kulingana na salio la Shilingi trilioni 1.979 kwa mwaka ulioishia 30 Juni 2016.

**72. Mheshimiwa Spika,** Pia kulikuwepo na ongezeko kubwa la deni la gharama za matibabu nje ya nchi kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto katika hospitali za India kutoka kiasi cha Shilingi 28,609,803,615.40 kilichoripotiwa tarehe 30 Juni 2017 hadi kiasi cha Shilingi 45,731,070,267.31 kufikia tarehe 31 Desemba, 2017 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 37.44 kwa kipindi cha miezi sita tu.

**73. Mheshimiwa Spika,** Matumizi ambayo hayajalipwa ya gharama za matibabu ya wagonjwa waliotibiwa katika Hospitali za rufaa nchini India, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2018 gharama za hospitali zilikuwa kiasi cha Sh.29,172,371,931.26 ukilinganisha na mwaka wa fedha uliopita gharama zilikuwa kiasi cha Sh.28,609,803,615.40 kuna ongezeko la kiasi cha Sh.562,568,315.80, sawa na asilimia mbili.

**74. Mheshimiwa Spika,** tunafahamu kuwa kupatiwa matibabu kwa mtanzania ni haki yake na pale sheria zinapotoa utaratibu wa haki hiyo, lakini kumekuwapo na utaratibu usioridhisha wa kiupendeleo kwa wagonjwa wanaostahili kupatiwa matibabu nje ya nchi kulingana na maradhi yanayowakabili. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa kitendo hicho cha kibaguzi katika matibabu kwa watanzania kinaleta hisia kwamba kuna watanzania wa daraja la kwanza, daraja la pili na la tatu wakati watanzania wote hao wanalipa kodi moja kwa moja au sio moja kwa moja (direct or indirect tax payers).

**75. Mheshimiwa Spika,** kwa muktadha huo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa mchanganuo mzuri wa fedha zilizotumika kwa matibabu ya vigogo nje ya nchi ili ionekana wazi kwa walipa kodi jinsi kodi zao zinavyotumika.

#### **x. Taasisi ya Chakula na Lishe**

**76. Mheshimiwa Spika,** Randama ya Wizara Fungu 52 inaonyesha kwamba; Mradi Na. 5496, (*Tanzania Food and Nutrition Center*) katika Taasisi ya Chakula na Lishe; haukutengewa fedha yoyote kwa mwaka wa fedha 2017/

18; na pia kwa mwaka mpya wa fedha 2018/19. Katika kitabu cha taarifa za utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa kipindi cha Julai mpaka Februari 2018 kimeonyesha kuwa serikali ina azma ya kupunguza vifo vya watoto vitokanavyo na udumavu, ukosefu wa madini joto na vitamin A.

**77. Mheshimiwa Spika**, Upungufu wa vitamin na madini joto ni tatizo kubwa sana inalowaathiri watoto na wanawake walio katika umri wa kuzaa. Kwa mujibu wa Taarifa ya Demographic Health Survey 2010 Takwimu zinaonyesha kwamba takribani asilimia 59 ya watoto wadogo na asilimia 41 ya kina mama wajawazito wanaathiriwa na ukosefu wa madini joto. Pamoja na kwamba kitabu cha randama ukurasa wa 70 serikali imeonyesha kuwa inatoa Vitamini A na dawa za kutibu minyoo kwa watoto wadogo takribani nchi nzima lakini uhalisia wa utekelezaji wa azma hii ya serikali unatia mashaka sana.

**78. Mheshimiwa Spika**, katika mpango wa bajeti kwa mwaka 2018/19 taasisi haikutengewa fedha yoyote. Lakini katika taarifa ya utekelezaji kwa taasisi hii inaonesha kuwa katika kipindi cha Julai 2018 hadi Februari, 2019 taasisi imetoa mafunzo kwa wazalishaji wa chumvi 706 na Maafisa wa Afya, Maafisa Lishe na Wataalam wa Maabara wapatao 65, katika halmashauri mbalimbali zinazozalisha chumvi kwa wingi. Hoja ya msingi fedha zimetoka wapi katika kutekeleza majukumu hayo? Na kwa bahati mbaya pia kwa mwaka huu wa fedha 2019/20 taasisi hiyo kwa fedha za maendeleo haikutengewa fedha yoyote.

**79. Mheshimiwa Spika**, mwaka fedha 2017/18, Kambi Rasmi ya Upinzani ilizungumzia kwa kina tatizo kubwa la udumavu nchini. Tatizo hili lina athari kubwa sana kwa taifa kwani kwa kadiri ongezeko la watoto wenye udumavu nchini linafumbiwa macho ndivyo hivyo taifa hili linavyozidi kuzalisha watoto wasio na uwezo wa kujifunza darasani na wasio na uwezo wa ung'amuzi wa mambo (reasoning ability) yaani 'vilaza au mbumbumbu'. Kwa mujibu wa utafiti wa REPOA wa mwaka 2014 takribani watoto milioni 2.4 nchini walikuwa na tatizo la udumavu. Hali hii inatisha sana na inazidi kukua

kutokana na ukweli kwamba siku hizi watoto wengi mashuleni hawapati lishe kutokana na serikali kupiga marufuku michango mashuleni na huku ikijua wazi haina uwezo wakugawa vyakula mashuleni. Jambo hili linazidi kuhatarisha zaidi afya za watoto hususani wale wanaotoka katika kaya maskini ambapo watoto walitegemea kula mlo mmoja tu shuleni kwa kuwa familia zao zinashindwa kupata angalau milo miwili kwa siku.

**80. Mheshimiwa Spika**, tatizo hili la udumavu lina athari za muda mfupi na zile za muda mrefu. Hata kama mtoto aliathirika na udumavu utotoni athari zake zinaweza kuonekana pale anapokuwa mtu mzima. Tatizo hili huonekana pia sio katika elimu pekee bali pia katika uwezo wa kawaida wa ubunifu na ufikiri wa hali ya juu. Jambo hili linajidhihirisha wazi kwani katika mkutano wa wafanyabiashara na Rais uliofanyika Ikulu Mwezi Machi 2018 mmoja wa wafanyabiashara alilalamikia uwepo wa waajiriwa wenye Shahada ya Pili (Masters) lakini hawawezi kuandika barua za kitaalamu. Na ni kweli pia tumeona wasomi wa PHD wanashindwa kutimiza majukumu yao kwa mujibu wa sheria na katiba na kuipeleka jamii katika mtafaruku usio na sababu.

**81. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inarudia nukuu iliyoitoa katika hotuba yake ya Afya kwa Mwaka wa fedha 2017/2018 iliyosema “Hatuwezi kupata viongozi wa serikali wenye uwezo mkubwa wa kutafuta suluhu ya matatizo yanayolikabili Taifa kama utotoni waliwahi kuugua tatizo la udumavu au hawakupata lishe bora, kamwe hatuwezi kutengeneza think tank ya taifa kama taifa limejaa watoto wenye udumavu au walioathirika na udumavu utotoni. *“Udumavu hudumaza akili, husababisha ubongo wa mtoto au mtu mzima kushindwa kufanya kazi kwa haraka na kwa ufasaha”*.

**82. Mheshimiwa Spika**, pamoja na hilo, kitendo cha Wizara kushindwa kutoa fedha katika kitengo hiki cha lishe maana yake ni kuwa tutakuwa na ongezeko kubwa la watoto wanaougua minyoo au walioathirika na minyoo

jambo ambalo ni hatari sana kwani wapo minyoo ambao huathiri ubongo na uwezo wa kufikiri wa mtoto.

**83. Mheshimiwa Spika**, tunakumbuka katika serikali zilizopita kitengo hiki hakikuwahi kukosa fedha hata kidogo. Tafiti za magonjwa yatokanayo na lishe zinaweza vipi kufanyika endapo kitengo hiki muhimu kinakosa fedha. Je, serikali hii ya awamu ya tano ina mkakati gani wa kupunguza tatizo la idadi kubwa ya watoto walio katika hatari ya kuwa 'vilaza' kutokana na ukosefu wa lishe bora ikiwa kitengo muhimu kinachohusika na utatuzi wa tatizo kiko taabani kwa ukosefu wa fedha?

**xi. Hali ya Afya ya Akili Nchini (Generalized Anxiety Disorder- Gad)**

**84. Mheshimiwa Spika**, Hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara hii; kwa miaka miwili mfululizo, imezungumzia kushamiri kwa ugonjwa wa akili nchini. Katika hotuba ya mwaka wa fedha 2017/2018 tulionyesha kwamba takribani watu 150-200 huhudhuria kliniki kwenye hospitali zinazotoa huduma kwa watu wenye matatizo ya akili kwa wiki kwa Mkoa wa Dar es Salaam pekee. Idadi hii ni kubwa mno!!!

**85. Mheshimiwa Spika**, pamoja na kwamba jambo hili linaonekana kupuuzwa na kutotiliwa mkazo na Wizara pamoja na wadau mbalimbali nchini vikiwemo vyombo vya habari, ni muhimu serikali hii ikatambua kuwa kumekuwa na ongezeko la matukio ya kujua, kuuana ndani ya familia, watu kutembea wakizungumza wenyewe barabarani n.k. Hali hii pengine inaweza kuchangiwa na wasiwasi kupita kiasi juu ya maisha ya kila siku pamoja na matukio yake hali inayopelekea watu wengi kuwa na wasiwasi na hofu za maisha.

**86. Mheshimiwa Spika**, Katika hotuba ya Kambi ya Upinzani tulikwenda mbali zaidi kueleza idadi ya madaktari ambao ni wataalamu wa magonjwa haya ya akili ambapo mpaka mwaka jana 2017; idadi ya madaktari hao

walikuwa 26 tu kwa nchi nzima, huku hospitali Kuu ya Magonjwa ya akili Dodoma ikiwa na madaktari 5 tu.

**87. Mheshimiwa Spika**, hali ya hofu isiyo na kikomo huathiri zaidi uwezo wa mtu katika kufikiri na baadae huweza kuleta matatizo makubwa zaidi. Katika maadhimisho ya siku ya Afya ya Akili Duniani ambayo huadhimishwa kila tarehe 10 ya mwezi Oktoba kila mwaka, kwa mwaka 2017, kauli mbiu ilikuwa ***Afya ya Akili Mahali pa Kazi.***

**88. Mheshimiwa Spika**, magonjwa ya akili ni magonjwa ambayo yanaathiri au yanapeleka mabadiliko katika kufikiri, kuhisi, kutambua na kutenda mambo. Hata hivyo mabadiliko ya kitabia au mwenendo wa mtu huweza kuwa wa tofauti na usioendana na mwenendo wa jamii husika, mila au desturi. Magonjwa ya akili huathiri ufanisi wa utendaji kazi, na hivyo husababisha migogoro, na kuathiri uhusiano wa mtu husika na kuathiri jamii nzima inayomzunguka. Ni vyema pia jamii ikatambua matatizo ya afya ya akili hayaathiri watu maskini peke yao, bali pia hata viongozi. ***Tatizo hili lisipotafutiwa ufumbuzi linaweza kuleta athari kubwa hasa kwa watu walio katika ngazi za maamuzi (decision making)***

**89. Mheshimiwa Spika**, Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua je, kutokana na uhaba mkubwa wa watumishi katika vitengo vya afya nchini, serikali ina mkakati gani mahususi wa kuongeza rasilimali watu katika hospitali na vitengo vinavyoshughulikia matatizo ya afya ya akili? Je, serikali inampango gani kupunguza matatizo ya afya ya akili mahali pa kazi na kuielimisha jamii kwa ujumla kuhusiana na matatizo ya afya ya akili ili kupunguza athari za matatizo yanayotokana na changamoto za kimaisha hususani hali ngumu ya maisha, madeni, unyanyapaa au kubaguliwa katika familia au jamii kwa ujumla.

xii. **Afya na usafi wa mazingira**

**90. Mheshimiwa Spika, katika kikao ambacho** Mkurugenzi Mkuu wa WHO Tedros Adhanom Ghebreyesus, Mkurugenzi Mkuu wa Mazingira wa Umoja wa Mataifa Erik Solheim na Katibu Mkuu wa World Meteorological Organisation- Petteri Taalas waliwaalika wajumbe katika Mkutano wa Afya wa Dunia unaofanyika kila mwaka juu ya vipaumbele, fursa na changamoto katika miezi na miaka ijayo kuhusu afya ya dunia.

**91. Mheshimiwa Spika, Dr Tedros alisema kwamba** *“Ikiwa tunataka kufikia Afya kwa Wote, tutahitaji kuweka gharama katika afya kwenye mambo makuu, na hiyo ina maanisha mambo makuu hayo matatu ni: kuzuia, kuzuia, kuzuia”*. Aidha, alisema kwamba; *“lazima tuhakikishe watu wanaweza kupumua hewa safi, kunywa maji salama, kuishi katika hali nzuri na kula chakula cha lishe bila ya uchafuzi.”*

**92. Mheshimiwa Spika, Kulingana na takwimu za WHO,** wastani wa watu milioni 7 hufa kila mwaka kutokana na magonjwa yanayohusiana na uchafuzi wa hewa, ikiwa ni pamoja na viharusi na ugonjwa wa moyo, ugonjwa wa kupumua na kansa. Uchafuzi wa hewa katika miji mikubwa mikubwa unazidi viwango vya ubora wa hewa vya WHO.

**93. Mheshimiwa Spika, hivyo basi kama ambavyo** tumekuwa tukisema kwamba Mazingira ni mtambuka, na inategemea mazingira inatumika katika muktadha upi, katika sekta ya afya mazingira yanahusisha mambo kadhaa na machache tayari yameongelewa katika nukuu ya Mkurugenzi Mkuu wa WHO.

**94. Mheshimiwa Spika, ni ukweli kwamba mazingira katika** sekta afya ni muunganiko mzima wa njia safi na salama ya matumizi ya vyoo, uteketezaji wa taka zinazotoka mahospitalini, usafi wa miili yetu kabla na baada ya kula chakula, usafi wa mazingira kwenye maeneo tunayoishi ili kudhibiti magonjwa ya mlipuko na vievile kuangamiza mazalia ya wadudu waletao magonjwa.



95. **Mheshimiwa Spika**, taarifa ya utekelezaji inaonesha tu kazi zilizofanyika hadi Februari, 2019, lakini haioneshi kazi hizo zilitakiwa zitumie kiasi gani cha fedha na fedha zilizotumika ni kiasi gani ili Bunge liwezi kupima, thamani ya fedha za walipa kodi kama zimetumika vyema.

## C. MAENDELEO YA JAMII

96. Mheshimiwa Spika, sekta hii miongoni mwa majukumu yake ya msingi ni kushirikisha jamii katika kujiletea maendeleo, kukuza usawa wa kijinsia na uwezesaji wanawake, kukuza haki za mtoto na maendeleo ya familia katika jamii kuimarisha upatikanaji wa haki na huduma za ustawi wa jamii katika makundi maalumu.

97. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2018/19 Sekta hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi 32,140,649,000.00 lakini kati ya fedha hizo matumizi mengineyo zilitengwa shilingi 12,109,842,000.00 na fedha za maendeleo zilitengwa shilingi 4,913,845,000.00 hadi mwezi Februari fedha za maendeleo zilizokuwa zimepokelewa ni shilingi 1,133,506,431.00 zote zikiwa ni fedha kutoka nje kwa wafadhili.

98. **Mheshimiwa Spika**, kama ambavyo mara zote Kambi Rasmi ya Upinzani inasema tusiweke rehani kwa wafadhili mambo yanayohusu maendeleo ya wananchi wetu, iwe kwenye afya (uhai), iwe kwenye elimu na ustawi mwingine uonahusu wananchi. Hili ni kosa ambalo linapelekea kuingiziwa mambo ambayo sio mila na tamaduni zetu katika mchakato mzima wa misaada hasa kwenye maendeleo na huduma kwenye jamii zetu.

### i. Maendeleo na makuzi ya awali kwa mtoto—Early Childhood Development (ECD)

99. **Mheshimiwa Spika**, eneo muhimu katika maendeleo ya binadamu ni malezi na makuzi ya mtoto katika siku 1,000 za mwanzo (Early Childhood Development). Inakadiriwa kuwa takribani asilimia 80 ya makuzi ya ubongo wa mtoto hufanyika kipindi hiki. Maendeleo na makuzi ya mtoto katika

siku hizi 1,000 yana umuhimu katika maisha ya utu uzima kimwili, kihisia, kisaikolojia. Hivyo kuwekeza katika umri huu ni kutengeneza ustawi mzuri wa watu wazima wa baadae.

**100. Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Benki ya Dunia, kuwekeza dola moja katika kipindi hiki kunakadiriwa kurudisha dola kati ya 6 mpaka 17<sup>10</sup>. Madhara ya kutowekeza katika makuzi ya watoto yanaathiri katika kipindi chote cha maisha. Madhara hayo huwa katika maeneo ya uwezo wa kufikiri, afya, uwezo wa kuzalisha (Human Capital), kipato na usawia (equity). Kikubwa zaidi ni udumavu wa akili ambao unajitokeza katika kipindi ambacho mtu mzima anafanya maamuzi yake kulingana na mazingira yaliyomzunguka.

**101. Mheshimiwa Spika**; hotuba ya Mheshimiwa Waziri mwaka wa fedha 2018/19 kuanzia aya ya 179 hadi 181 alilitaarifu Bunge kuhusu idadi ya vituo vya kulelea watoto (Day care centers) vimefikia 1,046 na kuwa chuo cha Kisangara ndicho pekee kinachodahili na kutoa wahitimu. Na kuwa Serikali ilifundisha walezi 600 kutoka manispaa nne za Dar Es Salaaam (Ubungo, Temeke, Ilala na Kigamboni). Serikali haikubainisha mikakati ya kuwafikia watoto wengine katika mikoa na wilaya nyingine za Tanzania na huko ndiko jamii kubwa ya wananchi ilipo.

**102. Mheshimiwa Spika**; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri serikali kulipa eneo hili kipaumbelee kwa kupanga mikakati ya kuwa na vyuo vya kufundisha wataalamu wa malezi na watoto wadogo, Kupanua wigo wa ECD zaidi ya Early Childhood Education (ECE), Kutenga bajeti maalumu kwa ajili ya eneo hili, kuweka mkakati wa kufikia wilaya zote kwenye eneo la ECD ili kuwa na kizazi chenye ubora.

**103. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inahitaji majibu kwa maswali yafuatayo:

- Je, serikali ina mpango gani wa kupanua wigo wa ECD kutoka ECE na kushirikisha maeneo ya afya, lische na maji.

---

<sup>10</sup> The World Bank -Investing in the Early Years in Tanzania (P164758)

- Wizara imepanga kiasi gani cha fedha kwa mwaka huu kwa ajili ya ECD? Na Kwa vile Bank ya Dunia iko tayari kuikopesha Tanzania Dola za Marekani Milioni 200 toka Nov. 2017, ni lini Serikali itachukua hatua ya kuomba hela hiyo?
- Je, Serikali inaongeza lini vyuo vya kufundisha wataalamu wa ECD ili kukidhi mahitaji ya nchi kulingana ili kulingana na sense ya watoto chini ya miaka mitano?
- Je, serikali ina mpango gani kufundisha walezi kwenye halmashauri zingine mbali na wale waliofundishwa kwenye manispaa za mkoa wa Dar Es Salaam?

ii. **Matumizi Mabaya ya Madaraka na Athari zake kwa Watoto**

**104. Mheshimiwa Spika**, sote tunatambua kwamba; mwaka 2009 serikali ilipitisha sheria ya kulinda haki za watoto (Law of the Child Act 2009). Pamoja na mambo mengine, sheria hiyo inalinda uhai, utu na heshima ya mtoto. Mnamo Mwezi Aprili, 2018; Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam aliwaita kina mama wote ambao wametelekezwa na wazazi wenza katika malezi ya watoto ili ofisi yake iwapatie msaada wa kisheria.

**105. Mheshimiwa Spika**, Kitendo alichokifanya Mkuu huyo wa Mkoa kilikiuka kwa kiwango kikubwa haki za watoto. Pamoja na kwamba pengine Mkuu wa Mkoa hakuwa na utaalamu wa masuala ya haki za watoto, lakini ilikuwa ni muhimu sana wito huo uwe na tahadhari ya kulinda haki za watoto; kwa kuhakikisha watoto hao wanalindwa dhidi ya vyombo vya habari na mitandao ya kijamii. Matumizi mabaya ya picha za watoto hao kwenye mitandao yana athari mbaya za kisaikolojia kwao kwa siku za baadae. Kimsingi kitendo hicho ni kinyume kabisa na Mkatiba wa kimataifa wa kulinda haki za watoto (Child Rights Conventions) na ni kinyume na Sheria za haki za watoto.

**106. Mheshimiwa Spika**, Sheria zinatambua kuwa mambo ya kifamilia hususani migogoro inayohusu watoto hutatuliwa katika njia za kisheria na njia ambazo ni faragha ili kumlinda mtoto. Vilevile katika taratibu za mila na desturi zetu tunatambua kwamba migogoro ya kifamilia inaposhindikana katika ngazi za familia basi tuna Ofisi za Maafisa Ustawi wa Jamii ambao kimsingi ndio waliokabidhiwa kushughulikia migogoro hiyo na pale inaposhindikana sheria zaidi huchukua mkondo wake.

**107. Mheshimiwa Spika**, masuala yoyote yanayohusu kulinda haki na utu wa mtoto yasichukuliwe kisiasa hata kidogo kwani madhara yake ni makubwa kwa watoto. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawataka viongozi wa kisiasa kufuata sheria za nchi zilizopo na sio kujiamulia mambo kwa utashi wao binafsi. Kambi Rasmi ya Upinzani inakemea na itazidi kukemea tabia hizi zisizo za kistaarabu zinazoendelea kushamiri kila uchwao ambapo baadhi ya wanasiasa wanadhani wao wako juu ya sheria. Tuna wajibu wa kutengeneza taasisi Imara ndani ya nchi yetu na sio kumtengeneza mtu kwani kwa kufanya hivyo tunaathiri mifumo mingi ya utoaji haki na utendaji kazi serikalini. Tuziachie taasisi zifanye kazi yake.

### iii. Kukithiri kwa wimbi la mauaji ya watoto nchini

**108. Mheshimiwa Spika**, licha ya kuwepo na taarifa mbalimbali zinazoonesha kuwa tatizo la utekaji na uuaji wa watoto nchini limepungua ama kudhibitiwa bado matukio ya upoteaji na mauaji ya watoto yamendelea kuripotiwa sehemu mbalimbali nchini. Ikumbukwe kuwa Taifa lilianza kupata hofu ya mauaji ya watoto kwa kasi iliyoanza katika Mkoa wa Njombe, kusini mwa Tanzania. Lakini pamoja na kuwa vyombo vya usalama vimetoa ripoti ya kuonesha kudhibiti matukio hayo kwa mkoa wa Njombe, matukio haya ya kusikitisha yameendelea kuripotiwa sehemu mbalimbali nchini na kuhusishwa na masuala ya imani za kishirikina.

**109. Mheshimiwa Spika**, Sheria ya kudhibiti uchawi namba 12 ya mwaka 1998 (The Witchcraft Act) inaainisha wazi

adhabu kwa watu wanaoendesha vitendo vya kishirikina vinavyoweza kuwadhuru wengine lakini mpaka sasa Mamlaka husika hasa vyombo vya dola vimeshindwa kutoa idadi ama takwimu ya watu ambao tayari wameadhibiwa kwa mujibu wa Sheria hii na hivyo kuendelea kutoa mwanya kwa mitandao ya utekaji na mauaji ya watoto nchini kujenga mizizi.

**110. Mheshimiwa Spika**, hivi karibuni kwa Mwezi April matukio ya watoto kukutwa wamefariki yameendelea katika mikoa ya TABORA, KILIMANJARO, SIMIYU n.k. Kambi Rasmi ya Upinzani inazitaka mamlaka zenye dhamana ya kusimamia ulinzi wa watoto kuwajibika ipasavyo kwa kushindwa kuwalinda watoto chini ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria ya Haki ya Kuishi ya Mwaka 1984. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji; ni kwa nini vyombo vya dola huweza kupata intelijensia ya vurugu za mikutano ya wapinzani nchini lakini ishindwe kupata intelijensia ya raia wake wadogo wasio na hatia?

**iv. Ukiukwaji Mkubwa wa Haki za Watoto unaofanywa na Jeshi la Polisi**

**111. Mheshimiwa Spika**, Mwezi wa Aprill, 2018 palitokea kifo cha mtoto wa miezi sita kwa jina la Halfani Lema ambaye alikuwa mkazi wa Ibanda Kata ya Nyegezi jijini Mwanza. Mtoto huyo alifariki saa chache baada ya mama yake kuachiwa kutoka kituo cha Polisi cha Igogo Nyegezi. Mtoto Halfani aliingia mahabusu na mama yake akiwa mzima na baada ya siku mbili alitoka akiwa na hali mbaya sana iliyopelekea umauti wake. Pamoja na kuwa mama huyo alitoa taarifa ya kubadilika kwa hali ya afya ya mtoto wake lakini polisi hawakujali.

**112. Mheshimiwa Spika**, kitendo cha kumuweka mama huyu mahabusu na mtoto mchanga, na hata alipoomba apewe ruhusu ya kumpeleka mwanaye hospitali alikataliwa mpaka hali ilipokuwa mbaya na kupelekea kifo cha mtoto huyo kutokea ni kitendo cha kinyama na kilaaniwe na kila

Mtanzania mwenye mapenzi mema. Uhai ni mali. Uhai wa mtoto ni maandalio ya nguvu kazi ya taifa.

**113. Mheshimiwa Spika**, ili kukomesha matukio ya vifo kwa watoto vinavyosababishwa na uzembe au ukatili wa baadhi ya watendaji wa serikali waliopewa dhamana ya kulinda maisha ya watu na mali zao; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa maelezo mbele ya Bunge hili; ni hatua gani ilizochukua dhidi ya waliohusika kusababisha vifo vya watoto; Halfan ambaye mama yake alinyimwa ruhusa na Polisi kumpeleka hospitali, pamoja na mtoto wa miaka 17 aliyejulikana kwa jina la Allen Mapunda aliyepigwa na polisi mpaka kufa na vingine vyote vilivyowahi tokea.

**v. Sheria ya ndoa na ndoa za utotoni**

**114. Mheshimiwa Spika**, ikiwa leo ni mwaka 2019, ni wazi kuwa Bunge linatakiwa liwalinde na kuwatengenezea mazingira bora zaidi watoto wa Tanzania ili kuendana na kasi ya dunia nzima ya kupinga ndoa za utotoni. Mojawapo ya Sheria tata ambayo imeendelea kuwa tanuri kwa watoto wa kike nchini ni Sheria ya ndoa ya 1971 (LMA, 1971) ambayo kimsingi inaruhusu wasichana wadogo wa miaka 15 kuolewa. Kwa wavulana umri huwekwa miaka 18.

**115. Mheshimiwa Spika**, katika majukumu ambayo Bunge tunayo na ndiyo yenye msingi wa uwepo wetu ni; 1. Kuwa wawakilishi wa wananchi lakini jukumu kubwa ambalo wananchi hawa wametuwekea dhamana; 2. Kutunga Sheria. Lakini ni dhahiri kuwa kuna baadhi ya sheria zimepitwa na wakati na sisi kama wawakilishi wa wananchi tuna jukumu la kutunga Sheria kuendana na mahitaji ya muda, mazingira lakini vilevile tamaduni zetu na kwa kuangalia Sheria nyengine ambazo zinalinda maslahi ya watu waliotupa dhamana.

**116. Mheshimiwa Spika**, ni dhahiri kuwa Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 inahitaji mjadala mpana na ndio maana hata sasa zipo Sheria ambazo zinakinzana na sheria ya ndoa na ambazo zilipitishwa na Bunge ili kumlinda mtoto wa kike. Hizi ni pamoja na Kanuni za Adhabu, Sehemu 130(2)(e) na

138, ambazo zinasema kuwa mtu anayefanya ngono kwa ridhaa au bila ridhaa na msichana chini ya miaka 18 anakuwa amebaka. Ikumbukwe kuwa Sheria ya Ndoa inaruhusu msichana mwenye umri wa miaka 14 aolewe kwa ridhaa ya mahakama na kwamba ndoa imekamilika tendo la ndoa likifanyika. Chini ya Kanuni za Adhabu, ukamilifu huo ni kosa na hivyo kustahili adhabu.

**117. Mheshimiwa Spika**, Vilevile, tunayo Sheria ya Elimu, Marekebisho ya 2016, ambayo inasema ni kinyume cha sheria kuwa na mahusiano ya kingono au kumpa mimba msichana mwanafunzi. Lakini hapa hapa kuna mtanziko wa Kisheria kwa kuwa Sheria ya Ndoa hii imetoa mwanya wa wasichana wa miaka chini ya 18 kuolewa.

**118. Mheshmimwia Spika**, ni kwa masikitiko makubwa kuwa pamoja na kuwa sisi wabunge hasa Wabunge Wanawake tuna Mtandao wa wabunge wanawake hapa Bungeni bila kujali itikadi yetu TWPG, tumeweka msimamo wa pamoja wa kutaka Sheria hii ya Ndoa irekebishwe na kufuta kipengele kinachotambua ndoa ya mtoto wa kike kuanzia miaka 14. Lakini inapokuja katika kusimamia utekelezaji wa Azimio hili la TWPG, wabunge wanawake tunabebwa na misimamo ya vyama na sio maslahi ya pamoja ya kumlinda mtoto wa kike.

**119. Mheshimiwa Spika**, katika muktadha huu tunataka umma wa watanzania utambue kuwa iwapo Mtandao wa Wabunge Wanawake hautasimamia utekelezaji wa Azimio lake la Pamoja la kutaka Sheria ya Ndoa ibatilishe kifungu hicho cha kuruhusu ndoa kwa mtoto wa kike chini ya miaka 18, basi Kambi Rasmi ya Upinzani itajitoe Rasmi kwenye umoja huu mapema iwezekanavyo ili kulinda maslahi ya watoto wa kike na kuanzisha Mtandao wa Hiyari ili kuhakikisha kipengele hicho kandamizi kinabadilishwa kabla ya Bajeti ya mwaka 2020/21.

**120. Mheshimiwa Spika**, Aidha, tunapenda kueleza masikitiko yetu juu ya upotoshwaji mkubwa uliofanywa na Profesa Kabudi kuwa bado kuna nchi zinazotekeleza ndoa

za chini ya miaka 18 akitolea mfano nchi ya Uingereza chini ya Canon Law. Kwanza ikumbukwe; Tanzania ni Jamhuri lakini haifungani na Sheria za nchi yoyote pia; pili; Serikali haina dini; Lakini pia kigezo kuwa kuna nchi zinaruhusu ndoa za chini ya miaka 18; je kwa kuwa nchi hizo zimehalalisha pia mapenzi ya jinsia moja, basi na Tanzania tuhalalishe ili tupate uhalali wa Sheria?

**121. Mheshimiwa Spika**, Vilevile, Nchi jirani ya Malawi, ambayo ni sehemu ya SADC, mwezi Februari 2017 ilibadilisha katiba yao ili kuzuia ndoa za utotoni kwa kuweka umri wa ndoa kuwa 18 kwa Wavulana na Wasichana.

**122. Mheshimiwa Spika**, Kambi ya Upinzani inahoji ni kwa nini sheria nyingi zinazoathiri wanawake na watoto ndio ambazo zimekwama, miaka nenda miaka rudi lakini miswada mingine inapitishwa kwa dharura?

Utamaduni na Dini havipaswi kuwa sababu ya kumnyima mtoto wa kike haki zake za msingi. Kwa hiyo tunapaswa kuacha tofauti zetu za dini na za chama na tunahitaji kudai hii haki kwa kurekebisha Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971.

**vi. Jukumu la serikali katika kuwasaidia watoto wa kike mashuleni**

**123. Mheshimiwa Spika**, katika lengo namba nne la Maendeleo Endelevu (SDG's) linasema "*Achieving inclusive and equitable quality education for all*" na katika lengo namba tano linasema "*Achieving gender equality and empower all women and girls*". Kwa tafsiri isiyorasmi ni kuwa malengo haya mawili yanaitaka serikali kuhakikisha ushirikishwaji wa makundi yote kwa kuzingatia jinsia katika kupata elimu bora huku watoto wa kike wakipewa kipaumbele kutokana na changamoto kubwa za kiafya zinazo wakabili ikiwa ni pamoja na changamoto za kibaiolojia na za kimazingira.

**124. Mheshimiwa Spika**, katika harakati za kumsaidia mtoto wa kike katika kupambana na ujinga, umaskini na



maradhi ni pamoja na kutatua changamoto anazokumbana nazo kila siku katika jitihada zake za kujiletea maendeleo. Ni hivi karibuni ndani ya Bunge lako Mheshimiwa Upendo Furaha Peneza alileta hoja ya kuitaka serikali kuanza kugawa taulo za kike mashuleni ili kunusuru afya za watoto wengi wa kike ambazo zipo hatarini kutokana na kukosa taulo safi za kujihifadhi wakati wa hedhi.

**125. Mheshimiwa Spika**, katika tafiti mbalimbali zinaonyesha ukosefu za taulo safi za kike kwa watoto wa kike mashuleni imekuwa ni miongoni mwa sababu za watoto wa kike kushindwa kuendelea na masomo, kukosa ufaulu mzuri na hata chanzo cha matatizo mengi ya uzazi na kansa. Ni dhahiri kabisa afya za watoto wa kike hususani maeneo ya vijijini yako hatarini kutokana na mifumo mibovu na mazingira duni yanayowafanya watoto wa kike wawapo katika siku zao kushindwa kuhudhuria masomo<sup>11</sup>

**126. Mheshimiwa Spika**, shule nyingi nchini hazina vyoo vya kutosha na hata vilivyopo havina mazingira mazuri kwa mabinti kubadili taulo zao wakati wa hedhi. Hivyo wengi huzitupa hovyoyote na wengine kulazimika kukaa nazo muda mrefu jambo linaloathiri afya zao.<sup>12</sup>

**127. Mheshimiwa Spika**, hivi karibuni Rais wa Kenya Mheshimiwa Uhuru Kenyatta alisaini sheria ya marekebisha ya sheria ya *elimu ya msingi, kuweka wajibu wa kutoa taulo za usafi (pads) za kutosha na zenye ubora kwa kila mtoto msichana aliyesajiliwa na kujandikisha katika taasisi ya elimu ya msingi ya umma*. Hii ni kuonyesha kuwa serikali ya Kenya imejidhatiti kwa vitendo katika kumsaidia mtoto wa kike na sio maneno matupu.

**128. Mheshimiwa Spika**, inashangaza sana kuona pamoja na jitihada mbalimbali za wadau na sekta binafsi, serikali hii

---

<sup>11</sup> Oloo S.(2010), Influence of sanitary towels on girls child performance in primary schools. A case of girl child in Tana River Nairobi.

<sup>12</sup><http://www.thecitizen.co.tz/magazine/success/How-lack-of-sanitary-pads-affects-school-girls/1843788-4274452-cfs9uhz/index.html>

ya awamu ya tano imekuwa mstari wa mbele katika kukwamisha jitihada za mtoto wa kike katika kujikwamua kwenye lindi la ujinga na maradhi yanayozidi kuwatesa wanawake kila kukicha. Serikali hii ya hapa kazi tu imekuwa mzigo mzito kwa watoto wa kike kwani haki zao nyingi zimekuwa zikivunjwa bila kuangalia athari za muda mrefu (long term impact). Kwa mfano, kitendo cha kukwepa au 'kupotezea' mjadala mzito wa kugawa taulo kwa watoto wa kike maana yake ni kutaka watoto wa kike wa taifa hili wazidi kudhalilika na kuathirika kiafya na kielimu. Na sio hivyo tu, wengine hujikuta katika matatizo ya kupata ujauzito kutokana na kurubuniwa wakati wakitafuta fedha za kununulia taulo (pads) nyakati za hedhi ili kukwepa fedheha. Na hivyo watoto hawa hujikuta kwenye matatizo makubwa zaidi ikiwemo kufukuzwa masomo. Jambo hilo linazidi kuwazamisha katika lindi la umaskini, ujinga na maradhi.

**129. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali hii kuacha 'hadaa' na 'kuwanyanyapaa' watoto wa kike kwa kuwa elimu na afya bora kwa mtoto wa kike ni msingi wa kuzalisha taifa bora la baadae. *Mama bora wa leo huleta mtoto mwenye matumaini ya kesho*. Bila kuwekeza kwa mtoto wa kike hatuwezi kamwe kupata viongozi bora wa kesho na wataalam wazuri kama vile; madaktari, walimu, makandarasi, wanasheria n.k wenye weledi katika kujenga kesho ya taifa letu.

**vii. Pensheni wa wazee**

**130. Mheshimiwa Spika**, kwa muda mrefu sasa Wazee ndani ya taifa hili wamekuwa na kilio kilichoshindwa kupata suluhu katika awamu zote za utawala wa Chama cha Mapinduzi. Ni masikitiko kuona watu walioliumikia taifa kwa nguvu zao zote wakipata manyanyaso makubwa katika nyakati ambazo nguvu zao zinakwenda zikiisha.

**131. Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa taarifa rasmi za Bunge (HANSARD) za tarehe 21/04/2016 uk. 32 & 33 zinaonesha kuwa Serikali ilitoa tamko kwamba nyongeza ya pensheni za wazee kutoka shilingi 50,000 hadi 100,000 zitalipwa pamoja na malimbikizo yake kuanzia mwaka wa fedha 2017/18. Lakini

Wastaafu waliokuwa wako PPF walilipwa kuanzia Januari 2017 bila ya malimbikizo yao ya kuanzia mwaka 2015. Kwa masikitiko makubwa kwamba mifuko ya hifadhi mingine iligoma kuwalipa wazee nyongeza zao na malimbikizo.

**132. Mheshimiwa Spika**, mdhibiti wa mifuko ya hifadhi – SSRA ameshindwa kusimamia au kuchukua hatua dhidi ya mifuko ambayo imekataa kwa makusudi kutekeleza agizo la Serikali kuhusu kulipa nyongeza malimbikizo kwa wazee. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze wazee ni lini sasa nyongeza na malimbikizo ya pensheni mifuko ya hifadhi itaanza kuwalipa wazee wote kulingana na nani anatakiwa kulipwa nini katika nyongeza na malimbikizo au vyote viwili?

**133. Mheshimiwa Spika**, sote tunatambua kijana wa leo ni mzee wa kesho na hivyo hatuna budi kuwajali wazee wetu na kuhakikisha wanaishi maisha ya furaha baada ya kustaafu. Pamoja na malalamiko ya muda mrefu ya wazee yaliyotokana na sheria kandamizi mfano; sheria ile ya kikoloni iliyojulikana kama “The Pensions Ordinance of 1954” iliyoanyiwa mabadiliko mwaka 1999 na baada ya hapo ikatungwa sheria nyingine iliyojulikana kama “The Public Service Retirement Act ya mwaka 1999” iliyoanza kutumika kuanzia tarehe 01Julai, 1999. Pamoja na sheria hiyo ilienda sambamba na sheria ya “The Political Pensions Act No 3 ya mwaka 1999” ambayo nayo iliwalenga watumishi wenye nafasi za kisiasa.

**134. Mheshimiwa Spika**, tunatambua moja ya ajenda kuu ya serikali ya awamu ya nne kwa wazee ilikuwa ni kuandaa mfumo wa pensheni kwa wazee wote yaani “universal pension”. Katika mijadala mbalimbali ya kitaifa iliyohusu haki za wazee iliwigawa wazee katika makundi makuu mawili. Kundi la kwanza ni wazee waliokuwa wakifanya kazi katika mfumo rasmi na kundi la pili ni lile ambalo linajumuisha takribani asilimia 94 ya wazee wote walio katika mfumo usio rasmi. Kundi hili linahusisha asilimia kubwa ya wazee waishio vijijini wakiwemo wakulima, wafugaji, wavuvi, mafundi mchundo, wafanyabiashara ndogondogo wakiwemo mama lische, n.k

**135. Mheshimiwa Spika**, pamoja na makundi hayo wazee waliokuwa katika mfumo rasmi nao wamegawanyika. Wapo wazee waliofanya kazi kwa mikataba (on contract basis) wapo wazee ambao waliajiriwa na serikali kwa muda mfupi tu (temporary terms) na wapo wazee ambao walioajiriwa kwa masharti ya kudumu (Permanent and pensionable terms).

**136. Mheshimiwa Spika**, pamoja na ahadi hiyo ya uongozi wa awamu ya nne utawala huu wa serikali ya awamu ya tano uliwahi kuzungumzia kuleta Bungeni Sheria ya Wazee. Tutakumbuka mwaka 2016, tarehe 29 Aprili aliyekuwa Naibu Waziri wa Afya alizungumzia kuanzishwa kwa Sheria ya Wazee ili kutatua changamoto mbalimbali za kisheria zinazowakabili wazee. Jambo hili limezungumzwa mara nyingi na Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kuwa Kambi inaamini Wazee ni hazina ya taifa letu.

**137. Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa katika Randama za Wizara ya Afya hakuna kipengele kinachozungumzia ahadi ya uwepo wa Pensheni ya wazee wote kama serikali ya Chama cha Mapinduzi kilivyowaahidi wazee, hivyo basi Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua je, serikali hii ya awamu ya tano imeifuta rasmi hoja ya kuanzisha malipo ya pensheni kwa wazee wote? Vilevile, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua mchakato wa kuuleta Muswada wa Sheria ya Wazee Bungeni umefikia wapi ili kuhakikisha kuwa changamoto zinazowakabili wazee zinatatuliwa. Pamoja na hayo serikali ione umuhimu wa kuanzisha chombo kitakachowaleta wazee pamoja kama chombo cha kuwasemea na kutetea maslahi yao kama vilivyo vyombo vingine vilivyoanzishwa kutetea maslahi ya kada mbalimbali.

**D. MAOMBI YA FEDHA ZA KUTEKELEZA MPANGO WA MAENDELEO 2019/20**

**138. Mheshimiwa Spika**, sekta ya afya Fungu 52 inaomba kuidhinishwa na Bunge jumla ya shilingi 415,014,262,000.00 zikiwa ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi

544,137,902,597.00 zikiwa ni fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo na kati ya hizo shilingi 270,600,000,000.00 ni fedha za ndani na shilingi 273,537,902,597.00 ni fedha za kutoka kwa wadau wa maendeleo wa nje.

**139. Mheshimiwa Spika**, katika miradi ambayo haimo katika mgawo wa fedha hiyo, huduma za dawa, fedha za maendeleo kwa Tanzania Food and Nutrition Centre-TFNC, mafunzo na maendeleo ya wataalam, kuimarisha vyo vya mafunzo ya afya haikupewa hata shilingi. Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza ni kwavipi tutaweza kujitegemea katika sekta ya afya kama mipango ya bajeti zetu hailengi kutatua tatizo la upatikanaji wa wataalam sambamba na kuwaongezea utalam wale waliopo?

**140. Aidha, Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Fungu 53, Wizara imeomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 31,537,431,013.00 kati ya hizo za matumizi mengineyo ni shilingi 15,825,478,000.00 na shilingi 2,760,061,013.00 ni fedha za maendeleo. Katika hizo fedha za maendeleo shilingi 1,760,061,031.00 ni fedha za nje.

**141. Mheshimiwa Spika**, Sekta hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ni idara muhimu sana katika kujenga jamii inayowajibika na hivyo kujenga taifa linalowajibika, hivyo fedha zinazotengwa kwa sekta hii ni kidogo kiasi cha kuleta mabadiliko katika jamii na nchi kwa ujumla. Kwani ukiangalia vyo vyote nane vya maendeleo ya jamii vinavyosimamiwa na Wizara vimepewa jumla ya shilingi bilioni 1 tu kwa ajili ya kufanyiwa ukarabati, hivyo hakuna fedha kwa ajili ya uboreshaji wa mazingira ya kujifunzia kwa wanafunzi na wakufunzi.

**142. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema ni muda mwafaka sasa kwa Serikali kuliona hili la kuwezesha Idara hii ya Maendeleo ya Jamii ili kujenga Tanzania mpya yenye maadili na mtazamo chanya wa kujitegemea maendeleo na sio kutegemea wahisani kama ilivyo sasa.

E. HITIMISHO

**143. Mheshimiwa Spika**,Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kwamba afya ya taifa ni jambo muhimu kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii, na kwamba utoaji wa huduma za afya za kibingwa kwa wakati zinaokoa muda wa uzalishaji na hivyo kuongeza ufanisi. Aidha, utoaji wa dawa za kuzuia magonjwa (chanjo) ni muhimu sawa na dawa za kuponya magonjwa kwa kuwa zinasaidia kwa kiwango kikubwa kujenga ustawi na Taifa kuwa na afya.

**144. Mheshimiwa Spika**, katika kufikia azma ya taifa lenye afya, Kambi Rasmi ya Upinzani kupitia Sera ya Afya ya CHADEMA itashirikisha sekta binafsi kupitia ubia na sekta ya umma (PPP), kujenga,kuendeleza na kutumia miundombinu ya afya, pia kuongeza udahili wa mafunzo ya watendaji katika sekta ya afya ili kukidhi mahitaji ya jamii kwa mfumo wa ubia lakini serikali ikibakia kuwa ni mbia mkuu.

**145. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani tunaamini kuwa teknolojia ya afya ni matokeo ya tafiti bora za kitabibu, ambapo matumizi ya ujuzi na elimu katika sekta ya afya hususan dawa, vifaa tiba, chanjo na mbinu vinatumika kutatua matatizo ya kiafya na kuboresha maisha ya wananchi. Hivyo tutahakikisha tunakuza sayansi ya tiba na kuboresha vifaa tiba na mbinu mbalimbali za utoaji wa huduma bora za kitabibu. Sambamba na hilo tutahakikisha usajili wa taasisi za ndani za utafiti, tiba asili na tiba mbadala kwa ajili ya kuboresha sekta ya afya. ***Rejea sera za CHADEMA uk 44 -48***

**146. Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani naomba kuwasilisha.

.....  
Esther N. Matiko (Mb)

Kny: **MSEMAJI MKUU WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

07 Mei, 2019

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Esther Matiko. Tunaanza mjadala wetu wa jumla. Tutaanza na Mheshimiwa Maftaha Nachuma, baadaye Mheshimiwa Benardetha Mushashu na Mheshimiwa Anna Lupembe wajiandae.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu na nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kwanza niweze kuchangia Wizara hii muhimu sana kwa wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wizara ya Afya kwa sababu bila afya njema hakuna Taifa la Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati fulani hivi nilizungumza tukiwa katika Vikao vyetu vya *Briefing* nikamweleza Mheshimiwa Waziri Ummu Mwalimu, kwamba kuna tatizo kubwa la Ugonjwa wa Malaria Tanzania na hasa ukiangalia maeneo yetu ya Pwani, kwa mfano, Jimbo la Mtwara Mjini, pale Mikindani na ukanda mzima wa Pwani kwa sababu kuna mazalia mengi ya mbu kutokana na chaneli za bahari ambazo zinaingia nchi kavi zinazalisha mbu wengi sana na Malaria umekuwa ni ugonjwa ambao unaua sana Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti nilimweleza Mheshimiwa Waziri wa Afya kwamba, wakati nasoma kidato cha kwanza mwaka 2000, niliweza kusikia taarifa za nchi mbalimbali duniani wamedhibiti ugonjwa huu wa *malaria* kwa kutoa chanjo ya *malaria*, nilipewa majibu ambayo sikuridhika nayo sana, lakini baada ya juzi Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutembelea nchi ya Malawi tukasikia kule Malawi kwamba wameingiza mpango wa kutoa chanjo ya *malaria* ikiwa ni nchi ya kwanza barani Afrika. Niwapongeze sana, hawa watu wa Malawi na jambo hili nimwombe Mheshimiwa Ummu Mwalimu, kama kweli tuna nia ya dhati ya kudhibiti tatizo la *malaria* Tanzania, basi tutoe chanjo ya *malaria* kwa wananchi wa ukanda huu wa pwani ambapo kuna mazalia mengi ya mbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linawezekana, Mheshimiwa Waziri atuletee mpango wa kuleta chanjo ya

*malaria* hapa Tanzania kwa sababu ni ugonjwa ambao unaua sana sana na wazungu wanasema *failure to plan is plan to fail* kama Wizara haina mkakati wa kuweka utaratibu wa kuwa na chanjo ya *malaria* maana yake *malaria* haiwezi kuondoka Tanzania. Tunaomba Watanzania wapewe chanjo ya ugonjwa huu *malaria* na hii inawezekana, kama wenzetu wa Malawi wameweza kanchi kadogo tu haka inakuwaje sisi Watanzania wenye *resources* nyingi kwenye bahari hii kubwa sana ambayo imeleta *channel* nyingi za kusababisha mazalia ya mbu kuwa mengi hapa nchini Tanzania. Tunaomba Watanzania wapewe chanjo ya *malaria*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine pale Kibaha kuna Kiwanda cha Viuadudu, kiwanda ambacho kwa muda mrefu hivi sasa, Serikali ama Wizara haijaweka mpango mzuri wa kuhakikisha kwamba zile dawa zinazotengenezwa hapa Tanzania zinapelekwa kwenye halmashauri zote nchini ili ziweze kupulizia kwenye mazalia ya mbu. Kiwanda kinazalisha dawa nyingi sana, tulitembelea pale kama Kamati, cha ajabu, wale wataalam wanasema zile dawa soko lao kubwa liko nje ya nchi wakati Tanzania hapa watu wanaugua *malaria*, watu wanakufa kwa *malaria* kuliko ugonjwa hata wa UKIMWI, *malaria* inaua kuliko hata UKIMWI, Kiwanda cha dawa za kuondoa mazalia ya mbu kipo Kibaha Tanzania, lakini soko lake lipo nje, wakati huku watu wanakufa kwa *malaria*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ije na mkakati na mpango maalum kwamba zile dawa za kuondoa mazalia ya mbu hasa kwenye miji ya pwani kwa mfano Mji wa Mikindani, Tarafa ya Mikindani pale Mtwara Mjini, watu wanakufa sana kwa *malaria*, kwa sababu kuna *channel* nyingi za mbu. Tunaomba hii Wizara iweke mikakati wa kuleta dawa katika halmashauri zote na kuanzia Mtwara Mjini ili wananchi wa Jimbo la Mtwara Mjini wasife kwa *malaria* kwa sababu dawa zinapatikana hapa nchini Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zikipulizwa kwenye *channels* zote, kwenye vile vyanzo vya maji tukapuliza hii dawa



ambayo inazalishwa pale Kibaha, ugonjwa wa *malaria* utaondoka Tanzania, tudhibiti kwanza kwa sababu watu wanasema *vaccination is better than cure*, kwamba kinga ni bora kuliko kutibu sasa tuisubiri, tuisubiri watu wanaugua *malaria* then sisi tuweze kuomba misaada kwa hisani ya wananchi wa nchi za Ulaya ama nchi ya Marekani, tunaomba Serikali iweke kwenye bajeti Wizara hii, ije na mpango maalum wa kuhakikisha kwamba dawa zinazozalishwa pale Kibaha zinaenda kuondoa mazalia ya mbu Tanzania nzima na hii inawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo naomba kuzungumzia ni hospitali za wilaya; Mheshimiwa Waziri amezungumza hapa kwamba tuna mpango wa kujenga hospitali za wilaya Tanzania, lakini ukiangalia kwenye mpango huu, Mtwara Mjini sisi hatuna hospitali ya Wilaya na kila mwaka nimekuwa nazungumza kwa nini wasiweke kwenye bajeti kwamba kama yale maeneo yote ambayo tunahitaji kujenga hospitali za wilaya, basi yapewe kipaumbele yale ambayo hayana hospitali za Wilaya. Kwa hiyo naomba sana Mtwara Mjini, Manispaa ya Mtwara hatuna hospitali ya wilaya, tunaomba Mheshimiwa Ummu Mwalimu atulettee hospitali ya wilaya, wananchi wa Jimbo la Mtwara Mjini wanataka watibiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo naomba kuzungumza hapa ni kwamba, tumezungumza kwa muda mrefu kuhusu Hospitali ya Mkoa wa Mtwara na hii hospitali Mheshimiwa Ummu Mwalimu amekuwa akiizungumza kwa muda mrefu kwamba imepandishwa hadhi na kuwa hospitali ya rufaa. Jambo la ajabu, hii hospitali hata *specialist* hakuna, nimekuwa nazungumza miaka yote hapa ndani ya Bunge hili, kwamba tunahitaji *specialist* hakuna. Nimetembelea pale, kila siku nakuwepo pale, naongea na Madaktari wananiambia Mheshimiwa Mbunge katufikishie kilio chetu hiki, hatuna *specialist* hapa na hii hospitali inasaidia mkoa mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo namwomba sana Mheshimiwa Ummu Mwalimu, hii hospitali nimezungumza

sana na wanasema kwamba wameipandisha hadhi kuwa ni hospitali ya rufaa, haina vifaa tiba pia, hata *x-ray* ni mbovu. Mwaka jana nimezungumza hapa *x-ray* ya hospitali ya Ligula ya Mkoa ambayo inahudumia mkoa mzima ni mbovu, kwa maana hiyo hatuna *x-ray*, hatuna vifaa tiba, ukienda pale dawa zenyewe hakuna dawa, yaani unatibiwa lakini hakuna dawa, unaambiwa uende ukanunue. Kila siku tunazungumza maneno haya, naomba Wizara iiangalie hii hospitali ya mkoa ambayo inahudumia wananchi wote wa Mkoa wa Mtwara na wananchi wengine kutoka nchi za jirani kama Mozambique.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwenye hospitali hii, nimekuwa nazungumza sana, niliongea wakati nachangia Wizara ya TAMISEMI hapa kwamba, sasa hivi hospitali zote zimewekwa utaratibu wa kulindwa na watu wa Suma JKT, lakini hawa Suma JKT hawapewi utaratibu mzuri za kuweza kuwapokea wagonjwa kama walinzi pale magetini, wakati mwingine wanawapiga wagonjwa, wanawadhalilisha wagonjwa, eti kwa sababu wamepita milango ambayo siyo sahihi. Mfano mzuri ni hii Hospitali ya Ligula, kuna walinzi wa Suma JKT, wananchi wameniletea malalamiko haya mengi sana, wameniambia kwenye mikutano ya hadhara, wameniambia nyumbani kwangu, Ofisini kwangu, wameniletea kwamba wanapigwa wanapoenda kutibiwa pale Hospitali ya Ligula na walinzi waliowekwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri kwa sababu tatizo hili siyo la Mtwara tu, siyo Ligula tu ni katika maeneo mengi, hawa walinzi awaangalie kwa sababu mtu anakwenda hospitali akiwa anaumwa, halafu anaenda kusumbuliwa, anapigwa ni jambo la ajabu sana, tunaomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tumezungumza hapa kwamba Serikali imeweka mkakati ya kuwa na hospitali za kanda Tanzania na kila mwaka tunazungumza Kanda ya Kusini hatuna hospitali ya kanda ya rufaa. Katika maeneo mengi ya Tanzania kuna hospitali

za kanda, maeneo haya yote na Serikali inapeleka fedha nyingi na mwaka jana hapa Mheshimiwa Waziri alitambua kwenye bajeti kwamba ametenga bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa *OPD* pale Mtwara. Hiyo bilioni moja haijaletwa Mtwara, bilioni moja hiyo haijaletwa kwa ajili ya kujenga hospitali ya kanda ambayo inatakiwa ijengwe pale Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni jambo la ajabu sana, tumekuwa tukizungumza kwa muda mrefu, kila mwaka Mheshimiwa anatenga bajeti, anatumambua tunapeleka bilioni moja na bilioni moja hata kama ingepeleka bado haiwezi kukidhi haja. Tunaomba kama kweli tuna nia ya dhiti ya kuboresha hospitali hizi za kanda au kujenga hospitali ya kanda, basi kule Mtwara ambako ndiko kunatakiwa kuwe na hospitali ya kanda kusini walete fedha ya kutosha kama wanavyopeleka maeneo mengine ili na sisi wananchi wa Mikoa ya Kusini tuwe na hospitali ya kanda ambayo tutaweza kuitumia kwa ajili ya kujitibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana safari hii, Mheshimiwa Ummu Mwalimu namweleza kabisa, kama hatatenga na kuleta fedha hii nang'ang'ania shilingi yake atatoka bila mshahara kwenye Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza hayo kwa niaba ya wananchi wa Mtwara kwa sababu wamenituma nje kuwaeleza wana tatizo la afya na Wanamtware mnanisikia nazungumza ndani ya Bunge tukufu, Mheshimiwa Waziri ananisikia ninavyozungumza kwamba yale maneno mliyoniambia nje kumwambia Mheshimiwa Waziri aboreshe afya Mtwara, leo hii nazungumza na Mwenyezi Mungu ananisikia, ni siku ya kwanza ya Ramadhani nimefikisha kilio chenu wananchi wa Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri Ummu arekebishe mambo ya afya, amebaki yeye tu, mambo mengine yote Mtwara yako safi isipokuwa kwenye afya. Mheshimiwa Ummu Mwalimu namwaminia sana dada yangu, aje atuboreshee afya Mtwara. Ahsante sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahasante sana Mheshimiwa Maftah. Tunaendelea na Mheshimiwa Benardetha Mushashu.

**MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha vizuri, lakini vilevile nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kazi kubwa nzuri inayoonekana ndani ya Sekta ya Afya. Wote ni mashuhuda tumeona bajeti ya afya ilivyopanda juu, wote tumeona hospitali nyingi kwa wakati mmoja zikijengwa za ngazi ya wilaya, lakini wote tumeona vituo vya afya zaidi ya 300 vinajengwa kwa wakati mmoja ndani ya Tanzania, wote tumeona tunavyonufaika na upatikanaji wa dawa ambayo sasa hivi huko zaidi ya asilimia 94, lakini wote tumeona huduma za matibabu ya kibingwa zinavyopatikana pale Muhimbili, Moi, Jakaya Kikwete, Benjamini Mkapa na *Ocean Road*. Tunasema hongera sana, Wizara wanafanya vizuri sana, sekta ya afya inafanya vizuri sana, kwa hiyo tunampongeza Jemedari wetu Mheshimiwa Rais Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa kazi nzuri ya kuboresha afya ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ukiangalia Mkoani Kagera tulikuwa na hospitali kumi na nne, hospitali kumi na nne kati ya hizo kumi na mbili zilikuwa za mashirika ya dini, moja ya binafsi tulikuwa na hospitali mbili tu za Serikali, lakini katika muda mfupi kwenye bajeti iliyopita wametupatia bilioni nne na nusu tunajenga hospitali za wilaya tatu na kwenye bajeti hii naona wanatuongezea mbili, tunasema ahsante sana. Vile vile, tulikuwa na vituo vya afya 34 na kati ya hivyo ni vituo vitano tu vilivyokuwa na *theatre* ambazo zingeweza kuwasaidia akinamama wanaopata uzazi kinzani, wameshatupatia bilioni 5.9, tumekarabati vituo vya afya 14 ambavyo vitaongeza utoaji wa huduma nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za matibabu ni kubwa mno, hakuna mtu anayeweza kuzimudu kirahisi, ndiyo maana tunasema bima ya afya ndiyo mkombozi, hata ukienda kwenye nchi za wenzetu walioendelea kitu cha kwanza wanahakikisha kwamba binadamu yeyote anakuwa

na bima ya afya. Ukija kwa Tanzania kwa bahati mbaya mpaka sasa hivi watu walio kwenye mfumo wa afya wa bima ya afya ni asilimia 33 tu. Kwa hiyo, ina maana kwamba zaidi ya asilimia 60 hawapo kwenye mfumo wowote wa bima ya afya. Ni asilimia moja wanatumia bima za afya za binafsi, asilimia saba wanatumia Bima ya Afya ya Taifa na asilimia 25 ndiyo wako kwenye Bima ya Afya ya Jamii hii CHF, lakini CHF ingeweza kuwa mkombozi kwa mfano kule Mkoani Kagera kwa mtu kulipa 30 tu, anatibiwa yeye, mke na watoto wane, kwa hiyo watu sita wanatibiwa kwa elfu 30 kwa mwaka mzima na katika kituo chochote kile katika mkoa. Kwa hiyo hii naona kwamba ndiyo imekuwa mkombozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoiomba Wizara ingeweka mkakati wa makusudi wa kuhakikisha kwamba sasa wanaenda kuhamasisha kwenye vijiji vyote kuhakikisha kwamba Watanzania sasa wanaingia kwenye hii CHF iliyoboreshwa ili waweze kupata huduma ya afya na kama tunaweza kuipandisha sasa, watu walioko kwenye CHF wakatoka kwenye asilimia 25 ya sasa, tukaenda mpaka asilimia 60, hata wanapokuja kuzungumzia Bima ya Afya kwa kila mtu itakuwa ni rahisi, watakuwa wameshazoea, wameshajua utamu wa Bima ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kagera inaitwa Bukoba *Referral Governemnt Hospital*, lakini hospitali hii ina changamoto kubwa sana. Wote mnajua Mkoa wa Kagera upo pembezoni jamani, unakwenda weee unavuka Ziwa Victoria upande ule karibu na Uganda, Rwanda na Burundi ndiyo Mkoa wa Kagera ulipo. Kwa hiyo hospitali tunayoitegemea ni hiyo Hospitali ya Rufaa ya Bukoba, lakini bado ina changamoto kibao, kuna upungufu mkubwa sana wa watumishi, kati ya watumishi 6,265 wanaohitajika, wako watumishi elfu mbili mia tatu sabini na kitu ambayo ni asilimia 37.9 tu, tunaomba tupatiwe watumishi, Madaktari, Wauguzi na Madaktari Bingwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kule Mkoani Kagera hatuko kwenye *grid* ya Taifa kwa maana ya umeme. Kwa hiyo tunatumia umeme wa Uganda na umeme

unakatikakatika, pale hospitali kuna *generator* ndogo sana ambayo haiwezi ku-*supply* umeme kwenye majengo yote. Tunaomba *generator* kubwa ya kutosha kuweza ku-*supply* umeme kwenye majengo yote ya Hospitali ya Rufaa ya Bukoba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nilizungumza kwa uchungu nikiomba *ambulance* kwamba hospitali ile ya rufaa inayotegemewa na watu watakaoshindikana Kyerwa, Karagwe, Ngara, Biharamulo, Muleba, Misenyi na Bukoba yenyewe haina *ambulance*. Mtu akipata rufaa anaenda kwenye hospitali ya kanda ipo Mwanza, ni mwendo wa masaa nane mpaka kumi kwa basi. Sasa unakuta kwamba wakishakosa *ambulance* wanamweka mgonjwa kwenye basi pamoja *nurse* anamsindikiza kwa masaa hayo mpaka Bungando, ni hatari, anaweza kupoteza hata maisha. Niliomba mwaka jana Mheshimiwa Waziri aliniahidi, lakini sijapata hata Waziri Mkuu nilimwendea na mwenyewe akaahidi bado hatujapata. Tunaomba tupatiwe *ambulance* ili tuwasafirisha watu wanaokuwa wamezidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niishukuru Serikali kwa sababu kwa sababu hospitali ile wanatupanulia kwenye wodi ya wazazi wanaongeza *theatre* ili akinamama wanaopata uzazi pingamizi waweze kufanyiwa upasuaji. Hapo awali ilikuwa kama mama anapaswa kwenda kufanya operesheni anapelekwa kwenye *general theatre*, akikuta kuna mtu mwingine anafanyiwa *operation* ya magonjwa mengine, inabidi asubiri, akinamama mnaojifungua una uzazi, mtoto anataka kutoka, unasubirije? Kwa hiyo nawashukuru sana kwa kutujengea hiyo *theatre*, lakini basi watuletee na fedha tununue vifaa kusudi *theatre* hiyo iweze ku-*operate*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendelea kuboresha hiyo Hospitali yetu ya Rufaa ya Bukoba, tunaomba wodi ya watoto ipanuliwe, ijengwe *ICU* ya watoto, lakini vile vile sasa hivi kuna tatizo kubwa watu wanazaa watoto njiti, tuwekewe na vyumba vya kulea njiti. Hospitali ya Bukoba inawachanganya wagonjwa wenye matatizo ya akili ambao tunawaita vichaa pamoja na wagonjwa wa kawaida. Sasa

yule ziki-charge anaweza akawaumiza na wenzake. Tunaomba tujengewe hospitali ya watu ambao wana matatizo ya kiakili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinga ni bora kuliko tiba, tunayo kada ya wahudumu wa afya ambayo wanaitwa *Community Health Workers*, karibu elfu kumi na tatu katika Tanzania ambao walio-pata mafunzo, lakini kwa bahati mbaya mpaka sasa hivi hawajaajiriwa. Hawa wakiweza kuajiriwa kwa sababu wanakaa karibu na wananchi wanaweza kwenda kule kwa sababu wanayaelewa matatizo yaliyoko kule kwenye jamii wataamasisha ujenzi wa vyoo bora, kunywa maji safi na salama, lakini umuhimu wa kutumia vyandarua, watawafuatilia wajawazito kuhakikisha wewe mama ni mjamzito mbona hujaenda kliniki? Watawafuatilia akinamama kuwakumbusha kwenda kujifungulia kwenye vituo vinavyotoa huduma mapema, lakini vile vile wataangalia lishe na namna tunavyokula hiyo milo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwaajiri hawa tutapunguza magonjwa yanayotokana na uchafu kwa mfano kuhara, kuhara damu, kipindupindu, lakini watu watatumia vyandarua, kwa hiyo tutapunguza malaria na vilevile tutapunguza vifo vya mama na mtoto ambavyo vinatokana kwa sababu wengine hawaendi kwenye vituo vya afya. Rwanda wenzetu wamefanikiwa kupunguza vifo vya mama na mtoto kwa sababu wanatumia *Community Health Workers* ambao kila wakati wanao akinamama kule kwenye vijiji wanawahamasisha na kuwafundisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa kwa kutumia hawa watu tutakuwa tumepunguza gharama kubwa kwa sababu tutazuia magonjwa mengi, tutakuwa tumepunguza gharama ambayo sasa ingetumika kutibu hayo magonjwa na wote tunatambua kwamba kinga ni bora kuliko tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Benardetha Mushashu. Muda wetu kwa mchana huu umemalizika, kwa hiyo, jioni tutaanza na Mheshimiwa Anna Lupembe, baadaye Mheshimiwa Abdallah Mtolea na Fakharia Shomar.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi kamili jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilitishwa mpaka Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano, tunaanza na Mheshimiwa Anna Lupembe na Mheshimiwa Abdallah Mtolea na Mheshimiwa Fakharia Shomar wajiandae.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi siku ya leo kuweza kuchangia Wizara hii muhimu sana katika maisha ya wanadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mungu ambaye ametuumba na kutupa uzima na uhai na ametupa kibali siku ya leo, tu wazima tukiendelea kutenda kazi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa ambayo anaifanya kwenye sekta hii ya afya. Mkoa wa Katavi tunajivunia sana jinsi pesa za Wilaya pamoja na Mkoa zilivyokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwapongeze Waziri pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Ummy hongera sana kwa kazi. Mwanamke mwenzetu unafanya kazi lazima tukusifie na tunaendelea kukuomba Mungu aendeleo kukupa nguvu kwa sababu Wizara hii ni ngumu, inahusu



wanadamu, tunaendelea kumsihi Mungu aendelee kukutetea katika kazi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wa Mkoa wa Katavi tushukuru katika bajeti ya mwaka 2017/2018 tuliletewa shilingi bilioni 1 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Mkoa. Vilevile katika Wilaya za Tanganyika na Mlele pamoja na Jimbo la Kavuu tumeletewa pesa kwa ajili ya kujengewa Hospitali ya Wilaya. Tunaishukuru sana Serikali kwa kazi kubwa wanayoendelea kuifanya kwa ajili ya kuwatibu Watanzania hususan wa Mkoa wa Katavi. Sisi tunajivunia sasa vifo vya akina mama wajawazito na vifo vya utotoni vitapungua kwa asilimia kubwa sana kwa sababu tulikuwa tuna asilimia kubwa sana. Kupitia jitihada kubwa za Serikali mambo yataendelea kuwa mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Mkoa wetu wa Katavi, Manispaa ya Mpanda tuna Hospitali Teule ambayo imeteuliwa kama ndiyo sasa Hospitali ya Mkoa. Hii hospitali ina mabweni manne tu. Katika wodi ya wazazi kuna sehemu wameweka kwa ajili ya kulea watoto njiti. Naomba sana Wizara itusaidie kwa sababu hospitali zote za Mkoa na hii tayari teule Mheshimiwa Umyy na wewe uliniahidi kuwa utatujengea bwani moja katika Hospitali ile Teule ya Mkoa wa Katavi, Manispaa ya Mpanda. Wale watoto njiti wanakaa pamoja na mama zao humohumo watu wakienda kuwatizama, nafikiri unajua watoto njiti wanatakiwa wakae katika hali ya usalama zaidi ili waweze ku-*survive*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na matatizo ya mabweni haya kuwa machache, wodi ile ya magonjwa mchanganyiko ipo moja tu. Wodi ile wanalazwa watu wazima, watoto kuanzia miaka 5 mpaka 13, ina maana hawa watoto ni wadogo. Pia wagonjwa wanaoingia katika wodi ile ni mahtuti watoto wale wanashuhudia vifo vya wagonjwa mle ndani, ina maana tunawapa woga wakiwa wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mkoa wa Katavi hususan Wilaya ya Mpanda Manispaa tunaomba Mheshimiwa Umyy utujengee mabweni mawili mengine...

**MBUNGE FULANI:** Ni wodi.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Wodi ndiyo mabweni Waheshimiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba tujengewe wodi mbili ili hawa watoto umri wa kuanzia miaka mitano wawe wana wodi yao kwa sababu kisaikolojia tunawapa uwoga kwa sababu wakati mwingine wako kitanda kimoja na mkubwa yule mkubwa anafariki pale yeye anaendelea kuweweseka. Katika maisha yake anakuwa na uwoga, tunamjenga hofu katika maisha yake yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Umyy alishakuja Mkoa wa Katavi Manispaa na aliona hospitali ile jinsi ilivyo tunaomba tujengewe wodi mbili. Tunashukuru mmetuletea shilingi bilioni 1 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Mkoa na jumla ya fedha zote mpaka hospitali iishe ni shilingi bilioni tisa. Mmetupa shilingi bilioni 1 nafikiri na sasa hivi mtatupa shilingi bilioni 1 ina maana mpaka ujenzi uishe ni miaka tisa ijayo tutakuwa bado tuna matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Waziri utuongeze fedha ili Hospitali ya Mkoa iweze kuisha haraka. Tukipiga hesabu ya shilingi bilioni moja moja ile hospitali itaisha baada ya miaka tisa mbele ya safari. Ina maana kuwa lazima tupate msaada wowote ili ile Hospitali Teule iweze kurekebishwa mambo mbalimbali ili iweze kukidhi haja ya wananchi wa Mkoa wa Katavi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya hospitali hii watumishi ni wachache sana na ndiyo teule na tunaitegemea kama Hospitali ya Mkoa. Hatuna madaktari bingwa wanaokidhi haja ya kutibu magonjwa mbalimbali. Ndiyo maana unakuta wananchi wengi wa Mkoa wa Katavi wanahangaika sana. Wengine wanafia nyumbani kwa sababu akienda hospitali kumefurika, hapati matibabu halisia, vifaatiba hatuna na manesi ni wachache. Tunaomba mtusaidie ili hospitali hii iweze kukidhi vigezo vinavyohitajika

kimkoa. Wakati mnaoendelea kutuletea pesa na hii hospitali iendelee kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuja upande wa bima ya afya. Bima ya afya ni kiwango kikubwa sana na Watanzania uwezo wao bado ni mdogo, Sh.1,500,000 mtu aweze kukata bima ya afya ni pesa nyingi sana. Wengi wanakufa wakiwa nyumbani kwao na mimi mwenyewe nashuhudia. Sasa hivi tuna maradhi makubwa makubwa ya moyo, kansa, figo aje Benjamin huku na hana bima matokeo yake huyu mtu anakufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ile bima ya afya tuliweka ya vikundi ya Sh.79,000 tuichanganue akate mtu mmoja mmoja mwenye uwezo, tumpe fursa akate hiyo bima. Naomba niipongeze Serikali mmeleta bima ya mkoa ya Sh.30,000 wananchi wameitikia lakini sasa unakwenda kwenye Hospitali ya Mkoa hakuna vile vifaa mfano moyo umepanuka wanakwambia nenda Muhimbili, ukienda Muhimbili ile bima haifiki kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hii bima tui-*separate* tufanye hata Sh.100,000 yule mwenye uwezo aweze kukaa Bima hii ya Taifa ili aweze kutibiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kwenye kitabu chake ukurasa wa 85, Mheshimiwa Ummy anataka kuleta sheria kwa ajili ya bima ya afya. Naomba nikupongeze sana, tulettee hii sheria tuweze kurekebisha yale mapungufu ili Watanzania waweze kupona. Watanzania wengi wanakufa majumbani, kuna wagonjwa majumbani mpaka unashangaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye magari ya wagonjwa ndani ya Mkoa wetu wa Katavi. Jiografia ya Mkoa wa Katavi ni ngumu mno. Tunaomba mama yetu atupe hata *ambulance* tatu tu ziweze kutusaidia kwani tuna shida. Mheshimiwa Ummy ni msikivu naamini atatusaidia haya magari ya wagonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wale mabinti zako wa *Kalema Girls* Mheshimiwa Waziri wanakukumbusha ile bajaji uliowaahidi kwa ajili ya matibabu ya asubuhi. Usisahau, naomba nalo unijibu utawaletea lini hiyo bajaji. Nafikiri ulisahau, naomba nikukumbushe bajaji *Kalema Girls*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende maendeleo ya jamii. Ndani ya Mkoa wetu tuna Chuo cha Msaginya na safari hii kimepata bahati mbaya kimeshaungua mara mbili. Katika hotuba ya Waziri kuna vyyo ambavyo vimepatiwa pesa ya marekebisho na amesema vimefanya kazi nzuri kwa ajili ya hamasa mbalimbali. Nakuomba Mheshimiwa Waziri utusaidie hiki Chuo cha Msaginya kiweze kufanya kazi kama Vyyo vingine vya Maendeleo ya Jamii. Chuo hiki kwa Wanakatavi ndiyo kitakuwa msaada mkubwa sana kwa sababu tumeona vyyo vya wenzetu vimefanya kazi nzuri. Ukitupatia fedha na kikafanyiwa marekebisho mazuri, nafikiri Wanakatavi wanaoishia darasa la saba wataenda kujifunza kozi mbalimbali na kupata manufaa ya Chuo hiki cha Msaginya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia 100.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Anna Lupembe. Tunaendelea na Mheshimiwa Abdallah Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia uhai na kuanza Mfungo wa Ramadhani vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niipongeze Serikali hasa Wizara ya Afya kwa kazi kubwa ambayo mnaifanya ya kuhakikisha kwamba afya za Watanzania zinakuwa katika mikono salama. Uwekezaji mkubwa mnaufanya kwa maana ya kutenga fedha, kuzipeleka na kuzisimamia lakini kuhakikisha kwamba vifaa tiba vinapatikana na wauguzi wanakuwepo. Hili ni jambo kubwa, muendeleo kufanya hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nisiache kumshukuru Mheshimiwa Angellah Kairuki, Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Uwekezaji ambaye aliamua kwa makusudi katika kuadhimisha siku ya Wanawake Duniani yeye akishirikiana na wanawake wanaofanya kazi na Benki ya UBA walijitolea kuleta mashuka katika Hospitali ya Temeke. Wananchi wa Temeke wanakushukuru sana na kwao hawakuoni tu kama kiongozi lakini wanakuona kama ndugu yao wa karibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Waziri Mkuu ambaye alifanya ziara ya kushtukiza katika Hospitali ya Temeke. Ziara yake imekuwa na tija sana, amerekebisha mambo kadha wa kadha lakini pia alisisitiza baadhi ya mambo ambayo Wizara ilibidi muendeleo kuyashughulikia. Moja, ilikuwa ni kuhakikisha kwamba tunapata mashine ya kufulia katika Hospitali ya Temeke. Ni kweli hakuna tatizo la kufua kwa sababu wanakwenda kufua Muhimbili lakini kwa upekee wa Hospitali ya Temeke ambayo pia ni kituo cha magonjwa ya mlipuko si vizuri sana wakawa wanaenda kufua katika eneo linguine. Ni vizuri kwa ubora ambao mmeboresha hospitali ile basi tungekuwa pia na mashine za kisasa za kufulia ili shughuli zote zifanyike pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla hospitali ile haijakabidhiwa kwa Wizara wakati ilipokuwa chini ya Halmashauri tulianza kujenga jengo la *emergency* kwa kushirikiana na Mkuu wa Mkoa lakini pia na Ubalizi wa China. Sasa wakati tunakabidhi ujenzi ule ulikuwa bado haujakamilika na mpaka leo umesimama. Si vizuri kwa wadau wa maendeleo ambao wametuchangia halafu waone lile zoezi haliendelei. Tunaomba katika hiyo shilingi bilioni 10 ambayo Mheshimiwa Waziri umesema unayo basi tuelekeze hiyo shilingi milioni 100 iende pale ikamalize lile jengo la *emergency*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna changamoto ya *generator* upande huu wa utawala. Hii imekuwa ni tatizo sana kwamba umeme unapokatika madaktari wanakosa *standby generator* ya kuwasaidia kwa sababu ile *generator* kila siku

imeharibika. *TEMESA* wanaambiwa kwamba ile *generator* imekufa watoe kibali ili hospitali ikanunue *generator* lakini hawataki kila siku wanataka wawe wanalitengeneza baada ya siku mbili limekufa. Naomba mtusaidie waambieni hao *TEMESA* watoe hicho kibali hospitali ikanunue *generator* nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwashukuru kwa hayo mazuri mnayoyafanya, nina kero moja nataka niifikishe na hii ni kero kubwa kwa wananchi siyo tu wa Temeke lakini yawezekana ni Watanzania nzima na hili ni tatizo la kuzuia maiti eti kisa kuna deni hospitali. Kumekuwa na utaratibu huo hasa katika Hospitali ya Muhimbili na Mloganzila kwamba marehemu anapofariki kama anadaiwa iwe Sh.20,000, Sh.100,000 au kiasi chochote maiti inazuiwa isitoke hospitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili si la kibinadamu, linaondoa utu ambapo kama Watanzania tulizoea kuheshimu maiti. Hata barabarani maiti ikiwa inapita, unasimama unaacha maiti ipite. Huu ujasiri wa mtu kuzuia maiti unatoka wapi? Kwa nini maiti izuliwe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwenye mazingira ya kawaida kabla hatujaenda kuzika huwa tunatangaza jamani anayemdai marehemu ajitokeze, tunamkabidhi kwa ndugu wa marehemu wataendelea na shughuli za kudaiana baadaye lakini sisi tunaenda kuzika. Wengine kuzika ni ibada na sisi Waislamu tunasisitizwa mtu akishafariki awahishwe akazikwe lakini leo tunashindwa hata kuitekeleza hii ibada yetu kwa sababu badala ya kuchukua maiti mkazike mnaanza kupita na daftari la kukusanya michango.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keissy, taarifa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa mzungumzaji amegusia Uislamu lakini

Mwislamu kabla hajazikwa Mashekhe wanasema kwamba alipe madeni yake yote ndiyo azikwe. (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdallah Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nafikiri Mheshimiwa Mbunge anachanganya, nimesema hapo awali kwamba ni utaratibu kabla hatujaenda kuzika tunatangaza wanaomdai marehemu wajitokeze, wanaodaiwa na marehemu wajitokeze, kisha tunawakabidhi kwa familia waendeleo na taratibu za kulipana lakini hatuzui kwenda kuzika. Sasa sijui yeye anazungumzia Uisalamu katika kitabu gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu hapa ni kwamba, kwanza wakati mwingine unakuta maiti inayozuiliwa kwenye hospitali hiyo kwa sababu anadaiwa Sh.120,000 tayari labda ameshaugua hapo miezi miwili na bili nyingine ameshalipa yaani unakuta mgonjwa ameshalipa zaidi ya shilingi milioni 2 siku anakufa kwa sababu tu kuna siku mbili za mwisho bili yake haikulipwa eti tunazuia maiti, hii siyo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia dhamira ya Mheshimiwa Rais ya kuweka fedha nyingi kwenye huduma za afya na kutatua kero za wananchi haiendani na jambo hili linalofanyika la kuzuia maiti hospitalini. Dhamira ya kuwekeza katika hospitali si kufanya biashara ni kuboresha huduma lakini hata ingekuwa biashara mabenki haya yanakopesha hayadai maiti, mtu akifa deni lile limekufa inakuwaje hapa hospitalini? Tulitegemea sasa hivi tuwe tunakwenda mbele zaidi kwamba mgonjwa ambaye ameugua miezi miwili, mitatu hospitali na alikuwa analipa bili akifa hospitali hata itoe *incentives* ya kusafirisha ile maiti kwa sababu alikuwa wa kwao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anaonekana anaguswa na maisha ya wananchi lakini anaguswa pia na misiba inayotokea, ndiyo maana hata kwenye hotuba ameanza kwa kuwapa pole watu ambao

wamepoteza ndugu zao. Sasa kauli hii haiwezi kuleta tija endapo bado maiti za watu zinazuiliwa hospitalini. Siyo kila jambo tumwachie mpaka Mheshimiwa Rais ndiyo siku asimame atoe maamuzi, hili mbona liko ndani ya mikono yenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anachapa kazi sana, Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Ndungulile namfahamu ni mtu ambaye amenyooka sana, anapenda kuhakikisha kwamba kero za wananchi zinaondoka, kwa nini hili hatuliangalii na linabaki kuwa kero Mloganzila na Muhimbili peke yake? Kwa nini hatulalamikii Temeke, Ilala au Mwananyamala kwani huko watu hawafi, kote huko watu wanafariki kila siku lakini haya hayatokei, mtuondolee na hili katika hizo hospitali mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kuamini kwamba hizi maiti zinazozuiliwa eti zikiachiwa ndio Mloganzila na Muhimbili zitapata hasara sana zitashindwa kutoa huduma sio kweli. Lakini kama tatizo ni fedha leo tuna makapuni haya ya bima za afya yanapata fedha kutokea kwa wagonjwa wanaopelekwa hospitalini. Na ni mara chache utasikia haya makampuni ya bima za afya yanafanya hiyo *cooperate social responsibilities* maana yake hata ile asilimia moja ya faida ambayo wanatakiwa kutoa kwa jamii hawatoi. Kwa nini msiweke utaratibu basi wailekeze huko iwe ina fidia hawa watu ambao hawana watu... (Makofi)

## TAARIFA

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa ndugu yangu Mheshimiwa Mtolea kuwa sio Mloganzila tu wala Muhimbili pia Hospitali ya Mwananyama ndugu yako akifia wadini kila siku 20,000 unalipa na maiti akitokea nyumbani wakimleta pale kumhifadhi ni 30,000 kwa hiyo tatizo hili ni kero kubwa katika Mkoa wa Dar es Salaam.



**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Mtolea ukimaliza kupokea taarifa hiyo kengele ya pili itakuwa imeshamalizika.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti taarifa hiyo naipokea lakini nizidi kutoa angalizo kwamba, Serikali yetu imejikita katika kuondoa kero kwa wananchi hasa wananchi maskini na wanaoshindwa kutoa maiti zao kwa kuzuliwa huko hospitalini wala sio matajiri ni wananchi maskini twende tukawasaidie tuondoe hii kero nakushuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mtolea tunaendelea Mheshimiwa Fakharia Shomari baadaye Mheshimiwa Wilifred Lwakatare.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, sina budi kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na taasisi yote ya Wizara yake kwa bajeti nzuri walivyotuletea ambayo inaeleweka na pia Mheshimiwa Waziri jinsi alivyo-*present* hapa pia unataka kumsikiliza vilevile sina budi kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchagua majembe akayaweka Wizara ya afya yanatufanyia kazi nzuri na tunaridhika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitakuja kwenye ile kinga ya kansa ya kizazi. nakumbuka mwaka jana kulikuwa na kampeni ya watoto wetu wa miaka tisa mpaka miaka kumi na nne ambao hawa wafanyiwe chanjo ile ya kinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna baadhi mikoa nasikia kuna vijana hawakwenda wazazi wao wamewazuia sijui kama taarifa hiyo mnayo. Na kama mnayo kwanini waliwazuia wakati Serikali ilishagharimika ilishatafuta pesa na hii ni kinga kwa wao wenyewe itakayo wasaidia huko mbele watakapo endelea na maisha yao lakini wakawa hawakuwapeleka ingawa mlitumia shule mkaenda mkafanya hiyo lakini bahati mbaya baadhi ya wazazi waliwazua watoto wao. Sasa tunataka kujua kwa nini ilitokea

hivyo na kama ni kweli nyinyi mnajua na mmechukua hatua gani? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja nyingine kwenye *fistula* kwa kina mama suala hili hata mwaka jana lilizungumzwa. Kwa sababu CCBRT wao ndio wanashughulika na suala *fistula* lakini utakuta kuna watu wapo mikoa tofauti na *fistula* wanapata. *Fistula* hachagui ni bahati mbaya tu unaweza ukapata, sasa kwanini hamsomeshi watu wenye fani hii mkawasambaza katika hospitali za mkoa, hospitali za kanda ili wakaweza kuwa mabingwa wa ainai ile mtu likimtokea jambo hili asiweze kuhangaika anajua mimi hiki kimenitokea na madaktari hapa wapo wenyewe wataona na wanaweza wakamtibu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri nataka hili mliangalie kama madaktari wa fani hiyo hawana msomeshe ili muweze kupata madaktari waweze kuwatibu wananchi bila matatizo maana kuwa na *fistula* wakati haja inatoka bila kawaida ni tatizo kwa binadamu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja suala la watoto njiti, mama anapobeba mimba sijui kwa uzoefu anajua kuwa mimi nitazaa njiti au nitazaa mtoto aliyekamika. Sasa ninataka nijue wakati wanapokwenda kliniki mnatoa elimu au na wale madaktari wanakuwa hawajui kama atazaa mtoto njiti? Kwa sababu unapomzaa na baadhi ya hospitali haina vifaa utaambiwa umuweke kufuani, umuwekee tumboni apate joto hilo tatizo. Unajua kama mama wakati mwingine ana joto la kutosha? Mama wengine wapo baridi tu. Sasa kama mkiwa hamjaangalia mkawa mnatoa elimu toka watu wapo kliniki kwamba mtoto njiti yuko hivi mzazi unatakiwa kuwa hivi au unahisi kabla hujazaa uko hivi ili mama anakwenda kuzaa tayari anakuwa na elimu ya kutosha anakuwa hana wasiwasi na hata atakapo mzaa yule mtoto anajua huyu mtoto anajua huyu mtoto nimemzaa wa aina fulani na nitakiwa nimuhudumie vipi ili makuzi yake yawee vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye suala lingine la *sober house*. Unajua kila siku tunahangaika na vijana wetu

wanaokula unga, na hili ni tatizo sugu. Nashukuru Wizara ya Mambo ya Ndani wanavyohangaika nalo, lakini je Wizara ya Afya wamechukua hatua gani? Kwa sababu wanatakiwa lazima kuwa na dawa za kutosha zakuweza kuwatibu hawa vijana wetu. Mambo ya Ndani kazi yake yeye ni kutafuta na kupembua na kukamata lakini wa kutibu ni Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa naomba Wizara ya Afya mshirikiane na Mambo ya Ndani ili muweze hili jambo kulimaliza, mlimalize kabisa. Kwa sababu watoto wetu wanaumia na wao ndio nguvu kazi bila ya wao wakiwa hawataweza kufanya kazi taifa letu litadolola. Sasa nakuombeni Wizara ya Afya wakati Mambo ya Ndani tayari wanalishughulikia mshirikiane nao kwa kuwaweza kuwatibu wale vijana wetu ambao tayari wameathirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mweyekiti, lingine bima ya afya bila ya afya kwa upande wa Zanzibar naomba iboreshwe. Kwa sababu unapokuwa na bima ya afya Zanzibar inabidi uende Vialeni, Globaly, Arhma au Hospitali zilizokuwa chini ya vyombo vya ulinzi kama jeshini au polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwetu kwa upande wa pili ni tatizo kwa sababu tunazo *Cortege* hospitali kama moja ipo Makunduchi, nyingine ipo Mkwajuni sasa wa Kaskazini watakwenda zoa kule. Wapo watu wanafanya kazi za muungano kuna Wabunge wana familia zoa wanazo bima za afya na wengine kuna polisi kuna wanajeshi wataweza kutumia. Na wa Kusini watakuwa wanakwenda Makunduchi. Lakini sote tunakimbilia mijini huko mjini napo kuna matatizo yake kwa sababu utaambiwa dawa hakuna, hiki hakuna, Na itabidi matatizo. Sasa namuomba Mheshimiwa Waziri najua bima ya afya ipo kwenu mtuboreshee na Zanzibar iweze kuwa na uwezo wa kufanya kazi na uwezo wa kutibu na kila mmoja alidhike na fedha yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kama Mbunge nakwenda hospitali naambiwa dawa hakuna nikiitizama bima yangu natakiwa kila kitu niifanyiwe. Lakini hakuna kwa sababu hamjaboresha kule. Wanakwambia hakuna, sasa

naomba muwe mnalingalia suala hili kwa jicho la rehema ili liweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja suala la mwisho, Usambazaji wa dawa za baridi na moto katika *Pharmacy* zetu. Najua kuna kanuni zinazongumza dawa aina gani ziende zikauzwe mitaani. Lakini naona hizo kanuni hazifuatwi naweza jirani yangu kaenda hospitali katibiwa nami maradhi yale nikaja nikayapata akaniambia nenda dawa fulani mimi nilipewa wakati mie cheti sina nitakwenda *pharmacy* na *pharmacy* atanipa ile dawa na siku nyingine dawa ya moto lakini anayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama mtafanya ziara ya kushtukiza mkawa mna kwenda mara kwa mara mnaangalia kwa sababu hii mnasaidia tiba ya raia wenu ambao ndio raia wa Tanzania watakao weza kufanya majukumu yao na kuwaondoshea matatizo katika miili yao na afya zao. Nafikiri hayo naunga mkono hoja mia kwa mia nawapongeza kwa kazi yao nzuri nashukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Fakharia Shomari tunaendelea na Mheshimiwa Wilfred Lwakatare baadaye Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru, kwanza kabisa katika mchango wangu niungane na watanzania wote na *IPP Media* kutoa pole kwa kuondokewa na mwekezaji makini na mahiri bwana Dkt. Reginald Mengi, naamini tunapozungumzia pengo, Dkt. Mengi ameacha pengo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na katika historia nafikiri tukichimbua historia ni mtanzania ambaye ameacha rekodi ambayo haijawekwa na mtanzania tangu nchi hii iumbwe katika rekodi tulizonazo. Ni mojawapo ya matajiri, wapo matajiri wanaomzidi fedha lakini moyo wake na nafsi yake imefanya mengi kama jina lake lilivyo. Nathubutu kusema hata kama kuna mabaya ambayo anayo kama binadamu

lakini mazuri yanafunika mara mia tano mara elfu moja.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nipende kupongeza bayana hotuba ya Kambi ya Upinzani na pia hotuba ya Kamati Huduma ya Jamii. Naamini Mheshimiwa Waziri na Msaidizi wake na watendaji wao wakizisoma vizuri hotuba hizi na ushauri ulitolewa nafikiri tutapiga hatua moja kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, napenda tutambue kabisa unapozungumzia afya, unapozungumzia ustawi wa jamii ndio msingi wa shughuli zingine zozote ambazo zinafanywa ndani ya nchi. Ni kama mtu ambaye ninaamini hawezi kuanza kununua tairi kabla hajanunua gari, kununua *spear* tairi inakuja baada ya kununua gari. Mambo yote yanayofanyika bila Wizara hii bila idara ya Wizara hii kupewa bajeti kadri tunavyozipitisha ndani ya Bunge hili tutakuwa hatuwatendei haki watanzania tunao wawakilisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kila Mbunge anayesimama hapa ambaye amezungumza mapungufu mengi yaliyopo. Hotuba zote mbili za Upinzani pamoja na Kamati ya Huduma za Jamii zimeeleza hali halisi iliyopo huko. Lakini pia tunapozungumzia ukosefu wa fedha inasikitisha inapokwenda au inapopelekea kwamba hata pesa zinazopitishwa ndani ya Bunge hili, sasa zinapolewa pungufu kwa kweli inaonekana sisi wenyewe wasimamizi tunaosimamia Serikali au wapishi wetu ambao ndio waliokabidhiwa dhamana ya kuweza kusimamia hii mifuko na hazina fedha ya nchi hii kuna matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ukosefu wa bajeti au kutotimilisha bajeti maana yake ni kutotimiza huduma zilizotarajiwa kwa wananchi wetu. Ninaamini huenda na hili ndiyo tatizo ambalo hata ndani ya Manispaa yangu ya Bukoba katika bajeti hii tunayoelekea kuimaliza tulipangiwa 1.5 bilioni kwa ajili ya hospitali yetu inayotakiwa kuwa hospitali ya wilaya ambayo mpaka sasa hivi ina jengo moja tu linalohudumia watu wa *OPD*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sasa tunashindwa kuiita hospitali ya wilaya au kituo cha afya, nashindwa kuelewa, sasa kwa kuwa labda imebakia miezi kama miwili hivi, nafikiri Mheshimiwa Ummy atakapokuja na Msaidizi wake mtaniambia labda miezi miwili hii fedha itatoka ili tuwe na hospitali ya Wilaya. Na katika hili nafikiri ifike mahala nchi yetu uwekwe utaratibu kitu gani kinapelekea hospitali iitwe hospitali ya Wilaya, Hospitali ya Mkoa, Hospitali ya Rufaa, Zahanati, kituo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiriki tuchukue hatua tuweke *category* kama tunataka hospitali iitwe ya Wilaya au ya Rufaa basi iwe imetimiza masharti fulani, iwe na vifaa vya aina fulani, iwe na *capacity* ya aina fulani isiwe ni majengo tu, kukuta bango ndio hospitali ya Mkoa, hospitali Rufaa *X-ray*hamna *MRI*hamna, madaktari hamna. Kwa kweli nafikiri ni ushauri wangu kama yanayofanyika kwenye hoteli, unapojua unakwenda *five star* unajua utakuta huduma ya aina gani sasa hili lipelekwe hata kwenye *hospital* zetu vinginevyo tutakuwa tunadanganyana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala jingine niseme kabisa nimnufaika wa *NHIF* na ninawapongeza sana taasisi hii kwa afya yangu wamekuwa wadau muhimu kwa kuendelea kuwa na afya njema nawapongeza sana wamenihudumia sana. Nimekuwa nahudumiwa vizuri bila shaka kwa sababu bima yangu ni kubwa. Ambayo inaniruhusu kupata matibabu yoyote na weza nikapata madawa yoyote naweza nikapata vipimo vyoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kuwa nimekuwa nahudhuria katika matibabu pia nimegundua wananchi wa kawaida wanavyo kufa. Watu wana kufa si kwa sababu ya kile ambacho tunaambiwa kwamba bwana ametoa na bwana ametwaa. Nafikiri Bwana anatoa lakini wapanga mipango wanatwaa kwa sababu naamini asilimia 95 ya magonjwa yameshafanyiwa *research* namna ya kutibiwa. Sasa watu wanakufa kwa utapia mlo, watu wana kufa kwa sababu utumbo umejikunja kwa kweli naamini bwana akweli anatoa tunashukuru na tutakuwa jina halihimidiwi bali

tunadhahi jina la Mwenyezi Mungu tukienda namna hii.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maslahi ya watumishi nafikiri kuna haja ya hata kuweka *category* tunapojumuisha kwamba watumishi wote wasipandishwe mishahara, watumishi wote wasilipwe pesheni. Lakini naamini kuna kila sababu ya kuwaangalia watumishi wetu wa idara hii, kuna kila sababu tukianza watu wote, nafikiri mlkwenda shule. Katika shule zetu na vyuo vyetu watu wanaominika kuchimba sana na kubundi ni madaktari, na wanasoma kwa miaka mingi tukiwapeleka jumla jumla na watumishi wengine hatuwatendei haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza watumishi wa Idara ya Afya, miongoni mwa watu wanaokwenda sambamba na kiapo chao ni watu wa sekta hii. Ni watu ambao hata wafanyiwe vituko gani wanakomaa wanatimiza viapo vyao. Hebu fikiria kuna idara, kuna sekta ambayo anaweza akaenda akachakachua *cement*, kwenye kujenga daraja, lakini hakuna daktari au nesi ambaye ameambiwa akupige dawa ya kiwango fulani akakudunga sindano ambayo inazidi kiwango kile ili ufe au daktari pamoja na uwezo wake wakati wa kufanya *operation* au kukupiga nusu kaputi ile anaweza akakumaliza. Lakini pamoja na kwamba hajalipwa mishahara, hajalipwa mapunjo anakomaa anaamua kutimiza kiapo chake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri tufike mahali tuwaangalie watu hawa ili tuweze kuwatimizia haki sambamba na huduma na aina ya *commitment* ambayo wanakuwa nayo katika kazi yao.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Kama haiwezekani nafikiri yale masharti ambayo yaliwekwa ya watu kutofanya kazi za ziada, naomba daktari aruhusiwe kuweza kutafuta kipato cha ziada cha kufidia pato dogo mnalomlipa. Nafikiri ipo haja kubadilisha utaratibu hawa watu wakapata fursa

ya kujiongezea kipato kama mmeshindwa kuwalipa sawa sawa na haki yao. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiarika kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Lwakatare kengele ya pili ililia.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Haya tunaendelea na Mheshimiwa Magdalena Sakaya baadaye Mheshimiwa Daniel Mtuka na Mheshimiwa Mansoor Shanif ajiandae.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kunipa nafasi kuweza kuchangia kwenye hotuba ya afya ya Mheshimiwa Waziri ambayo ipo mbele yetu. Narudia tena kwa mara nyingine nilisema kwenye bajeti ya Waziri Mkuu na baada ya kupongeza juhudi zilizofanyika kwenye hospitali ya Muhimbili kuweza kuweka vipimo vya kutosha na vifaa tiba nikaiomba Serikali ihakikishe imepeleka vifaa tiba vya kutosha na vya kisasa kwenye hospitali zote za kanda na hospitali zote za rufaa Mikoa Tanzania nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tulipo sasa hivi, Hospitali yetu ya Kitete, ambayo ni Hospitali ya Rufaa na Hospitali ya Mkoa wa Tabora, ukienda pale haina sifa ya kuweza kuwa Hospitali ya Rufaa kwa sababu haiwezi kutoa huduma za Hospitali ya Rufaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wagonjwa wengi ambao wanakuwa *referred* kutoka kwenye Hospitali za Wilaya wanakwenda Bugando, Muhimbili na maeneo mengine. Sasa fikiria mtu atoke Tabora mpaka Bugando, atoke Tabora mpaka Muhimbili na maeneo mengine.



Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kuweza kufanya, naomba Serikali ihakikishe kwamba inaweza kuweka vifaa tiba vya kutosha katika Hospitali zote, Hospitali ya Itete na Hospitali nyingine za Tanzania nzima kwa kweli, tutaweza kusogeza huduma karibu wale wananchi masikini ambao hawana uwezo wa kupata hata nauli ya kutoka Tabora, kuweza kwenda mpaka Muhimbili au kuweza kwenda Bugando waweze kupata huduma kwa maeneo ambayo wapo na maeneo ambayo ni ya karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tabora hata ile Hospitali ya Nkinga tu yenyewe inatoa huduma bora zaidi kuliko hata Hospitali ya Kitete. Kwa hiyo, naomba jicho la pekee kabisa kwenye Hospitali ya Kitete ya Mkoa wa Tabora ili wananchi wa Mkoa wa Tabora wanaopata rufaa kwenye Wilaya yetu waweze kupata huduma pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la huduma za afya kwa Wilaya ya Kaliua. Nashukuru kwamba tumetengewa fedha mwaka huu shilingi bilioni 1.5 ya kuweza kumaliza Hospitali yetu ambayo tumeijenga kwa fedha za ndani, tumekamilisha *almost* karibu nusu. Jengo la *OPD* tayari, jengo la akina mama na watoto tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoiomba Serikali, najua kwamba miundombinu iko kwenye Wizara ya TAMISEMI, lakini kwa msukumo wa Mheshimiwa Waziri kwa kuwa alifika kule akaona kazi inayofanyika, naomba aweze kusukuma fedha hii itoke ili Hospitali ile ifunguliwe, kwa sababu mwenyewe alituhidi kwamba tukimaliza jengo la akina mama tunaweza tukapata kibali cha muda ifunguliwe tuendeleo na majengo mengine. Naomba msukumo wa Wizara ili tuweze kufungua Hospitali ile wananchi wa Kaliua ambao kiukweli wengi wao wanapata huduma mbali na Wilaya waweze kupata huduma pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni dawa. Tumekuwa tunapata dawa na dawa zimeboreshwa kwenye Vituo vya Afya na kwenye Zahanati zetu, lakini kuna Zahanati

ambazo zina idadi ya watu wengi sana ambapo ule mgao wa huduma ya Zahanati hauwatoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Zahanati ya Usinge nimeshaleta maombi kwa Mheshimiwa Waziri na kwa Mheshimiwa Naibu Waziri. Zahanati ya Usinge ina tibu watu 35,000 kwa mwezi, inahudumia Kata mbili na pale hamna Kituo cha Afya. Tukawaomba Zahanati kama ile ya Usinge watu 35,000 kwa mwezi, Zahanati ya Igagala watu 28,000 kwa mwezi wapewe mgao wa Kituo cha Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu wananchi wanaona kabisa kwamba hawapati dawa kwa sababu zikiletwa ndani ya wiki mbili zimeisha. Kwa hiyo, wakienda wanaambiwa dawa hamna kwa sababu idadi ya watu wanaopata huduma pale ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri ahadi yake ya kuweza kutupatia Zahanati hasa hizi mbili; Zahanati ya Usinge na Igagala waweze kupata mgao wa dawa unaofaa kwa Kituo cha Afya ili wananchi walioko maeneo yale waendeleo kupata huduma kwa *quarter* zima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni huduma za wazee. Mheshimiwa Waziri ametuambia tuna Makazi ya Wazee 17 ya Serikali, lakini pia tuna makazi ya Wazee 14 ya Taasisi za Umma, Watu binafsi pamoja na Taasisi za Mashirika ya Dini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makazi ya Wazee ya Serikali yana hali mbaya sana. Wazee wengi walioko kule wanateseka hawana huduma. Hakuna chakula na hakuna mavazi. Mfano mmoja mdogo, Wabunge wengi wanapita njia hii ya kwenda Tabora pamoja na Singida, ukipita pale Sukamahela, ule mlima pale, kuna wazee kibao wamekaa pale wanaomba barabarani. Wamechoka kukaa kule Kituo cha Sukamahela, wanakuja kukaa barabarani kuja kuomba. Ukiangalia mavazi waliyovaa, wako pale wanadonoa chawa kwenye nguo zao, kwa maana kwamba hata hali ni mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi naomba kama mmeamua kuwaweka kwenye vituo, wapate huduma ili ukipita pale ukiwa na mkate uwape, ukiwa na maji uwape. Wale ni wazee ambao wamefanya kazi kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, kile Kituo cha Sukamahela kwa kweli kinatia huruma. Mimi mpaka siku nilienda kukitembelea japokuwa siyo Jimbo langu, nikasema hebu nikaone hao wazee wanakaa maeneo gani? Wanatia huruma, wategemee mkate wa barabarani kweli! Magari yapite na bahati mbaya pale ni mlimani, likiharibika gari pale ndiyo wapate chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazee hawa wamefanya kazi kubwa. Leo tuko hapa kwa sababu walikuwepo hawa wazee huku nyuma. Naomba vituo vyote vya Serikali vihudumiwe vizuri. Ukienda angalau kwenye Taasisi za dini zina unafuu, kwa sababu wanapeleka misaada mbalimbali, watu wanaenda kutoa sadaka kule, lakini hivi vya Serikali havitembelewi mara kwa mara na watu ambao ni wasamaria wema. Kwa hiyo, naomba sana wazee hawa waweze kupata huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni huduma za wazee za Bima ya Afya. Serikali kwa muda wa miaka minne imekuwa ikisisitiza wazee wapatiwe vitambulisho vya kutibiwa bure, lakini bado *speed* za Halmashauri kutoa vitambulisho hivi ni ndogo sana. Mpaka leo wazee wengi hawana vitambulisho vya kutibiwa bure. Mojawapo ni Wilaya yangu ya Kaliua, tunasisitiza kila vikao wazee wapewe vile vitambulisho, lakini mpaka leo, zaidi ya robo tatu hawajapata vile vitambulisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba msukumo wa Serikali, wazee hawa, wapate vitambulisho wawe na dirisha lao waweze kupata haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni migogoro ndani ya ndoa. Mheshimiwa Waziri ameeleza kwa umakini

mkubwa sana kwenye hotuba yake, migogoro imekuwa mingi sana ndani ya ndoa na wanaopata matatizo ni wanawake. Leo migogoro ni kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia imezuka tabia nyingine hapa Tanzania, mimi naishangaa sana. Wanawake wanaojifungua mapacha zaidi ya watoto watatu mpaka wanne waume zao wanawakimbia. Yaani baraka inakuja nyumbani, halafu wanawake ambao wamepata mapacha wanakimbiwa. Nimekuwa nafuatilia mpaka nashangaa. Wengi wanasaidiwa sana na watu kwenye mitandao, waanze kuchangiwa shilingi 100/=, shilingi 200/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ituambie, wana mpango gani kwa watoto hawa wanazaliwa wanne mpaka watano kwa familia ambazo ni masikini halafu wanawake wanakimbiwa na waume zao. Wanaume wengine sijui ni mashetani! Unapata baraka, halafu unakimbia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano binti mmoja ambaye aliomba mimba kwa muda wa miaka minne hajapata mimba. Kapata mimba mwaka 2018 kajifungua mwaka huu watoto watatu, mwanaume kamwachia wale watoto kakimbia. Yaani mpaka unashangaa. Hivi huyu ni binadamu au mtu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naiomba Serikali, watoto ni baraka ya Taifa, watoto ndiyo raslimali, nguvu kazi ya Taifa. Watoto hawa wanaozaliwa kwa familia masikini, mapacha watatu, wanne, watano, Serikali inawasaidiaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nakua nilikuwa nasikia kuna kitu ambapo ukijifungua watoto zaidi ya watatu Serikali inakusaidia kuwale watoto mpaka inawasomesha. Siku hizi nadhani hicho kitu sijui hakipo! Kwa hiyo, naomba Serikali itusaidie sana katika kuhakikisha kwamba watoto hawa waliozaliwa kwenye familia masikini ambao ni

mapacha waweze kupata huduma nzuri, waweze kuwa ni Taifa nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la Sheria ya Ndoa, migogoro imezidi, akina mama wana mizigo mikubwa ya kuweza kulea watoto wenyewe. Tunaomba Sheria ya Ndoa ije Bungeni, iliyopo imepitwa na wakati. Tumeongea sana muda mrefu kwenye Bunge hili. Kwa nini Sheria ya Ndoa haiji Bungeni tuifanyie marekebisho ili watoto wapate stahiki zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani akina baba wanawakimbia watoto. Ie Sheria ya Ndoa ukiangalia viwango vilivyoko kule ni vidogo. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atusaidie Sheria ije Bungeni tuiptishe ili watoto wanaoachwa mzigo kwa akina mama wapatiwe huduma stahiki za kusoma za kula vizuri na huduma nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Magdalena Sakaya. Tunaendelea na Mheshimiwa Daniel Mtuka, baadaye Mheshimiwa Mansoor Shanif na Mheshimiwa Amina Mollel wajiandae.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii nami niweze kutoa mchango wangu katika bajeti hii ya Afya. Kwanza nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai, kwa kutuwezesha leo kuwepo katika Bunge lako hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nampongeza Rais wangu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi kubwa anayoifanya. Tunaiona na kila mmoja anaiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza pia Mheshimiwa Waziri, pamoja na Naibu Waziri, Makatibu Wakuu

wale wawili na timu nzima ya Wizara hii kwa kubwa ambayo wanaifanya kutuhudumia hasa katika eneo la Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naipongeza Serikali kwamba katika Bajeti ya dawa imeongezeka sana kutoka shilingi bilioni 31 ambayo tulikuwa tunaizungumzia mwaka 2015/2016 sasa tunazungumzia shilingi bilioni 270 hivi sasa ninavyozungumza. Naipongeze sana Serikali kwa kweli kupitia Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naipongeza Wizara na Serikali kwa Mkoa wangu wa Singida. Mkoa wangu umekuwa wa pili kwa kupata upatikanaji wa dawa zile 30 muhimu kwa Mkoa wa Singida. Mpaka sasa hivi tunapata asilimia 96.6, ni wa pili kutoka Mbeya ambao wanapata asilimia 97.1. Kiambatanisho Na. 5 cha Rejea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilete maombi machache sasa baada ya pongezi hizo. Ombi langu la kwanza, Mheshimiwa aliyemaliza kuzungumza dada yangu Mheshimiwa Sakaya amezungumzia Kituo cha Makazi ya Wazee wasiojiweza pale Sukamahela. Mheshimiwa Naibu Waziri alifika tarehe 29 mwezi wa 10 mwaka 2018 pale akaongea na wale Wazee na pia alituhidi kwamba katika yale makazi 17, Mikoa 17 katika nchi nzima, akasema wana mpango sasa wa kuyapunguza na kuboresha yakawa machache kugawa katika Kanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walisema mojawapo ya Kanda nadhani Sukamahela itakuwa ni Kanda mojawapo. Nilisimama siku ile na kusema kwamba tunawakaribisha kwa sababu Sukamahela lile eneo ni kubwa, tunazo ekari 80 pale za kutosha kabisa, pia ni barabara kuu imepita pale, tunayo maji, tunao umeme, kwa hiyo, huduma zote zipo, tunawakaribisha sana; na wananchi wako tayari sana ili muweze kufanya eneo lile kwa kanda ya makazi kwa Kanda ya Kati. Tunaikaribisha sana Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu la pili, ulipofika Mheshimiwa Naibu Waziri tarehe 29 hiyo mwezi wa 10 mwaka

2018, tulikuomba pamoja na mambo mengine *ambulance*. Mpaka sasa hivi bado hali ni ngumu, *catchment population* ya Hospitali ya Wilaya ya Manyoni kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012 ni 250,000, lakini hivi ninavyozungumza nadhani sasa inakwenda kwenye 500,000 na zaidi kwa sababu maeneo mengi sana wanakuja; Sikonge wanakuja, maeneo ya jirani, Bahi huko wanakuja. Kwa hiyo, imesha-*double* ile *catchment population*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kwa kweli pamoja na huduma nyingine, lakini *ambulance* tunahitaji sana. Tulikuwa nayo lakini sasa imechakaa, iko kwenye mawe. Tufikirie sana kama Wizara, mgao utakaotokea wowote ule, Manyoni muifikirie sana kwa ile Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu lingine la tatu, Wilaya ya Manyoni sasa ni kubwa imekuwa, kile kilikuwa Kituo tu cha Afya, tukakikuzi na tukakipandisha hadhi lakini majengo yale Mheshimwia Naibu Waziri amefika hata Mheshimiwa Waziri ameshafika pale. Ie siyo hadhi ya Wilaya kwa yale majengo. Mnapofikiria kujenga Hospitali za Wilaya katika nchi hii kwa mgao unaofuata, naomba sana muifikirie Wilaya ya Manyoni. Tunalo eneo tumelitenga, tumelipima, pana zuri, nasi mtupe huo mgao wa kujenga sasa Hospitali ya Wilaya, maana sasa Wilaya ya Manyoni imekua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu lingine la mwisho ni Ikama. Kama nilivyosema Wilaya ya Manyoni imekua sana, tunapokea wagonjwa wengi sana sasa hivi; pamoja na Vituo vya Afya vile viwili tulivyojengewa, tunashukuru, lakini bado ile Wilaya tunapokea wagonjwa wengi sana. Tunao Madaktari wanne tu. Watatu wanafanya kazi, lakini mmoja pia ni *DMO*, sasa ni watatu tu ambapo ilitakiwa wawe 14 mpaka 20, lakini ni wanne tu. Hebu fikiria hiyo *situation*, ni ngumu sana. Mtufikirie sana ikama kwa maana ya Madaktari pamoja na Wahudumu wengine kama Manesi. Kwa kweli hali ni ngumu, wamezidiwa sana kihuduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, nashukuru sana, niachie na wengine wazungumze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naunga mkono hoja Wizara hiyo. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Daniel Mtuka, tunaendelea na Mheshimiwa Mansoor Shanif, baadaye Mheshimiwa Amina Mollel na Mheshimiwa Ritta Kabati wajandae.

**MHE. MANSOOR S. HIRAN:** Mheshimiwa Mheshimiwa, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja ambayo iko mbele yetu. Kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa pumzi nami nipate nafasi ya kusimama hapa na kuzungumza ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara ya Afya kwa kazi nzuri ambayo wanafanya. Naomba kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kutupatia *ambulace* ambayo ilikuwa ni shida kubwa kwenye Kituo chetu cha Afya cha Mwamashimba. Ilikuwa ni ahadi yangu wakati wa kampeni na nashukuru sana amenisaidia *ambulance* mpya, ambayo nimetimiza ahadi ya wananchi wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Kwimba Makao Makuu yetu ni Wilaya ya Ngudu Mjini. Ngudu Mjini tuna Kituo cha Afya ambacho tunakitumia kama Hospitali ya Wilaya. Kituo cha Afya hiki kina changamoto nyingi.

Naomba niseme baadhi ya changamoto ambazo tunazo. Kwanza, hatuna mashine ya kufua nguo. Hospitali ile ni kubwa, inatoa huduma kwa wagonjwa wengi, kuna magonjwa ya kuambukiza, unakuta shuka zile zote zinaoshwa na binadamu ambaye anaweza akapata magonjwa, anapata shida sana kuosha hizo shuka. Kwa hiyo,



namwoamba sana Mheshimiwa Waziri mashine ya kufulia nguo ili Hospitali yetu iweze kutoa huduma inayostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine tuliyonayo ni kwamba kuna *extra machine* ambayo ni *analogy*, tuliletewa zaidi ya miaka 15, tuna *X-Ray machine* ya zamani sana ambayo kwa kweli inaharibika mara kwa mara. Tunaomba sana tuletewe *X-Ray machine* ya *digital* kwa sababu huduma ya *X-Ray machine* ni kubwa sana kwa sababu ile ina Majimbo mawili, tuna changamoto ya wagonjwa wengi sana na *X-Ray* inapatikana pale Wilaya ya Ngudu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ningependa kusema tatizo tulilonalo kwenye Hospitali yetu ya Wilaya ni kwamba tuliletewa Daktari wa macho, miaka miwili yuko pale, lakini hana vifaa vya kufanya kazi, hana chumba cha kufanyia kazi. Kwa hiyo, amekaa pale, anaangalia, anatoa huduma pale huku amekaa nje. Naiomba Wizara itutengenezee chumba, itupe vifaa ili huyo Daktari atoe huduma ya macho kwa wananchi wa Wilaya ya Kwimba. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine tunaomba tupate *pharmacy* ya duka la *MSD* la dawa. Dawa ni shida, zinapatikana mitaani kwa bei kubwa sana, naomba *MSD* wafungue duka la dawa kwenye Hospitali yetu ya Wilaya angalau wananchi wapate huduma ya kununua dawa kwa bei nafuu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ningependa kusema ni kwamba sisi mji wetu wa Hungumarwa unakuwa kwa kasi kubwa sana, tuna Zahanati pale ambayo inatoa huduma sawa na Kituo cha Afya. Tunaomba sana tujengewe Kituo cha Afya kwenye Kata yetu ya Hongumarwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine napenda kusema ambacho kinanipa shida sana, Mheshimiwa Waziri anisikie kwa usikivu kidogo ni kwamba watoto wetu shuleni wanapata shida. Wengi wanapoteza maisha yao kwa sababu wanaugua. Kuna magongwa matatu ambayo

watoto wanapata mara kwa mara; ugonwa wa pumu, *Sickle cell* na Kisukari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwa Wizara, tungeweza kupata *First Aid Kit* ambazo tungezipeleka kwenye shule zetu zote za msingi na sekondari na pia walimu tukawafundisha ili waweze kutoa *First Aid*. Mara nyingi tunakuta unapoteza watoto kwa sababu shuleni wanapougua mwalimu anachofanya ni kumpeleka mtoto nyumbani badala ya kumpa *First Aid* na kumpeleka Hospitalini, anampeleka nyumbani unakuta mtoto anapoteza maisha yake, kitu ambacho tungeweza kuepusha, mtoto akapata *First Aid* shuleni ili akifika hospitalini anakuwa ameshapata *First Aid*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mengi ya kusema, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mansoor Shanif. Tunaendelea na Mheshimiwa Amina Mollel, baadaye Mheshimiwa Ritta Kabati na Mheshimiwa Peter Msigwa ajiandae.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kipekee kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu, kila tunaposimama hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, natangua tu kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki kwa kifo cha mpendwa wetu Dkt. Reginald Mengi. Natambua mchango wake hasa kwa sisi watu wenye ulemavu, alitupenda, alituthamini na alitusaidia. Kwa kweli tutamkumbuka kwa mengi. Kipekee kabisa Dkt. Reginald Mengi ataendelea kuishi ndani ya mioyo yetu. Ninamfananisha Dkt. Reginald Mengi na Mama Theresa wa Calcutta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, *inshallah* Mwenyezi Mungu hapo kesho tutakwenda nasi kujumuika nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu kwa kusema kwamba kwa wanafunzi wenzetu wanaosoma Vyuo Vikuu, niombe kwa Wizara kwa sababu kuna utaratibu wa Bima ya Afya ambayo wanakatiwa au wanakata wanafunzi wale na huu ni utaratibu mzuri ambao umeandaliwa na Serikali. Kipekee kabisa nampongeza mwanamke jasiri, shupavu Mheshimiwa Ummu Mwalimu, pamoja na Naibu wako, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wote kwa kazi nzuri wanayoifanya. Hakika matunda tunayaona na Mwenyezi Mungu aendelee kuwapa Afya ili mwendelee kuwatumikia Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri kufuatilia Bima za Afya kwa sababu vyuo vingi hapa nchini, pamoja na kwamba wanafunzi wanatoa pesa, lakini hawapati hizo Bima za Afya kwa wakati. Pia wengine wanatoa zaidi ya kile kiwango kinachohitajika, wanatoa shilingi 100,000/= . Hawa wanafunzi wakati mwingine wasipotoa hawaruhusiwi hata kufanya mitihani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba sana dada yangu Mheshimiwa Ummu Mwalimu alifuatilie hili na hata ikibidi, basi uwe utaratibu wanafunzi wanapoanza mwaka wa kwanza kuwepo na watu wa Bima ya Afya ili waweze kuwakatia vitambulisho kutokana na mikopo wanayopata ili kuondoa usumbufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hili lipo kwa shule za sekondari na hata hizi *English Medium*, tuwasaidie wazazi. Kama kweli zinatolewa hizo pesa, basi ziweze kukatiwa bima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine pia nizungumzie kuhusiana na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, vingi vimechoka, vimechakaa na vinahitaji ukarabati.

Namuomba Mheshimiwa Ummu Mwalimu kuhakikisha kwamba Vyuo hivi vya Maendeleo ya Jamii vinafanyiwa ukarabati. Pia ikiwa ni pamoja na Maafisa Maendeleo ya Jamii kuweza kuwasaidia vitendea kazi ili waweze kufanya kazi ambayo wamepatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakemea pia baadhi ya Wahadhiri wa Vyuo Vikuu na hili hata Mheshimiwa Rais pia amelizungumza, baadhi ya Wahadhiri wa Vyuo Vikuu wanaowanyanyasa watoto wa kike kingono na wamediriki wakati mwingine hata kuwafelisha kwa sababu tu wamekataliwa kingono, tumefika mahali pabaya sana. Namwomba Mheshimiwa Waziri yeye ni Waziri pamoja na afya lakini jinsia, alisimamie hili kuwanusuru watoto wetu wanaokwenda shule ili waweze kusoma kwa amani na utulivu kama nchi yetu ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitalizungumzia kwa mapana zaidi suala la mapambano dhidi ya UKIMWI. Hali ya mapambano dhidi ya UKIMWI ni mbaya. Takwimu zinazooneshwa na zimesomwa hapa, hivi sasa kila mwaka watu 72,000 wanaambukizwa virusi vya UKIMWI na ni kati ya miaka 15 mpaka 64. Miaka kuanzia 15 mpaka 24 hao ni vijana ambao maambukizi yako kwa asilimia 49 na kati ya hao ni watoto wa kike ndio wameathirika, tunalipeleka wapi Taifa letu? Nchi yetu tunasema nchi ya viwanda na viwanda tunategemea pia hata hawa ambao wako vyuoni waje kwenda kule, je, vijana hawa ambao hivi sasa wapo katika janga la maambukizi ya virusi vya UKIMWI tunawasaidiaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha atuambie ni mkakati upi unaandaliwa ili kuona kwamba tunanusuru maisha ya watoto wetu na hasa watoto wa kike, ndio ambao wanaangamia kwa kiasi kikubwa. Naomba sana tuone ni kwa jinsi gani tunawasaidia, leo hii tunasema kwamba mpaka tunapomaliza siku watu 197 wanaambukizwa virusi vya UKIMWI. Hili sio jambo la mzaha ni jambo kwa kweli pamoja na jitihada nzuri za Serikali na hasa kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu na mimi nikiwa kama Mjumbe wa Kamati ya UKIMWI na Dawa za Kulevya na bahati nzuri na Kifua Kikuu hali ni mbaya huko tunakokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo utaratibu ambao tunafanya kampeni kwenye shule zetu, lakini maeneo mengi wale wahusika wamejisahau, tunaomba wawakumbushe ili

tuone ni kwa jinsi gani basi kama ni kampeni au ni jinsi gani ya kuweza kukinusuru kizazi hiki ili kiepukane na hili janga la UKIMWI. Mimi naumia sana kama mwanamke, watoto ambao tunawategemea kwamba ndio viongozi tukiondoka hapa, wanakwenda chuo wanakwenda shule, wakirudi badala yak u-graduate na A wanarudi na virusi vya UKIMWI. Hili linaumiza sana, namwomba Mheshimiwa Waziri pia na Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na hizo jitihada na nipongeze sana pia Serikali yetu kwa jinsi ambavyo inalichukilia suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa kondomu hazipatikani, Mheshimiwa Waziri atakapokuja naomba atuambie ni kwa nini kumekuwa na uhaba mkubwa wa kondomu na pengine hili ndilo linalosaidia au linalochangia kuendelea kuenea kwa maambukizi ya virusi vya UKIMWI, tujue ni idadi ngapi pia wanapokea kwa mwaka hizo kondomu, kwa sababu najua siku za nyuma walikuwa wanapokea zaidi 18,000, lakini ni taarifa zilizopo ambazo Mheshimiwa Waziri atakuja kutuambia walipata kondomu 9000. Je, tatizo liko wapi, atueleze Mheshimiwa Waziri ili tuweze kunusu kizazi hiki ambacho kinaangamia na ugonjwa huu wa UKIMWI?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia malengo haya ya 90, 90 kwa kweli Serikali inafanya kazi kubwa, lakini watendaji kule chini bado ni tatizo. Tulipokwenda kwenye kampeni baadhi hawajui unapomwambia 90, 90 anakwambia ni kitu gani na wakati mwingine ni mtu mwenye dhamana ya kuweza kusaidia katika hili. Kwa hiyo, naomba sana kwa kweli, mimi nalia sana na UKIMWI na hasa watoto wa kike tuone ni kwa jinsi gani tutawasaidia watoto wetu ili kuwaepusha na huu ugonjwa wa UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, nimalizie tu kwa kusema kwamba, unyanyasaji wa kijinsia kwa wanawake bado pia hili ni tatizo katika maeneo mengi. Mwisho kabisa niseme kwamba, kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii tunaiona na Mheshimiwa Ummy anaacha alama katika Wizara hii pamoja na Naibu wake. Kikubwa tunachokifurahia

na tunaona kabisa kwamba kazi nzuri ya Mheshimiwa Rais kwamba yupo hapo lakini Dkt. Ndugulile, ni Daktari, kwa hiyo hakuna mtu atakayeweza kuwadanganya katika Wizara. Tunawaomba sana waendeleo kusaidia na kuhakikisha kwamba vituo vya afya ambavyo Serikali hii ya Awamu ya Tano imeviboresha, basi tuone vifaa vinapelekwa ili tuweze kupunguza tatizo la vifo vya wanawake na watoto kwa sababu hawa wanawake ndiyo nguvu kazi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, kwa mara nyingine tena, tuendeleo kumwomba Dkt. Reginald Mengi. Pia tujiulize kwa sababu tunao matajiri wengi, sisi wenyewe binafsi je, tunasaidiaje watu wenye uhitaji? Katika maeneo mengi tunao tunawaona na wana shida ambayo kweli wanahitaji kusaidiwa na hata matajiri waliojaliwa tunawasaidiaje, tunaacha alama gani, Dkt. Reginald Mengi, kilio cha Watanzania na huko anakokwenda basi Mungu anaona. Kwa hiyo na sisi iwe ni somo kwetu ni jinsi gani tunakwenda kuwasaidia Watanzania wenye uhitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, nampongeza sana Mheshimiwa Ummy pamoja na Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote Wizarani, waendeleo kuchapa kazi, tuko pamoja na wao, *a luta continua*, mapambano bado yanaendelea. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Amina Mollel, tunaendelea na Mheshimiwa Ritta Kabati.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Wizara hii muhimu sana jioni hii. Kwanza kabisa naomba nimtangulize sana Mwenyezi Mungu katika mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na pongezi kubwa sana kwa Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri sana ambayo anaifanya kwa kuboresha Wizara ya Afya. Kwa kweli mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni, Mheshimiwa Rais toka amechaguliwa ameweza kufanya kazi kubwa sana na

hii kazi inaonekana hata huko vijijini kote anakokwenda pongezi nyingi amekuwa akizipata. Kwa hiyo kwa kweli tumpongeze na tupongeze Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuwachagua hawa Mawaziri, hajafanya kosa, dada yetu Mheshimiwa Ummu anafanya kazi nzuri sana. Hii Wizara nakumbuka kuna siku moja mtu mmoja alisema kwamba huyu dada anafanya kazi kama mwanaume, nikasema hapana, wanawake tunapiga kazi sio kwamba lazima awe mwanaume. Kwa hiyo dada Ummu anatumendea haki sisi wanawake wote. Vile vile Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, Naibu Waziri pia kwa kweli anajituma, wakati wowote yuko tayari tukimwita anaitika na amekuwa anatusaidia kazi nyingi sana ambazo anatumfanyia. Niwapongeze sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwapongeze Makatibu Wakuu, tena yuko mwanamke kwenye Wizara hii, hiyo ndio inahakikisha kwamba wanawake wanaweza, wachape mzigo, waoneshe kwamba sisi wanawake tukipewa kazi tunafanya kweli kweli, niwapongeze na watendaji wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo kuipongeza Serikali kwanza kabisa kwa kutenga pesa kwa ajili ya hospitali za wilaya 67, hospitali za mikoa nane, vituo vya afya 332 nchini na sisi katika mkoa wetu tuliweza kupata bilioni 4.5 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali mpya ambazo kwa kweli tunashukuru Hospitali ya Kilolo, wakati wowote Mheshimiwa Rais atakuja kuizindua tunashukuru sana. Vilevile tumepewa pesa kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya ya Mufindi na Hospitali ya Iringa DC. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe, hili ni ombi maalum tunayo Hospitali ya *Frelimo* ambayo yenyewe siyo inajengwa tayari ishajengwa kuanzia 2008 imeanza kufanya kazi. Sasa niombe kwa kweli Serikali ifanye utaratibu, hospitali ambazo tayari zinafanya kazi zina upungufu kwa mfano ile ya *Frelimo* ni kujengewa tu wodi za akinamama, akinababa na watoto ili kupunguza msongamano mkubwa kabisa uliopo katika

hospitali ya mkoa. Kwa hiyo wangukuwa wanatoa kipaumbele kwa hospitali ambazo tayari zinafanya kazi na zinaweza kupunguza msongamano kwenye hospitali zetu za mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe pia Serikali iboreshesasa vituo vya afya ambavyo vimeshajengwa ili kupunguza vifo vya akinamama na watoto kwa sababu kujenga ni kitu kingine, lakini tusipoboresha bado tatizo la vifo litabaki kuwa pale pale. Sasa niombe vifaa tiba vipelekwe, manesi wapelekwe ili kuhakikisha kwamba vituo vyote vinapatiwa pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie sasa hospitali yetu ya mkoa. Hospitali yetu ya Mkoa ina changamoto nyingi sana; ya kwanza, Madaktari Bingwa wa Upasuaji wote hawapo, wameondolewa, wananchi wanapata shida mno, mno. Sasa hivi mgonjwa akitaka kufanya upasuaji, aidha apelekwe Muhimbili au aletwe Dodoma kwenye hospitali yetu ya Benjamin Mkapa. Bado kuna tatizo kubwa sana la magari, *ambulance* tuliyonayo imepewa jina la Ummy Mwalimu *ambulance*, ambayo kwa kweli kwanza ni ya petroli lakini imekuwa ndio hiyo hiyo moja nyingine zote ni mbovu, aidha wale Madaktari waweze kuchukua katika vituo vya afya na vituo vya afya bado vinakosa *ambulance*.

Kwa hiyo nimwomba Mheshimiwa dada Ummy kwa heshima na taadhima kwanza kabisa aje pale Iringa atembelee hospitali yetu au Naibu azungumze na wafanyakazi walioko pale na Madaktari ili kwa kweli awape hata moyo tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna upungufu wa watumishi, kuna upungufu wa Manesi, kuna upungufu pia wa nyumba na sio upungufu hakujawahi kujengwa nyumba za Madaktari kutokana na ufinyu wa eneo. Sasa niombe kabisa tufanye utaratibu wa kuhakikisha kwamba Madaktari wetu wanapatiwa nyumba kwa sababu hata *call allowances* zile zimekuwa ni shida mno kupatiwa pamoja na kuwa hawana nyumba, wanapokwenda kutibu wagonjwa usiku.



Mheshimiwa Mwenyekiti, naona changamoto kubwa zilizopo katika hospitali zetu kwanza kabisa kukosekana kwa hizi mashine wagonjwa wanakufa mno kwa sababu ugonjwa wanaotibiwa wanakuwa hawaujui. Madaktari sasa wana-*guess* aidha huyu mtu anaweza akawa anaumwa homa au akiwa na homa pengine ana mafua au *malaria*. Sasa ni vizuri pengine kutokana na changamoto hii ya vifaa tungefanya hata miradi ile ya *PPP* ili waweze kufunga katika hospitali zetu, ni bora tulipie hiyo huduma kuliko kwenda kuitafuta hiyo huduma Muhimbili au kuja Dodoma. Kwa sababu ukienda Muhimbili bado utatumia gharama kubwa, lakini tukipata wawekezaji wakawekeza katika hospitali zetu itatusaidia, wagonjwa watatibiwa magonjwa ambayo kwa kweli yatusaidia kwamba watakuwa wanajua anachotibiwa mgonjwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nipongeze Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Taasisi ya Saratani *Ocean Road*, Hospitali ya Benjamini Mkapa, kwa kweli hizi hospitali hata katika hotuba yake ametueleza kwamba zimefanya kazi kubwa kweli kweli, badala ya wagonjwa kupeleka nje ya nchi sasa hivi wanatibiwa hapa nchini. Hii ni kazi kubwa ya Chama hiki cha Mapinduzi na Rais wetu na Serikali hii kuhakikisha kwamba wananchi wanatibiwa hapa nchini. Hata hivyo, kuna changamoto, naomba Mheshimiwa Waziri anisikilize vizuri, wanapokwenda kutibiwa kwenye hizo hospitali, wanavyosubiri sasa tiba hizo labda kufanyiwa mionzi ya kansa au figo hawana pa kukaa, wamekuwa wakupata shida mno. Niombe sasa kama kuna uwezekano ufanywe utaratibu, watengenezewe maeneo maalum ya kuhakikisha kwamba wakati wanasubiria basi wanakaa pale, kwa sababu tumekuwa tukifanya michango kwa wagonjwa ambao wamekuwa wakitoka nje kwenda kusubiri hayo matibabu, kwa kweli hili naliomba liangaliwe kwa hali ya juu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwapongeze pia *MSD*, wanafanya kazi nzuri mno ya kusambaza dawa, nakumbuka kipindi kilichopita kila aliyekuwa anachangia alikuwa anasema upungufu wa madawa, lakini *MSD* sasa hivi inafanya kazi nzuri mno hata katika Mkoa wetu wa Iringa

wamekuwa wakisambaza dawa, nimefanya ziara nimekuta wanafanya kazi nzuri sana. Kwa hiyo niwaombe waendeleo kufanya kazi hiyo nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu Bima ya Afya; nipongeze Bima ya Afya kwa Wote, kwa kweli huu mpango najua utachukua muda mrefu, lakini uwepo mchakato na wenzangu wamelizungumzia sana, uwepo mchakato wa haraka kuhakikisha wale ambao hawana Bima ya Afya sasa hivi wanakufa, kuna wengine ambao hawatibiwi, tufanye mchakato kwa sababu najua walio wengi na ndio wanyonge na Serikali hii inawajali wanyonge, sasa tuhakikishe hawa wanyonge wetu ambao hawana bima za afya tuwaweke utaratibu mzuri wa kuwatibu ili waweze kutibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie huduma ya afya kwa watu wenye ulemavu; Mheshimiwa Ummy alishakuja kujionea kwenye kongamano la watu wenye ulemavu kwa *Ikupa Trust Fund*. Nami pia ni Mjumbe katika Kamati ya Watu Wenye Ulemavu, hawa watu wanapata shida sana kutokuwa na mkalimali wa kuwasaidia wakati wanaenda kwa Daktari. Sasa je, Serikali inawasaidiaje? Kuna mmoja alisema kwamba alipoteza mpaka mtoto wake, yeye ni kipofu lakini ameenda kujifungua mtoto kabadilishiwa mtoto, sasa wawekewe utaratibu mzuri kuhakikisha Watu Wenye Ulemavu nao wanatendewa haki katika matibabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie dawa za uti wa mgongo, ni ghali mno, watu wengi sana wanakufa mimi niliona, waweke utaratibu dawa hizi zipunguzwe bei ili watu waweze kutibiwa, zinaua watu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie Bima ya Wazee na Watu Wenye Ulemavu; hii bima pamoja na kuwa vitambulisho sisi kwetu wamepata wengi sana, lakini bado dirisha lile lina dawa kiasi kidogo sana, wengi hawapatiwi, ukizungumza na wazee unaona wanalalamika kwamba dawa zile hawapatiwi zote na kuna baadhi ya vipimo

hawapimwi na wazee kila wakati ni kuumwa, ni migongo, ni nini, lakini dawa hawapatiwi. Niombe kwa kweli Serikali iangalie wazee wetu wapatiwe dawa ambazo zinahitajika katika kile kitambulisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tutakuwa hatuwatendei haki wadau ambao wamekuwa wakichangia huduma za afya katika mkoa wetu. Tumpongeze sana Mheshimiwa Asas m-NEC wetu wa Mkoa, kwanza kabisa ametujengea jengo la damu salama katika mkoa wetu, lakini ametujengea jengo la watoto njiti, vilevile ICU, jamani Mwenyezi Mungu ampe nini huyu baba, tunamshukuru sana. Pia kajenga jengo la wazee, zuri, Mheshimiwa Waziri aje atutembelee aone wazee wanaishi kwa raha mustarehe. Hii yote ni kazi ya m-NEC wetu wa mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama cha Mapinduzi Wilaya, pia kimeleta mashine za kufulia mashuka. Kwa hiyo hata Chama chetu cha Mapinduzi kinafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo kwa kweli na mimi nitoe pole kwa Mheshimiwa Mengi, pole nyingi sana kwa sababu ni baba ambaye ametufundisha mambo mengi sana na Mwenyezi Mungu amrehemu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Peter Msigwa ajiandae Mheshimiwa Janeth Masaburi

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kumwomba Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema peponi Mheshimiwa Mengi ambaye amekuwa na mchango mkubwa katika Taifa letu. Pia niwashukuru Madaktari wote nchini, Manesi na Wauguzi wote nchini, kwa kweli wamekuwa wakifanya kazi

kubwa, kazi ngumu, kazi ya wito, kazi ya kujitolea. Niwashukuru wote kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Iringa Mjini kwa kazi kubwa ambayo wamekuwa wakiifanya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niseme mawili matatu yanayohusu jimbo langu na mengine nitaangalia yanayohusiana na Taifa. Amezungumza Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum hapa kuhusiana na Hospitali yetu ya *FRELIMO* ya Manispaa ya Iringa, asubuhi nimeuliza swali hapa, nashukuru Waziri amejibu lakini niombe wizara wasaidiane na TAMISEMI, wilaya zingine zote zilipewa fedha zile karibu bilioni moja kusaidia vifaa, hospitali yetu ile ni ya muhimu, ikiwezesha itasababisha hospitali ya rufaa ipunguziwe mzigo. Niombe sana tusaidiane kuhakikisha haya mambo yanafanyika kama Waziri alivyosema wa TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa Mheshimiwa Ritta hajasema sana, hospitali ya mkoa kwa sasa hivi hakuna bingwa wa mifupa, Daktari wa Mifupa wala Bingwa wa *surgery*. Hii yote aliyosababisha ni Mkuu wa Mkoa katika ziara yake aliyosema Iringa mpya. Katika Iringa yake mpya imekuwa ni ya kubomoa. Sasa hivi pale Hospitali ya Rufaa kuna matatizo makubwa sana, wagonjwa wanategemea Walimu wanaokuja kuwafundisha wanafunzi wa *UDOM* kuja kufanya upasuaji, kwa hiyo imekuwa ni ngumu sana. Niombe sana Wizara na Serikali kwa ujumla, hebu tuangalie viongozi wasiwe wana-*demoralize* wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hao Madaktari wanasomeshwa na nchi kwa gharama kubwa sana na wanafanya kazi kubwa sana, kama kuna matatizo ya *management*, ya kiutendaji, zifuatwe *procedures* za namna ya ku-*deal* nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakumbuka Mkuu wa Mkoa alimdhaliisha Daktari Nyakioto, ni bingwa, amefanya kazi kubwa sana, pia kuna Daktari Rehema naye ameondoka lakini hawa watu wote wamekimbia Iringa ni kwa sababu ya utendaji wa hovywa wa wanasiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Wizara *iji-commit* kwa sababu Wakuu wa Wilaya wala Wakuu wa Mikoa siyo ngazi za kutoa adabu kwa watendaji. Naomba mnapotoa majibu hapa mtangazie Tanzania kwamba wao wala viongozi wa chama kama kule Arumeru, kiongozi wa kata tu anampa maagizo daktari eti dakika 15 umefika. Naomba Serikali itangaze kwamba wao siyo ngazi za kuwawajibisha, madaktari hawa wanafanya kazi kubwa sana. Niombe hilo mlifanyie kazi ili madaktari na manesi wetu wafanye kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, madaktari na wauguzi wetu wanahitaji kutiwa moyo, ni watu ambao wanashika vinyesi, mikojo na mautumbo yetu, lazima tuongee hizo ni kazi za kujitolea. Viongozi wa kiserikali na wenye vyeo tunatakiwa tuwape moyo, *tusiwa-demoralize*, tuwape moyo wafanye kazi vizuri kama ambavyo tuna mategemeo mazuri kutoka kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba yetu ya Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Esther ameorodhesha viongozi wengi wa kisiasa na amewataja. Namba hili suala mlitolee maamuzi ya msingi kabisa ili utendaji kazi uende sawasawa kama sheria na taratibu zinavyotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ni hili ambalo na Mheshimiwa Sakaya amelizungumza ni la wazee kwenye masuala ya pensheni, mliahidi kabisa kwamba mtawaongeza kutoka Sh.50,000 kwenda Sh.100,000, wale waliokuwa *PPF* wameongezwa wengine wamekuwa wakidai hawajapata. Ni lini sasa fedha zao ambazo wanatakiwa waongezewe watapewa? Hawa ni wazee ambao wamefanya kazi kubwa katika Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wataalam wengine wanasema *we are just dwarf standing on the shoulder of the giants*. Sisi ni matokeo ya hao wazee waliotangulia. Tutakuwa ni taifa la namna gani tusipowaenzi wazee. Tukumbuke na sisi tuta-*phase out*, tutazeeeka. Hiyo nafasi uliyonayo hapo Mheshimiwa Waziri na Naibu wako kuna wengine walikuwepo

wameondoka. Hata mimi nafasi yangu ya Ubunge niliyonayo hapa kuna wengine walikuwepo wameondoka. Tunapofika mahali kama taifa wazee hatuwaheshimu, hatuwatunzi kwa kweli hatuwatendei haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri katika maeneo haya ya kutunza wazee, hebu tusilaaniwe na Mwenyezi Mungu tunapokuwa tumewasahau wazee. Tupange bajeti za kutosha kuwasaidia hawa wazee. Wazee wengi ukiwakuta katika maeneo mbalimbali wanalalamika.

**MBUNGE FULANI:** Akina Mzee Lubeleje.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Wanalalamika hawapati huduma zinazotakiwa. Ndiyo maana wakati mwingine tunalazimika kurudi Bungeni humu kwa sababu hali ni ngumu huko mitaani.

**MBUNGE FULANI:** Usituseme bwana.

**MBUNGE FULANI:** Akina Mzee Lubeleje.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya bajeti ya Wizara hii imeendelea kushuka, sasa hawa wazee tunawasaidiaje? Wizara hii ni nyeti, amezungumza Mheshimiwa Lwakatare hapa, kweli kuna vifo vingi ambavyo kimsingi siyo Bwana ametwaa, ni kwa sababu hazijapatikana huduma za msingi ambazo zingeweza kuokoa maisha ya watu wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wengi wanakufa kwa sababu hawajapata huduma zinazostahili. Akina mama wajawazito wengi wanakufa kwa sababu hawakupata huduma zinazostahili. Watu waliopata ajali wengi wamekufa si kwa sababu walitakiwa kufa, ni kwa sababu hawakupata huduma zinazostahili. Tumekuwa hatuna vifaa vya kutosha, hatuna madaktari wa kutosha lakini hata hao madaktari wachache walioko bado tuna wa-*frustrate*. Naomba sana katika eneo hili Mheshimiwa Ummu na kweli wengine

wamesema mara nyingi ukipigiwa simu umekuwa una-*respond* pamoja na Naibu wako...

**MBUNGE FULANI:** Wanachapa kazi.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Una-*respond* na unajibu kwa wakati, ningeomba hii ishuke mpaka huku chini na madaktari hao walindwe. Wana chama chao, wana namna yako ya kuwalinda, walindwe hawa madaktari kama wana makosa mimi siwatetei lakini hatuwezi kuwaadhibu madaktari wetu kwenye mikutano ya hadhara, hatuwezi kuwaumbua madaktari wetu kwenye vikao vya kisiasa. Wahukumiwe, waadhibiwe kwenye *proper channel*, inaumiza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkutano mmoja wa siasa umeathiri hospitali yangu hakuna madaktari bingwa, ina maumivu makubwa sana. Nikuombe Mheshimiwa Ummu Mwalimu, hili linaniumiza sana kwa sababu hapa napata meseji liringa kama unavyoiona, tumeitengeneza *Southern Circuit* ili tukuze utalii, tunahitaji tuwe na hospitali za kutosha. liringa ni mahali pazuri, pana hewa nzuri, tuna mazingira mazuri lakini inapofika mahali tunakosa madaktari tunaongeza matatizo yasiyokuwa ya lazima katika Manispaa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo Waziri amekuwa aki-*respond* nimwombe katika suala hili alisaidie taifa zima kwamba tuheshimu madaktari wetu ili wafanye kazi kwa weledi. Anafika Mkuu wa Mkoa anasema, eti sasa hivi daktari ni marufuku kumwekea *drip* mgonjwa kabla hujampima. Sasa Mkuu wa Mkoa amesomea wapi kazi hiyo?

**MBUNGE FULANI:** Na mgonjwa kama anaharisha?

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Ndiyo, kama mgonjwa anaharisha daktari si ndiyo anajua kazi yake? Leo Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya anajua utaratibu huo, pamoja na kwamba mnasema Chama cha Mapinduzi, ina maana chama ndiyo kinatuma watu wawaambie hivyo madaktari? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mambo ambayo kama Bunge lazima tukemee, madaktari wetu walindwe, waheshimiwe, wasikoselewe kwenye mikutano ya hadhara. Hii Mkuu wa Mkoa wa Iringa anisikie, imeleta shida safari hii, ziara yake ya Iringa mpya imekuwa matatizo katika Mkoa wa Iringa, hatukuwa na mazoea haya. Najua Mheshimiwa Kabati ameogopa kusema kwa sababu ya mambo ya ki-*protoca*llakini Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa ametuletea tatizo katika Mkoa wetu wa Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Peter Msigwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Janeth Masaburi na Mheshimiwa Hassan Masala ajiandae.

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai ambayo amenijalia na kuniruhusu leo hii kusimama na kutoa mchango wangu kwa maslahi ya taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii pia kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Ummy, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Watendaji wote wa Wizara na madaktari na wauguzi wote nchini kwa kazi nzuri na njema na takatifu wanayoifanya kuhakikisha afya za Watanzania zinaimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyezi Mungu aliumba mbingu na nchi, naomba ninukuu Biblia, Kitabu cha Mwanzo, kinasema: “Mungu akasema, iwe nuru; ikawa nuru. Mungu akaiona nuru, ya kuwa ni njema; Mungu akatenga nuru na giza”. Mwisho wa kunukuu. Maana yake ni nini? Mwenyezi Mungu alifanya tathmini ya uumbaji wake hatua kwa hatua. Hata alipomuumba mwanadamu, alimuumba mwanaume kisha akatathmini akamuumba mwanamke. *(Makofi)*



Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Watanzania wenzangu tufanye tathmini ya kazi kubwa inayoifanywa Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi wa Mheshimwa Dkt. John Pombe Magufuli akisaidiwa na Mawaziri, Makatibu Wakuu, watendaji na madaktari na wauguzi hapa nchini. Mabadiliko makubwa yamefanyika kusema ukweli, mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini asilimia kubwa hata na ndugu zetu hapa wanaamini na wanatambua amefanya kazi kubwa lakini haya huwa wanafanya tathmini wakiwa wamejifungia kwenye vyumba vyao. Hapa ni kawaida kwa sababu hata kwa Mungu pia kuna viumbe ambao hawamuungi mkono Mwenyezi Mungu, ni kawaida hiyo.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Hebu nyamazeni pale.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Mmepata hiyo, katika kipindi hiki cha uongozi Awamu ya Tano chini ya jemedari wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ameidhihirishia ulimwengu na hata mataifa yanapongeza juhudi na kazi kubwa anayofanya, ni lazima tuseme. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Taasisi ya Jakaya Kikwete imefanya kazi kubwa sana chini ya uongozi wa Dkt. Janab, Dkt. Kisenge na madaktari wengine ambapo kwa sasa kwa asilimia 85 huduma za moyo zinafanyika nchini. Mtakumbuka siku za nyuma Watanzania wengi walikuwa wanachangiwa kwenda kupata matibabu nchini India, sasa hivi hiyo ni historia ni lazima tupongeze Serikali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali ya Muhimbili inaendelea kufanya kazi vizuri na wameboresha maeneo mengi hata kule ndani ukienda utatambua ni hospitali ya taifa. Taasisi ya Mifupa (MOI), inafanya vizuri. Taasisi ya *Ocean Road* inafanya vizuri. Hospitali ya Mlonganzila inafanya vizuri. Hospitali ya Benjamin Mkapa inafanya vizuri na hasa katika magonjwa ya figo. Hivi karibuni tumeambiwa kwamba hata viongozi na baadhi ya Mabalazi wamekuja kutibiwa katika hospitali zetu, haijapata kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nauliza ni lini tutawapa tuzo madaktari wetu, tuwatambue kwa kazi njema wanayofanya. Tusingoje mtu akifaa ndiyo tunaanza kusema maneno mengi. Tuwatambue kwa kazi njema wanazofanya za kuokoa uhai na hasa madaktari bingwa, tuna madaktari wengi sana wanaofanya vizuri. Nitatoa mfano, tuna Profesa Janab, Profesa Mseru na madaktari bingwa wengine, Dkt. Magandi, tuna wataalam wengi sana hapa tunaomba tuwatambue hata kwa kuwapa tuzo. Mheshimiwa Ummy nakuomba Wizara ifanye mchakato wa kuwatambua madaktari na wauguzi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuboresha hospitali za Wilaya. Hivi karibuni tumepata taarifa wamejenga vituo vya afya 352 katika kipindi kifupi sana, haijawahi kutokea na itaendelea kuwauma sana. Hospitali mpya za Wilaya 67 zimejengwa katika Mikoa ya Simiyu, Geita, kazi nzuri imefanyika katika sekta ya afya. Kwa sababu inauma na mnatambua kwamba kazi njema imefanyika na majibu tunayo, Chama cha Mapinduzi kimeendelea kuielekeza Serikali kutimiza haja ya Watanzania na hasa walio wanyonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kutambua kwamba kinga ni bora kuliko tiba. Taasisi ya Chakula na Lishe kama itawezekana iundiwe Wizara yake au itengewe fedha za kutosha ili kuweza kuhamasisha wananchi wajue jinsi ya kula chakula bora, kufanya mazoezi ili kuzuia magonjwa mengi ambayo siyo ya lazima. Magonjwa haya yanailazimu Serikali kutumia fedha nyingi sana. Kwa hiyo, kinga ni bora

kuliko tiba, nakuomba Mheshimiwa Waziri hili ni jambo la muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati fulani nilibahatika kwenda China katika Mji wa Shanghai, nilikuta kuna wazee wanakaribia miaka 80 mpaka 90 lakini wako mtaani wanafanya kazi na wana nguvu. Hiyo yote inatokana na ulaji wenye kuzingatia ubora wa chakula na mazoezi. Hiyo inasaidia hata kupunguza gharama za matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwaambia Waheshimiwa Wabunge tufanye mazoezi na wenye *Gym* wengine hapa wanapiga debe. Pia tuzingatie kula kwa wakati chakula bora na kulala mapema, yote ni katika kuzuia maradhi mengine yasiyokuwa na lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kuwapongeza madaktari wote nchini. Kusema ukweli wanafanya kazi njema na kazi ya Mungu, wanafanya kazi ya wito. Mimi nasema daktari hana tofauti na Mchungaji, Askofu au Shekhe, wanafanya kazi ya kumsaidia Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, naiomba Serikali iwaangalie, kuwaheshimu, kuwajali na kuwathamini madaktari wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nikupongeza Mheshimiwa Waziri na timu yako, Mwenyezi Mungu azidi kukulinda. Nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kukuteua mwanamke hodari na Naibu wako mmefanya kazi nzuri ya kutuongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Janeth Masaburi. Tunaendelea na Mheshimiwa Hassan Masala.

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kunipa nafasi na mimi pia niweze kuchangia Wizara hii ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Wabunge wenzangu kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi nzuri na kubwa ambayo anaifanya ya kuhakikisha Watanzania wanapata huduma bora katika eneo hili la afya ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nimpongeze kiupekee sana Waziri wa Afya, dada yangu Mheshimiwa Umyy Mwalimu akisaidiana na Mheshimiwa Dkt. Ndugulile kwa kazi nzuri na kubwa ambayo wanaendelea kuifanya ya kuhakikisha sekta ya afya inaendelea kutoa huduma kama ambavyo imeahidiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mtovu wa fadhila kama sitasimama hapa na kutoa neno la pongezi kwa Serikali hii kutokana na kazi kubwa ambayo wameifanya. Wananchi wa Jimbo la Nachingwea kwa sehemu kubwa wamekuwa wanapata huduma za afya katika hospitali kubwa ya Wilaya ambayo Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu mmetembelea mara kadhaa. Kwa kweli naomba nitoe neno la shukrani kutoka kwa wananchi wale kwa namna ambavyo mmejali kwa kuja kukagua mazingira, lakini pia kwa kusikiliza maombi mbalimbali ambayo tumeyatoa kwenu kama Wizara na kwa kweli mmetuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niliona nitumie nafasi hii kuwashukuru sana lakini bado tunaendelea kuwaomba yale ambayo tumeyaleta mezani kwenu basi muendeleee kutuunga mkono ili wananchi wale waweze kupata huduma kama ambavyo tumeahidi. Hapa ninapozungumza sasa hivi, uko ujenzi wa Jengo la *OPD* kupitia shilingi milioni 400 ambazo zimetoka katika Serikali yetu. Lengo kubwa ni kuhakikisha huduma za afya kwa wananchi zinaendelea kuimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nishukuru wananchi wetu wamekuwa wanapata huduma pia katika Hospitali ya Rufaa pale Sokoine, Lindi. Hospitali ya Sokoine, Lindi sasa hivi ni kubwa na inatoa huduma katika maeneo

mengi sana. Uboreshaji mkubwa umefanyika katika upatikanaji wa maji lakini pia uboreshaji wa mazingira yale ya hospitali ambayo wananchi wetu wengi wanaotoka katika Wilaya za Mkoa wamekuwa wanaenda pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi letu ambalo ningependa kuliwasilisha kwenu ni kutuongezea wataalam hasa madaktari bingwa katika hospitali. Madaktari hawa watakwenda kuhakikisha wananchi wanaotoka katika maeneo ya Nachingwea, Liwale na maeneo mengine hawaendi sasa Muhimbili badala yake huduma zote wanazipata katika hospitali ile ya Rufaa ya Sokoine ambayo Serikali imefanya kazi kubwa sana kuhakikisha mambo yanakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nilitaka nijaribu pia kutoa ushauri na kuomba watu wa Wizara, Mheshimiwa Ummy utakumbuka tulifanya ziara Naipanga. Naipanga ni sehemu ya Tarafa lakini idadi ya wananchi pale ni zaidi ya watu 14,000, umuhimu wa kujenga kituo cha afya na kwa ahadi ya Serikali nafikiri pia utakumbuka na Naibu wako Waziri Mheshimiwa Dkt. Ndugulile tulifanya ziara pale. Nawaomba sana hebu tufanye yale ambayo tuliwaahidi wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama wananchi wa eneo lile tayari tumeshaanza kufanya jitihada za kuhakikisha tunatenga eneo. Hata hivyo, kwa sababu lengo ni kupandisha hadhi ile zahanati iliyoko basi, naamini ahadi ile wakati mnaenda kuhitimisha basi hamtatusahau ili wananchi waweze kupata huduma pale wasitembee umbali mrefu wa kwenda Hospitali ya Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenda Hospitali ya Wilaya maana yake tunaweka wingi wa watu usiokuwa na ulazima. Kwa hiyo, ili kuepuka umbali lakini pia kuwasogezea wale wananchi huduma, naomba niwakumbushe kwa sababu ni eneo ambalo tayari wenyewe mmeshaona mazingira halisi ya pale na namna ambavyo wananchi wamekuwa wanapata shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kiko kituo kingine cha Marambo. Kituo hiki kiko ndani ya Tarafa pia ya Ruponda, idadi kubwa ya wananchi wanatembea umbali mrefu kwenda Hospitali ya Wilaya. Naomba kupitia bajeti hii na mikakati mingine ambayo mnaendelea nayo kama Wizara, basi muone umuhimu pia wa kutuunga mkono ili tuweze kupandisha na kuboresha kituo kile cha afya kiweze kutoa huduma kwa wananchi wote wanaotoka Ukanda wa Marambo. Kule watahudumia wananchi wanaotoka Mkoka, Marambo yenyewe, Chilola pamoja na maeneo ya jirani ambayo wananchi wamekuwa wanategemea kituo kile kwa ajili ya kupata huduma zote muhimu ikiwemo upasuaji pamoja na kupata tiba nyingine muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho ambalo niliona pia nilizungumze, ndani ya Wilaya ya Nachingwea tuna kituo cha *Mission* cha Mnero. Kituo hiki ni cha zamani kidogo na kinahudumia wananchi wanaotoka Tarafa ya Ruponda. Kwa muda mrefu kituo hiki huduma zake zimekuwa za kusuasua. Tunashukuru Serikali kwa sababu imekuwa inapekeleka *Basket Fund* ingawaje siyo fedha ya kutosha sana lakini jitihada zozote zitakazofanyika za kuhakikisha kituo kile kinapatiwa fedha za kutosha naamini kitaenda kuondoa uwingi wa watu wanahitaji huduma katika Hospitali ya Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, pamoja na watalam wako hebu nawaomba sana pamoja na mikakati mingine mnayoendele a kuifanya, hebu tukiangalie kituo hiki ambacho kwakweli kinatusaidia sana sambamba na kituo kile cha Ndanda ambacho nacho pia kinafanywa kwa mtindo huo kwa sababu kiko chini ya *Mission* lakini bado mkitoa fedha za kuhakikisha huduma zinapatikana katika maeneo haya basi wananchi wetu wengi wataenda kunufaika na huduma bora ambazo zitaenda kutusaidia kuondokana na kero za wananchi kukosa huduma bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nikuombe Mheshimiwa Waziri, bado tunachangamoto ya huduma ya

magari kwa ajili ya kusafirishia wagonjwa. Kwanza katiak hospitali ya wilaya bado *ambulance* tuliyonayo ni moja, haitoshelezi mahitaji hivyo tunalazimika kuchukua magari mengine nje ya *ambulance* kwa ajili ya kutoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunacho kituo cha afya cha Kilimarondo ambacho ninaishukuru Serikali imetupatia milioni 400 kituo kimekamilika lakini bado tuna changamoto ya kupata gari ya wagonjwa na ni umbali wa zaidi ya kilometa 120 ambayo wananchi wale kwa kukosa gari wamekuwa wanapata changamoto kubwa kwa muda mrefu. Kwa hiyo, ninaomba pamoja na kazi nzuri iliyofanyika, bado nilete maombi kwenu watu wa Wizara muweze kutusaidia katika mgao wa magari basi maeneo haya mawili yapate magari ya wagonjwa ili wananchi waweze kupata huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hassan, tunaendelea na Mheshimiwa *Engineer* Gerson Lwenge.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uzima na kuweza kufanya mambo ya kuwasaidia Watanzania katika kujiletea maendeleo. Awali ya yote nitoe pole nyingi kwa msiba wa Dkt. Reginald Mengi, ni kweli kwamba maandiko yanasema hakuna mji udumuo na kwamba kila nafsi itaonja mauti. Basi naomba kifo cha Dkt. Mengi kiwe ni fundisho kwa sisi tulio baki kwam ba iko siku yetu na kila mmoja ataulizwa nini amefanya kwa ajili ya jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kumpongeza sana Waziri wa Afya pamoja na Naibu wake, Katibu Mkuu na viongozi wote kwa namna wanavyoiongoza Wizara hii. Wilaya ya Wanging'ombe haina hospitali ya wilaya, nishukuru katiak bajeti ya mwaka huu fedha zimetolewa, tumeanz akujenga hospitali ya Wilaya na nafikiri kufika mwezi wa Saba tutakuwa

tumemaliza. Lakini pia nishukuru kwa uboreshaji wa vituo vya afya viwili, kituo cha Wa nging'ombe pamoja na Parangawani. Wananchi wale walikuwa wameanza kujenga kwa nguvu zao na Serikali imewaunga mkono. Basi naomba kwa sababu wameshamaliza, vifaa tiba na vifaa vinavyohitajika pamoja na wahudumu wa hospitali zile waweze kuleta m apema ili huduma ya afya iweze kufanyika.

Mheshimwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka 2018/19 na kwa sababu Serikali ni moja, na nimemuona Mheshimiwa Dkt. Mpango yuko hapa, kulikuwa na ahadi ya kutolewa karibu billioni moja kwa kila halmashauri ili kukamilisha maboma ya vituo vya afya pamoja na shule za msingi. Fedha ile haikutolewa mpaka leo na sisi tulikuwa tumewahamasisha wananchi wamejenga maboma kwa wingi kweli kweli. Wilaya ya Wanging'ombe tunavyo vituo vya afya saba, zahanati 13, wodi za wazazi mbili, nyumba za waganga tatu ambazo kukamilisha kwao kunahitaji karibu bilioni 2.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wananchi wale walikuwa wanategemea sana fedha ile itoke. Naomba sana kabla ya Bunge hili sisi ili tusionekane tunawadanganya wananchi. Tujitahidi Serikali iweze kuleta fedha hizi ili kwa juhudi hizi ambazo wananchi wanaendelea kuunga mkono kazi nzuri anayofanya Dkt. John Pombe Magufuli, basi fedha zile zitoke tuweze kukamilisha majengo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika Awamu ya Nne, Rais Dkt. Kikwete aliahidi gari la wagonjwa katika kituo cha afya cha Makoga. Sasa ni miaka sita gari lile halijapatikana. Najua Serikali yangu ni sikivu, basi naomba sana gari la wagonjwa lililoahidiwa na Rais liweze kutolewa kwa kituo cha afya cha Makoga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie pia katika hoja ya Waziri, kwanza pia nimpongeze nimeona pamoja na kwamba yeye ni Waziri wa Afya, amekuwa anashiriki katika ujenzi wa bweni la watoto wa kike katika sekondari ya Kilale katika Jiji la Tanga. Basi nimtakie kila la kheri hiyo azma



aliyonayo katika wananchi wa Tanga. Lakini nikukaribishe pia kule Wilaya ya Wanging'ombe tuna shule ya wasichana ya Maria Nyerere na tuna tatizo la bwalo, basi naomba pia ukiweza kuja kuhamasisha wananchi tutafurahi sana ukitembelea wilaya ile. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia Bima ya Afya kwa wote, ni kweli katika eneo hili nafikiri tufanye kazi ya ziada zaidi. Hizi bima za afya ambazo zinatolewa katika kiwango cha kaya inakuwa haikidhi kupata matibabu wakienda kwenye hospitali zingine. Sasa nilifikiri huu mpango wa kuleta hii sheria tuwe na Bima ya Afya kwa wote. Kwa kweli naiunga mkono na ningepomba jambo hili lifanywe haraka. Lisichukue muda mrefu ili kusudi wananchi wote wapate huduma za afya mahali popote watakapoweza kwenda katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za afya zinazotolewa na Bima ya Afya kwenye hotuba amesema ni asilimia 8 tu ya Watanzania wote na hii nyingine ni asilimia 25 tu. Kwa hiyo, inakuwa haitoshi, kwa hiyo wananchi wengi wanapata shida katika kuweza kupata huduma kwa kutumia Bima za Afya.

Pia kuna ahadi kwamba wazee wanaokuwa na zaidi ya miaka 60 watapata matibabu bure. Mipango ya kutoa hivi vitambulisho inakwenda polepole sielewi kwanini kwa sababu katika wilaya yangu hakuna hata mzee mmoja aliyepewa kitambulisho cha kupata matibabu bure na inawezekana na wilaya zingine hali kama hiii na tumeisema kwa muda mrefu. Kwa hiyo naomba sana mharakisha katika mpango huu kuhakikisha wazee wetu kweli wanapata tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nipongeze utaratibu kwamba mna makazi ya wazee wasiojiweza 17. Basi naomba sana yaboreshwe makazi haya na wapate huduma zote ambazo ni za msingi wazee wetu ambao wameta mchango mkubwa sana kwa ujenzi wa Taifa hili. Tusiwaache wanakuwa ombaomba na Serikali yetu sikivu na ina uwezo wa kufanya mambo makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi naomba sana suala hili la wazee ulipe umuhimu wa pekee. Pia kwenye hizo hospitali ni kweli liwepo dirisha maalum, wazee wakifika pale wasikilizwe kwanza kabla ya watu wengine. Hili ni jambo ambalo litakuwa jambo jema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja hii na ninakubaliana na mawazo yote ya Waheshimiwa Wabunge kwamba Wizara hii kwa kweli imepata wanaoweza kuleta ufanisi mkubwa. Waziri na Naibu kwa kweli mnafanya kazi nzuri. Mnajibu maswali mazuri, kila mtu huwa anaridhika katika majibu yenu. Nashukuru kwa kupata nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa *Engineer* Gerson. Tunaendelea na Mheshimiwa Suzana Mgonokulima, baadaye Mheshimiwa Mwantumu Dau atamalizia kwa dakika tano.

**MHE. SUZANA C. MGONOKULIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mungu kunipa uzima kuwepo mahali hapa jioni ya leo niweze kuchangia Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti ya CAG ya 2017/18 inaonesha kuna ujenzi wa hospitali m bili za rufaa Mkoa huu mmoja na hospitali hizo zinazojengwa Chato imetengewa bilioni 9.9, Geita billioni 5.9 kwa mkoa mmoja tu ni bilioni 16. Hizo ni hospitali za rufaa kwenye mkoa mmoja. Ukizingatia huu mkoa wa Geita, wananchi wa mkoa huo wapo milioni 1.7. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuchukue Kanda ya Kusini yenye mikoa mitatu, Lindi, Mtwara, Ruvuma haina hata hospitali ya rufaa na tukichukua hii mikoa mitatu ina watu milioni 3.6. Ninashindwa kuelewa Wizara ina maana gani? Tunaposema tunataka kujenga hospitali za rufaa tunaangalia uwiano upi kwa wananchi wa maeneo husika? Nitamtaka Waziri anapokuja kuhitimisha hoja hii aje na majibu yanayotuongia mpango wa Wizara yake inaangalia eneo

labda la kiongozi fulani lakini sio inaangalia tija kwa wananchi waliopo eneo husika kupeleka hospitali za rufaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafikiri tunazungumzia upungufu wa watumishi Sekta ya Afya tena hawa watumishi wenye ujuzi wa kutoa huduma kwenye vituo. Tunapozungumzia hivi sasa hivi tuna upungufu wa asilimia 56, ni tatizo kubwa sana kwa Taifa. Nafikiri kwenye kitabu cha maendeleo sijaona mahali ambapo pameonesha kwamba katika mikoa ile niliyoitaja mitatu ya Kusini kwenye kitavbu cha maendeleo hakijatengewa hata bajeti. Hivi watu wa Kusini sisi tuna tatizo gani? Geita ni mkoa mpya kama Mkoa wa Njombe, Njombe ni ukweli usiopingika kuna matatizo yaliyozidi kuliko hata watu wa Geita lakini hakuna kinachoonekana kama Serikali inaangaliaje hivi vipaumbele katika hii mikoa mipya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nije na uwiano. Kwenye kitabu hiki nimejaribu kusoma vizuri sana, sikuona mahali panapoonyesha hospitali teule ya Kibong'oto iliyopo Mkoani Kilimanjaro kama imetengewa fedha ili waweze kuiboresha ukiangaliano uwiano wa ugonjwa huu wa kifua kikuu kuwa watu 10 wazima, watu 30 wanaohakikiwa wanakuwa na kifua kikuu. Ukiangalia kwenye uwiano wa Watanzania milioni 55 kwa sasa ukipiga mahesabu ina maana Taifa letu lina watu wenye ugonjwa wa Kifua kifuu milioni 18, hili si jambo dogo! Milioni 18 ambapo ukiangalia asilimia 30 ya wenye...

## T A A R I F A

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Mbunge asipotoshe. Kwa mujibu wa Taarifa za Wizara ya Afya na Shirika la Afya Duniani Tanzania inahisiwa kuwa na wagonjwa wa kifua kikuu 154,000 tu na sio milioni kumi na ngapi kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suzana.

**MHE. SUZANA C. MGONOKULIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najua yeye ndiye mwenye Wizara yake tunayojadili, bado alikuwa na muda mkubwa wa kuja kujibu hii hoja kama nilivyomtaka wakati wa kujibu aje aseme.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suzan, kama unakosea haifai kwa sababu unakuwa unapotosha umma na yeye ndiyo anaelewa...

**MHE. SUZANA C. MGONOKULIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea. Niachie niendeleee. Nimesema katika watu 10,000 wazima, wapato 30 ambao wana hakikiwa, wana ugonjwa wa *TB*, tumefundishwa, *NGO* zinakuja hapa kutoa elimu na watu tunaandika ili tuje tuisaidie Serikali katika kuboresha kwenye bajeti. Sio kosa langu mimi, basi ni kosa la *NGO* zinazokuja kuelimisha kama wanatupotosha sio hoja yangu mimi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleee. Basi sasa katika hilo kama alivyosema Waziri hata kwa idadi hiyo, hiyo hospitali niliyoitaja kwenye kitabu chako hiki hujaitengea bajeti ili uiboreshe vizuri. Naomba niendeleee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilinde, umenipa muda mdogo nilikuwa na dakika 10 sasa dakika zangu nimepewa chache. Huduma ya lishe, nchi yetu ya Tanzania duniani ni ya 10, Afrika ni ya tatu, nchi ya Tanzania ilivyo, Mungu alivyoipendelea ina eneo kubwa, tunazalisha aina ya vyakula tatizo hapa ni elimu na elimu tunaipata wapi? Kwa Maafisa Maendeleo wa Jamii ambao katika Taifa letu wamekuwa ni wachache sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa maafisa maendeleo wa jamii wanaishia ngazi ya kati, elimu hii ili itusaidie kuangalia watu wapate chakula, lishe bora ianzie kwenye vitongoji vyetu tunakoishi. Tuitake Serikali ianjiri maana vyo vya maendeleo ya jamii vimepata wahitimu wengi ambao hawa na ajira, wamebaki mitaani. Hawa wangetoa elimu ya lishe nafikiri Taifa letu lisingefikia mahali hapa kulinganisha na neema ambazo Mungu nchi ya Tanzania aliipa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naingia kwenye suala la tiba asilia. Tulikuwa na mafunzo Mkoa wetu wa Iringa mwezi uliopita ambapo kuna NGO iliendesha hayo mafunzo. Mkoa wa Iringa tu hili naomba Waziri ulichukulie kwa sababu waliomba Wizara iangalie upya jinsi ya kusajili waganga wa jadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Iringa tu hadi sasa tunapozungumza umeshasajili waganga 878 na ambao hawajasajiliwa ni 900. Kwanini watu wameomba tulilite Bungeni? Imeonekana katika usajili huu nafikiri hakuna mpango mkakati ambao umeelekezwa hawa wanasajiliwa na afisa watendaji kwenye kata kiasi kwamba mtu anatoa hela anasajiliwa wanaanza kupotosha imani za watu ambao wanawadanganya kuwa akienda anasema kaleta kiungo cha albino...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa na m u da umekwisha.

**MHE. SUZANA C. MGONOKULIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa kuunga mkono hoja. Mheshimiwa Mwantumu Dau. Tuendeleo. Mheshimiwa Mwantumu Dau.

**MHE. SUZANA C. MGONOKULIMA:** Nimesema naunga mkono hoja hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dau tuendeleo.

**MHE. SUZANA C. MGONOKULIMA:** Siwezi kuunga hoja ya Dada Umyy.

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwantumu Dau tunaomba umalizie kwa dakika chache zilizobaki.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Dakika zangu umenipatia chache lakini hizi hizi naona zinaweza kutosha kidogo kwa mambo niliyokuwa nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa na hali ya uzima na afya na kutujaalia kuwa na mfungo wa Ramadan na leo ndiyo kwanza siku ya kwanza. Kwa hiyo Mungu atusaidie tufunge Ramadan kwa salama ana amani na tupendane sote humu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake ya Wizara ya Afya iliyojaa maono, haina mjadala. Mzungu amesema *no discussion*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuendelea, dakika zangu tano nataka kuzungumzia suala la mradi wa magonjwa yasiyo ambukizika. Kuna magonjwa yasiyo ambukiziki ni magonjwa ya sukari, presha pamoja na magonjwa ya shinikizo la damu. Magonjwa ya sukari haya ni magonjwa tutasema mfano kama yanapunguza ile hofu ya mgonjwa hasa atakapokuwa anapata dawa zake za uhakika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wagonjwa wa sukari ambao wagonjwa hawa wa sukari na presha zinaendana pamoja na shinikizo la damu lakini wagonjwa hawa wengine wanyonge, maskini hawana hata ile bima ya kuweza kununulia zile dawa zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, dawa ziko nyingi sana nakupongeza sana lakini hizi dawa kama huna pesa au humu bima unakuwa huwezi kuzinunua baadhi ya dawa nyingine maana kuna dawa nyingine zinashusha hata sukari, unapata nne, tano, saba, nane lakini kuna dawa nyingine zinakuwa hazishushi. Sukari ile inakuwa inapanda pamoja na presha hasa kuna dawa hizi za mizizi ambazo tunapewa humu nje. Dawa zile Mheshimiwa Waziri yanaua

kongosho la *euclin* kwa hiyo, yanapoua lile kongosho la *euclin* basi uhakikishe wewe mgonjwa wa sukari tayari umeshapata ganzi, tayari umeshapata hofu, tayari unakuwa huna nguvu za mwili ambao ukaweza kufanya harakati zako ulizokuwa nazo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, nakuomba naiomba Serikali yangu hivi sasa hivi kwamba itafute dawa ambazo zipunguze gharama ili na wale wengine waliokuwa hawana zile bima au hawana ile pesa waweze kuzinunua hizi dawa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwantumu Dau.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa suala langu hili la kuhusu magonjwa yasiyoambukizi ni hili. lakini la pili, nataka kuzungumzia...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwantumu muda wako umekwisha nashukuru sana kwa mchango mzuri. (*Makofi*)

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja lakini mmenipa dakika kidogo. Ahsante sana, pia nashukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujamaliza shughuli yetu nina mwongozo wa Spika ulioombwa na Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko kuhusu haki za watoto wanaoishi Magereza pamoja na mama zao.

Waheshimiwa Wabunge, leo asubuhi katika Kikao cha Ishirini na Mbili tarehe 7 Mei, 2019 niliombwa Mwongozo na Mheshimiwa Esther Matiko kutokana na majibu yaliyotokana na Serikali katika swali la msingi namba 180 iliyoulizwa na Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi kuhusu haki za watoto wanaoishi ndani ya Magereza pamoja na mama zao. Pamoja na maelezo mengine, Mheshimiwa Esther Matiko katika Mwongozo wake alisema kama ifuatavyo, nanukuu; wanakaa miezi sita na watoto wadogo wanakusanywa

wakati kuna *alternative* Serikali ingeweza kufanya isipeleke wale watoto pale gerezani. Kwa hiyo naomba Mwongozo wako Serikali iweze kusimamia haki na watoto na kuhakikisha ya kwamba wale watoto ambao wanakaa kule waweze kuondolewa magerezani.

Mheshimiwa Matiko (Mbunge) katika mwongozo wake ameonesha nia nje ya kuitaka Serikali kuchukua hatua zaidi za kusimamia haki za watoto walio magerezani. hata hivyo, baada ya kupitia Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) nimeridhika kuwa Serikali imetoa majibu yanayoridhisha na yanayojitosheleza kuhusu jambo hilo. Serikali ilitoa majibu kuwa watoto hao wamejikuta wao magerezani kutokana na mama zao kuhukumwa kutumia kutumia adhabu ya kifungo wakiwa katika hali ya ujauzito au watoto waliopolekwa huko pamoja na mama zao kutokana na kuwa na umri wa chini ya miaka miwili hivyo wanapaswa kupata haki ya kunyonya maziwa ya mama. (*Makofi*)

Serikali iliendelea kutoa ufafanuzi kuwa watoto hao wanapata malezi katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana (*day care center's*) kwa madhumuni ya kupata huduma ya malezo changamshi awali kuchochea ukuaji wa maendeleo ya kiakili, kimwili, kihisia, kijamii na kimaadili. Pia kwa mujibu wa sheria, wanapata mlo kamili, virutubisho, huduma za afya pamoja na chanjo kwa watoto chini ya miaka miwili.

Majibu ya Serikali yalimridhisha muuliza swali la msingi ambaye alisema kama ifuatavyo; nanukuu "pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo nimeridhika nayo na napenda nitoe pongezi kwa Mkuu wa Gereza la Segerea kwa kutekeleza hayo yote ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyasema na kupeleka watoto kwenye *nursery* na kuwarudisha gerezani"

Waheshimiwa Wabunge, mara kwa mara kiti kimekuwa kikitoa mwongozo kuwa endapo Mbunge muuliza swali la msingi ameridhika na majibu ya Serikali, Mbunge mwingine hawezi kuomba Mwongozo wa kutoridhika na



majibu ya swali hilo. Kiti kimekuwa kikitoa mwongozo kuwa Mbunge ambaye hakuridhika na majibu ya Serikali anayo nafasi ya kuleta swali la msingi kuhusu jambo hili ili aweze kupata majibu fasaha ya Serikali.

Hivyo basi, Mheshimiwa Esther Matiko (Mbunge) kama bado unalo jambo mahsusi la kuitaka Serikali ilifanyie kazi katika eneo hili la watoto walio magerezani unashauriwa kullileta kwa njia ya utaratibu wa swali la msingi au hoja mahsusi kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya Kudumu ya Bunge ili kuwezesha Serikali kufanyia kazi jambo hilo na huo ndiyo Mwongozo wangu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusoma tangazo hilo, nawashukuru kwa kazi nzuri mliyofanya na ninaahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 12.01 Jioni Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano,  
Tarehe 8 Mei, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*